

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Saba - Tarehe 5 Februari, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Naomba tukae Waheshimiwa. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nane, leo ni Kikao chetu cha Saba. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Nakushukuru sana kwa niaba ya Kamati. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Karibu Mheshimiwa Mariam Ditopile, Makamu Mwenyekiti

**MHE. MARIAM D. MZUZURI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Japhary, uliza swali lako tafadhali.

Na. 81

### Hitaji la Hospitali ya Wilaya - Manispaa ya Moshi

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL** aliuliza:-

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi haina Hospitali ya Wilaya na kuifanya Hospitali ya Mkoa ya Mawenzi izidiwe na idadi ya wagonjwa:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha ili kujenga Hospitali ya Wilaya katika Manispaa ya Moshi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Kandege, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha taratibu za kukabidhi majengo na ardhi ya Kituo cha Afya Moshi Arusha kwa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ili kipanuliwe na kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Halmashauri. Baada ya kukamilika kwa taratibu hizo, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu inayohitajika kwa hadhi ya Hospitali ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa sasa wananchi wa Manispaa ya Moshi wanapata huduma katika Hospitali Teule ya Mtakatifu Joseph ambayo inafuata miongozo ya Serikali kwa kutoa matibabu bure kwa wazee, watoto chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhary, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mpango huu wa Serikali wa kupandisha hadhi Kituo cha Afya cha Moshi Arusha, lakini nilikuwa naomba Serikali, kwa sababu tunaelekea kwenye bajeti; na kwa sababu mchakato huo wa kupandisha hadhi kituo cha afya ni wa muda mrefu kidogo; ni lini sasa mpango huo utakamilika ili bajeti ya kukarabati hiyo miundombinu kwa ajili ya kuwa Hospitali ya Wilaya iweze kuingizwa katika bajeti ya mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, bado Moshi tuna tatizo kubwa la Vituo vya Afya. Tuna Vituo vya Afya viwili tu ambavyo vimeshazidiwa tayari; Kituo cha Afya cha Pasua na Kituo cha Afya cha Majengo. Nami naishukuru Serikali kwa kutupa shilingi milioni 400. Tumeleta maombi ya muda mrefu Serikalini ya kutusaidia kupandisha hadhi Vituo vya Afya vya Shirimatunda, Longuo B na Msaranga.

Je, ni lini Serikali itakubaliana na ombi letu? Kama hilo ombi haliwezekani, ni lini sasa itatujengea kituo kingine kimoja cha afya katika Manispaa ya Moshi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Josephat Sinkamba Kandege, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu yeye ni sehemu ya Madiwani na katika mchakato wa kuhakikisha kwamba tunabadilisha hicho Kituo cha Afya ni pamoja na wao kutekeleza wajibu wao. Atusaidie kusukuma Halmashauri yake kufanya taratibu zile ambazo anatakiwa kuzifanya halafu sisi tuweze kumaliza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameongelea juu ya suala zima la kubadilisha Zahanati kuwa Vituo vya Afya, ametaja nyingi lakini pia akawa na ombi kuwa, kama hilo haliwezekani ni vizuri basi tukafikiria suala la kujenga Kituo cha Afya kingine. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Zahanati zinaendelea kuwepo kama Zahanati kwa sababu Zahanati na Vituo vya Afya ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, siyo azma ya Serikali kubadilisha Zahanati kuwa Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, Zahanati zile zilizoziendelee kuwa Zahanati ila ombi la kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Afya kipya, hilo tunaliweka katika matazamiao ya siku za usoni.

**SPIKA:** Tulibakize swali hilo huko huko Moshi, Mheshimiwa James Mbatia tafadhali.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa swali la msingi ni kuhusu Hospitali ya Mawenzi na Hospitali ya Mawenzi kusema ukweli imezidiwa sana; namna gani Serikali inaona umuhimu wa kuimarisha hivi Vituo vya Afya kama alivyouliza Mheshimiwa Japhary Michael na hasa Kituo cha Afya cha Kirua Vunjo Magharibi ambapo tangu kimefungulia wa Mheshimiwa Abdu Jumbe mwaka 1973 miundombinu yake ni chakavu sana na wala hakina hadhi ya kuwa Zahanati ili kiimarike kiweze kutoa huduma kama vituo vingine vya afya?

**SPIKA:** Sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri amewahi kufika Kirua. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali ya Kituo cha Afya cha huko Kirua Vunjo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba vile Vituo vya Afya vilivyojengwa miaka ya zamani vilikidhi haja kwa kipindi hicho. Ukilinganisha na Vituo vya Afya ambavyo vimejengwa sasa, vile vingine vyote vya zamani vinaoneka vimechakaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwanza tulianza kukarabati vile ambavyo vipo lakini pia tukaanza kujenga upya. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vyote vya afya vinakuwa na hadhi ya Vituo vya Afya ili viweze kutoa upasuaji wa dharura kwa mama mjamzito.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbatia, kama ambavyo Serikali imekuwa ikipitia kuona takwimu Vituo vya Afya vipi vichakavu na cha kwake tutakipitia.

**SPIKA:** Ahsante. Bado tuko TAMISEMI, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu. Mheshimiwa uliza swali lako.

Na. 82

**Elimu ya Utawala na Usimamizi wa Fedha kwa Madaktari**

**MHE. ZAYNABU M. VULU** aliuliza:-

Kazi zote za Utawala na fedha katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya zinasimamiwa na Mganga Mfawidhi wa Wilaya wa eneo husika:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa elimu ya Utawala na Usimamizi wa Fedha Madaktari hao ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliajiri Wahasibu Wasaidizi 335 na kuwapanga kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kuimarisha usimamizi wa fedha kwenye Vituo vya Afya kupitia mfumo wa kielektroniki wa *Facility Financing, Accounting and Reporting System (FARS)*. Aidha, ili kukabiliana na upungufu uliopo wa wataalam hao wa utawala na usimamizi wa fedha, Waganga Wafawidhi katika Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati wamepatiwa mafunzo ya utawala na usimamizi wa fedha yaliyofanyika kuanzia tarehe 24 Desemba, 2018 hadi tarehe 22 Januari, 2019 katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea uwezo wataalam hao kwenye masuala ya fedha na utawala katika vituo wanavyovisimamia. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imewasilisha maombi ya kibali cha kuajiri zaidi watumishi wa kada za Wahasibu Wasaidizi kwa lengo la kuimarisha utawala na usimamizi wa fedha kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, swali la nyongeza nimekuona.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa ruhusa yako naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais, Jemedari Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa juhudi zake na msimamo wake wa kuhakikisha Watanzania tunapata huduma za afya. Ukiangalia kwenye Mkoa wetu wa Pwani, Vituo vingi vya Afya, Zahanati na Hospitali za Mkoa zimepata vifaa tiba na wataalam mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza: Kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameonyesha njia ya kutaka Watanzania wapate huduma bora na sahihi kwa wananchi wake: Je, hawaoni kwamba kwa kuwafanya Waganga Wafawidhi na wa Vituo vya Afya au Zahanati kusimamia masuala ya Uhasibu ni kuipelekea kada hiyo kuacha kazi zake za kutibu na kuhangaika maeneo mbalimbali kwenda kununua dawa, kwenda kufuata vifaa tiba na kuacha kutibu wagonjwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Kwa kuwa Serikali imeonyesha nia ya kuomba kibali kwa ajili ya Wahasibu na mpaka leo hii hicho kibali hakijapatikana; kwa nini msichukue wataalam wa uhasibu ambao wamemaliza masomo yao, wako maeneo mbalimbali Tanzania na wakafanya kazi hizo kwa kujitolea?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, niruhusu kwa niaba ya Serikali nipokee pongezi ambazo Mheshimiwa Mbunge ametoa. Naye amekuwa ni miongoni mwa *champions* ambao wamekuwa wakipigania suala zima la afya, naye anastahili pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake anaongelea suala zima la kwamba Waganga wanaacha kazi zao za kitaaluma na wanaanza kufanya kazi ya fedha; katika majibu yangu ya msingi nimemwambia kwamba tumeajiri watumishi wa Kada ya Uhasibu 335.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kwa muda mfupi ambao tumewapa hiyo taaluma ni ili wawe na uelewa wa jumla, lakini Uhasibu ni *professional* ambayo haiwezi ikasomewa ndani ya muda mfupi huo. Kwa hiyo, hawaachi kazi yao ambayo wameajiriwa nayo kuanza kufanya kazi ya usimamizi wa fedha, lakini ni vizuri *at least* wakajua nini ambacho kinaendelea kulikoni kutojua kabisa. Huo ndiyo msingi wa elimu ambayo imetolewa kwa hao Waganga.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anasema kwamba ni vizuri, pamoja na kwamba tumeomba kibalali cha kuajiri, sasa kuna wengine ambao wamemaliza taaluma ya Uhasibu wako Mtaani tuwaajiri wajitolee. Sina uhakika sana na kwa sera yetu haijatokea mahali hata pamoja ambapo tunataka mtu afanye kazi asilipwe.

Mheshimiwa Spika, tuendeleo kuwa na subira, Serikali ni sikivu na jana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya utawala alisema tunaenda kuajiri watumishi mbalimbali 45,000. Ni imani yangu kubwa katika hao watakaoajiriwa ni pamoja na Wahasibu wakaokwenda kufanya kazi hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Bado tuko TAMISEMI. Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI mfumo wa makusanyo ya fedha wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya ni tofauti kabisa na mfumo wa Halmashauri zote. Mifumo hii ni miwili *parallel*. Matokeo yake makusanyo kwenye Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali ni duni nchi nzima, kwa sababu ya mifumo ambayo haioani.

Kwa hiyo, uko umuhimu wa kuangalia huu mfumo wa afya ambao ni *very expensive*, haiwezekani kukaa kwenye Zahanati zote wala Vituo vya Afya vyote. Hata sijui ni kwa nini pawe na mifumo tofauti ya ukusanyaji fedha. Hakuna sababu!

Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na mfumo mmoja badala ya kuwa na mifumo tofauti ambayo inakwenda *parallel*. (*Makofi*)

Bado tuko Wizara ya Afya, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi.

Na. 83

### **Matibabu na Lishe Bora kwa Watu Wenye VVU**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD** aliuliza:-

Watu wanaoishi na VVU wanapata shida sana katika kupata lishe bora na matibabu ya uhakika:-

(a) Je, Serikali imejipangaje katika kuwapa mikopo itakayowasaidia kuendesha maisha yao kupitia vikundi mbalimbali?

(b) Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kutenga sehemu ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kundi hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Bado tuko TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri Josephat Sinkamba Kandege, bado tuko na wewe. Tafadhali, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inatoa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kwa wagonjwa wote wanaoishi na VVU ili kuimarisha afya zao na kuwakinga na magonjwa nyemelezi. Aidha, kwa kuwa watu wanaoishi na VVU wanashiriki kama kawaida katika shughuli za ujenzi wa Taifa, Serikali inawanashauri waendeleo kutumia fursa za mikopo zinazotolewa na taasisi za kifedha ikiwemo pamoja na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) na VICOBA.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauri na kusisitiza watu wanaoishi na VVU kuitumia fursa ya mikopo inayotolewa kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi na jumishi yatakayonufaisha makundi yote kiuchumi wakiwemo watu wanaoishi na VVU.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Hamad, Mbunge wa Wingwi.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikitegemea fedha kutoka kwa wafadhili katika kuhudumia waathirika wa gonjwa la UKIMWI fedha ambazo upatikanaji wake umekuwa na changamoto kubwa. Nilitaka kujua tu, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba sasa inatenga fedha za ndani katika kuhudumia kundi hili la wagonjwa wa UKIMWI? Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imekuwa inashirikiana na wadau katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na wadau wakubwa ni pamoja na *Global Fund* na *PEFA*.

Mheshimiwa Spika, katika kuliona hilo na kwa lengo la kuhakikisha kwamba hizi huduma za matibabu au huduma afua za VVU kwa waathirika zinakuwa endelevu, Serikali imeanzisha Mfuko wa Masuala ya UKIMWI ambao unaitwa *AIDS Trust Fund* ambapo Serikali inaweka fedha pale, inachangia fedha zake kwa lengo la kuhakikisha kwamba baadhi ya afua zinakuwa *funded* kwa kupitia mfuko huo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Naomba tuendeleo na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi. Mheshimiwa Mariam Kisangi tafadhali uliza swali lako.

Na. 84

**Kuendeleza Eneo la Chamazi Kitengo cha Afya ya Akili**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Eneo la Chamazi Mbagala katika Kitengo cha Afya ya Akili limetelekezwa na hakuna ukarabati wa majengo yaliyopo wala uendelezwaji wa eneo hilo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza eneo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ndugulile tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Chamazi lina ukubwa wa ekari 165 na linaendelea kutumika kwa shughuli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na ufugaji wa ngo'mbe, kuku wa mayai na nyama. Shamba hili pia linatumika kwa kilimo ambapo zaidi ni mazao ya mboga za majani, mahindi na nazi yanazalishwa. Pia kazi mbalimbali za mikono zinafanywa katika eneo hili zikiwemo kazi za ususi wa vikapu, mifuko, mikufu, bangili na mapambo mbalimbali kwa kutumia malighafi za asili. Kazi nyingine ni pamoja na ufumaji wa vitambaa, kofia na utengenezaji wa nguo za batiki.

Mheshimiwa Spika, shughuli hizi ni sehemu ya tiba kwa wagonjwa wa akili waliopata nafuu ili waweze kurudi katika hali ya kawaida na kushiriki katika shughuli za kiuchumi wanaporudi katika jamii. Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imeajiri Watalaamu wa Mifugo na Kilimo ili kuweza kusimamia shughuli za ufugaji na kilimo. Aidha Hospitali imekuwa ikisafisha shamba hilo kila mwaka kwa kuondoa vichaka na kukata majani.

Mheshimiwa Spika, mipango inaendelea katika mwaka wa Fedha 2019/2020. Hospitali ya Taifa Muhimbili imepanga kuanza ujenzi wa uzio kwa kuanzia eneo linapaka na maeneo yanamilikiwa na wananchi wanaoishi karibu na shamba hili. Sanjari na hilo Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kushirikiana na Kituo cha Afya cha Uwekezaji inaendelea kufanya mazungumzo na wabia kwa ajili ya kutumia sehemu ya shamba hili kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuzalisha vifaa tiba na dawa. Hospitali imeshafanya mazungumzo na wadau kutoka China, Hong kong, Uturuki, Tunisia na Jamhuri ya Czech.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi uliza swali la nyongeza

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa takwimu zinaonyesha wazi kwamba matatizo ya magonjwa ya akili yanaongezeka yanayotokana na msongo wa mawazo pamoja na matumizi ya madawa ya kulevya lakini hospitali maalum ya magonjwa hayo ni Milembe pakee. Je, Serikali haioni haja sasa ya kujenga hospitali kubwa ya magonjwa ya akili katika eneo hilo la Chamazi ili kusaidia wananchi wa Kanda ya Pwani waweze kupata matibabu lakini pia waweze

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kupata eneo ambalo wataendelea kufanya kazi mbalimbali pale za mifugo ili kujikimu kuliko vile walivyo watoto wetu walioharibiwa na madawa ya kulevya, kwamba hawana ajira na wanahangaika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Halmashauri ya Temeke imekuwa na tatizo kubwa la ardhi, na kwa kuwa idadi ya wagonjwa inaongezeka siku hadi siku katika Hospitali ya Zakiemu. Je, Serikali haioni haja sasa ya kushirikiana na Halmashauri ya Temeke ili kujenga hospitali pale katika eneo la Chamanzi Muhimbili ili iweze kuwasaidia wananchi wanaotoka Mbande, Chamazi, Mbagala, Maji Matitu pia na hata wale wa Wilaya ya Mkuranga?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri huku ukizingatia Dodoma tumeshazoea, kuna hali ya hewa nzuri sana ya kutoa tiba kwa wagonjwa wenye matatizo haya hapa Mileembe, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YAJAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kisangi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sasa hivi dunia imeweka msisitizo katika afya ya akili, na kwa sababu na sisi kama Serikali na dunia kwa ujumla inaona kwamba tatizo la afya ya akili linazidi kuongezeka kwa kasi sana na linahitaji msukumo na mtazamo wa aina ya pekee kabisa katika kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna hospitali moja kubwa ya Mirembe; na sisi kama Serikali mtazamo wetu wa mbele ni kuhakikisha kwamba, *especially* katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili badala ya kuwa na vitengo vidogo vidogo lengo letu sisi ni kwamba kila kitengo kuwa ni taasisi. Tumeanza na taasisi ya magonjwa ya moyo tumekwenda taasisi ya masuala ya mifupa; na lengo letu ni kwamba hata baadaye tuwe na taasisi ya magonjwa ya afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali lake la pili; ameongelea kwa nini Serikali isione umuhimu wa kujenga hospitali ya ziada katika eneo hili la Chamanzi. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zote ni taasisi za umma. Sisi kama Wizara hatujapokea ombi lolote kutoka halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Pindi tutakapokea ombi hilo tutalijadili na kulifanyia uamuzi kwa sababu tunaamini eneo lote hili ni kwa ajili ya utoaji huduma ya afya, na kwa sababu tuna eneo kubwa hatuoni sababu kwa nini tusingeze wigo wa utoaji huduma, *especially* katika eneo la Temeke ambapo kuna changamoto ya ardhi.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Lucy Owenye uliza swali lako

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Hospitali yetu ya Mawenzi nayo inayo kitengo cha afya ya wagonjwa wa akili na imejenga eneo katika eneo la Longuo; na kitengo hicho kinahudumia Kanda nzima ya Kaskazini. Hata hivyo katika kitengo kile hakuna uzio pia wahudumu hawako wa kutosha. Sasa nataka nijue, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanakarabati eneo lile na kuweka uzio na kuwepo na wahudumu wa kutosha kwa sababu inahudumia Kanda nzima ya Kaskazini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Owenya kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi eneo hili la afya ya akili sasa hivi limeanza kuwekewa msukumo kidunia na sisi kama nchi tumeanza kuliwekea nalo msisitizo. Tunatambua kwamba vitengo vyetu vingi vya afya ya akili vimekuwa na uchakavu na vinahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa watumishi. Watumishi katika kada hii ni wachache sana, na ndiyo maana sasa hivi Serikali imewekeza katika mafunzo ya wataalamu wa afya wa akili ili tuweze kwenda sambamba na changamoto na wimbi kubwa ambalo tunaliona katika jamii kwa wahanga wa afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, kadri ya uwezo wa kifedha unapopatikana na sisi kama wizara tutaendelea kufanya ukarabati wa kiuo hichi pamoja na vituo vingine vya afya ya akili nchini.

**SPIKA:** Bado tuko wizara hii swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq uliza swali lako tafadhali

Na.85

### **Ukatili Kwa Wanawake Na Watoto**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto bado unaendelea kwa kiwango kikubwa hapa nchini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwahudumia kwa unasahi na unasaha wahanga wa ukatili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tuko Wizara ya Afya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Ndugulile, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Viti Maalum) kutoka Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto hapa nchini. Kwa kuliona hilo, Serikali iliandaa mpango kazi wa kitaifa wa miaka mitano wa kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambao unatekelezwa kwa kipindi cha 2017/2018 na utaisha mwaka 2021/2022. Mpango mkakati huu unaainisha mikakati mbali mbali ya kupambana na kudhibiti ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha vituo 11 vya mkono kwa mkono (*One Stop Centres*) ambapo huduma za ushauri nasaha, huduma za kipolisi na huduma za matibabu zinapatikana katika eneo moja kwenye mikoa ya Dare es Salaam, Pwani, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza, Arusha, na Simiyu kwa ajili ya kuwahudumia waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Katika vituo hivi huduma za kipolisi, ushauri nasaha na huduma za afya zinatolewa kwenye kituo kimoja. Lengo la Serikali ni kuwa na kituo angalau kimoja kwa kila Mkoa na hii inaenda pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu katika eneo la utoaji huduma husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza, nina maswali mawili ya nyongeza. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake; lakini sambamba na hilo; kwa kuwa vituo vilivyopo katika haya maeneo havitoshelezi, hii imebainishakabisa katika majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nilipenda kujua, je, serikali ina Mkakati wowote wa kujenga vituo vya nyongeza katika bajeti ya mwaka ujao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa taarifa za ukatili hasa ulawiti kwa watoto wa kiume zimekuwa zikiongezeka, na inawezekana ni kutokana na utandawazi; je, Serikali ina mkakati wowote wa kuzuia hizi picha mbaya au picha za ngono ili kuweza kunusuru kizazi hiki?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza sana amekuwa ni mdau mkubwa sana wa kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusu afya ya mama na mtoto lakini vilevile masuala ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, nikupongeze sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kusudio la Serikali kuongeza vituo hivi; kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba tumeanza katika mikoa hii 11 na kusudio letu sisi kama Serikali nikufika katika mikoa yote. Ni kweli na ni lazima tukiri kwamba matokeo ya ukatili wa kijinsia yanazidi kuongeza ndani ya nchi yetu. Mwaka 2017 tulikuwa na matukio ya ukatili wa kijinsia takribani 41,000, mwaka 2018 yakawa zaidi ya 45,000 na sasa hivi tunafanya *compilation* ya matukio ya mwaka 2019. Lakini tunaamini kwamba matukio haya bado yanazidi kuongezeka na ndio maana sisi kama Serikali tumekuja na huu Mpango wa MTAKUWA ili kujaribu kuhakikisha tunadhiti kabisa matukio haya, ikiwa pia na kwa kwenda sambamba na kuhakikisha kwamba wale wahanga wa ukatili wa kijinsia wanapata huduma stahiki. Kwa hiyo kusudio letu la Serikali ni kwenda katika ngazi zote, katika ngazi ya mkoa na baada ya hapo tutaanza kushuka katika ngazi ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili aliongea matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto hususan watoto wa kiume, na mligusia hili kutokana na masuala ya kiutandawazi. Ni kweli matukio haya tunayapata na sisi kama Serikali, na mara nyingi matukio haya yanafanywa na watu wa karibu ndani ya familia. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri jana aliliongelea hapa ndani ya Bunge; kusema kwamba tunahitaji kwa kweli kama wazazi kuhakikisha tunakaa karibu zaidi na watoto wetu, tunafatilia maendeleo ya watoto wetu, tunakaa na kuongea na watoto wetu majumbani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tuna mkakati mwingine wa ziada wa kuhakikisha kwamba katika shule tunaweka madawati ya masuala ya ukatili wa kijinsia; kwa sababu ukatili wa kijinsia mara nyingi unafanywa na watu wa karibu na nyumbani na saa nyingine mtoto anaweza asiseme kwa kuhofia kupata adhabu kwa mtu ambaye amemfanyia ule ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasahivi tunafanya maongezi na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba kuna walimu katika kila shule ambao wamepata mafunzo haya ili watoto waweze kuyasema haya mashuleni na hawa walimu kuweza kusaidia kuchukua hatua. Vilevile tunashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Sanaa kuhakikisha kwamba kunawekwa misingi mzuri ya udhibiti wa mtangazo katika redio, television na vyombo vingine vya habari kwa

kuhakikisha kwamba zile *content* ambazo zipo zinaendana na maadili ya kwetu sisi kama Watanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Kemi

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi. Kwa kuwa ukatili wa kijinsia huathiri watu mbalimbali kisaikolojia na huathiri; afya ya akili na kwa kuwa ukishaathirika kisaikolojia afya ya akili inaleta kutokuzalisha vizuri kama ni shughuli za kutuletea uchumi au watoto ku-*perform* darasani kwa hiyo unakuwa na taifa ambalo halipo sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wale wanaoathirika kisaikolojia au afya ya akili wanakosa kupata huduma stahiki kwa sababu kuna changamoto ya gharama tiba na pia watalamu ambao wanafanya hizi shughuli za *counseling* wapo wachache nchini; sasa Serikali haioni ni muda muafaka wa kufanya tathmini wa hali hii na jinsi ya kuweza kuwapatia huduma wananchi wake stahiki inavyotakiwa kwa gharama ambayo wanaweza wakaimudu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sware Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hathari moja wapo ya ukatili wa kijinsia ni kuweka makovu ya kisaikolojia kwa watu wengi na napelekea baadhi ya watu hata kushindwa kufanya vizuri katika masomo, kushindwa kujenga mahusiano na watu wengine, kuwa na tabia ya kuwa na hasira na vitu vingi ambavyo vinamwathiri mtu kisaikolojia. Ni kweli hili tatizo linazidi kukuwa na sisi kama Serikali kupitia mpango wetu wa MTAKUWA tumeainisha baadhi ya mikakati ambayo tunaiweka katika kudhibiti hali hiyo. Tunatambua kwamba ni kweli tuna changamoto hii ya wigo wa ushauri nasaha kwa hawa wahanga na gharama za matibabu kwa hawa wahanga wa ukatili wa kijinsia. Tutafanya hiyo tathmini na kuangalia jinsi gani sasa ya kuweza kutoa huduma nzuri kwa hawa wahanga wa ukatili wa kijinsia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kemilembe nilikutaja

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mtakubaliana nami kwamba kuna mstari mdogo sana kati ya uzima na afya ya akili. Katika nchi ambazo tafiti zimefanyika kwa mfano Marekani inaonyesha katika kila watu wanne mmoja ana tatizo la afya ya akili, Uingereza katika kila watu watano mmoja ana tatizo la afya ya akili, Australia katika watu 6 mmoja ana tatizo la afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, nadhani wewe mwenyewe unaweza kuwa shahidi hata humu ndani wakati mwingine unajiuliza tuko salama kiasi gani. Nataka kufahamu je, Serikali yetu imefanya tafiti ya kujua ni idadi gani ya watu ambao wameathirika na ugonjwa wa afya ya akili Tanzania? Na kama tayari tafiti zimefanyika matokeo yake yakoje?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Hasa kwa wanyamwezi kule kuna shida kweli. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, mmefanya utafiti?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kemilembe Lwota Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli changamoto za afya ya akili zinazidi kuongezeka na ndio maana Shirika la Afya Duniani sasa hivi linaweka msukumo mkubwa katika kuliangalia suala la afya ya akili. Takwimu zake ziwezi nikazipinga, ni kweli takribani karibia asilimia moja ya katika jamii yetu ya Tanzania tunaamini kwamba wana tatizo la afya ya akili.

Kwa hiyo hata hili alilolisema, kwamba hata humu ndani inawezekana na sisi ile asilimia moja tuna changamoto kama hizo. Sisi kama Serikali bado hatujafanya utafiti wa kina wa kuangalia ni uzito wa jambo hili likoje aina gani ya magonjwa ya akili ambayo tunayo ndani ya nchi yetu. Tunalipokea hili Mheshimiwa Mbunge na tutaenda kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Viwanda na Biashara sasa *Chief Whip* wa Upinzani Mbunge Bunda Mjini uliza swali lako.

Na. 86

### **Ufufuaji Wa Kiwanda Cha Ushashi Ginnery**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani juu ya ufufuaji wa kiwanda cha USHASHI GINNERY kilichopo Bunda ili kukabiliana na changamoto ya ajira hasa kwa vijana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara *Enginner Stella* Manyanya tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Ushashi kwa sasa kinafanyiwa tathmini ili kubaini hali ya uchakavu na kuona namna bora ya kukifufua. Aidha, Mpango wa Serikali ni kuhamasisha na kuwezesha kiwanda hicho kisichofanya kazi kianze kufanya kazi baada ya kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, Wizara ya Kilimo na Benki ya Kilimo kwa kushirikiana na kuhakikisha viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na *Mara Cooperative Union (1984) Ltd* vinafufuliwa na kufanya kazi hivyo kuongeza fursa za ajira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya dada yangu; kwa sababu ameji-commit kwamba mnafanya utafiti ili kuona gharama halisi ambazo zitasababisha mfufue.

Mheshimiwa Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza Bunda tulikuwa tuna Ginnery tano ambayo ni Kibara, Ushashi, Mara Rint, Bulamba na Olam na zinazofanya kazi ni mbili. Tatu ukiwepo na Ushashi hazifanyi kazi zinafanya kazi Olam na Bulamba lakini Mara Rinti ni nzima na ina kila kitu tatizo lake ni mwekezaji. Sasa ni lini Serikali mtatafuta mwekezaji ili hii

*Ginerry* ya Mara Rinti ifanye kazi na ipo kwenye eneo *very strategic* na ikifanya kazi itapunguza changamoto ya ajira kwa akina mama na vijana wa Jimbo la Bunda Mjini na Wilaya nzima ya Bunda kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara tuna kiwanda cha nguo, kipo Musoma. Hata hivyo sasa hivi hiki kiwanda hakifanyi kazi kwa ufanisi na ukiuliza changamoto kubwa kwa nini kiwanda hiki hakifanyi kazi; na kuwepo kwa kiwanda hiki ni kutokana na malighafi ile ya pamba iliyopo kwenye Mkoa wetu wa Mara na maeneo jirani. Sasa nimeuliza changamoto ni mtaji, na kama hakifanyi kazi kwa ufanisi ina maana kunapunguza ajira kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kujua, ni lini Serikali mtaongeza mtaji ili akina mama, vijana na wazee wa Mkoa wa Mara wanufaike kwa ajira kutokana na kuwepo kwa kiwanda hiki katika Mkoa wa Mara?

Sasa ningependa kujua ni lini Serikali mtaongeza mtaji ili wamama, vijana na wazee wa Mkoa wa Mara wanufaike kwa ajira kuwepo na kiwanda hiki katika Mkoa wa Mara? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe, majibu ya maswali hayo tafadhali. Wa viwanda na biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu vizuri swali la msingi. Serikali imeona umuhimu wa kufanya uchambuzi katika kutekeleza Sera ya zao la pamba ya *cotton to cloth* kwa hiyo, lipo zoezi la kuhakikisha tunachambua na kuangalia namna bora ya kufufua *ginnery* zote za pamba kwa sababu *value chain* ya *cotton to cloth* inaanzia kwenye *ginnery* kufanya kazi mpaka kwenye *textile industries*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Bulaya kwamba hata kiwanda cha *MUTEX* kiko sehemu ya hili zoezi. Nimeshafika kwenye kiwanda hicho na ninakuhakikishia katika zoezi hili tutafia pia kwenye *ginnery* hizi ulizozitaja na tunashirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha zoezi hili linafanyika haraka sana iwezekanavyo. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nilikuona Mheshimiwa Chegeni, Mbunge wa Busega uliza swali lako.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na pamoja na jitihada nzuri za Serikali ya Awamu ya Tano ya kufufua viwanda, tayari kuna mpango ambao Serikali kupitia Mifuko ya Jamii inataka kufufua viwanda vya Ngasamo, na Nasa. Viwanda hivi viko katika Wilaya ya Busega na ni viwanda ambavyo vinatoa huduma nzuri sana kwa wakulima wa pamba. Nilitaka kujua tu ni lini Serikali sasa maana wanasema wanategemea, ni lini tutarajie kwamba kiwanda kama cha Ngasamo na kiwanda Nasa vitaanza kufanya kazi kuwahudumia wakulima wa pamba katika Wilaya ya Busega. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, *ginnery* za zamani hizo kabisa, Nasa Nyashimo, Ngasamo. Mheshimiwa Naibu waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, sijui kama nitakuwa na majibu mazuri zaidi sana ya yale ambayo amesema Mheshimiwa Waziri wangu. Kimsingi niseme tu zao la pamba ni kati ya mazao ya kimkakati na ni zao ambalo linategemewa sana

ikizingatiwa kwamba pale ambapo kunakuwa na uchakataji wa pamba katika hatua yoyote ile iwe ni kwenye pamba mwanzoni au kwenye utengenezaji wa nguo, ajira zinazotokea hapo ni nyingi sana. Kwa mfano kwenye kiwanda kama cha A to Z nilichokitembelea juzi unakuta kwamba ni watu zaidi ya 8,000 wameajiriwa pale kwa hiyo Serikali inaona umuhimu wa kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua tulizonazo pamoja na ambazo amezeleza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, tumekuwa tukikutana na wataalam wa aina mbalimbali lakini pia wataalam wetu kama *TILDO* wamekuwa wakienda kushirikiana katika kufuatilia wadau ambao tunaweza tukashirikiana nao. Hivi juzi tu tulikuwa na wataalam kutoka Korea na tunafikiria kwamba katika maeneo yote ambayo yanalima pamba, hizo *ginneries* pamoja na viwanda vya pamba katika kipindi hiki tunachoendelea nacho tuweze kuhakikisha kwamba angalau tunapata kiwanda kimoja kikubwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa James Millya, bado tuko Wizara ya Viwanda na Biashara, uliza swali lako Mbunge wa Simanjiro. Kwa niaba yake muulizie Mheshimiwa.

Na. 87

### Hitaji la Masoko ya Vitunguu Maji – Simanjiro

**MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y. MHE. JAMES K. MILLYA)** aliuliza:-

Jimbo la Simanjiro lina Wakulima wa vitunguu maji kwenye Kata za Ruvu, Remit, Ngage, Ngorika na Msitu wa Tembo kutokana na maji ya uhakika toka Mto Pangani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia masoko Wakulima hawa ambao ni Watanzania wanaopambana ili kujikwamua kiuchumi na kuongezea nchi mapato?

(b) Wafanyabiashara kutoka nchi jirani ya Kenya wanatumia fursa ya ukosekanaji wa masoko kwa Wakulima wetu kwa kuwanyonya: Je, Serikali inawezaje kuweka mkakati wa uhakika ili kuwasaidia Wakulima wetu wasinyonywe?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Simanjiro lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa *ASDP I* Serikali iliwezesha ujenzi wa maghala ya kuhifadha vitunguu katika vijiji vya Ngage, Lemkuna na msitu wa Tembo katika Wilaya ya Simanjiro. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha ujenzi wa vituo maalum vya ununuzi wa mazao vyenye maghala ya kuhifadha mazao. Vituo vya aina hiyo vitasaidia wakulima kuwa na nguvu ya pamoja ya kujadiliana na wanunuzi, ili kupata bei yenye ushindani wa haki katika soko. Vituo hivyo kwa uratibu wa halmashauri vitakuwa ndivyo sehemu maalum kwa wanunuzi wa ndani na nje ya nchi. Kupitia mkakati huo, wakulima na halmashauri watanufaika na mauzo ya mazao kwa kupata bei ya ushindani, takwimu na mazao yatauzwa yakiwa na ubora.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanza kutambua Kampuni za kitanzania zinazouza vitunguu nje ya nchi na kuendelea kuzihamasisha kununua mazao ya ndani na kuyatafutia soko nje ya nchi. Kwa kipindi cha Mwezi Januari 2019 hadi Disemba 2019, jumla ya Kampuni 19 za Kitanzania zilipewa vibali vya kuuza tani 19,630 za vitunguu katika nchi za Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Kenya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu Vijijini uliza swali lako.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa masoko haya ya vitunguu yamekuwa tatizo karibu maeneo mengi, je, kuna mpango gani sasa kama Serikali kusaidia eneo hilo la msitu wa tembo na maeneo hayo ili wachuuzi wanapokuja basi waweze kuuza vitunguu vyao katika hali ya biashara.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa eneo la Simanjiro ni kubwa sana na walima vitunguu kwa maeneo hayo. Je, unaonaje, uko tayari kushirikiana na Mbunge wa Simanjiro ili kusaidia ujenzi wa soko la vitunguu katika Jimbo la Simanjiro? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara Engineer Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba katika mikakati ya Tanzania kwa ujumla wake na hasa katika kuwezesha biashara kufanyika katika mazingira mazuri, suala la ujenzi wa masoko pamoja na kuweka muunganiko kati ya wafanyabiashara na wazalishaji ni jambo muhimu sana. Kwa hiyo, kwa ujumla wake niseme tu kwamba kwa kushirikiana na ofisi ya Rais TAMISEMI Wizara ya Viwanda na Biashara lakini pia pamoja na uwekezaji kwa pamoja tunaangalia kwanza kusaidia katika suala la kuongeza thamani mazao hayo kwa kuwezesha kuwepo kwa viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa. Vilevile kuhakikisha kwamba bei zinazotumika zinakuwa ni nzuri na sio zile za kuwanyonya wakulima ikizingatiwa pia suala la vipimo.

**SPIKA:** Tunaendelea na Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, tafadhali.

Na. 88

#### **Mkakati wa Kuongeza Pato Litokanalo na Utalii**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Nchi yetu imebarikiwa kuwa na Hifadhi nyingi zenye wanyama wengi wa kuvutia lakini mapato yatokanayo na utalii ni kidogo: Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza mapato ya utalii.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo na Mheshimiwa Mbunge wa Ulanga, Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine Kanyasu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii imeendelea kukua mwaka hadi mwaka. Mathalan

idadi ya watalii imeongezeka kutoka 1,137,182 mwaka 2015 hadi kufikia watalii 1,505,702 mwaka 2018. Katika kipindi cha mwaka 2018 pekee Sekta hii imechangia katika uchumi wa nchi Dola za Marekani bilioni 2.4, sawa na takriban trilion 5.4. Sekta hii imechangia kwa wastani wa asilimia 17 ya Pato la Taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni. Aidha, inatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja milioni 1.6. Hata hivyo, kiwango cha mchango wa sekta hii bado ni kidogo ukilinganisha na rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Wizara yangu imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini na mchango utokanao na sekta hii. Mikakati hiyo ni pamoja na kupanua wigo wa mazao ya utalii kijiografia kupitia Mradi wa *REGROW* ambapo Serikali inaendelea kufungua utalii katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kwa kuimarisha miundombinu ili kuboresha shughuli za utalii hususani katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Nyerere. Aidha, Serikali imeanzisha Hifadhi mpya za Taifa sita ambazo ni pamoja na Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa, Rumanyika-Karagwe, Mto Ugalla, Nyerere na Kigosi. Lengo la Serikali ni kufungua na kutumia fursa za utalii nchini katika mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Serikali imekusudia kuongeza mazao ya utalii. Hivi sasa, hapa nchini tumejikita zaidi katika kuziendeleza hifadhi za Taifa. Tunataka kuhakikisha kwamba mazao mengine ya utalii kama utalii wa kuvinjari kwa meli, utalii wa kupunga upepo fukwe na utalii wa mikutano ukiongezeka.

Mheshimiwa Spika, sanjari na juhudi hizo, Mwezi Septemba, 2019 Wizara yangu kwa kushirikiana na Nyanda za Juu Kusini iliandaa kwa kushirikiana na Sekta Binafsi maonesho makubwa ya utalii Jukwaa la Uwekezaji yajulikanayo kama Karibu Utalii Kusini ambapo zaidi ya washiriki mia tano kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki. Vilevile, Mwezi Oktoba, 2019 Wizara iliandaa Onesho la Kimataifa la Utalii la *Swahili International Tourism Expo* lililohusisha wafanyabiashara wakubwa wa utalii takribani 400 na Mawakala wa Kimataifa 200 kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kigoma na Tabora imeanza maandalizi ya maonesho makubwa ya Kimataifa ya jukwaa la utalii na uwekezaji yanayojulikanayo kama *Great Lakes International Tourism Expo* ambayo yatafanyika Mwezi Juni, 2020. Imani yangu kuwa mikakati hii itasaidia kutangaza vivutio vya utalii, vya uwekezaji na kuongeza watalii nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati hiyo, Wizara imeendelea kuimarisha shughuli za utangazaji wa vivutio vya utalii wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na kufungua masoko mapya nchini China, India, Urusi na Israeli. Aidha, katika kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali, Wizara imekamilisha ujenzi wa mfumo funganishi wa kieletroniki kwa ajili ya kusajili na kutoa leseni, na kukusanya takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Awamu ya Tano, katika kuboresha miundombinu nchini ikiwemo viwanja vya ndege, ujenzi wa reli, upanuzi wa bandari, kuimarika kwa Shirika la Ndege ambalo limeanza kuhudumia watalii wa ndani na nje ya nchi. Juhudi hizi zitasaidia sana kukuza Sekta ya Utalii nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga, swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba niipongeze Serikali kwa dhati kabisa kwa juhudi zake za dhati za kuboresha utalii katika nchi yetu. Kama Mbunge,



nimesikitishwa na kauli za baadhi ya Wabunge wa Upinzani kubeza juhudi za Serikali za kuboresha utalii na kuchochea kwa kutumia wasanii wa ndani. Niwaambie tu wasanii, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua mchango wao mkubwa katika kujenga nchi yetu. Kwa hiyo iwapuuze hao, hii ni tabia yao na ndivyo walivyo.

Mheshimiwa Spika, swali langu namba moja, maeneo au halmashauri nyingi ambazo zimezungukwa na *National Park* hawanufaiki na shughuli za utalii kwa kuwa hoteli zile zimejengwa ndani ya zile mbuga. Sasa je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuweka utaratibu wa kujenga hoteli zile za kitalii nje ya zile hifadhi ili wananchi wa maeneo yale waweze kunufaika kama kodi na vitu vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, tunafahamu nyamapori ni tamu sana. Mtalii anapoona akatamani na akala, itavutia watalii wengi sana kuja hasa wa ndani. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati iweke utaratibu wa kuweka vigenge vya nyama choma ndani ya mbuga zile ili mtalii anapoona nyama ile anaitamani halafu anaila sio aone, atamani, aondoke. Ahsante.

**SPIKA:** Eh, watu wale nyamachoma kama ilivyo *carnival* kule Nairobi. Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, MALIAISILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kipekee kabisa naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mlinga, watu wengi wanapomuona hapa Bungeni huwa wanafikiri ni mtu wa vituko lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mlinga ni mfuatiliaji mkubwa sana wa masuala ya uhifadhi lakini na masuala ya kiuchumi yanayohusu wananchi wake na halmashauri yake. kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Mlinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni tumefanya mabadiliko ya Kanuni na tunaandaa Kanuni ili kuruhusu matumizi ya nyama ya wanyamapori kwa watu wengi na katika kufanya hivyo tunapitia upya kanuni ili tuweze kuruhusu uwindaji wa ndani lakini pia kufunguliwa kwa mabucha ambayo yatakuwepo katika maeneo mbalimbali na kuyasajili. Kwa hiyo, taratibu hizo zitasaidia pia kuhakikisha kwamba nyama hii ya wanyamapori inapatikana katika maeneo yote yaliyoko katika hifadhi na maeneo ya mapori ya akiba ambapo wafanyabiashara watataka kupeleka nyama hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili Mheshimiwa Mlinga anataka kujua maoni ya Serikali ni kwanini hoteli zisijengwe nje ya hifadhi. Nakubaliana na Mheshimiwa Mlinga kwamba hivi sasa kwa mfano katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, nafasi ya kujenga hoteli ndani zimejaa na uzoefu tulionao ni kwamba kadri hoteli nyingi zinavyozidi kujengwa ndani ndivyo uharibifu wa mazingira unazidi kuondoa uhalisia wa hifadhi yenyewe ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwa sasa kwamba wawekezaji wote wapya tutawapeleka nje ya Hifadhi ya Serengeti na hifadhi zingine za Taifa ili kuvutia pia wananchi wanaozunguka maeneo hayo kuweza kujishughulisha na biashara ndogondogo moja kwa moja na hoteli hizo. Kwa hiyo, tunauchukua huo kama ushauri ingawa hauwezi kutumika hivyo katika hifadhi zote kwa sababu zipo hifadhi ambazo bado zina nafasi ambazo zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Nimekuona Waziri wa Maliasili na Mheshimiwa mama Salma. Maswali mafupi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nina swali moja dogo. Kwa mujibu wa *United Nation World Tourism Organization* mwaka 2018 dunia

nzima imekuwa na watalii bilioni 1.4 ni kwanini Tanzania imeendelea kusuasua imeshindwa ku-*capitalize* kuwavutia watalii hawa kuja nchini ikizingatiwa kuwa watalii kutoka Israel na kutoka Ulaya hususan Ujerumani wamekuwa ni wale wale wanaokuja kutoka enzi za utawala uliopita.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, Constantine Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mchungaji Msigwa ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa hiyo ninaamini kwamba kama ana mchango wowote utakaosababisha watalii waje nchini anaweza kuutoa kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi tumetoka kwenye watalii 1,100,000 mpaka 1,500,000 watalii ni tofauti kabisa na mzigo wa mahindi kwamba unaweza ukaamka asubuhi ukawa na tani 10 kesho ukaleta tani 100. Wanahitaji maandalizi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikitokea leo Tanzania ikapata watalii 3,000,000 kwanza nafikiri takwimu wanazo, Tanzania kwa ujumla wake na hoteli zake zote hatujazidi vitanda 30,000. Sasa ikatokea leo tukapata watalii 2,000,000 kwa mpigo, Tanzania nzima itajaa watalii na inawezekana hata sehemu ya kuwapeleka hakuna. Lakini tunahitaji miundombinu. Katika nchi nyingi ambazo unaona zinapata watalii wengi, hakuna *seasonal* za utalii. Watalii wanafanya utalii mwaka mzima. Sisi katika kipindi kifupi cha mwaka tuna *high season* ambacho ndicho tunachopokea watalii 1,500,000 tunachofanya sasa hivi ni kuimarisha miundombinu, tunafungua barabara zipitike mwaka mzima, tunaimarisha usafiri tuwe na shirika ambalo linaweza likasafirisha watalii ndani na tunaendelea kuyafikia masoko na kuhamasiha uwekezaji ili tuweze ku-*accommodate* idadi kubwa ya watalii ambao wanakuja nchini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Msigwa kwamba idadi ya watalii wanaokuja sasa anaweza akawa ni yule yule kutokana na *experience* aliyopata Tanzania nafikiri unafahamu kauli yetu ya Tanzania *unforgettable* kwa hiyo mtu anaweza kutamani kurudi mara kumi lakini tunaendelea kuyafikia masoko mengine nje na hivi sasa tunaendelea kufika Urusi, China, India masoko ambayo hatukuweza kuyazoea awali. Kwa hiyo naamini kwa muda mfupi ujao tutafikia watalii ambao anawataka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwa muda mfupi ujao tutafikia watalii wengi ambao anawataka Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Hivi Wizara ya Maliasili inajua kwamba katika vivutio vikubwa vya watalii wa ndani, Bunge la Tanzania linaongoza kuliko hata hifadhi nyingine yoyote? *(Makofi)*

Ukiangalia *gallery* zetu zinavyojaa kila wakati, kwa mwaka mzima, tukijumlisha watalii wa ndani wanaokuja hapa Bungeni, sisi ni nambari *one*. Kwa hiyo, mtuweke Bunge la Tanzania katika vivutio vya watalii Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Salma Kikwete nilikuona, tafadhali uliza swali lako.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Tunatambua na tunajua kuwa maliasili ni kitu muhimu sana katika ustawi wa Taifa letu la Tanzania na huchangia pato la asilimia 17 kutokana na utalii huo. Mkoa wetu wa Lindi ni miongoni mwa sehemu ambazo zinapitiwa na Selous ambayo sasa hivi ni *Mwalimu Nyerere National Park*.

Mheshimiwa Spika, sasa katika Mkoa huu wa Lindi, kuna tatizo ambalo lipo katika Tarafa ya Melola, Kata ya Milola na Tarafa ya Mkinga, Kata ya Mchinga ambalo hili ni Jimbo la

Mchinga. Wanyama kama tembo wanaingia katika maeneo hayo hata Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa Bobali ana ushahidi juu ya jambo hili. Pia wanyama hawa wanapoingia wanaleta uharibifu wa mazao na vilevile wanasababisha baadhi ya watu kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatuambia nini au inawaambia nini wananchi hawa juu ya uharibufu huo ambao umetokea katika maeneo hayo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali. (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kanyasu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba nikiri kwamba kutokana na mafanikio makubwa ya uhifadhi ambayo yametokea katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, migogoro mingi ya wanyama na binadamu imeripotiwa katika *almost* nchi nzima. Nakubaliana na Mheshimiwa Mama Salma kwamba katika maeneo ya Melola imeripotiwa sana kwamba tembo wanavamia makazi ya watu na kula mazao; lakini siyo huko tu, ni maeneo mengi, *almost* nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tumeafanya nini kama Wizara? Moja, tumeelekeza taasisi zetu zote ikiwemo TAWA, TANAPA, TFS na Ngorongoro kuimarisha vitengo vinavyo-respond na matukio haya. Wote tumewaambia wawe na kikosi ambacho kipo tayari. Hata hivyo, imetokea mara nyingi kwamba wakati wanyama wanakuwepo kijiji kingine, wakati mwingine tumeshindwa kuwahi. Naomba nitumie fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tumetoa maelekezo na suala hili tunalifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia ya mazao, Wizara imerekebisha kanuni ili kuweza kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kinachoridhisha. Kanuni hizo zimekamilika, tutahakikisha kwamba malipo haya yanawahi kwa waathirika ili kuweza angalau kuwafuta machozi na jasho kwa muda mu Nakushukuru sana. (Makofi)

Na.89

#### **Ushirikiano Kati ya TFS na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliluliza:-

Je, ni kwa namna gani Wakala wa Misitu (TFS) inashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, hususan Wilaya katika kusimamia misitu hapa nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Naibu Waziri wa Maliasili, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Tathmini ya Rasilimali za Misitu Tanzania (*National Forest Resources Monitoring and Assessment - NAFORMA*) ya mwaka 2015, Tanzania ina rasilimali za misitu zinazokadiriwa kufikia hekta milioni 48.1 ambapo asilimia 34 inasimamiwa na Serikali Kuu, asilimia 6.5 inasimamiwa na Halmashauri, asilimia 45.7 inasimamiwa na vijiji, asilimia 7.3 inasimamiwa na Sekta Binafsi na asilimia 6.0 ya misitu

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

iko katika ardhi huria (*general land*). Kulingana na taratibu za Serikali, misitu ya Tanzania inasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Mamlaka za Usimamizi wa Misitu Nchini zipo katika Wizara mbili, nayo ni Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo imekasimu mamlaka hayo kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*) ambapo una jukumu la kusimamia misitu ya Hifadhi ya Serikali Kuu na misitu mingine yote ambayo haijahifadhiwa kisheria; na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*) inayosimamia misitu iliyopo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Halmashauri na Vijiji*).

Mheshimiwa Spika, kwa taffiti zilizopo, misitu ya Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa mbili; kwanza, uharibifu mkubwa wa misitu ambao kwa sasa umefikia kiasi cha hekta 470,000 kwa mwaka; na pili, mahitaji ya mazao ya misitu yanayozidi uwezo wa misitu kwa zaidi ya meta za ujazo milioni 19.5. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kufanya jitihada za pamoja kati ya Wizara hizi mbili zinazosimamia rasilimali za misitu. Kupitia ushirikiano huo, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia taasisi yake ya *TFS* imekuwa ikishirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango huo wa pamoja, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumekubaliana kushirikiana katika maeneo mbalimbali ambayo ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa misitu na ufuatiliaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Misitu Tanzania. Ushirikiano huo unashirikisha ngazi ya wilaya ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Uvunaji wa Mazao ya Misitu katika Wilaya ni Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Afisa Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ni Mjumbe wa Vikao vya Uvunaji na ndiye anayetoa leseni za uvunaji wa mazao ya misitu katika Wilaya husika. Vilevile, ushirikiano mwingine upo katika kutoa elimu kwa Umma, kuhifadhi misitu kwa njia shirikishi, kuanzisha magulio ya mkaa na kusimamia doria za kudhibiti uvunaji na usafirishaji haramu wa mazao na bidhaa za misitu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano huo, tarehe 26 Mei, 2016 Wizara ya Maliasili na Utalii ilisaini Mkataba wa Makubaliano na Ofisi ya Rais, *TAMISEMI* ya kuimarisha zaidi ushirikiano katika usimamizi wa misitu nchini na utawala bora. Kufuatia makubaliano hayo, vikao vya pamoja katika ngazi ya wilaya vya kujadili utekelezaji vimekuwa vikifanyika kila mwaka ili kuchambua changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla utunzaji na uendelezaji wa misitu nchini unakabiliwa na changamoto mbalimbali kulingana na mazingira ya mikoa na wilaya husika.

Hata hivyo, Serikali kupitia Wizara hizi mbili itaendelea kuweka mikakati mbalimbali ili kuwezesha rasilimali za misitu kuendelea kutumika kwa kufuata taratibu zilizopo ili rasilimali hizo zinufaishe vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, najipongeza Wizara kwa majibu mazuri na vilevile najipongeza *TFS* kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, leo ni tarehe 5 mwezi wa Pili, *Happy Birthday* kwa Chama cha Mapinduzi. Mungu aendelee kukibariki chama chetu. (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Mheshimiwa umesema leo ni...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Tarehe 5 mwezi wa Pili, Chama cha Mapinduzi kinatimiza miaka 43 tangu kizaliwe. (*Makofi/Vigelegele*)

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Makofi haya hayatoshi kwa Wabunge wa CCM. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliimba wimbo wa birthday)*

**SPIKA:** Nashangaa Wapinzani hawajapongeza leo *happy birthday* ya CCM jamani. Mheshimiwa Mollel endelea. *(Kicheko)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa mdogo nakumbuka ule wimbo ukisema kwamba: "Kuzaliwa kwa chama kipya, tarehe 5 mwezi wa Pili Sabini na Saba, eeh Mungu, kipe baraka. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Mollel kuuliza swali lako, tafadhali.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Baada ya kusema hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, misitu ni uhai na kama misitu ni uhai, kila mmoja wetu...

**SPIKA:** Jamani tumsikilize Mheshimiwa. Unajua kuna Vyama vya Siasa havijui hata vilizaliwa tarehe ngapi mwaka gani? Endelea Mollel. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Vipo vipo tu!

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** ...kila mmoja wetu ana jukumu la kulinda misitu. Pamoja na jitihada nzuri za Serikali, ningependa kufahamu kwamba kumekuwepo na utaratibu wa kusafirisha magogo kwenda nje ya nchi; hii pia ni mojawapo ya chanzo cha uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba inalinda misitu yetu na misitu hii iendeleo kutulinda na sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, itakapofika mwaka 2022 tunafahamu kwamba bwawa la Mwalimu Nyerere la kuzalisha umeme litakamilika na ni dhahiri kwamba litapunguza gharama kubwa za umeme. Vile vile tukitumia gesi yetu itakuwa ni njia mojawapo pia ya kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba gesi tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu hapa nchini inafanya jitihada gani kuhakikisha kwamba wananchi wanaingia katika zoezi zima la kutumia gesi kuweza kulinda mazingira yetu? Nini jitihada za haraka za Serikali?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Mollel tafadhali. Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana kwa mwuliza swali. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kufuatilia matumizi ya gesi katika mkakati wa kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwanza mkaa unaoingia katika Jiji la Dar es Salaam kwa kila siku ni zaidi ya magunia 400,000 mpaka 500,000 na hiyo yote inahusisha ukataji wa miti na kuharibu mazingira. Vile vile kuni zinazotumika vijijini pamoja na mkaa ni zaidi ya wananchi zaidi ya asilimia 71. Sasa mkakati ulipo kwa sasa ni kuhakikisha kwamba gesi hii inatumika katika shughuli za majumbani ili kupunguza ukataji wa miti unaoharibu mazingira.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kwa niaba ya Watanzania wanaosikiliza, zaidi ya wananchi 600 wameshaanza kutumia gesi na wiki iliyopita nimeunganisha gesi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa wafanyakazi 110 na cafeteria nne zimeanza kutumia gesi. Huu ni mkakati mzuri sana wa kupambana na mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niongeze tu, awamu ya pili tunakwenda katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa kuanza kusafirisha mitungi iliyoshindiliwa na gesi na kujenga mabomba katika mikoa hiyo ili nako kuanza kusambaza katika vijiji vyote ikiwa ni harakati ya kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali zuri sana la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos. Mheshimiwa Tauhida tafadhali.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, bado swali la kwanza la nyongeza halijapatiwa majibu, limejiibiwa swali la pili.

**SPIKA:** Okay, basi kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu ya muda tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la kwanza la Mheshimiwa Amina Mollel. Kwanza naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Amina Mollel ambaye ni Balozi wetu wa Utalii kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya. Mheshimiwa Amina Mollel alipata hati ya kutambuliwa kama Balozi wa Utalii wakati wa Maadhimisho ya Miaka 60 ya Ngorongoro na Serengeti na anafanya kazi nzuri sana yeye pamoja na wenzake. Nampongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amina Mollel ametaka kujua, kwa nini Serikali inaendelea kuruhusu usafirishaji wa magogo nje ya nchi wakati usafirishaji huu ni chanzo kikubwa sana cha uharibifu wa mazingira? Ni kweli kwamba hapo awali Serikali ilikuwa ikiruhusu usafirishaji wa magogo ya miti migumu nje ya nchi lakini kwa takribani miaka mitatu sasa, Wizara itzuia usafirishaji wa magogo ambayo hayajaongezewa thamani kwenda nje ya nchi. Ni nia ya Wizara kuona kwamba mauzo yoyote ya mazao ya misitu nje ya nchi yanakuwa ni mauzo ya mazao yaliyoongezewa thamani. Kwa hiyo, jitihada hizo katika Wizara zinaendelea na sasa hivi tumefunga uuzaji wa magogo hayo na tutakapofungua tutatoa masharti na maelekezo ya namna ya kufanya biashara hiyo. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa nilishakutaja uliza swali lako, Mheshimiwa Tauhida.

Na. 90

### Kufunga Kamera Ndani ya Vituo vya Polisi Nchini

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO (K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS)** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufunga Kamera ndani ya Vituo vya Polisi sasa ili kupunguza malalamiko kwa baadhi ya wananchi wanapohudumiwa kwa kumwezesha Mkuu wa Kituo kufuatilia mwenendo wa shughuli za Kituo akiwa Ofisini au kwa kutunza kumbukumbu za matukio yanayotokea kwenye vituo hivyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la matumizi ya CCTV Camera katika vituo vyetu ni la umuhimu mkubwa katika kuhakikisha huduma ya Polisi kwa wananchi zinatolewa kwa weledi na kwa kuzingatia maadili ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina nia ya kufanya maboresho yakiwemo matumizi ya TEHAMA kwa kufunga kamera katika vituo vyake ili kuwapa nafasi Viongozi wa Kamandi kufuatilia matukio mbalimbali yanayotokea vituoni ikiwemo namna Askari wa chini wanavyohudumia wananchi.

Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti unaochangiwa na wingi wa changamoto, Jeshi la Polisi kwa sasa halina bajeti hiyo. Hata hivyo, limeruhusu wadau katika maeneo mbalimbali kuwezesha ufungaji wa kamera za ufuatiliaji kwa nia ya kuboresha na kufuatilia utendaji wa Askari.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikisha wadau katika maeneo yao kuchangia upatikanaji na ufungaji wa CCTV Camera vituoni ili kupunguza malalamiko ya huduma isiyo na weledi ya Askari kwa wananchi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Mawaziri mkiwa na majibu mafupi kama ya Mambo ya Ndani tutajikuta tunatumia muda wetu vizuri. Mnaona tumebakiza dakika 10 lakini bado tuna maswali kibao ndani.

Mheshimiwa Chikambo, swali la nyongeza tafadhali kwa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri; lakini kama ilivyoelezwa kwenye swali la msingi kwamba kumekuwa na malalamiko mengi katika Vituo vyetu vya Polisi pale wananchi wetu wanapokwenda kuhudumiwa katika maeneo yale:

Sasa je, ni mkakati gani wa Serikali katika kuhakikisha siku zijazo kunafungwa CCTV Camera katika hayo maeneo ili kuleta ushahidi katika yale matukio wanayofanyiwa wananchi pale? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba Serikali ina dhamira ya dhati katika kuhakikisha Jeshi la Polisi linafanya vizuri, lakini kama litaifanya vizuri bila kutunza kumbukumbu haitasaidia. Ni lini sasa mkakati wa Serikali katika kuhakikisha matukio yote yanakuwa katika kumbukumbu ili linapohitajika jambo lolote kwa mtuhumiwa yeyote linapatikana kwa urahisi? Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali, Mheshimiwa Eng. Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kwa maswali yake mazuri. Nimhakikishie kwamba kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, ni kwamba dhamira hiyo Serikali kupitia Jeshi la Polisi ya kufanya maboresho katika mfumo mzima wa TEHAMA ikiwemo maeneo mawili ambayo ameyazungumza ya mfumo ya CCTV na kumbukumbu kwa kutumia teknolojia ya kisasa, dhamira hiyo ipo na pale ambapo bajeti itaruhusu, basi sisi tutakamilisha huo mpango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Nanyumbu, uliza swali lako kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na.91

**Hitaji la Kituo Cha Polisi Cha Wilaya – Nanyumbu**

**MHE. WILLIAM D. NKURUA** aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nanyumbu kinatumia majengo ya nyumba za kuishi Askari Polisi:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Nanyumbu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Dua Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu ni miongoni mwa wilaya mpya ambayo ilianzishwa mwaka 2007 hivyo baada ya mabadiliko haya ililazimu jengo ambalo lilikuwa likitumika kama Kituo kidogo cha Polisi kata kuanza kutumika kama Kituo cha Polisi Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatambua changamoto za ukosefu wa vituo vya polisi na ofisi katika wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni ikiwemo Wilaya ya Nanyumbu. Jitihada zinaendelea kufanyika za ujenzi wa vituo vya polisi na ofisi za wakuu wa polisi wa wilaya hizo kadiri fedha kutoka kwenye bajeti ya maendeleo na vyanzo vingine vinavyopatikana.

**SPIKA:**Mheshimwia William Nkurua.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nitoe shukrani zangu kwa Serikali kwa sababu Wilaya yetu ya Nanyumbu pia tulikuwa na matatizo ya usafiri kwa Jeshi la Polisi lakini siku za hivi karibuni Serikali imetupatia na sasa polisi wana uwezo wa kufanya kazi kiurahisi. Hata hivyo, pamoja na shukrani hizo, nataka niongeze swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekiri kwamba Nanyumbu ni miongoni mwa wilaya mpya na hatuna jengo lenye hadhi ya kuwa na hadhi ya Kituo Kikuu cha Polisi cha Wilaya. Sasa kwa kuwa Serikali inajua hilo.

Je, nitarajie sasa kwenye bajeti ijayo kuona haya maandalizi ambayo Serikali imesema ipo katika maandalizi ya ujenzi wa kituo hicho; je, kwenye bajeti hii ijayo nitarajie kuona hiyo bajeti inasomwa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nanyumbu, Mheshimiwa William Dua Nkurua, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa William Dua, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba kama ambavyo alivyokuja kulizungumzia suala la mapungufu ya usafiri na tukalifanyia kazi, basi na suala la kuhakikisha kwamba



tunafanya kila linalowezezana ili kuimarisha kituo cha polisi katika Wilaya ya Nanyumbu nacho vilevile tutachukulia kwa uzito kama ambavyo tumechukulia uzito wa suala la changamoto ya gari katika wilaya yake.

**SPIKA:** Wizara ya Madini, swali linaulizwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

Na. 92

### **Aina ya Madini Tanzania**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, kwa sasa Tanzania ina aina ngapi za madini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Madini Mwenyewe, Mheshimiwa Doto Biteko tafadhali.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina aina mbalimbali za madini ambayo kijiosayansi yamegawanyika katika makundi matano ambayo ni; madini ya metali kama vile dhahabu, madini ya fedha, chuma, shaba, risasi, *aluminum*, *nickel*, *niobium*, bati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, yako pia aina nyingine ya madini, ambayo ni madini ya vito (*gemstones*) ambayo ni pamoja na madini ya Tanzanite, almasi, rubi pamoja na mengineyo

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni la madini ya viwandani, ambayo yanaintwa *industrial minerals* kama vile *kaolin*, mawe ya chokaa, jasi, *phosphate* pamoja na chumvi na na mchanga wa ufukweni.

Mheshimiwa Spika, madini ya ujenzi ni kundi lingine la madini ambayo ni madini ya nakshi kama vile mawe, kokoto, udongo wa mfinyanzi, mchanga na mawe ya nakshi. Aidha, yapo pia madini ya nishati kama vile makaa ya mawe, gesi na *uranium*.

Mheshimiwa Spika, madini haya ni muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda na kuongeza mchango wa uchumi kwa madini katika Pato la Taifa. Madini haya ni muhimu katika maendeleo ya wananchi kwa kuwa yanatumika katika shughuli mbalimbali za ujenzi, viwanda, mapambo na kuleta fedha za kigeni nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, anakiri kabisa kwamba madini haya ni muhimu katika kujenga uchumi wa taifa. Mheshimiwa Waziri, ningependa kukuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; tumeshuhudia bei ya tanzanite ikiendelea kushuka kila siku. Ningependa kujua mkakati wa Serikali; mna mkakati gani wa ziada wa kuendelea kulinda thamani ya tanzanite?

Swali la pili; katika aina ya tano ya madini umezungumzia madini ya nishati ambayo ni makaa ya mawe pamoja na gesi. Mkoa wetu wa Rukwa tuna aina ya madini ambayo ni *helium*, tangu imegundulika ni muda mrefu sasa. Kama ulivyosema dhana ni kujenga uchumi, ningependa kujua na Wanarukwa wafahamu; ni lini madini haya yataanza kuchimbwa ili yawasaidia Wanarukwa na uchumi wa taifa kwa ujumla? (Makofi)

**SPIKA:** Una maana ya *helium gas*. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Madini.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni lile analoulizia madini ya gesi ya *helium* yataanza kuchimbwa lini. Naomba nimhakikishie kwamba Serikali tulishatoa leseni ya kuchimba madini ya *helium* katika Ziwa Rukwa. Tatizo tulilionalo pale ni kwamba katika eneo hilo ambalo tumetoa mashapo ya kuchimba *helium* ipo pia leseni ya kampuni nyingine ya *Heritage* ambayo inachimba madini ya gesi ambayo ipo inasimamiwa na Sheria ya Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali tunachofanya ni ku-*harmonize* hawa watu wa *Heritage* pamoja na *helium* ili waweze kukubaliana tuweze kuanza kuchimba. Hata hivyo, tumeshawapa maelekeo watu wa *Helium One* waanze kuchimba kwenye eneo ambalo halina mgogoro na watu wa *Heritage* na mashauriano yanaendelea ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, la pili ni hili alilozungumzia, kuhusu madini ya nishati. Naomba nimhakikishie kwamba Serikali tunaendelea kuwasimamia watu waweze kuchimba haya madini ili yaweze kuongeza uchumi wa nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Igunga, uliza swali lako tafadhali.

Na. 93

### **Madini ya Tanzanite Kutangazwa Kuwa Nyara za Serikali**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Madini ya Tanzanite yanapatikana nchini Tanzania pekee, juhudi za kufanya madini haya kuchimbwa na Watanzania pekee kwa Kanuni za Madini za mwaka 2004 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 hazijaweza kuzaa matunda:-

(a) Je, kwa nini Tanzania isiyatangaze madini ya Tanzanite kuwa ni Nyara za Taifa itayovunwa na Serikali pekee ili kuongeza manufaa ya kiuchumi kwa Taifa letu?

(b) Je, kwa nini Serikali isiende kujifunza nchini Zimbabwe kuona jinsi ilivyofanikiwa kuyafanya madini ya Almasi kuwa Nyara ya Serikali na hivyo kuleta manufaa makubwa sana kwa nchi hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Madini tafadhali, Mheshimiwa Doto Biteko.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatambua upekee na umuhimu wa madini ya Tanzanite.

Kwa muktadha huo, ilipelekea tarehe 20/9/2017 kulihamuru Jeshi la Wananchi wa Tanzania kujenga ukuta wenye urefu wa kilometa 24.5 kuzunguka eneo hilo. Lengo likiwa ni kudhibiti utoroshwaji wa madini ili kupata manufaa stahiki ya kiuchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mirerani ambako Tanzanite inapatikana lilitangazwa kuwa eneo lililodhibitiwa (*Mirerani Controlled Area*) kwa GN 450 ya mwaka 2002. Lengo la hatua hiyo ni pamoja na kuthamini upekee na umuhimu wa madini hayo na kudhibiti upotevu wa mapato yanayotokana wa Madini ya Tanzanite ili kuongeza manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Madini ya Tanzanite yanachimbwa na Watanzania katika Vitalu A, B, C na D-extension. Aidha, kitalu C kimekuwa kikichimbwa kwa ubia kati ya Shirika la STAMICO na Kampuni ya kigeni ya *TanzaniteOne Mining Limited (TML)*. Hata hivyo, tarehe 23 Desemba 2019, STAMICO na TML waliachia eneo hilo na kupewa *surrender certificate* ya leseni yao na sasa eneo hilo limerudishwa kwenye usimamizi wa Serikali. Baada ya kuachiwa kwa eneo hilo, utaratibu maalum unaandaliwa wa namna bora ya kuligawa kwa kutoa leseni za uchimbaji wa kati kwa Watanzania wenye uwezo wa kulichimba na kuongeza mchango katika uchumi wa madini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kuyafanya madini ya Tanzanite kuwa Nyara za Taifa na kwenda kujifunza katika nchi kama Zimbabwe, ushauri huo tunaupokea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dalaly, Mbunge wa Igunga, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwaka 2002, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kanuni ililitangaza eneo lile kuwa eneo maalum lakini pia iliamua kujengwe ukuta na mwisho tanzanite itangazwe kuwa nyara. Naishukuru sana Serikali kwa kutekeleza hasa ujenzi wa ukuta, Serikali inayoongozwa na jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wanafanya vizuri sana kuiendeleza sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, naomba basi niulize swali dogo la nyongeza; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali ushauri wangu, ni lini basi ushauri huu atautekeleza? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko tafadhali.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, mjiolojia mbobezi hapa nchini wa madini; nataka tu nimtoe wasiwasi kwamba jambo hili ndani ya Serikali tumeanza kulijadili kwa muda mrefu na katika hatua mbalimbali tulizowahi kufikia ni pamoja na mashauriano ya kuona namna gani ili tuweze kuyafanya madini haya ya tanzanite kuwa nyara ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kwamba tunalichukua kwa uzito wake, lakini ilikuwa lazima tuanze kwa hatua ya kwanza ya udhibiti, na hatua ya kwanza ya udhibiti ilikuwa kujenga ukuta na kuweka mifumo ya usimamizi wa madini ya tanzanite.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo unakumbuka, katika madini ambayo yalikuwa hayajawahi kusimamiwa vizuri hapa nchini ni madini ya tanzanite yaliyopelekea kiasi cha madini ya tanzanite ambayo tulikuwa tunayaona kwenye mfumo rasmi wa Kiserikali ilikuwa ni asilimia tan tu ya madini yaayochimbwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nafurahi kusema kwamba hatua ya mwanzo ya kuweka mifumo imeshakamilika, hatua ya pili ilikuwa kujenga masoko ili tuwe na uhakika wa mahali pa kuyauza, hatua ya tatu ni kuweka mitambo au viwanda kwa ajili ya kukata madini ili uongezaji wa thamani uweze kufanyika ndani ya ukuta.

Sasa hatua ya mwisho ni hiyo sasa ya kutangaza haya madini kuwa nyara ya Serikali, hili na lenyewe Serikali inalitafakari, baada ya muda wakati wa mashauriano Mheshimiwa Dkt. Kafumu na yeye tutazingatia kuchukua ushauri wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, uliza swali lako. Bado tuko Wizara ya Madini.

Na. 94

### **Kuweka Utaratibu wa Uchimbaji Madini – Sakale Muheza**

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB** aliuliza:-

Katika Kata ya Mbomole maeneo ya Sakale Wilayani Muheza kuna madini ya dhahabu ambayo wananchi wamekuwa wakichimba bila vibali na hivyo kukamatwa kwa kuharibu chanzo cha maji cha Mto Zigi:-

(a) Je, ni lini Serikali itatuma wataalam ili kuweza kujua eneo hilo lina madini gani?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu mzuri ambao utahakikisha kuwa wachimbaji hao wanachimba eneo ambalo hawatasumbuliwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Madini; Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 02/10/2018, Timu ya Wataalamu wa Madini, Mazingira na Maji kutoka Ofisi ya Tume ya Madini Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC) walitembelea na kukagua eneo la Sakale ili kuangalia athari za uchimbaji uliokuwa unafanywa na wachimbaji wadogo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ukaguzi wa timu hiyo, timu ya wataalam ilibaini uharibifu mkubwa wa mazingira uliofanywa katika vyanzo vya maji na Msitu wa Amani na hivyo shughuli za uchimbaji madini zilisitishwa katika eneo hilo ili kunusuru mazingira, vyanzo vya Maji na Msitu wa Amani katika Kata ya Mbomole.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali za awali zilizofanywa na Taasisi ya Jiolojia Tanzania (GST) ilibaini uwepo wa madini ya dhahabu katika Vijiji vya Mindu, Tengenji, Segoma na Mbambara Muheza na Korogwe.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wachimbaji wadogo wa Kata ya Mbomole eneo la Sakale kuangalia maeneo mengine nje ya Bonde la Mto Zigi ili kufanya shughuli za uchimbaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu alifika eneo la Sakale na akazungumza na wananchi wa Sakale, na pili haikuchukua muda mrefu akawatuma hao wataalam mbalimbali ambao walikwenda wakaangalia hiyo sehemu.

Mheshimiwa Spika, tulishakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba sehemu hiyo hatutaingilia eneo la Bonde la Mto Zigi ili kuepuka chanzo cha maji, na tulikubaliana kwamba tutafute wawekezaji wakubwa ambao wanaweza kuchimba eneo lile.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni, taarifa nzuri ni wawekezaji wameanza kupatikana lakini kuna tatizo la wawekezaji kuruhusiwa kuanza kuchukua *sample* pale na kuweza kujua kuna madini ya kiasi gani. Je, Wizara iko tayari kurahisisha utaratibu huo ili wawekezaji wale waweze kuangalia kuna madini ya kiasi gani pale Sakale?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni la ujumla tu la kutaka kujua, kwamba mpaka sasa hivi Wizara ina utaalum gani ambao unaweza kujua mgodi fulani kuna madini ya kiasi gani pale, kama ni dhahabu au almasi; je, utaalum huo tunao au bado hatuna?

Mheshimiwa Spika, ni hayo tu, ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Doto Biteko tafadhali.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa moyo wa dharti kabisa ninaomba nikiri kwamba Mheshimiwa Balozi Adadi kwa watu wa Muheza na kwenye hilo eneo alilolitaja la uchimbaji, yeye amekuwa *champion* mkubwa wa kuhakikisha kwamba uchimbaji unaanza kwenye kazi hiyo kwa sababu wananchi wa pale kwa kweli ukienda wanategemea sana hilo eneo ili waweze kuchimba na kujipatia mapato na kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyokuwepo ni kwamba eneo hilo haliwezi kuchimbwa kwa uchimbaji mdogo kwa maana ya matumizi ya *mercury* ambayo yanaweza kingie kwenye Mto Zigi na kuathiri chanzo cha maji ambacho kwa kweli katika Bwawa la Mbayani ambalo linapeleka maji kule Tanga Mjini, Korogwe pamoja na Muheza, ukiruhusu hiyo watu wote wale maji yale yataweza kuchafuliwa na mazingira. Uchimbaji ambao unaweza kuruhusiwa pale ni ule tu uchimbaji wa kati ambao unakuwa na EIA ambayo NEMC wataitoa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna wataalam ama kuna watu wanaotaka kuchukua sampuli, hakuna mahali popote wanazuia, kwa mujibu wa sheria wanaweza kuchukua sampuli na kupima na kuweza kujua kuna madini kiasi gani. Kwanza ni jambo la faida kwetu kwa

sababu wanafanya utafiti kwa niaba ya Serikali na hivyo wanaweza kuchukua wakati wowote. Kama kuna mtu yeyote anawazuia kuchukua sampuli naomba nitoe wito wafuate taratibu zote zilizowekwa wachukue sampuli waweze kwenda kupima na hatimaye wapate taarifa wanazohitaji.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni je, Wizara tuna utaalum wa kujua kuna kiasi gani cha madini mahali fulani? Naomba nijibu tu kwa kifupi kwamba Serikali inayo huo uwezo kupitia Shirika letu la Serikali la GST, tuna uwezo wa kutambua kuna kiasi gani cha mashapo na kuna kiasi gani cha madini kinachoweza kuchimbwa. Kama kuna eneo ambalo analo, kwa kutumia Shirika letu la STAMICO, nimuombe Mheshimiwa Mbunge awasiliane na STAMICO waweze kujua ni kitu gani kinaweza kufanyika.

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Seneta Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa.

Na. 95

### **Kukamilisha Miradi ya Umeme Vijijini – Wilayani Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya umeme Vijijini katika vijiji ambavyo bado havijafikiwa Wilayani Chunya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi kabambe wa kusambaza umeme vijijini ambapo kwa sasa unatekelezwa kupitia Awamu ya III Mzunguko wa Kwanza unaoendelea utakaokamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ina vijiji 43, kati ya vijiji hivyo, vijiji 37 tayari vimeshapatiwa umeme vikiwemo Vijiji vya Chokaa, Ifumbo, Isewe, Kibaoni, Lola, Kiwanja, Mlimanjiwa pamoja na Lupatingatinga. Utekelezaji wa kazi hii umekamilishwa na Mkandarasi STEG International Services na uligharimu shilingi bilioni 4.2.

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyobaki katika Wilaya ya Chunya vitapelekewa umeme kupitia Mradi wa REA Mzunguko wa Pili pamoja na miradi mingine ya *densification* kwa maana ya ujazilizi, itakayoanza mwezi Februari, mwaka huu 2020 na kukamilika ifikapo mwezi Juni, mwaka 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Mwambalasa uliza swali.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na majibu ya Serikali ambayo yanaonesha kwamba vijiji vingi vimepata umeme kwenye Wilaya ya Chunya, wilaya kongwe, na vijiji vilivyobaki vitapata umeme kwenye REA III inayoanza mwezi huu mpaka mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, nataka niweke tu rekodi sahihi kwamba katika Kata ya Sangambi, Kijiji cha Shoga – lakini sio shoga ya watu wa ughaibuni hapana, shoga ya Kitanzania ya urafiki – Kijiji cha Shoga; kwenye Kata ya Upendo Kijiji cha Nkwangu; Kata ya Nkung'ungu Kijiji cha Nkung'ungu, Majengo na Magunga; Kata ya Lualaje Kijiji cha Lualaje na Mwiji; Kata ya Matwiga Kijiji cha Mazimbo; Kata ya Mafieko Kijiji cha Mafieko na Biti Manyanga; Kata ya Kambikatoto Kijiji cha Kambikatoto na Sipa, je, vitapewa umeme kwenye REA Awamu ya III inayoanza mwezi huu? Ninafurahi sana na majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nina swala dogo tu la nyongeza, katika Vijiji vyote hivi ambayo vilibaki kuna Kijiji cha Itumbi ambapo Serikali inaweka *central of excellence* yaani inaweka shule ya kuwafundisha wachimbaji wadogo na kwenye Kijiji hicho kuna makarasha zaidi ya 100 ya wachimbaji wadogo.

Je, Serikali iaweza ikatumia umuhimu wa pekee kuweza kumpa huyu ukandarasi ana *addition BOQ* ili Kijiji hicho kipate umeme mapema kuliko Vijiji vingine? (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona Wabunge wazoefu Vijiji vyake vyote vyenye matatizo anavyo kwenye *fingertips*, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemami tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kabisa maeneo yote ya Jimbo lake yanaelekea kupata umeme kufikia mwezi Juni mwaka huu na hongera sana Mheshimiwa kwa kazi kubwa uliyofanya kwa niaba ya wana Jimbo.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Itumbi ambapo *central of excellence* kwa wachimbaji wadogo itafanyika, mkakati wa Serikali umeshaanza, kwanza mbali na kupeleka Itumbi Mheshimiwa Mwambalaswa aliwaomba migodi ya wachimbaji takribani minne na hivi sasa mradi wa Matundasi ambao na wachimbaji wadogo wameshapata umeme migodi ya Makongorosi nayo imeshapata umeme na pia migodi ya wachimbaji kwa kuwa *Sunshine* nayo ilishapata umeme. Sasa kazi inayoendelea sasahivi nikupeleka umeme katika Kijiji cha Itumbi ambako kutakuwa na makarasha zaidi ya 128 na tumeshaandaa transfoma sita zenye uwezo wa kilovoti 115 kila mmoja na transfoma moja tutaifunga kwenye Kitongoji cha Matondo karibu kabisa na Itumbi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Kijiji cha Itumbi pamja na wachimbaji wadogo wenye makarasha na pamoja na maosheo watapata umeme tena mkubwa wa wachimbaji kuanzia mwezi Mei mwaka huu, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambalaswa ulishauliza swali la nyongeza, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge mtaona muda wetu kwa kweli haupo upande wetu. Naomba tuishie hapo, wageni waliopo Bungeni siku ya leo ni wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni mtanzania mfupi zaidi duniani aliyeweka rekodi ya dunia kwa kupanda mlima Kilimanjaro ndugu Masoudi Juma, yuko wapi Masoudi hebu mtu wa kamera tembeza huko hatunae ilikuwa vizuri angekuwa mgeni wangu kukaa pale hebu kama yupo Surgent at Arms mwamishieni kwenye *gallery* ya Spika huyo Masoudi Juma na wengine ni Samweli Malugu na Edward Shirima, tutamuomba Masoudi Juma kama yupo ahamie *gallery* ya Spika halafu awe juu juu kule. (*Makofi*)

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni wawili wqa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni viongozi wa Asasi za Kiraia Mazingira na Maendeleo kutoka Mkuranga Mkoa wa Pwani ndugu Ally Ngalema na ndugu Abdallah Kawambwa, karibuni sana, wageni watatu wa Mheshimiwa Daima Mpakate ambao ni viongozi wa Taasisi ya *help for Underserved communities* kutoka Jijini Dar es Salam ndugu William Kenneth na ndugu Salimu Kanyika na ndugu Christina Moude.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa mzee Minjori na ndugu Katibu Mwandu karibuni, wageni 22 wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda viongozi ikiwa ni Madiwani na rafiki zake kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na Kissa Swilla, karibuni wale wageni wa, kumbe ni kundi kubwa wote mmetoka Mbeya ninyi? Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni rafiki zake na wanakamati, Kamati ya arusi ya Mwenyekiti wa Shivyawata Taifa wakiongozwa na Mwenyekiti mwenyewe ndugu Ummu Nderiananga, karibuni sana. Mgeni wa Mheshimiwa Allani Kiula ambaye ni ndugu yake kutoka Mkalama ndugu Mpazi Paul, mgeni wa Mheshimiwa Tunza Malapo ndugu Tony Lawrence , mgeni wa Mheshimiwa Prosper Mbena ndugu Maureen Mbena mtoto wake huyu Maureen, ahsante sana mgeni wqa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambaye ni mwalimu na Mwandishi wa Vitabu vya Ujasiriamali ndugu Charles Ligonja, karibu sana tumekuona. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto Mathew Menick na Said Kiponza, wageni wanne wa Mheshimiwa Kemirembe Lwota ambao ni wakaguzi wa ndani wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Emmanuel Johanes, karibuni sana, wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 88 na walimu tisa kutoka shule ya Msingi Msisi Juu, Wilayani Bahi Mkoani Dodoma wakiongozwa na mwalimu William Mahimbo, watoto wa kutoka Bahi kule karibuni sana, watoto wetu wamependeza kweli watoto. *(Makofi)*

Wanafunzi 54 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara CBE tawi la Dodoma, CBE Dodoma karibuni sana majirani zetu. Wageni 8 kutoka Taasisi ya Sauti ya Jamii Tanzania kutoka Dodoma wakiongozwa na ndugu Deus Lugaila, karibuni sana, bado sijaletewa wanafunzi wa kutoka kule hebu naomba wasaidizi wangu mnapatie shule ile ni shule ni shule gani na wametoka nitawatangaza hapo baadaye kidogo.

Mheshimiwa Shally Raymond anawatangazia wanaibada leo saa saba mchana ibada itakuwepo baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge pale ghorofa ya pili Shally Rymond Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomasi More. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge naomba niwatangazieni tangazo muhimu kwamba Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa katika Bunge letu ametunukiwa Shahada ya Uzamivu ya PHD, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa amefuzu Shahada hiyo ya Uzamivu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tarehe 28 Novemba, 2019, *PHD Doctor of Philosophy* kuanzia sasa tunaendelea kumtambua Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa wadhifa huo, Waheshimiwa Wabunge kwa niaba yenu nampongeza sana Mheshimiwa Dkt, Mary Mwanjelwa na nawasihi Waheshimiwa Wabunge wengine kujiendeleza kielimu kwani elimu haina mwisho. PHD yake ni katika masuala ya utawala bora eneo ambalo ndiyo anafanyia kazi hivi sasa. *(Makofi/Vigelele)*

Katibu!

**NDG.NEEMA MSANGI-KATIBU MEZANI:**



HOJA ZA KAMATI

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA  
USALAMA KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019**

NA

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU SHUGHULI  
ZA KAMATI KWA MWAKA 2019**

**SPIKA:** Mwenyekiti wa Mambo ya Nje, ahsante sana anakuja Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti ambaye ndiyo Kaimu Mwenyekiti, Mwenyekiti endelea na hotuba yako.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Afrika Mashariki, Ulinzi na Usalama...

**SPIKA:** Ongeza sauti Mwenyekiti usikike na hiyo Mic iweke vizuri payuko.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa hii iingie katika Taarifa Rasmi ni ya Bunge (*Hansard*) kama ilivyowasilishwa mezani leo mapema na Mheshimiwa Kapufi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kamati ya Bunge Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zinazovikabili vyombo hivyo na kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha nawapongeza Wakuu wa vyombo hivyo kwa kuendelea kuwa shupavu na makini katika kutekeleza majukumu makubwa waliyonayo na kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi hii ndio kipaumbele namba moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa niaba ya Kamati, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kamati inamtakia utendaji bora kama alivyoendesha Kamati ya Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa katika kipindi chote cha uwenyekiti wake. Aidha, tunampongeza Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Ndugu Christopher Kadio kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Kwa niaba ya Kamati tunawaahidi kufanya nao kazi kwa ushirikiano mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kanuni za Kudumu za Bunge naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na likubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Mwaka ndio ya mwisho katika kipindi hichi cha pili cha mwisho wa uhai wa Kamati ya kipindi kilichobaki cha uhai wa Bunge la 11. Kwa kuzingatia hilo, naomba niwashukuru Wajumbe ishirini na tano (25) wa Kamati hii ambao katika kipindi chote

cha miaka miwili na nusu cha uhai wa Kamati wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii katika kipindi chote cha nusu ya mwisho wa uhai wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020. Aidha, masuala yanayoainishwa kwenye Taarifa hii ni yale ya ambayo Kamati inaona kuwa utekelezaji wake unahitaji juhudi zaidi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, taarifa inayowasilishwa imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zinazotekelezwa (Ukurasa wa 4 mpaka wa 6);

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati (Ukurasa 14 mpaka wa 40);na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati (Ukurasa 41 mpaka 51); na

(iv) Sehemu ya Nne ni majumuisho (Ukurasa wa 52 mpaka 53).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari 2019 na Januari, 2020 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, moja kwanza ni semina, katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilishiriki Semina mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zimewajenga uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala ya Uchambuzi wa Bajeti, Masuala ya Jinsia, Masuala ya UKIMWI na masuala yanayohusu Usalama wa Barabarani.

Mheshimiwa Spika, Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazosisimamia pamoja na Taasisi zake. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili taarifa hizo kwa kina, yapo masuala ambayo yalibainika na kufafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, moja kutembelea na kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu Kamati ya Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Januari 2020, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Jumla ya Miradi Mitano (5) ilikaguliwa katika mikoa ya Morogoro na Dodoma katika kipindi cha Mwezi wa Machi, 2019.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi uliofanywa, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yaliyosaidia au kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mbili, moja *point* mbili, Uchambuzi wa Taarifa wa Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2018 na 2019 na kamadirio ya Mapato ya Matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara iliyosimamia kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ikichambua kwa kina Bajeti ya Wizara zote tatu (3) zinazoisimamia na Kamati hii na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, Kuchambua Mikataba/Itifaki za Kimataifa zinazopendekezwa kuridhiwa na Bunge zilizo chini ya Wizara inazosimamia, katika kipindi kinachotolewa Taarifa ya Kamati ilishughulikia Itifaki ya Kinga ya Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2019 yaani (*Protocol on Privileges and Immunities of the East African Community, 2019*). Kamati ilichambua kwa kina Itifaki hii na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama mbalimbali vya Kibunge, Bunge la Afrika Mashariki, SADC-PF na Bunge la Afrika, kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge, Bunge la Afrika Mashariki, SADC - PF na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7(2) (iii) mpaka ya (iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kularifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Februari mwaka 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za wawakilishi wa Bunge katika Bunge la (SADC – PF).

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, masuala yanayoainishwa na taarifa hii ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake inahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa. Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati yanaonekana katika Ukurasa wa 14 mpaka 40 wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, maoni ya jumala kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kutokana na matokeo ya ziada ya ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa chini ya fungu 38 Ngome na fungu 93 Uhamiaji; Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa miradi hii na kutenga fedha za utekelezaji wake nje ya Bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia ya dhati iliyooneshwa na Serikali katika kutoa fedha za maendeleo ikiwemo utaratibu wa kutoa fedha nje ya Bajeti kama ilivyooneshwa kwenye miradi miwili iliyotajwa hapo awali, bado Kamati ina maoni kuwa kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara hizi hususan Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Maoni Mahsusi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(i) Ugumu wa kupata vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wengi kumepelekea watanzania wengi kuwa wazito katika ushiriki kwenye zoezi la kujiandikisha na wengine kujitokeza katika hatua za mwisho hususan pale wanapohajika kuwa navyo kwa ajili ya mambo ya Kitaifa kama vile kusajili namba za simu, jambo ambalo linachangia zoezi hilo kuwa gumu;

(ii) Msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani umeendelea kuwa changamoto kwa Magereza nchini licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali;

(iii) Kutokutumika kwa utaratibu wa "retention" kwa Majeshi yaliyopo chini ya Wizara hii kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya vyombo hivyo hususan kwa kuzingatia kuwa fedha nyingi za OC hazitolewi inavyostahiki;

(iv) Kucheleweshwa kwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani kunaendelea kusababisha majeruhi na vifo kutokana na kukosekana kwa Sheria ya Usalama Barabarani iliyojitoshesheza katika vyanzo vyote;

(v) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji bado halijapewa umuhimu unaostahili na Serikali ikilinganishwa na majukumu mazito na muhimu ya Jeshi hilo na jinsi linavyoheshimika duniani kote;

(vi) Kuwepo kwa uelewa mdogo wa baadhi ya Wananchi juu ya Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa watu unaoendeshwa na NIDA unachangia wananchi wengi kuwa wazito katika kushiriki kwenye zoezi na wengine kujitokeza katika hatua za mwisho;

(vii) Upo umuhimu kwa Serikali kuangalia upya hadhi za wakimbizi wanaopewa uraia wa Tanzania kulingana na Sheria za Kimataifa ili kuondoa changamoto za kiusalama zinazoendelea kujitokeza kutokana na wakimbizi hao kupewa uraia wa kudumu; (*Makofi*)

(viii) Upo umuhimu wa Serikali kuendelea kulipa uzito unaostahili suala la kuwasambaza wakimbizi waliopewa uraia nchini katika maeneo mbalimbali ili kuepusha changamoto za kiusalama zinazoweza kujitokeza katika maeneo wanayoishi; na

(ix) Upo umuhimu wa Serikali kutunga Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi ili kuratibu masuala ya ulinzi na usalama yanayofanywa na Makampuni binafsi.

(d) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(i) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (*National Defence Policy*) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;

(ii) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (*beacons*) kwa baadhi ya maeneo na kuwepo kwa vipenyo visivyo rasmi kunachangia uvamizi wa raia wa kigeni katika baadhi ya maeneo ya mipaka jambo ambalo linaweza kuathiri ulinzi na usalama wa nchi;

(iii) Kuendelea kuwepo kwa madeni ya muda mrefu mathalan madeni ya matreta yaliyotolewa kwa mkopo na SUMA JKT kwa taasisi za Serikali na watu binafsi yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa shirika hilo; na

(iv) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kwa Shirika la Nyumbu kumeendelea kuathiri shughuli za kitafiti na za kibunifu za Shirika hilo.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(c) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

(i) Kutokamilika kwa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Nchi kunasababisha sera iliyopo kuendelea kutumika ilhali haiendani na kasi ya maendeleo ya kiuchumi iliyopo sasa duniani;

(ii) Kutokuwepo kwa Sera ya *Diaspora* kunachangia Serikali kuendelea kukosa mapato na faida nyingine nyingi ambazo zingepatikana kutokana na kuwepo kwa sera hiyo; na

(iii) Kuwepo wa watumishi wachache katika Balozi za Tanzania nje ya nchi kunaathiri utendaji wa Balozi hizo hususan katika kutekeleza kwa ufanisi Diplomasia ya uchumi.

(d) Vyama vya Kibunge:-

Mheshimiwa Spika, changamoto ya upatikanaji wa fedha za safari kwa wakati kunasababisha mtiririko usio mzuri wa ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kibunge ya Kikanda jambo ambalo halileti taswira nzuri ya Bunge letu katika Mikutano hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida.

KWA KUWA, majeshi yaliyo chini ya Wizara hii pamoja na Idara ya Uhamiaji yamekuwa yakitengewa fedha pungufu za undeshaji (OC) kulingana na mahitaji halisi ya Majeshi hayo;

NA KWA KUWA, upungufu huo unaathiri shughuli za msingi za Majeshi hayo ikiwemo kuwa na uhaba wa vituo vya zimamoto na uokoaji kutokufanyika kikamilifu kwa misako na doria ya wahamiaji haramu kushindwa kufuatilia upelelezi wa kesi na kufanya *operation* za mara kwa mara; (*Makofi*)

KWA HIYO BASI, Serikali ihakikishe inatenga Bajeti ya kutosha na fedha zote kutolewa zinazoidhinishwa na Bunge ili kuviwezesha vyombo hivyo kujiendesha ipasavyo. Aidha, kuzingatia umuhimu wa Vyombo hivyo pale ambapo ikibidi, Serikali iruhusu vibaki na sehemu ya mapato yao (*retention*) ili kukabiliana na changamoto za kibajeti zilizopo. (*Makofi*)

(b) Ujenzi wa nyumba za maafisa na Askari.

KWA KUWA, majeshi yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yanakabiliwa na upungufu mkubwa wa nyumba za Askari na watumishi na kati ya nyumba chache zilizopo nyingi zao ni chakavu sana;

NA KWA KUWA, upungufu huo wa nyumba unasababisha baadhi ya Askari kuishi uraiani katika nyumba za kupanga jambo ambalo ni hatari kiusalama na vilevile linaathiri maadili ya kikazi ya Askari hao;

KWA HIYO BASI, Serikali ione umuhimu wa kutumia ujuzi na nguvu kazi iliyopo Jeshi la Magereza katika ujenzi wa nyumba za ubunifu ikiwa ni pamoja na kuwa na kampeni maalum ya kufyatua matofali kupitia Magereza kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za majeshi yaliyopo chini ya Wizara hii.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

(c) Hali ya msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Gerezani.

KWA KUWA, uwezo wa magereza yaliyopo nchini ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kwa siku na hadi sasa yanahifadhi wahalifu kati ya 36,000 mpaka 39,000 kwa siku;

NA KWA KUWA, msongamano huo wa wahalifu unachangiwa na idadi kubwa ya mahabusu ambao wanasubiri maamuzi ya kesi zao mbalimbali;

NA KWA KUWA, Kamati inatambua kuwa jukumu la kupunguza msongamano Magerezani linajumuisha Taasisi mbalimbali.

KWA HIYO BASI, Serikali:-

(i) lendelee kutenga fedha kwa ajili ya kujenga na kukarabati Magereza katika Mikoa na Wilaya ili kuhimili uhifadhi wa wafungwa na mahabusu;

(ii) Isimamie Kamati za Kusukuma kesi kukutana mara kwa mara ili kumaliza changamoto za uendeshwaji wa kesi Mahakamani;

(iii) Ihakikishe upelelezi wa kesi hususan zile ambazo siyo za jinai hauchukui muda mrefu;

(iv) lendelee kutumia utaratibu wa Mahakama inayotembea 'mobile courts' ili kushughulikia kesi nyingi zaidi; na

(v) landae mpango mkakati wa kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

(d) Usalama barabarani.

KWA KUWA, makosa ya usalama barabarani yanandelea kusababisha ajali ambazo wakati mwingi husababisha mauti hata ulemavu wa kudumu;

NA KWA KUWA, Serikali imeonesha nia ya dhafi ya kupunguza makosa ya usalama barabarani ambapo makosa hayo yamepungua kwa asilimia 27.5% ikilinganishwa na mwaka 2018;

NA KWA KUWA, bado kuna umuhimu wa kupunguza kabisa ajali zinazosababishwa na makosa ya barabarani;

KWA HIYO BASI, Jeshi la Polisi lione umuhimu wa kuharakisha mchakato wa kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani ili kupunguza kabisa ajali zinazotokana na makosa ya usalama barabarani. Aidha, elimu ya Umma iendelee kutolewa kwa madereva wa vyombo vya moto wakiwemo madereva wa pikipiki na Umma kwa ujumla kuhusu usalama barabarani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

(a) Utekelezaji wa majukumu ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

KWA KUWA, baadhi ya Balozi za Tanzania nje ya nchi zina upungufu wa watumishi hususan wenye taaluma ya masuala ya uchumi;

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NA KWA KUWA, upungufu huo unaathiri shughuli za Balozi katika ukelezaji diplomasia ya uchumi hususan katika kutangaza vivutio vya utalii na kutafuta fursa za ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi;

KWA HIYO BASI, Serikali ipeleke watumishi zaidi ambao wana taaluma ya masuala ya uchumi ili kuziwezesha Balozi zetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

(b) Ukamilishaji wa Sera ya Mambo ya Nje.

KWA KUWA, Serikali imechukua muda mrefu wa kukamilisha Sera Mpya ya Mambo ya Nje;

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa sera hiyo kunaifanya Serikali kufahamika kuwa bado inatumia sera ya mwaka 2001;

HIVYO BASI, Serikali ikamilishe kwa haraka iwezekanavyo Sera Mpya ya Mambo ya Nje na kuanza kutumika rasmi mara moja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati hususan utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola. Pia nawashukuru Naibu Waziri wa mambo ya Ndani Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Balozi Profesa Palamagamba John Aidan Kabudi na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro pamoja na watendaji wote wa Wizara hizi kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge pamoja na Wakurugenzi Wasaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Ndugu Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya, wasaidizi Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyokuwemo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI  
NA USALAMA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2019 - JANUARI, 2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za  
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

**SEHEMU YA KWANZA**

**MAELEZO YA JUMLA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zinazovikabili vyombo hivyo na kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha nawapongeza Wakuu wa vyombo hivyo kwa kuendelea kuwa shupavu na makini katika kutekeleza majukumu makubwa waliyonayo ya kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi ndio kipaumbele namba moja.

**Mheshimiwa Spika**, aidha kwa niaba ya Kamati, napenda kumpongeza sana Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb. aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kamati inamtakia utendaji bora kama alivyoendesha Kamati na Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa katika kipindi chote cha uwenyekiti wake. Aidha, tunampongeza Mhe. George Simbachawene, MB kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, pamoja na Ndg. Christopher Kadio kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Kwa niaba ya Kamati tunawaahidi kufanya nao kazi kwa ushirikiano.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 [Kanuni za Kudumu za Bunge] naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Mwaka ndio ya mwisho katika kipindi cha pili na cha mwisho cha uhai wa Kamati kwa kipindi kilichobaki cha uhai wa Bunge la 11. Kwa kuzingatia hilo, naomba niwashukuru Wajumbe ishirini na tano (25) wa Kamati ambao katika kipindi chote cha miaka miwili na nusu cha uhai wa Kamati wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni: -

- |   |              |
|---|--------------|
| 1. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb-        | M/Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb-         | Mjumbe       |
| 3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb-        | “            |
| 4. Mhe. Prosper J. Mbeni, Mb-           | “            |
| 5. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb- | “            |
| 6. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb-    | “            |
| 7. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb-          | “            |



8.Mhe. Joseph Mkundi, Mb-	“
9.Mhe. Joram Hongoli, Mb-	“
10.Mhe. Cosato David Chumi, Mb-	“
11.Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb-	“
12.Mhe. Bonnah Kamoli, Mb-	“
13.Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb-	“
14.Mhe. DKt. Suleiman Ally Yussuf, Mb-	“
15.Mhe. Augostino Mayanda Masele, Mb-	“
16.Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb-	“
17.Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb-	“
18.Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb-	“
19.Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb-	“
20.Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb-	“
21.Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb-	“
22.Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb-	“
23.Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb-	“
24.Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb-	“
25.Mhe. Charles Tizeba, Mb-	“

Aidha, namshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb- aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii katika kipindi chote cha nusu ya mwisho ya uhai wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020. Aidha, masuala yanayoainishwa kwenye Taarifa hii ni yale tu ambayo Kamati inaona kuwa utekelezaji wake unahitaji juhudi zaidi kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa inayowasilishwa imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na

(iv) Sehemu ya Nne ni hitimisho.

#### 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 ikisomwa pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu (3) ambazo ni: -

i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

ii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na

iii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii ni: -

i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

- ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;
- iii. Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara zilizoainishwa hapo juu, Kamati ina majukumu ya nyongeza matano (5) yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni: -

- i. Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
- ii. Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;
- iii. Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;
- iv. Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na
- v. Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

## 1.2 Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3) (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2018/2019 na 2019/2020. Njia zilizotumika ni:-

- i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;
- ii. Vikao na wawakilishi wa Vyama mbalimbali vya Kibunge kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Vyama hivyo;
- iii. Kuwataka Mawaziri kutoa maelezo na ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi;
- iv. Ziara za kukagua utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;
- v. Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020;
- vi. Kutoa taarifa maalumu ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana juu ya masuala ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekebisha kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (17);
- vii. Kuhoji namna ambavyo Wizara zimezingatia masuala ya Jinsia wakati zinapotekeleza majukumu yake; na

viii. Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Serikali na Asasi za Kiraia.

### 1.3 Shughuli zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari 2019 - Januari, 2020 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo: -

#### 1.3.1 Semina

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilishiriki Semina mbali mbali zikiwemo zifuatazo:-

i) Semina kuhusu Maandalizi ya Bajeti ya Serikali tarehe 23 na 24 Machi, 2019

ii) Semina kuhusu Dhana kuu ya Jinsia na Uchambuzi wa mfumo wa dhana ya Kijinsia katika fikra na kinadharia na vitendo, na uhusishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge, iliyoratibiwa na Bunge kupitia mradi wa LSP II, tarehe 18 na 19 Mei, 2019

iii) Semina kuhusu Masuala ya UKIMWI tarehe 21 Juni, 2019

iv) Semina kuhusu masuala ya usalama barabarani iliyoratibiwa na *Tanzania Women Lawyers Association* (TAWLA)

**Mheshimiwa Spika**, naomba kukiri kuwa Semina hizo kwa kiasi kikubwa zimewajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala yanayohusu Uchambuzi wa Bajeti, Masuala ya Jinsia, Masuala ya UKIMWI na masuala yanayohusu Usalama Barabarani.

#### 1.3.2 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazosisimamia pamoja na Taasisi zake. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kujadili taarifa hizo kwa kina, yapo masuala ambayo yalibainika na yanafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

#### 1.3.3 Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Jumla ya Miradi Mitano (5) ilikaguliwa katika mikoa ya Morogoro na Dodoma katika kipindi cha Mwezi Machi, 2019. Miradi hiyo pamoja na vifungu vyake ni ifuatayo:-

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

<b>SN</b>	<b>Fungu</b>	<b>Simbo ya Mradi</b>	<b>Jina la Mradi</b>	<b>Mahali Mradi ulipo</b>	<b>Thamani ya mradi (Tsh)</b>
1.	28	6107	Technical Equipment – Digital Mobile Radio	Dodoma mjini	1,000,000.00
2.		6303	Ukarabati wa Chuo cha Polisi (Kidatu)	Kidatu, Morogoro	1,027,000,000.00
3.	29	4002	Mradi wa Kiwanda cha Ufundi seramala wa Gereza la Msalato	Msalato, Dodoma	2,000,000,000.00
4.	38	6327	Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa	Kikombo, Dodoma	5,740,750,000.00
5.	93	6301	Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji	Dodoma mjini	10,000,000,000.00

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi uliofanywa, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yaliyosaidia au kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

**1.3.4 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua kwa kina Bajeti za Wizara zote tatu (3) zinazosimamiwa na Kamati hii na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.

**1.3.5 Kuchambua Mikataba/Itifaki za Kimataifa zinazopendekezwa kuridhiwa na Bunge zilizo chini ya Wizara inazozisimamia**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilishughulikia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2019 (*Protocol on Privileges and Immunities of the East African Community, 2019*). Kamati ilichambua kwa kina Itifaki hii na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.

1.3.6 **Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama mbalimbali vya Kibunge, Bunge la Afrika Mashariki, SADC - PF na Bunge la Afrika**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoielezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge, Bunge la Afrika Mashariki, SADC - PF na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (iii & iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Februari 2019-Januari, 2020, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Bunge la SADC (SADC – PF).

**SEHEMU YA PILI**

**UCHAMBUZI NA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**2.0 MAELEZO YA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari 2019 hadi Januari, 2020, sasa naomba kutoa taarifa ya matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala mbalimbali yaliyobainika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyoielezwa hapo awali, masuala yanayoainishwa na taarifa hii ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa.

**2.1 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati**

**2.1.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Usimamizi wake**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo mitano (5) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mikoa ya Dodoma na Morogoro.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa kuhusu utekelezaji wake kabla ya ziara na baadae ilitembelea maeneo ya miradi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nianze taarifa hiyo kwa kueleza kuwa, katika mafungu matatu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo miradi hiyo ipo chini yake, yaani Fungu 28- Jeshi la Polisi, Fungu 29- Jeshi la Magereza, na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji, hakukuwa na fedha zozote za Maendeleo zilizotolewa kutoka katika Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, aidha kwa upande wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilielezwa kuwa Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi utatekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Serikali ya Watu wa China itashughulikia ujenzi wa majengo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itagharamia ujenzi wa miondombinu wezeshi ya utekelezaji wa Mradi huo. Taarifa zaidi ilieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Mradi huo ulipelekewa Shilingi Bilioni 5 nje ya Bajeti kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

### 2.1.2 Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje hususan Diplomasia ya Kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi kinachotolewa taarifa, Wizara iliendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje kwa kuratibu Mikataba na Makubaliano mbalimbali, kuratibu ziara za viongozi wa Kitaifa nje ya nchi, kutangaza vivutio vya utalii nje ya nchi, kuvutia uwekezaji na kukuza biashara nchini, utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, kukuza lugha ya Kiswahili, kutafuta fursa za mafunzo nje ya nchi na kuratibu makongamano, mikutani na maonesho ya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ambapo kwa upande wa kutangaza utalii imeendelea kutangaza vivutio husika kupitia majukwaa mbalimbali ya kimataifa. Juhudi hizi zimechangia idadi ya watalii waliotembelea Tanzania kuongezeka kutoka 1,327,143 mwaka 2017 hadi 1,505,702 mwaka 2018. Aidha, kamati inaipongeza juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukifanya Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha za kazi katika jumuiya mbalimbali za kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika na Umoja wa Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, pamoja na juhudi zinazoonekana za Wizara katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kutumia Sera ya Mambo ya Nje iliyopo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa upo umuhimu wa kuwa na Sera Mpya ya Mambo ya Nje kama ambavyo imekuwa ikishauri tangu Kamati hii ilipoundwa Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyoorodheshwa, Kamati imebaini zipo changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa Sera ya Nje hususan Diplomasia ya uchumi. Changamoto hizo ni pamoja na Upungufu wa watumishi Balozini ambapo hadi kufikia Mwezi Agosti, 2019 watumishi waliokuwepo walikuwa 102 badala ya Watumishi 200 kama Ikama mpya inavyoonesha hivyo kuwa na upungufu wa Watumishi 98. Aidha, Wizara imeendelea kukabiliwa na Upungufu na uchakavu wa majengo Balozini Jambo ambalo linasababisha baadhi ya Balozini kuendelea kupanga na kusababisha mzigo mkubwa wa pango ya kodi kwa Serikali.

### 2.1.3 Utekelezaji wa Miradi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Septemba 2019, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mikakati ya utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kamati ilipokea taarifa kuwa, katika kutatua changamoto ya uchakavu, ujenzi na ununuzi wa majengo Balozini, Wizara imejiwekea Mpango wa miaka kumi na tano wa awamu ya pili ulioanza mwaka wa fedha wa 2017/2018 na kutarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2031/2032 baada ya Mpango wa kwanza wa Mwaka 2002/2003 hadi Mwaka 2016/2017 kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilitenga kiasi cha Shilingi Bilion 4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Balozini za Tanzania nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan, Zambia, Canada, Kenya, Chuo cha Diplomasia na Wizarani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwani katika robo ya kwanza ya Mwaka, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 487,905,996.40 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya

fedha hizo, shilingi 150,000,000 ni za ukarabati wa makazi ya Balozzi wa Tanzania nchini Canada na shilingi 337,905,996.40 ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na Mkakati wake wa miaka 15 wa kuwezesha ukarabati, ujenzi na ununuzi wa nyumba za Balozini. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iweke juhudi madhubuti katika kutekeleza mkakati huo kwa kuendelea kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya Mkakati huo. Hii itaokoa fedha nyingi za walipa kodi ambazo zinatumiwa kwa ajili ya kodi ya pango ya majengo ya ubalozini, lakini vilevile itaongezea mapato ya Serikali kwa kukodisha majengo yake kama ilivyo kwa Jengo la ubalozzi wetu nchini Msumbiji.

#### 2.1.4 Utekelezaji wa Shughuli za Diaspora

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu namna ambavyo shughuli za Diaspora zinachangia katika Diplomasia ya Uchumi. Vile vile Kamati ilitaka kujua mipango ya Serikali katika kuhamasisha shughuli za Diaspora ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotaka kujua zaidi kuhusu Mikakati iliyopo katika kuratibu shughuli za diaspora ilielezwa kuwa, pamoja na mambo mengine, Balozzi zetu zimeelekezwa kuhakikisa zinawatambua Watanzania wanaoishi katika maeneo yao ili kuwa na takwimu sahihi na kuweka mazingira wezeshi ya kuchangia maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa Serikali bado haina takwimu sahihi za Diaspora ambapo idadi iliyopo hadi sasa ni ya watu 98, 658 tu. Kamati inaendelea kusisitiza Balozzi zetu nje ya nchi kuhamasisha diaspora kujiandikaisha na kutoa Taarifa zao Ubalozini. Aidha, Kamati ilibaini kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Septemba, 2019 Diaspora walinunua nyumba zenye thamani ya shilingi bilioni 2.53 hapa nchini. Kamati inaamini kuwa mazingira wezeshi yakiwekwa kwa ajili ya Diaspora, wataendelea kuchangia pato kubwa zaidi katika uchumi wa Tanzania. Hili linawezekana endapo tu Sera ya Diapsora itakamilika mapema na kuanza kutumika kama ambavyo Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya utafiti ilibaini kuwa, nchi jirani ya Kenya tayari ina Sera ya Diaspora tangu mwaka 2014. Aidha, Taarifa ya Benki ya Dunia ya Masuala ya Uhamiaji na Maendeleo ya Mwaka 2019 (The World Bank's 2019 Migration and Development report) ilieleza kuwa mchango wa Diaspora nchini Kenya uliongezeka hadi kufikia USD bilioni 2.72 kwa Mwaka 2018 kutoka USD bilioni 1.96 mwaka 2017 ikiwa ni mchango wa zaidi ya asilimia 3 ya GDP kwa nchi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Ni rai ya Kamati kuwa mchakato wa utayarishwaji wa Sera ya Diaspora umalizike haraka kwa kuwa ndio mwongozo wa namna ambavyo wadau wataweza kushiriki katika hatua mbalimbali za kuwashirikisha watanzania wanaoishi nje ya nchi kuleta maendeleo yenye tija nchini.

#### 2.1.5 Hali ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika**, moja ya majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuratibu na kusimamia masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki (EAC).

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Agosti, 2019, Kamati ilielezwa kuwa Wizara imeratibu masuala mbalimbali yanayohusu Mtangamano wa Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja

na kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Itifaki ya Umoja wa Sarafu wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa hiyo, ilibaini changamoto mbalimbali ambazo Wizara inakabiliana nazo katika Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Wadau na washirika wa Maendeleo kutokutoa kwa wakati ahadi zao za kifedha za utekelezaji wa program na miradi ya kimaendeleo. Jambo hili husababisha utekelezaji wa miradi hiyo kuchukua muda mrefu au kutotekelezwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Serikali za nchi wanachama ziendeele kutenga na kutoa fedha za miradi ya maendeleo kila Mwaka kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kipaumbele ya Jumuiya bila kutegemea wahisani kwa kiasi kikubwa.

#### 2.1.6 Taarifa za Utekelezaji wa Masuala yanayoratibiwa Kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki zinazohusu masuala mbalimbali ya Kimataifa. Taarifa hizo ni pamoja na:-

- a) Upatikanaji wa fedha za kuendeshea Mfuko wa Mabadiliko ya Tabia Nchi;
- b) Changamoto ya Vikosi vya Tanzania kwenye misheni za Ulinzi na Usalama za Umoja wa Mataifa
- c) Matukio ya Chuki dhidi ya Raia wa Kigeni wenye asili ya Afrika Nchini Afrika Kusini (Xenophobia)
- d) Uridhiwaji wa Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Jamhui ya Muungano wa Tanzania
- e) Azimio la Umoja wa Mataifa katika Mkutano Mkuu wa Mabadiliko ya Tabia Nchi
- f) Changamoto za Mipaka kati ya Tanzania na Nchi Jirani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika Taarifa zote hizo zilizowasilishwa, Kamati iliridhika na maelezo yaliyotolewa na Serikali kuhusu namna masuala hayo yanavyoratibiwa, changamoto zilizopo na mikakati ya kuzitatua. Aidha, Kamati ilitoa rai kuwa Serikali iendeele kusuluhisha migogoro ya mipaka kwa njia ya kidiplomasia hususan kwa mpaka wa Tanzania na Malawi na Tanzania na Uganda ili kuepusha migogoro mikubwa inayoweza kutokea.

#### 2.1.7 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2019

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwezi Januari, 2020 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Julai hadi Disemba, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwa mtiririko wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni mzuri kwani hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 88,746,964,622.93 sawa na asilimia 53 (53%) ya Shilingi 166,926,820,000 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Matumizi yote ya Wizara. Vile vile, hadi kufikia mwezi



Disemba, 2019, Wizara iliweza kukusanya shilingi 4,922,184,201.72 sawa na asilimia 386 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli ya Shilingi 1,275,439,536.00.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu ongezeko hili na kuhoji sababu zake. Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hili limetokana na baadhi ya Balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya viza ambayo yalipaswa kukusanywa na Idara ya Uhamiaji kupitia mtandao wa kielektroniki. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa tangu mwezi Novemba, 2019 Balozi zote ziliacha kukusanya maduhuli hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa mwenendo huu wa makusanyo ambao unadhihirisha kuwa Wizara itafikia malengo yake ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Disemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 487,905,996.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha hizo kwani katika kipindi kinachoripotiwa kwa mwaka 2018 hakukuwa na fedha zozote za maendeleo zilizokuwa zimetolewa.

#### 2.1.8 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikijadili Taarifa hii ilibaini kuwa utolewaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2019 ni wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Januari, 2020, Wizara hii ilikuwa imepokea asimilia 54 ya fedha zote zilizotengwa kwa Mafungu matatu ya Wizara hii. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kati ya fedha hizo shilingi 101,691,220,050.00 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa fedha hizo zilizotolewa zilikuwa na kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Wizara (Fungu 57) na Ngome (Fungu 38); wakati JKT (Fungu 39) halikupokea kiasi chochote.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, baada ya kupitia Taarifa hii kwa kina, Kamati ilibaini kuwa Mradi wa Matrika na Zana za Kilimo wa Shirika la uzalishaji mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) umeendelea kukabiliwa na changamoto sugu ya madeni kutoka kwa wateja waliokopesha matrika. Hadi kufikia Mwezi Julai, 2019 bado kulikuwa na deni la shilingi bilioni 35,034,132,702.32. Kamati inaendelea kuisisitiza wizara kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha madeni hayo yanalipwa ili kuliwezesha Shirika kujiendesha kibiashara.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa Mashirika ya Utafiti ya Mzinga na Nyumbu yameendelea kukabiliwa na changamoto ya upungufu wa rasilimali watu na fedha hivyo kuathiri shughuli za kitafiti za mashirika hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilihoji kuhusu ulipaji wa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi hususan katika eneo la Ras Mshindo Wilayani Kilwa. Kamati ilibaini kuwa bado familia 83 hazijalipwa fidia hiyo ikiwa ni shilingi takribani milioni 600. Ni rai ya kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutoa fidia hizo ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kikao hicho, Kamati pia ilitaka kujiridhisha kuhusu ukamilishwaji wa Sera ya Ulinzi na kuhoji kuhusu suala hilo. Kamati ilibaini kuwa Sera hiyo bado hajjakamilika japokuwa Kamati imekuwa ikishauri kuhusu umuhimu wa kuwa na Sera hiyo tangu Kamati ilipoundwa mwaka 2016.

### 2.1.9 Hali ya Msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwezi Agosti, 2019, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu hali ya Msongamano wa Mahabusu Magerezani. Kamati ilielezwa kuwa idadi ya wahalifu magerezani hubadilika kati ya 36,000 na 39,000 ilhali uwezo wa Magereza ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kwa siku. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 idadi ya wahalifu ilikuwa 37,574 ambapo kati ya hao mahabusu walikuwa 18,729.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizo zilizotolewa ni dhahiri kuwa ipo changamoto ya mahabusu wengi kukaa magerezani bila kesi zao kushughulikiwa na kumalizwa kwa muda mfupi. Kamati ilitaka kujua kuhusu hali inayosababisha msongamano wa mahabusu magerezani licha ya kuwa kamati imekuwa ikiishauri mara kwa mara Serikali kuhusu hatua za kuchukua ili kupunguza msongamano huo. Kamati iibaini kuwa, masuala yafuatayo yameendelea kuchangia msongamano huo: -

i) Magereza mengi yaliyopo yalijengwa muda mrefu uliopita kwa mahitaji ya huduma hiyo kwa wakati huo wa ukoloni. Licha ya idadi ya watu na uhalifu kuongezeka, hakuna nafasi zilizoongezeka kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya kuhifadhi wahalifu

ii) Magereza mengi ni chakavu kiasi cha baadhi ya mabweni ya wahalifu kutotumika tena hivyo kupunguza zaidi nafasi za kuhifadhi mahabusu

iii) Ukosefu wa magereza ya wilaya katika wilaya nyingi zilizopo na zilizoanzishwa umesababisha msongamano wa mahabusu katika maeneo ambayo inabidi kuhifadhi mahabusu wa Wilaya nyingine katika Wilaya husika. Kwa sasa Wilaya ambazo hazina magereza ni 52

iv) Ucheleweshaji wa kesi mahakamani ambao husababisha mahabusu kukaa magerezani kwa muda mrefu kabla ya mashauri yao kumalizika

v) Ongezeko kubwa la wahamiaji haramu wanaoingia nchini kinyume cha Sheria na kupelekwa magerezani

vi) Jeshi la magereza linakabiliwa na uhaba wa vyombo vya usafiri na usafirishaji yakiwemo magari ya kusafirisha mahabusu kwenda na kurudi mahakamani.

### 2.1.10 Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati vilevile ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya wasilisho Kamati ilibaini yafuatayo: -

i) Uhalifu wa makosa makubwa ya jinai yamepungua kutoka makosa 28,890 mwaka 2018 hadi makosa 28,252 mwaka 2019 sawa na asilimia 2.2.

ii) Makosa ya usalama barabarani yamepungua kutoka makosa 2220 mwaka 2018 hadi makosa 1610 mwaka 2019 sawa na asilimia 27.5%.

iii) Dhana ya ulinzi shirikishi imeendelea kuimarishwa ambapo Jeshi la Polisi limeanzisha miradi mbalimbali ili kuhakikisha jamii inashiriki katika kutatua matatizo ya kiusalama katika maeneo yao na nchini kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa jitihada zake na hatimaye kupunguza makosa ya uhalifu hususan katika makosa ya usalama barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio katika kupunguza uhalifu nchini, Jeshi la Polisi limeendelea kukabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ya matumizi mengineyo (OC). Ufinyu huu wa bajeti, pamoja na mambo mengine, unaathiri kufanyika kwa operesheni za mara kwa mara pamoja na ufuatiliaji na upepelezi wa kesi.

#### 2.1.11 Hali ya Nyumba za majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari 2019 hadi Disemba, 2019 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuboresha makazi ya askari waliopo chini ya Wizara hii kwa kujenga nyumba mpya na kukarabati zile zilizochakaa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kukarabati nyumba za askari lakini juhudi zaidi zinahitajika.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari, 2020 Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu namna ambavyo Serikali imeendelea kuboresha makazi ya askari. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya kamati ilibainisha kuwa suala la nyumba za askari na watumishi waliopo chini ya Wizara hii bado ni changamoto. Kamati ilibaini mambo yafuatayo kwa kila Jeshi: -

**a) Jeshi la Magereza** - Kamati ilibaini kuwa kwa sasa Jeshi lina jumla ya watumishi (maafisa, askari na watumishi ambao siyo askari) 13,319 ikilinganishwa na nyumba 5,027 zilizopo, ambazo nyingi kati ya hizo ni chakavu au hazikidhi mahitaji muhimu ya kifamilia. Hivyo kwa kuzingatia idadi ya watumishi waliopo kwa sasa kuna upungufu wa nyumba za maafisa na askari 8,292 nchi nzima.

Kamati ilibaini kuwa, huo huwalazimu maafisa na askari kuishi uraiani katika nyumba za kupanga au nyumba binafsi za familia zao, hali inayodhoofisha ulinzi na usalama wa Magereza na kambi, pamoja na kuhatarisha usalama wa maafisa na askari wanaoishi nje ya kambi.

**b) Idara ya Uhamiaji** - Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Idara ya Uhamiaji, ina uhitaji wa nyumba 5,176 kwa ajili ya makazi ya watumishi wake. Kwa sasa Idara ina nyumba 411 hivyo kubaki na upungufu wa nyumba 4,765. Nyumba hizo ni kwa ajili ya makazi ya watumishi katika mikoa yote nchini kulingana na idadi ya watumishi katika mikoa hiyo.

**c) Jeshi la Zimamoto** - Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina uhitaji mkubwa wa nyumba kwa ajili ya makazi ya Maafisa na Askari. Jeshi lina jumla ya Maafisa na Askari **2,088** na nyumba zilizopo ni **49** tu ambazo kati ya hizo baadhi ni chakavu.

**d) Jeshi la Polisi** - Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Polisi lina jumla ya Nyumba **11,973**. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa nyumba hizo ni chache ukilinganisha na idadi ya Askari waliopo hivi sasa, lakini pia idadi kubwa ya nyumba hizo takribani asilimia **68** ni chakavu. Kutokana na hali hiyo ya uhaba wa nyumba, idadi kubwa ya askari Polisi wanaishi nje ya kambi kinyume na Kanuni za Jeshi la Polisi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uhaba wa nyumba kwa majeshi, Askari wengi waishio nje ya kambi, wanaishi kwa hofu kwa sababu za kiusalama. Vile vile kwa mujibu wa asili ya kazi za Jeshi la Polisi, kuishi nje ya kambi kunathiri utekelezaji wa majukumu ya kazi za Polisi ikiwa ni pamoja na ugumu wa kuwapata Askari wakati wa dharura na wakati mwingine baadhi ya Askari hupata madhara ikiwemo kujeruhiwa, kuuawa na kuharibiwa mali zao. Aidha, hali hiyo inachangia kupungua kwa udhibiti wa nidhamu kwa askari hao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto ya makazi iliyoorodheshwa hapo juu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuweka jitihada katika kujenga nyumba za majeshi yake.

**Mheshimiwa Spika**, Katika hatua hii naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilishiriki uzinduzi wa nyumba za Jeshi la Polisi Nzuguni Dodoma, Mwezi Oktoba, 2019 na nyumba za magereza Dar es Salaam mwezi Januari, 2020 ambazo zote zilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dk. John Joseph Pombe Magufuli. Hata hivyo, changamoto ya makazi kwa Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji bado ni kubwa.

#### **2.1.12 Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2019**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Januari 2020, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara hiyo na Mafungu yake yote kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kujadili kwa kina kuhusu Taarifa hiyo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

- a) Jeshi la Zimamoto limeendelea Kupata fedha pungufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.
- b) Uchache wa vituo vya Zimamoto na Uokoaji nchini. Kwa sasa Jeshi hilo lina vituo venye magari ya kuzima moto **47** tu nchini ukilinganisha na mahitaji halisi ya vituo **128**. Aidha, wilaya **106** nchini hazina vituo vya Zimamoto na Uokoaji.
- c) Uhaba wa magari ya Kuzima moto na ya uokoaji pamoja na magari kwa ajili ya shughuli za utawala na kubebea wagonjwa (ambulances).
- d) Ufinyu wa ukomo wa bajeti ya matumizi mengineyo kwa Idara ya Uhamiaji inasababisha kazi za misako na doria kutofanyika kikamilifu kutokana upungufu wa mafuta na ubovu wa magari.
- e) Idara ya Uhamiaji Kutotengewa fedha za miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2019/20, hali hii inapelekea kutokamilika kwa ujenzi na ukarabati wa nyumba za makazi ya watumishi pamoja na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Mikoa, Wilaya na Vituo.
- f) Viwango au ukomo wa bajeti vinavyotolewa na Wizara ya fedha - Hazina haviendani na mahitaji halisi ya Jeshi la Polisi.
- g) Upungufu wa askari na watumishi kwa Jeshi la Polisi, Magereza na Zimamoto
- h) Jeshi la Magereza kwa muda mrefu limeendelea kupatiwa fedha kidogo kwa ajili ya matumizi ya kawaida (Other Charges) hali hii imeathiri utendaji kwa kiwango kikubwa.
- i) Kuwepo kwa uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi juu ya Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa watu unaoendeshwa na NIDA na hivyo kuwafanya kuwa wazito katika kushiriki kwenye zoezi na wengine kujitokeza katika hatua za mwisho.

j) Kasi ndogo ya urejeshwaji wa wakimbizi wa Burundi waliojiandikisha kwa hiari yao kwa nia ya kurejeshwa nchini kwao kutokana na kubadili nia ndani ya muda mfupi kabla ya kuondoka.

k) Kuwepo kwa vitendo vya kihalifu kwenye maeneo ya wakimbizi.

#### 2.1.13 Utekelezaji wa Maazimio ya bunge

**Mheshimiwa Spika**, katika Kipindi cha Mwezi Oktoba, 2019, Kamati ilipokea utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati hii iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa Taarifa kuwa, Maazimio mengi yaliyopitishwa na Bunge utekelezaji wake ni wa kuridhisha na kwa yale ambayo hayajatekelezwa kwa kiasi cha kuridhisha, Kamati imeendelea kuisisitiza Serikali kuyafanyia kazi kama itakavyoonekana kwenye sehemu ya tatu ya Taarifa hii kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati.

#### 2.1.14 Kuwasilisha Maoni kuhusu Azimio la Bunge

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Kamati hii iliwasilisha Bungeni maoni na Ushauri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Protocol on Privileges and Immunities of the East African Community*). Itifaki hii inalenga kuwawekea Kinga watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kulinda mali za Jumuiya popote zilipo katika nchi wanachama wa Jumuiya na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikifanya uchambuzi wake, ilibaini kuwa kinga za kidiplomasia zilitambuliwa rasmi na Mkataba wa Vienna wa kushughulikia Uhusiano wa Kidiplomasia uliosainiwa tarehe 18 Aprili, 1961. Tanzania ilisaini Mkataba huo tarehe 27 Februari, 1962 na kuuridhia tarehe 05 Novemba, 1962 na hivyo kuwa miongoni mwa nchi 192 ambazo zimekwisha kusaini Mkataba huo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida zilizo katika kuridhia Itifaki hii, uidhinishwaji wa misamaha ya kodi kutokana na utekelezaji wa Itifaki hii kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya misamaha hiyo inayotolewa na hivyo kuathiri maslahi mapana ya nchi. Kamati ilitoa maoni kuwa umakini unahitajika katika kufuatilia utekelezaji wa misamaha hiyo na kuhakikisha kuwa misamaha ya kodi inayotolewa izingatie maslahi mapana ya nchi yetu kwa kuweka mifumo imara na madhubiti ya kuidhinisha misamaha hiyo.

#### 2.1.15 Taarifa za Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

**Mheshimiwa Spika**, kama inavyofahamika, katika kutekeleza Diplomasia ya Kibunge, Mabunge huwa na uwakilishi katika Mabunge na Vyama mbalimbali vya Kibunge ili pamoja na mambo mengine, kuongeza ushirikiano miongoni mwa nchi mbalimbali na kuwakilisha vema wananchi wa nchi wanachama kwa kutetea maslahi yao kijamii, kiuchumi na kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inalipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge, ambapo limeendelea kuwa na Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na kuwawezesha Wawakilishi hao kushiriki vikao katika Vyama na Mabunge mbalimbali, kwa maslahi ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jukwaa la Kibunge la Nchi

Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika kwa Kipindi cha Julai 2018-Septemba, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikijadili taarifa hio ilielezwa kuwa shabaha ya kuanzishwa kwa Jukwa hilo ni kuwa na Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC – PARLIAMENT) kama ilivyo kwa kanda nyingine ambazo tayari zina Mabunge yao kama vile Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati ilipokuwa ikijadili Taarifa hiyo ilibaini kuwa SADC PF imeendelea kutoa kipaumbele katika masuala yanayohusu jinsia. Hii ni pamoja na kuwa na:-

i) Fursa sawa ya uwakilishi kwa wanawake kwa vyama vya siasa vyenye Wabunge

ii) Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake ambaye ataingia kwa nafasi yake Katika kila nafasi 5 za Wabunge wanaochaguliwa kutoka kila Bunge la nchi mwanachama

iii) Kamati ya Kudumu ya SADC PF inayoshughulikia masuala ya Jinsia – *Gender Equality, Women Advancement and Youth Development Committee*

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo mengine yaliyotolewa, Kamati ilielezwa kuwa suala ambalo lipo kwenye mchakato mkubwa ni kulifanya Jukwaa hili kuwa Bunge lenye mamlaka kamili ya kujiendesha kama Bunge la ukanda wa kusini mwa Afrika. Kamati iliona kuwa suala hili lina tija na inapongeza jitihada mbalimbali zilizokwisha fanyika katika kufanikisha jambo hili.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati inaipongeza Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kuwezesha Bunge letu kushiriki katika Mikutano mbalimbali ya Jukwaa hilo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa ushiriki wa Bunge sio mzuri sana kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za safari kwa wakati. Aidha, ufinyu wa Bajeti umeendelea kusababisha Bunge letu kushindwa kushiriki katika uangalizi wa chaguzi mbalimbali za nchi za SADC. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iipatie Ofisi ya Bunge fedha zilizotengwa kwenye Bajeti kwa wakati ili Wajumbe waweze kushiriki katika vikao vilivyopangwa kwa mtiririko na utaratibu unaofaa.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

#### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo: -

##### 3.1.1 Maoni ya Jumla kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa chini ya Fungu 38- Ngome na Fungu 93- Uhamiaji, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa miradi hii na kutenga fedha za utekelezaji wake nje ya Bajeti iliyotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia ya dhati iliyooneshwa na Serikali katika kutoa fedha za maendeleo ikiwemo utaratibu wa kutoa fedha nje ya Bajeti kama ilivyooneshwa kwenye miradi miwili iliyotajwa hapo awali, bado Kamati ina maoni kuwa, kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara hizi hususan Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

### 3.1.2 Maoni Mahsusi

#### a) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- i) Ugumu wa kupata vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wengi kumepekea watazania wengi kuwa wazito katika kushiriki kwenye zoezi la kujiandikisha na wengine kujitokeza katika hatua za mwisho hususan pale wanapohajika kuwa navyo kwa ajili ya mambo ya kitaifa kama vile kusajili namba za simu, jambo ambalo linachangia zoezi hillo kuwa gumu;
- ii) Msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani umeendelea kuwa changamoto kwa Magereza nchini licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali;
- iii) Kutokutumika kwa utaratibu wa “*retention*” kwa Majeshi yaliyopo chini ya Wizara hii kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Vyombo hivyo hususan kwa kuzingatia kuwa fedha nyingi za OC hazitolewi;
- iv) Kucheleweshwa kwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani kunaendelea kusababisha majeruhi na vifo kutokana na kukosekana kwa sheria ya usalama barabarani iliyojitosheleza katika nyanja zote;
- v) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji bado halijapewa umuhimu unaostahili na Serikali ikilinganishwa na majukumu mazito na muhimu ya Jeshi hilo na jinsi linavyoheshimika Duniani kote;
- vi) Kuwepo kwa uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi juu ya Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa watu unaoendeshwa na NIDA unachangia wananchi wengi kuwa wazito katika kushiriki kwenye zoezi na wengine kujitokeza katika hatua za mwisho;
- vii) Upo umuhimu kwa Serikali kuangalia upya hadhi za Wakimbizi wanaopewa uraia Tanzania kulingana na Sheria za Kimataifa ili kuondoa changamoto za Kiusalama zinazoendelea kujitokeza kutokana na Wakimbizi hao kupewa uraia wa kudumu;
- viii) Upo umuhimu wa Serikali kuendelea kulipa uzito unaostahili suala la kuwasambaza Wakimbizi waliopewa uraia nchini katika maeneo mbalimbali ili kuepusha changamoto za kiusalama zinazoweza kujitokeza katika maeneo wanayoishi;
- ix) Upo umuhimu wa Serikali kutunga Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi ili kuratibu masuala ya ulinzi na usalama yanayofanywa na makampuni Binafsi.

#### b) Wizara ya Ulinzi na JKT

- i) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (National Defence Policy) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;
- ii) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (beacons) kwa baadhi ya maeneo na kuwepo kwa vipenyo visivyo rasmi kunachangia uvamizi wa Raia wa kigeni katika baadhi ya maeneo ya mipaka jambo ambalo linaweza kuathiri ulinzi na usalama wa nchi;
- iii) Kuendelea kuwepo kwa Madeni ya muda mrefu mathalani madeni ya matreta yaliyotolewa kwa Mkopo na SUMA JKT kwa Taasisi za Serikali na watu binafsi yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa Shirika hilo;
- iv) Kutokutolewa kwa fedha za Maendeleo kwa Shirika la Nyumbu kumeendelea kuathiri shughuli za kitafiti na za kibunifu za Shirika hilo.

**c) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

- i) Kutokamilika kwa Sera Mpya ya Nje Mambo ya Nje kunasababisha Sera iliyopo kuendelea kutumika ilhali haiendani na kasi ya maendeleo ya kiuchumi iliyopo sasa Duniani;
- ii) Kutokuwepo kwa Sera ya Diaspora kunachangia Serikali kuendelea kukosa mapato na faida nyingine nyingi ambazo zingepatikana kutokana na kuwepo kwa Sera hiyo;
- iii) Uwepo wa watumishi wachache katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi kunaathiri utendaji wa Balozi hizo hususan katika kutekeleza kwa ufanisi Diplomasia ya uchumi;

**d) Vyama vya Kibunge**

Changamoto ya upatikanaji wa fedha za safari kwa wakati kunasababisha Mtiririko usio mzuri wa ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Mabunge ya Kikanda jambo ambalo halileti taswira nzuri ya Bunge letu katika Mikutano hiyo.

**3.2 Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**a) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida**

**Kwa kuwa** Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii pamoja na Idara ya Uhamiaji yamekuwa yakitengewa fedha pungufu za undeshaji (OC) kulingana na mahitaji halisi ya Majeshi hayo;

**Na kwa kuwa** upungufu huo unaathiri shughuli za msingi za Majeshi hayo ikiwemo kuwa na uhaba wa vituo vya zimamoto na uokoaji, kutofanyika kikamilifu kwa misako na doria ya wahamiaji haramu, kushindwa kufuatilia upelelezi wa kesi na kufanya opresheni za mara kwa mara;

**Kwa hiyo basi**, Serikali ihakikishe inatenga Bajeti ya kutosha na kutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge ili kuviwezesha vyombo hivyo kujiendesha ipasavyo. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa Vyombo hivyo, pale ambapo ikibidi, Serikali iruhusu vibaki na sehemu ya Mapato yao (retention) ili kukabiliana na changamoto za kibajeti zilizopo.

**b) Ujenzi wa Nyumba za Maafisa na Askari**

**Kwa kuwa** Majeshi yaliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yanakabiliwa na upungufu mkubwa wa nyumba za askari na Watumishi, na kati ya nyumba chache zilizopo nyingi ni chakavu;

**Na kwa kuwa** upungufu huo wa nyumba unasababisha baadhi ya askari kuishi uraiani katika nyumba za kupanga jambo ambalo ni hatari kiusalama na vilevile linaathiri maadili ya kazi za Askari;



**Kwa hiyo basi**, Serikali ione umuhimu wa kutumia ujuzi na nguvu kazi iliyopo Jeshi la Magereza katika ujenzi wa nyumba za ubunifu ikiwa ni pamoja na kuwa na Kampeni maalumu ya kufyatua matofali kupitia Magereza kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Majeshi yaliyopo chini ya Wizara hii.

**c) Hali ya msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Gerezani**

**Kwa kuwa** uwezo wa magereza yaliyopo nchini ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kwa siku, na hadi sasa yanahifadhi wahalifu kati ya 36,000 na 39,000;

**Na kwa kuwa** msongamano huo wa wahalifu unachangiwa na idadi kubwa ya mahabusu ambao wanasubiri maamuzi ya kesi zao mbalimbali;

**Na kwa kuwa** Kamati inatambua kuwa jukumu la kupunguza Msongamano Magerezani linajumuisha Taasisi mbalimbali;

**Kwa hiyo basi, Serikali: -**

i) lendelee kutenga fedha kwa ajili ya kujenga na kukarabati Magereza katika Mikoa na Wilaya ili kuhimili uhifadhi wa wafungwa na mahabusu;

ii) Isimamie Kamati za Kusukuma kesi kukutana mara kwa mara ili kumaliza changamoto ya ucheleweshwaji wa kesi mahakamani;

iii) Ihakikishe upelelezi wa kesi hususan zile ambazo si za jinai, hauchukui muda mrefu.

iv) lendelee kutumia utaratibu wa mahakama inayotembea 'mobile courts' ili kushughulikia kesi nyingi zaidi;

v) landae mpango mkakati wa kupunguza Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani.

**d) Usalama barabarani**

**Kwa kuwa** makosa ya usalama barabarani yameendelea kusababisha ajali ambazo wakati mwingine husababisha mauti hata ulemavu wa kudumu;

**Na kwa kuwa** Serikali imeonesha nia ya dhati ya kupunguza makossa ya usalama barabarani ambapo makosa hayo yamepungua kwa asilimia 27.5% ikilinganishwa na mwaka 2018;

**Na kwa kuwa** bado kuna umuhimu wa kupunguza kabisa ajali zinazosababishwa na makossa ya barabarani;

**Kwa hiyo basi**, Jeshi la Polisi lione umuhimu wa kuharakisha mchakato wa kurekebisha Sheria ya Usalama barabarani ili kupunguza kabisa ajali zinazotokana na makosa ya usalama barabarani. Aidha, elimu kwa umma iendelee kutolewa kwa madereva wa vyombo vya moto wakiwemo madereva wa pikipiki na umma kwa ujumla kuhusu usalama barabarani.

### 3.2.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

#### a) Utekelezaji wa majukumu ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

**Kwa kuwa** baadhi ya Balozi za Tanzania nje ya nchi zina upungufu wa watumishi hususan wenye taaluma ya masuala ya uchumi;

**Na kwa kuwa** upungufu huo unaathiri shughuli za Balozi katika kutekeleza Diplomasia ya uchumi hususan katika kutangaza vivutio vya utalii na kutafuta fursa za ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya Nchi;

**Kwa hiyo basi**, Serikali ipeleke watumishi zaidi ambao wana taaluma ya masuala ya uchumi ili kuziwezesha Balozi zetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

#### b) Ukamilishaji wa Sera ya Mambo ya Nje

**Kwa kuwa**, Serikali imechukua muda mrefu wa kukamilisha Sera Mpya ya Mambo ya Nje,

**Na kwa kuwa**, kutokamilika kwa Sera hiyo kunaifanya Serikali kufahamika kuwa bado inatumia Sera ya Mwaka 2001,

**Hivyo basi**, Serikali ikamilishe kwa haraka iwezekanavyo Sera Mpya ya Mambo ya Nje na Kuanza kutumika rasmi mara moja

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

#### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Kangi Lugola, (Mb). Pia nawashukuru Naibu Waziri wa mambo ya Ndani Mhe. Eng. Hamad Masauni, (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Kabudi, (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Dkt. Damas Ndumbo, (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge pamoja na Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto na Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

.....  
Salum Mwinyi Rehani, Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO**  
**YA NJE, ULINZI NA USALAMA**  
Februari, 2020

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Rehani kwa kusoma vizuri sana taarifa yako.

Kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama nakushukurusana Mwenyekiti wangu, umefanya vizuri ila jambo moja tu Mwenyekiti; unasikia Mheshimiwa Mwenyekiti! Unajua Kamati hizi ziko kwenye Mabunge yote ya Afrika Mashariki; Uganda, Kenya na kadhalika. Sasa wangukwepo Wenyeviti wa Kamati za Mambo ya Nje wa Mabunge ya wenzetu huko, wangetofautiana kwa kiwango kikubwa na wewe kwa mavazi.

Unapokuja hapa kama Mwenyekiti wa Mambo ya Nje unapiga vitu! Siyo unavaa kirejareja hivi kidogo, unaniangusha Mwenyekiti. Nami najua vitu unavyo, sasa sababu ni nini Bwana! Usifanane na Ally Saleh, kila siku vikaunda suti tu kila siku. Sijamwona Ally Saleh akiweka maneno vizuri; na Mheshimiwa Masoud naye hivyo hivyo kila siku vikaunda kaunda tu, jamani! Wabunge ninyi mjipende. Halafu leo wanaochangia Mambo ya Nje wawe wanapiga maneno. Siyo umepiga kikaunda halafu unaongea Mambo ya Nje. Nitakuwa naangalia hapa, kama umepiga kimaneno cha ovyo ovyo sikupi nafasi hapa. *(Kicheko)*

Ni kweli jamani, tunatembelewa na wageni wengi, sasa unapokuja, vitu vingine mnaviona kama vidogo lakini vina *impact* kubwa. Yaani huyu ndio Mwenyekiti wa *foreign*, alivyovaa anaonekana, haiwezekani hiyo! Lazima unakwenda na Kamati yako ilivyo, maana tunaaminia. Kwa hiyo, Mwenyekiti jioni utakuja kitofauti kidogo. *(Makofi)*

Wageni walioko Bungeni Waheshimiwa, watoto wetu wale hatukuwatambulisha wakati ule, hawa ni wanafunzi wanatoka Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Monica kutoka kule Arusha. Ni wanafunzi 88 na Walimu 10. Wale wa kutoka kwa Mtakatifu Monica naomba msimame. Ahsanteni sana, sana, sana. Karibuni sana. Mnaona jinsi shule ilivyopendeza hii ya Mtakatifu Monica ya Wasichana kutoka kule Arusha! Kwa kweli hongereni sana, sana, sana kwa kuja kututembelea Bungeni. Karibuni sana, nina hakika Maofisa wangu wataandaa program nzuri kwa ajili ya kuwaeleza habari za Bunge na mambo yanayoendelea.

Kuna *observation* moja naiona Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge, Shule za Wasichana nyingi ni nzuri kweli kweli! Hatuoni Shule za Wavulana zenye kiwango hiki, sasa sijui tunakwenda wapi? Sasa hilo hebu Serikali jaribuni kuliangalia, hawa wavulana wataachwa sana. Kwa kweli si mnawaona *St. Monica*? Viwango kabisa! Ahsanteni sana, mnaweza kukaa. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nimewasilisha salamu za rambirambi kwa Maspika wenzangu; Mheshimiwa Justine Muturi na Mheshimiwa Kenny Lusaka wa Kenya kufuatia kifo cha Rais Mstaafu wa Nchi hiyo, Hayati Daniel Toroitich Arap Moi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajaalie faraja watu wa Kenya katika kipindi hiki kigumu. Hayati Rais Moi atakumbukwa na Watanzania wengi akiwa ni mmoja wa Marais waliofufua Jumuiya ya Afrika Mashariki. (Makofi)

Tutakumbuka Wabunge tuliokuwepo wakati huo akistaafu, katika *program* yake ya kustaafu, Rais Moi alikuja katika Ukumbi ule wa Spika na kutuhutubia Wabunge hotuba ya kuaga akiwa tayari amejandaa kuondoka kustaafu katika nafasi ya Urais. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahli pema Peponi. Amina. (Makofi)

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Mwenyekiti wa Nishati na Madini, karibu tafadhali. Mwenyekiti anakuja hapa eeh, sawa sawa! Eeh, Nishati na Madini, Mheshimiwa Luka Kitandula, karibu tafadhali. (Kicheko/Makofi)

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kuwasilisha taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Shughuli za Kamati kwa Kipindi cha mwaka 2019/2020 na kwa sababu ya muda sitaweza kusoma taarifa yote kwa hiyo naomba taarifa yetu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, taarifa yetu imegawanyika katika sehemu Kuu nne ambazo sehemu ya kwanza inahusu majukumu yaliyotekelezwa na Kamati, ikionesha njia zilizotumika na Kamati kutekeleza majukumu yake. Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati, sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati na sehemu ya nne ni hitimisho na hoja yenyewe ya Kamati kwa Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Kamati. katika kipindi cha Januari 2019 hadi Januari 2020, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanuni kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni vikao kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara pamoja na taasisi zake, semina mbalimbali pamoja na Ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Ambapo jumla miradi sita ilikaguliwa na maelezo ya miradi iliyokaguliwa pamoja na maoni na ushauri wa Kamati ni kama inavyoonekana kuanzia ukurasa wa pili hadi wa 11 wa taarifa yetu. Aidha

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maelezo kuhusu semina kwa wajumbe wa Kamati ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 12 hadi 15 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kukupongeza wewe binafsi katika kuhakikisha vibali vinapatikana kwa wadau wa nje pale ambapo wanahitaji kufanya majadiliano na Kamati yako. Ni dhahiri kwamba unasimamia vyema Bunge hili na kutekeleza majukumu yako kikamilifu kwa kuzingatia misingi, Kanuni na miongozo ya kuendesha Bunge letu katika kutoa fursa mbalimbali. Aidha, kipekee niwashukuru wadau wote ambao walihusika katika kuendesha semina, na hii ikihusisha Wizara zetu zote mbili pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Disemba mwaka 2019 na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba mwaka 2019 Wizara ya Nishati ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 419.9 sawa na asilimia 58 ya lengo ya bajeti ya nusu mwaka. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa shilingi bilioni 7.4 ni fedha za matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 98.6 ya lengo la nusu mwaka na shilingi bilioni 4.84 ni mishahara, sawa na asilimia 85.7 ya lengo kwa nusu mwaka. Aidha shilingi bilioni 407.7 ni za miradi ya maendeleo sawa na asilimia 57.8 ya lengo la fedha za maendeleo kwa nusu mwaka.

Mheshimiwa Spika, fedha za ndani zilizopokelewa ni Shilingi Bilioni 365.3 sawa na asilimia 56.0 ya lengo la fedha za ndani, na Shilingi Bilioni 42.4 sawa na asilimia 79.4 ya lengo la Fedha za nje katika nusu mwaka. Kwa upande wa Wizara ya Madini hadi kufikia tarehe 31, Disemba 2019 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 20.6 sawa na asilimia 97.2 ya makadirio ya nusu mwaka kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.7 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 12.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa umeme Vijini REA. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha inatoa kipaumbele cha kutoa fedha zote na kuzidi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya REA. Pamoja na upatikanaji mzuri wa fedha za Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Kamati imebaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa wakala huu. Changamoto hizo ni kama vile:-

a) Kuwepo kwa hali isiyoridhisha ya utaratibu wa upatikanaji wa vifaa muhimu vya umeme vinavyozalishwa nchini kama Nguzo, Nyaya, Mashine umbwa na viunganishi (accessories) ambazo zinapatikana nje.

Sambamba na hilo, baadhi ya viwanda nchini havijawa na utaratibu wa aina moja au unaofanana wa utoaji wa vifaa hivyo kwa wakandarasi. Aidha, viunganishi vinavyoagizwa k u t o k a nje ya nchi kuchukua muda mrefu kuwasili nchini;

b) Upo mwamko mdogo wa wananchi katika kulipia gharama za kuunganishiwa huduma ya umeme katika baadhi ya maeneo ambayo tayari huduma ya umeme imefikishwa;

c) Mazingira magumu kwa baadhi ya maeneo ili kufikia ofisi za TANESCO imekuwa kikwazo kwa wananchi kuweza kupata huduma.

d) Viongozi wa maeneo ambayo miradi inatekelezwa bado hawashirikishwi ipasavyo katika kuamua wigo wa maeneo ya kutekeleza miradi hiyo;

e) Usimamizi usioridhisha kwa Wakandarasi katika baadhi ya maeneo ya kutolea Miradi hiyo.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini. Hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa hadi kufikia Disemba 31, 2019 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulifikia megawati 1565.72. Aidha, uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini unafikia jumla ya megawati 1,602.318 na mahitaji ya juu katika mfumo wa Gridi ya Taifa umefikia megawati 1120.12 ambayo yamefikia tarehe 27 Novemba 2019 ukilinganisha na megawati 1116.58 zilizokuwa zimefikia tarehe 30 Novemba 2018.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto mbalimbali zinazozikabili Shirika la Umeme nchini hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa na Shirika la TANESCO linaendelea kujendesha vizuri bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Napenda kutumia fursa hii kuipongeza Wizara kwa usimamizi mzuri wa Shirika hili; tunawatia shime waendeleo kulisimamia vizuri Shirika letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Gesi. Hadi kufikia Januari 2020, mikataba hai ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini ni 12 ambapo inatekelezwa na kampuni nane za Kimataifa na mikataba 3 kati ya hiyo ipo katika hatua za uzalishaji na mikataba tisa ipo katika hatua za utafutaji. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Nishati leseni nane za utafutaji na uendelezaji wa gesi hapa nchini zimemaliza muda wake wa matumizi na kwamba mchakato wa uhishaji wa leseni hizo umechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kutohuishwa kwa leseni hizo kumetokana na sababu za msingi ikiwemo kusubiri kukamilika kwa kazi ya mapitio ya mikataba ya utafutaji wa mafuta nchini (PSA) yanayolenga kuhakikisha kuwa Serikali inanufaika ipasavyo kupitia mikataba hiyo. Pamoja na ukweli huo athari zifuatazo zinaweza kutokea iwapo mchakato wa kuhuisha leseni hizo utachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, athari ya kwanza ni kupungua kwa shughuli za utafutaji wa mafta na asilia nchini. Kwa mujibu wa mikataba wa utafutaji wa uzalishaji wa mafuta iliyopo kila upande unaweza kutekeleza haki na wajibu wake ikiwa Serikali itatoa leseni za utafutaji na uendelezaji kwa TPDC. Adha, pale ambapo muda leseni unakuwa umekwisha na taratibu za kuhuisha leseni hizo unaendelea Sheria ya Petrolu ya mwaka 2015 inatoa fursa kwa wawekezaji kuendelea na shughuli baada ya kupewa *comfort letter* na Serikali ilimradi maombi hayo yakiwa yamekidhi vigezo kisheria. Hata hivyo, kufuatiwa mkwamo wa uhuishaji wa leseni hizo kwa sasa imebainika kuwa baadhi ya Bodi za Wakurugenzi wa Kampuni hizo zinasubiri kuhuishwa kwa leseni baada ya leseni za awali kwisha muda wake zimeonesha kutokuwa tayari kutoa fedha za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mfano wa kampuni hizo ni Swala *Oil and Gas Tanzania, Ndovu Resources, Shell* na *Equinor*. Hii inatokana na wakandarasi hao kuwa na wasiwasi wa hatma ya maamuzi ya maombi yao ya leseni zao.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kusudio la *Force Majeure*. Baadhi ya wawekezaji wameainisha uamuzi wa kutohuishwa leseni za utafutaji kuwa ni moja kati ya sababu zinazoweza kutafsiriwa kuwa janga. Baadhi ya wakandarasi, kama vile *Swala Oil and Gas Tanzania* wameipa Serikali na TPDC notisi kuhusisha uhuishaji wa leseni na matukio ya majanga kwa mujibu wa PSA.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Ushindani Katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Uwekezaji katika Sekta hii Uwekezaji katika sekta hii unahitaji mtaji mkubwa, ambapo Serikali nyingi duniani hushirikisha sekta binafsi kwenye utafutaji na uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia. Tanzania inashindana kuvutia uwekezaji na nchi mbalimbali za Afrika kama vile Kenya, Uganda, Angola, Ghana, Mozambique na Nigeria pamoja

na nchi za bara la Asia kama vile Qatar, Oman, Trinidad & Tobago na Papua New Guinea nakadhalika. Maamuzi ya Serikali yana mchango mkubwa katika kuvutia au kutokuvutia wawekezaji. Ikiwa Serikali haitahuisha leseni tajwa katika muda mwafaka, hali hii yote kunaweza kuwepo athari za kupunguza uwekezaji kwa muda katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kuhuisha leseni husika kwa wakati, madhara makubwa zaidi yanaweza kutokea endapo leseni hizo zitahuishwa bila kufanyika uchambuzi wa kina na wa kutosha katika mikataba iliyopo. Umakini mkubwa unahitajika katika zoezi hili la mapitio ya mikataba.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa kazi ya kupitia mikataba itakapokamilika itawezesha Serikali na Taifa kwa ujumla kunufaika ipasavyo na rasilimali ya gesi asilia. Aidha, ushauri wetu ni kwamba mapitio hayo ya mikataba yanayoendelea kufanywa na timu ya Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yakamilishwe haraka lakini bila kuathiri umakini unahitajika kwa ajili ya kupata matokeo yanayolenga kunufaisha pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini. Sekta ya madini kufuatiwa usimamizi wa umakini wa Serikali imeendelea kupata mafanikio katika nchi yetu. Katika kuendeleza sekta ya madini nchini Kamati inapenda kuipongea Serikali ya awau ya tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi anayofanya katika kuimarisha utendaji wa sekta ya madini hivyo kuleta chachu kubwa ya uwekezaji katika rasilimali madini na hatimaye kuifanya sekta kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupata sulubu ya mkwamo wa kiuwekezaji na hivyo kuanzisha ubia na kampuni ya Barrick. Ubia huu utaiwezesha Serikali kuwa na ushiriki katika maamuzi ya shughuli za uendeshaji wa mgodi wa North Mara, Bulyanhulu na Buzwagi; hali ambayo inaiwezesha Tanzania kama nchi kunufaika na rasilimali ya madini yetu. Aidha, Makubaliano hayo pia yanaidhinisha uundwaji wa Shirika la *Twiga Minerals* linalomilikiwa na Barrick kwa asilimia 84 na Serikali asilimia 16. Shirika litakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Barrick nchini. Ni matarajio yetu kuwa Serikali imelenga kuongeza manufaa zaidi ya kiuchumi katika mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na kukutana na Wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni yafuatayo;

1. Upo umuhimu wa Serikali kufuatilia kwa makini mchakato mzima wa zabuni za upatikanaji wa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA kwani kuna baadhi ya wakandarasi wanaonekana hawana uwezo wa kutosha kutekeleza kazi hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi hii kwa wakati;

2. Serikali iendeleo kusimamia kwa karibu uzalishaji wa viwanda vyetu na utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya kutekeleza miradi ya REA, kwasababu vipo viashiria vinavyoonyesha kuwa viwanda vya ndani vinazalisha chini ya uwezo wake.

Aidha, utaratibu wa wakandarasi kutoa oda za vifaa unapaswa kufuatiliwa ili wasiagize vifaa kwa baadhi ya kampuni na kuacha nyingine, hii itasaidia kupunguza foleni ya upatikanaji wa vifaa katika makampuni machache ya uzalishaji hivyo kutoathiri upatikanaji wa vifaa kwa wakati.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

3. Wizara ya Nishati inapaswa kuendeeza kufanya tathmini ya uhakiki wa miradi ya ujazilizi ili maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya umeme yaweze kufikiwa na wateja waweze kuuunganishwa na huduma ya umeme.

4. Serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya wakandarasi wanaosuasua katika kutekeleza miradi ya REA.

5. Kasi ya uunganishaji wateja kwenye huduma ya umeme kwenye maeneo ambayo miradi ya REA imekamilika bado ipo chini ipo katika kiwango cha chini, hivyo Serikali kupitia TANESCO wanapaswa kuongea kasi ya kuwaunganisha wateja kwa huduma ya umeme kwa sababu Serikali imewezeza na kutumia gharama kubwa katika miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini.

6. Mchakato wa kuwapata wawekezaji binafsi wa kuzalisha umeme kwa kutumia rasilimali tulizonazo kama jua, upepo na makaa ya mawe umechukua muda mrefu mno, hivyo ipo haja kwa Serikali kuangalia kwa makini mchakato unaoendelea kwa kupunguza urasimu wa mchakato huo ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali tulizonazo katika kuzalisha umeme.

7. Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI zinapaswa kuchukua hatua za haraka katika kuhakikisha zinamaliza changamoto ya utengenezaji wa barabara katika mradi wa Kiwira kuelekea Kabulo. Kwa kuwa kutokukelezwa kwa barabara hii kundaliingizia hasara Taifa kutokana na uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi huo kufanyika kwa gharama kubwa.

8. Eneo la uwekezaji wa mradi wa *Buckreef* Serikali kama wataona inafaa ni vyema wakavunja mkataba na kampuni ya Tanzam 2000, kwani kwa hali ilivyo sasa muwekezaji amevunja masharti mengi moja wapo ikiwa ni ununuzi wa mitambo bila kumshirikisha mbia. Aisha, STAMICO haikushirikishwa katika maamuzi haya.

9. Ni rai ya Kamati kuwa katika maeneo ambayo STAMICO inashindwa kuendeleza uzalishaji ni afadhali maeneo haya yakagawiwa kwa wachimbaji wadogo ili Serikali iendelee kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Baada ya kuainisha maoni ya ujumla ya Kamati kuhusu masuala ya msingi yaliyobainika katika Sekta ya Nishati na Madini kwa ujumla wake naomba kutoa ushauri na mapendekezo kama inavyofuata:-

Mheshimiwa Spika, wakala wa Nishati vijijini REA.

KWA KUWA Serikali iliazimia vifaa vinavyotumika kutekeleza miradi hii vitengenezwe hapa nchini,

NA KWA KUWA, imebainika kuwa wakandarasi huweka oda za vifaa kwa kampuni chache na kuacha kampuni mengine hivyo kusababisha foleni ya kusubiri vifaa kwa muda mrefu hali ambayo inaathiri utekelezaji wa miradi ya REA;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu madhubuti wa ufuatiliaji ili kuhakikisha vifaa vya kutekeleza miradi hii vinapatikana kwa wakati na vikiwa na ubora stahiki ili miradi iweze kutekelezwa na kuendana na mpango wa utekelezaji wa kumaliza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Wigo wa kutekeleza miradi.



## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

KWA KUWA, maneno mengi ya Vitongoji yanarukwa wakati wa usambazaji wa umeme;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababishwa na wakandarasi kupewa wigo mdogo wa maeneo ya kutekeleza mradi;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuhakikisha inawashirikisha kwa kiasi kikubwa Viongozi wa wananchi katika uainishaji wa maeneo ya kupelekwa umeme ili maeneo muhimu ya kijamii na kiuchumi yapewe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya REA.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli:-

KWA KUWA, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) linakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi mikubwa;

NA KWA KUWA, shirika limeainisha na kuanza utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ikiwemo usambazaji wa gesi viwandani na majumbani ambayo itasaidia kupatikana kwa fedha za ndani kwa muda mfupi;

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kupeleka fedha za maendeleo kwa wakati. Aidha, TPDC inapaswa kuendelea kutekeleza miradi michache yenye manufaa na ikibidi ipewe kibali cha kukopa mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha au kuingia ubia na sekta binafsi ili kuweza kupata fedha za kutekeleza miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Mradi wa *Liquified Natural Gas*:-

KWA KUWA, Serikali iliamua kutoa ardhi ya wananchi wa Lindi ili itumike kujenga miundombinu muhimu ya kuchakata gesi kwa makubaliano ya kuwapatia fidia;

NA KWA KUWA, tathmini ya awali ya fidia ya ardhi husika ilifanyika mwaka 2015 na kurejewa tena mwaka 2017 na kisha Wizara ya Fedha na Mipango kufanya uhakiki wa fidia hizo mnamo mwezi Septemba, 2019;

NA KWA KUWA, Bunge kwa kutambua haki ya wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa kwa miaka mingi bila kupewa fidia yoyote, liliidhinisha takribani shilingi bilioni saba katika bajeti ya mwaka 2019/2020 ili fedha hizo zitumike kuwalipa fidia wananchi;

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuwa kabla ya mwaka wa fedha wa 2019/2020 kumalizika, iwalipe stahili zao kikamilifu wananchi wote wanaodai fidia kutokana na ardhi yao kutwaliwa ili kupisha mradi.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Mikataba ya Gesi Asilia:-

KWA KUWA, PSA zipatazo nane kati ya 12 zilizopo leseni zake zimeisha muda wake na hivyo wawekezaji kusita kuendelea na shughuli za kutafiti na uwekezaji wa mitaji katika Sekta ya Gesi;

NA KWA KUWA, utolewaji wa leseni hizo unapaswa kusubiri kukamilika kwa mapitio ya mikataba hiyo kutokana na mikataba hiyo kuonekana kuikoshesha nchi mapato stahiki kwa mujibu wa sheria zilizopo sasa; na kwa kuzingatia ukweli kuwa zoezi la mapitio ya mikataba

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

limechukua muda mrefu kukamilika tangu mwaka 2017 Bunge lako lililoishauri Serikali kufanya mapitio; na kwamba sasa majadiliano ya *Host Government Agreement* yamesimama kusubiri hatma ya mapitio ya mikataba ambayo yatajenga misingi ya majadiliano ya Mradi wa LNG;

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuchukua hatua mahususi zitakazoweza zoezi la mapitio ya mikataba kukamilika ndani ya kipindi kifupi ili kuwezesha mchakato wa majadiliano ya mradi wa LNG kuendelea na hatimaye uwekezaji uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa rasilimali joto ardhi nchini:-

KWA KUWA, nchi yetu haina sheria mahususi ya joto ardhi;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa sheria mahususi kunakwamisha uwekezaji na uendelezaji wa rasilimali ya joto ardhi;

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kumaliza mchakato wa uandaaji wa rasimu ya mapendekezo ya kutunga sheria ya joto ardhi ili uweze kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya utungaji wa sheria mahususi ya joto ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme (TANESCO):-

KWA KUWA, shirika linakabiliwa na changamoto ya upotevu wa umeme na uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme kunakosababishwa na vitendo vya wizi na hujuma;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinasababisha hasara kubwa kwa shirika;

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuiwezesha TANESCO ili iweze kutumia teknolojia za kisasa katika kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, shirika liimarisha doria katika njia za umeme na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme kupitia mikataba na wananchi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini:-

KWA KUWA, Chuo cha Madini kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya msingi ya chuo kutokana na bajeti finyu;

NA KWA KUWA, Chuo pia kina upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali katika Campus ya Dodoma na Nzega kama vile Watunza Kumbukumbu, Wakutubi, Wahasibu na Wakufunzi katika nafasi ya uhandishi na usimamizi wa mazingira ya migodi;

HIVYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kukiongezea chuo fedha ili kuwezesha shughuli za utoaji wa mafunzo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi migodini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge na Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu. Napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua wote na majina yao yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge. (Makofi)

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemuni, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge na aliyekuwa Katibu Mkuu Dkt. Hamisi Mwinyimvua ambaye amemaliza muda wake wa utumishi kwa sasa pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ujumla wao.

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara ya Madini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Mbunge; na Naibu Waziri Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge; Katibu Mkuu Profesa Simon Msanjila pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa Kamati yetu. Pia, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Felister Mgonja na Ndugu Angelina Sanga pamoja na Msaidizi wa Kamati Grace Mwenye kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

### **TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

#### **SEHEMU YA KWANZA**

##### **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

##### **1.1. Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2019 hadi Januari 2020, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanuni kama ilivyocainishwa katika kifungu cha 7 (1) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Pamoja na majukumu mengine Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini;
- b) Kushughulikia Taarifa za Mwaka za Utendaji wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini pamoja na;
- c) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

##### **1.2. Njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni vikao kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara

pamoja na taasisi zake, semina mbalimbali pamoja na Ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

### 1.2.1 Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika**, Ziara hizo zilifanyika katika Mkoa ya Dodoma, Pwani (Rufiji), Njombe (Makambako), Ruvuma (Songea) na Iringa. Lengo la ziara hizo ni kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni kama ifuatavyo;

- i. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI);
- ii. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Madini (MTUMBA- DODOMA);
- iii. Mradi wa Nyerere Hydro Power Project (Rufiji) 2,115M;
- iv. Mradi wa Makambako - Songea 220 kV Transmission Line;
- v. Mradi wa Ujenzi wa kituo cha Umahiri (Songea);
- vi. Miradi ya umeme Vijijini REA III Mkoa wa Iringa.

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya miradi pamoja na changamoto ambazo Kamati ilizibaini kwa kila mradi wakati wa ukaguzi wake:

#### i. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI);

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (*Sustainable Management of Mineral Resources Project- SMMRP*) upo chini ya Wizara ya Madini na Utekelezaji wake umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilitekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwezi Septemba, 2009 hadi Juni 2016 chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Bajeti iliyotumika kutekeleza mradi huu ilikuwa Dola za marekani **milioni 55** ambapo Dola za marekani **milioni 50** zilitolewa na Benki ya Dunia na Dola za Marekani **milioni 5** zilitolewa na Serikali ya Tanzania.

Serikali ya Tanzania ilipata nyongeza ya fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia (*Additional Financing - AF*) kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi. Jumla ya Dola za Marekani **milioni 50** zilipangwa kutumika ambapo **Dola milioni 45** ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na **Dola milioni 5** zitatolewa na Serikali ya Tanzania (*counterpart fund*). Awamu ya Pili ya Mradi (SMMRP II-*Additional Financing*) imetekelezwa ndani ya miaka mitatu kuanzia mwezi Septemba 2015 hadi Disemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo kuu la mradi wa SMMRP ni kuboresha manufaa ya

kijamii na kiuchumi yatokanayo na uchimbaji wa madini nchini kwa kuimarisha zaidi sehemu ya miradi ya kiuchumi na kijamii iliyokuwa inatekelezwa na mradi wa awamu ya kwanza na hivyo kuhakikisha ukuaji mkubwa wa maendeleo ya pamoja na kupunguza umaskini.

Aidha, katika utekelezaji wa lengo hilo, pamoja na mambo mengine mradi ulipanga ujenzi wa Vituo Saba (7) vya umahiri (*Centers of Excellence*) katika maeneo ya Bariadi, Bukoba, Musoma, Handeni, Mpanda, Chunya, Songea na Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini ambalo ndani yake kutakuwa na ofisi ya Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Tanzania (TAWOMA).

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini ulianza kutekelezwa mara baada ya Wizara ya Madini kumkabidhi Mkandarasi SUMA JKT eneo la ujenzi lililopo ndani ya Plot 1-10, Block D (Mbwanga Area) lenye ukubwa wa mita za mraba 2,250 mnamo tarehe 14 Julai, 2018 na hatimaye kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 30 Julai, 2018. Ujenzi wa Jengo hilo umegharimu jumla ya takribani **Shilingi Bilioni 2.86**.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka wakati kamati yako ilipotembelea mradi, ujenzi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 65** ambapo hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 jumla ya takribani **Shilingi Bilioni 1.91** sawa na **asilimia 67** zilikuwa zimelipwa kwa Mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Jengo hilo lina manufaa yafuatayo:

1. Uwepo wa ofisi za Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Tanzania (TAWOMA) ambazo zinasaidia kuratibu mafunzo yatakayo waendeleza akina mama wachimbaji wa Madini;
2. Kumaliza tatizo la ukosefu wa ofisi kwa wakufunzi;
3. Kupunguza tatizo la ukosefu wa vyumba vya madarasa hivyo kutoa fursa kwa chuo kuongeza nafasi za udahili;
4. Kuongezeka kwa wataalam wenye weledi wa masuala ya madini na hivyo kusababisha kuongezeka kwa ufanisi na tija kwa kuboresha utendaji wa wachimbaji wadogo na wakubwa.

## ii. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Madini (MTUMBA DODOMA);

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Madini ilipokea Fedha za ujenzi **Shilingi Bilioni 1** tarehe **5/11/2018** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali Dodoma eneo la Mtumba. Mara baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ilianza mchakato wa ujenzi ikiwa ni pamoja na kufuatilia michoro kwa Wakala wa Majengo (TBA) na kuchagua kampuni ya ujenzi kati ya kampuni zilizokuwa zimeainishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Wizara ilifanikiwa kupata Kampuni ya ujenzi ya Mzinga Holding Co. Ltd na kusaini nayo mkataba wenye thamani ya takribani **Shilingi Milioni 975** pamoja na **VAT**. Kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 4/12/2018 na kutakiwa kukamilika tarehe 28/02/2019 kama ilivyo kwenye mkataba wa nyongeza (*addendum contract*). Hata hivyo hadi wakati kamati inatembelea mradi huo tarehe 13/03/2019 ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 80**.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wa mradi huu, kamati ilibaini changamoto zifuatazo;

1. Muda mfupi wa utekelezaji wa mkataba. Kwa mujibu wa mkataba mkandarasi alipaswa amalize mradi huo ndani ya mwezi mmoja ambao ulitimia mwezi Januari, 2019. Hata hivyo mkandarasi alishindwa kumaliza ndani ya mwezi mmoja na hivyo kupewa mkataba wa nyongeza kila mwezi (addendum contract);

2. Mvua zilizonyesha kati ya mwezi Disemba 2018 na Januari 2019 zilisababisha mradi kutokamilika kwa wakati.

### **iii. Mradi wa Nyerere Hydro Power (Rufiji) 2,115 MW;**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Nyerere utafua umeme wa kiasi cha MW 2,115 kwa kutumia maji katika bonde la Mto Rufiji. Mnamo tarehe 12 Disemba, 2018 Mkataba wa ujenzi wa mradi ulisainiwa kati ya TANESCO na Mkandarasi ambao ni Kampuni ya Arab Contractors iliyoingia ubia na Elsewedy Electric, zote za Misri; tukio ambalo lilishuhudiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Misri. Ujenzi wa mradi huu utachukua kipindi cha miezi 42, ambapo miezi 36 ni ya ujenzi na miezi sita ni kwa ajili ya maandalizi. Aidha, utekelezaji wa Mkataba huo umeanza toka tarehe 15 Disemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, Kazi ya ujenzi wa baadhi ya miundombinu mbalimbali ya kuwezesha mradi kufanyika kwa urahisi imekamilika na Serikali kupitia TANESCO ilikabidhi rasmi eneo la Mradi kwa Mkandarasi tarehe 14 Februari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wa mradi huu, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Barabara kutokuwa za kiwango cha kuhimili mvua na mizigo mizito hali ambayo huenda ikahitaji ukarabati wa mara kwa mara;

2. Kukosekana kwa mpango wa kutenga eneo kwa ajili ya matenki ya kuhifadhi mafuta wakati wa ujenzi wa mradi kwani ni wazi kwamba kiasi kikubwa cha mafuta kitahitajika wakati wa ujenzi.

Hata hivyo katika kumaliza changamoto hii, Kamati imearifiwa kuwa kwa sasa tayari Wizara ya Nishati imetenga maeneo maalum kwa ajili ya vituo vya mafuta ambayo yana ukubwa wa kilomita za mraba 914 hivyo, kuwezesha uwepo wa vituo vya mafuta vya muda katika sehemu ya eneo la mradi.

### **iv. Mradi wa Makambako - Songea 220 kV Transmission Line;**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la umeme Tanzania (TANESCO); na Serikali ya Sweden kupitia Shirika la maendeleo la Sweden (Sida). Kupitia ushirikiano huu, Serikali ya Tanzania imechangia jumla ya Dola za kimarekani (USD) 20 milioni (ambapo kati ya fedha hizo TANESCO inachangia **Dola milioni 7** na Serikali **Dola milioni 13** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya msongo wa kV 220 na Vituo vitatu vya kupozea umeme.

Aidha, Serikali ya Tanzania pia imetoa fedha za ulipaji wa fidia kwenye laini kubwa ya msongo wa kV 220 kiasi cha **shilingi Bilioni 7**. Kwa upande wa Serikali ya Sweden nayo imetoa Jumla ya fedha za Sweden, **Krona milioni 620**. Kati ya fedha hizo Msaada

ni jumla ya **Krona million 578** na mkopo ni Krona **milioni 42**. Jumla kuu ya gharama za mradi kwa fedha za Tanzania ni sawa na **shilingi billion 216**.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Makambako-Songea umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba; ujenzi wa vituo vipya vitatu (3) vya kupoza umeme katika eneo la Makambako, Madaba na Songea mjini na ujenzi wa njia za kusambaza umeme katika vijiji 122 vinavyopitiwa na njia ya umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa mradi umekamilika kama ilivyopangwa ambapo njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa km 250 ya msongo wa kV 220 pamoja na vituo vitatu vya kupoza umeme vya Makambako, Madaba na Songea umekamilika kwa **asilimia 100**. Mradi huu umewezesha mikoa ya Njombe na Ruvuma kuunganishwa katika Gridi ya Taifa ambapo iliungwa mwezi Novemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya manufaa makubwa ya utekelezaji wa mradi huu, pia, kumekuwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa mradi zikiwemo:

1) Uhaba wa nguzo za umeme kwa kipindi cha miezi 3 iliyotokea mkoani lringa mwishoni mwa mwaka 2018;

2) Nguzo za miti kuchomwa moto kutokana na shughuli za wananchi wakati wa kilimo;

3) Kurukwa kwa baadhi ya vijiji vilivyopitiwa na njia ya umeme;

4) Muitikio mdogo wa wananchi kuunganishwa na huduma ya umeme;

5) Ukosefu wa elimu kwa wananchi kuhusu gharama za kuunganishwa huduma ya umeme; na

6) Uhaba wa mita za umeme na vifaa vya kuunganisha umeme kwa wateja.

#### **v. Mradi wa Ujenzi wa kituo cha Umahiri - Songea (Centre of Excellence);**

**Mheshimiwa Spika**, Eneo la Mradi wa kituo cha Umahiri kwa ajili ya wachimbaji wadogo lipo katika kiwanja Namba 86 Angoni Ams-Manispaa ya Songea yenye Hati namba 26756. Mkandarasi SUMA JKT alikabidhiwa eneo la ujenzi rasmi tarehe 15 Julai, 2018 na mnamo tarehe 24 Julai, 2018 kazi ya ujenzi ilianza. Ujenzi wa kituo hicho unagharimu kiasi cha takribani **Shilingi Bilioni 1.27**.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kamati inatembelea mradi huo ujenzi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 40**. Aidha hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 kiasi cha **Shilingi milioni 373.99** zilikuwa zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Hata hivyo, kwa mujibu wa mkataba Ujenzi wa jengo hilo ulitarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wa mradi huu changamoto zifuatazo zilibainika;

1. Kukosekana kwa kibali cha kuvunja jengo la zamani hivyo kusababisha ujenzi kuchelewa kuanza;

2. Mkandarasi kukosa wafanyakazi wa kutosha na hivyo ujenzi kwenda kwa kusuasua;

vi. Uhaba wa upatikanaji kokoto katika eneo la mji wa Songea ulisababisha kusimama kwa utekelezaji wa mradi.

**vii. Miradi ya umeme Vijijini (REA III) Mkoa wa Iringa.**

**Mheshimiwa Spika**, Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Mikoa inayonufaika na miradi ya umeme vijijini awamu ya tatu. Miradi hii inatekelezwa katika Wilaya za Iringa vijijini, Kilolo na Mufindi; na ipo katika makundi matatu ambayo ni;

1. Miradi ya Ujazilizi (Densification);

2. Mradi wa Njia kuu ya kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kilovolti **400(BTIP-VEI)** na;

3. Mradi ya REA III Mzunguko wa Kwanza.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilikagua utekelezaji wa mradi wa REA III katika vijiji viwili kama ifuatavyo:-

i. **Kijiji cha Ngano**; Wigo wa usambazaji katika kijiji hiki ulihusisha Ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 7.1, njia ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 2.3 na ufungaji wa mashine umba moja(1) yenye uwezo wa 50Kva.

Ili kujiridhisha na kazi iliyofanyika, kamati ilitembelea na kukagua miundombinu ya umeme katika eneo husika na kushuhudia uzinduzi wa kisima cha maji katika shule ya msingi ngano. Kisima hicho kimeunganishwa na nishati ya umeme hivyo kuweza kupampu maji katika eneo la shule na wananchi wa kijiji hicho.

Aidha, kamati ilitembelea eneo la zahanati ya kijiji hicho na kushuhudia uwepo wa miundombinu ya umeme ulio unganishwa katika zahanati hiyo.

**Kijiji cha Ikuvala** - Wigo wa usambazaji katika kijiji hiki unahusisha Ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 3.5, njia ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 4.6 na ufungaji wa mashine umba moja(1) yenye uwezo wa 50Kva. Katika kijiji hiki Kamati ilitembelea na kukagua miundombinu ya umeme iliyounganishwa katika mashine ya kusaga nafaka iliyopo kijijini hapo na kujionea upelekwaji wa umeme katika mashine hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio katika miradi ya umeme mkoani Iringa, Kamati ilibaini changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Kukosekana kwa nguzo na hivyo kusababisha miradi kutokutekelezwa kwa wakati;

2. Baadhi ya Maeneo kutokuunganishwa na huduma ya umeme licha ya miundombinu ya umeme kupita karibu na maeneo hayo mfano; Kanisa Katoliki kijiji cha Ikuvala ambalo pia linatoa huduma kama Zahanati, Shule na Maktaba kwa wakazi wa kijiji hicho kutokana na taasisi hizo kutolipiwa gharama za kuunganisha umeme;

3. Utamaduni mbaya wa wananchi kutumia moto kusafisha mashamba wakati wa kiangazi badala ya kulima; hali ambayo inasababisha nguzo za umeme kuungua na hivyo kusababisha kuharibika kwa miundombinu ya umeme na hasara kwa shirika;

4. Kurukwa kwa vijiji ambavyo vimepitiwa na njia ya msongo wa umeme



mfano; kijiji cha iwanga ambapo umeme umepita ila vijiji havijaunganishwa;

5. Wigo "scope" finyu wa maeneo ya kazi unaotolewa kwa wakandarasi bado ni changamoto kubwa inayosababisha maeneo mengi kutofikiwa huduma ya umeme.

### **1.3. Maoni na Ushauri wa Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

1. Kutokana na maeneo mengi ya vijiji na vitongoji kurukwa wakati wa upelekaji wa umeme, Serikali inapaswa kuongeza wigo (scope) wa maeneo ya kazi unaotolewa kwa wakandarasi ili kuweza kukiidhi mahitaji ya wananchi kufikiwa na nishati ya umeme;

2. Serikali kupitia TANESCO inapaswa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya uunganishwaji wa huduma ya umeme ili wananchi wapate uelewa wa namna ya kuunganishwa na huduma ya umeme kwa kuhusisha gharama zinazopaswa kulipwa;

3. Miradi ya umeme vijijini bado inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa baadhi ya vifaa kwa wakati mfano mita, nguzo, nyaya n.k. Kamati inatoa rai kwa Serikali kufuatilia kwa karibu uzalishaji wa vifaa hivi ili kuhakikisha vifaa vinapatikana kwa wakati na kwa gharama nafuu.

4. Utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini uzingatie sana ushirikishwaji wa wananchi pamoja na viongozi wa maeneo wanaohusika;

5. Mikataba ya Ujenzi wa majengo ya Wizara unapaswa kuzingatia ubora wa majengo na muda wa kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika.

Hii itasaidia kuondokana na tatizo la miradi ya Serikali kuongezewa muda wa utekelezaji mara kwa mara na hivyo kuongeza gharama kwa Serikali;

6. Serikali inapaswa kuendelea kuwasimamia kwa karibu wakandarasi wanaopewa kazi za miradi ya Serikali kwani baadhi ya wakandarasi wamebainika kutokuwa na nguvu kazi ya kutosha hali ambayo imesababisha kuzorota kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi;

7. Ujenzi wa miradi unapaswa kuzingatia uwepo wa miundombinu na barabara imara ambazo zitahimili mizigo mizito na athari za mvua ili kuhakikisha miradi inaendelea kutekelezwa kwa nyakati zote, mfano; mradi wa umeme wa mto Rufiji, barabara ya kufika katika mradi ipo katika kiwango kisichoidhisha. Ikiwa hali ya barabara itaendelea kuwa kama ilivyo kwa sasa, barabara hizo hazitapitika wakati wa mvua na hivyo kukwamisha utekelezaji wa mradi;

8. Pamoja na kuwa TANESCO inafanya vizuri katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme nchini bado kumekuwana changamoto kubwa katika usambazaji wa umeme kwa wananchi na kusababisha wananchi wengi kukosa huduma ya umeme. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza na kuongeza kasi katika usambazaji wa umeme ili wananchi wengi waweze kuunganishwa na kufikiwa na huduma hii.

### **1.4. Semina kwa Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari 2019 hadi Januari 2020

Kamati iliweza kupata semina mbalimbali ambazo zililenga kuipatia fursa kufanya majadiliano ya kina na wadau mbalimbali katika sekta ya nishati na madini.

Aidha, Kupitia Semina hizo Kamati yako ya Nishati na Madini imekuwa na uelewa mpana kuhusu sekta ya madini, mafuta na gesi asilia ambazo inazisimamia hivyo kuelewa vyema mambo muhimu ya kuzingatia kama Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kushauri na kuisimamia vyema Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kukupongeza wewe binafsi katika kuhakikisha vibali vinapatikana kwa wadau wa nje pale ambapo wanahitaji kufanya majadiliano na Kamati yako. Ni dhahiri kwamba, unasimamia vyema Bunge hili na kutekeleza majukumu yako kikamilifu kwa kuzingatia misingi, kanuni na miongozo ya kuendesha Bunge katika kutoa fursa mbalimbali.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati yako imekuwa ikipata mafunzo mara kwa mara kutoka kwa Wizara na Taasisi inazosimamia kwa Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini. Wizara hizi zimekuwa zikiwajengea wajumbe uelewa katika sekta wanazosimamia za madini, nishati na gesi asilia. Aidha, Wizara hizi zimekuwa karibu sana na kamati katika kuhakikisha wajumbe wanashiriki katika ufunguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa hapa nchini mfano mradi wa Nyerere Hydropower, masoko ya madini, n.k. Kamati inachukua fursa hii kushukuru sana Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini katika kuendelea kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati na ushirikiano mkubwa wanao uonesha wakati pale mafunzo yanapohitajika.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria mafunzo kuanzia tarehe 11 hadi tarehe 16 Februari 2019 Mkoani Arusha. Mafunzo haya yaliratibiwa na Mashirika ya Serikali ya Marekani ambayo ni *United States Energy Associations-USEA, USAID* na *Power Africa*. Lengo la mafunzo hayo kwa wajumbe wa kamati ilikuwa ni kuwajengea uelewa wa kidunia kuhusiana na Masuala ya Usimamizi wa Sekta ya Nishati katika maeneo ya nishati jadidifu, uzalishaji, usambazi na uuzaji wa umeme, uendelezaji wa gesi asilia, na mahusiano ya sekta binafsi katika kuendelea nishati endelevu sambamba na kuziangalia fursa na changamoto zilizopo katika sekta ya nishati na kuboresha ili kuzalisha nishati ya uhakika na ya gharama nafuu nchini. Aidha, Ziara ya mafunzo haya ni muendeleo wa mahusiano mazuri ya kimaendeleo kati ya Serikali ya Marekani na Tanzania kupitia mradi wake wa *Power Africa*.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilihudhuria ziara ya mafunzo na kutembelea miradi ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati jadidifu kama vile nishati ya jua na mapomoroko ya maji kuanzia tarehe 8 hadi tarehe 11 Novemba 2019. Ziara hiyo iliratibiwa na Taasisi ya *Tanzania Renewable Energy Association (TAREA)*.**

Aidha, Wabunge na Sekretarieti waligawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza lilienda kujifunza katika mtambo wa umeme nuru (Solar Mini Grid) ulioko kijiji cha Ketumbeine, Wilaya ya Longido na kundi la pili lilikwenda kujifunza katika mtambo mdogo wa mapomoroko ya maji Mwenga, Mufindi.

**Mheshimiwa Spika, Katika kuendelea kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati yako, Ofisi ya Bunge imekua na utaratibu mzuri wa uandaaji wa semina elekezi kupitia mradi wa *UNDP (Legislative Support Program)* kuhusu masuala ya kutunga Sheria pamoja na Kanuni mbalimbali za uendeshaji wa Shughuli za Bunge. Mafunzo haya yamekua muhimu sana katika kuongeza uelewa mpana kwa wajumbe wa**

Kamati.

**Aidha, Katika kuelekea kwenye utekelezaji kwa vitendo kuhusu mfumo wa Bunge Mtandao (e-Parliament Portal) Ofisi ya Bunge imekuwa ikiandaa mafunzo kwa Wabunge katika kamati mbalimbali ili kuweza kujifunza kwa vitendo namna ya kutekeleza mfumo huo. Kamati inakushukuru sana Mheshimiwa Spika pamoja na Ofisi ya Bunge kwa namna ambavyo mmekuwa mkiwahusisha wabunge katika mafunzo hayo kwa vitendo ili kuweza kuendana na kasi kubwa ya matumizi ya Bunge mtandao.**

**Mheshimiwa Spika**, kamati inawashukuru wadau wote wanaoashirikiana nasi katika kutujengea uwezo, kutoa mafunzo mbalimbali ili kuendeleza Sekta ya Nishati na Sekta ya Madini. Aidha, michango yao, maoni yao (pindi yanapohitajika) na kutoa semina mbalimbali katika kamati imesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha uchambuzi na utekelezaji wa majukumu ya Kamati wakati wote. Wadau hao ni kama vile, Taasisi isiyo ya kiserikali ya *Natural Resource Government Institute (NRGI)*, *REPOA*, *Policy Forum*, *FEMATA*, *Haki Rasilimali*, *Forum C.C n.k.*

## SEHEMU YA PILI

### 2.1 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa Ujumla

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na hali ya upatikanaji wa Fedha, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) na Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa kipindi cha nusu mwaka (kuanzia Julai hadi Disemba 2019).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Wizara ya Nishati, Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka 2019/2020 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 2,116,454,000,000** sawa na **asilimia 98.8** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 1,956,372,000,000** sawa na **asilimia 92.4** ya Bajeti yote ya Maendeleo. Fedha nyingi za ndani za miradi ya maendeleo zimeelekezwa katika miradi mikubwa minne (4) ya kimkakati ambapo jumla ya **Shilingi trilioni 1.88**, sawa na **asilimia 95.9** ya Bajeti yote ya ndani imetengwa. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere, MW 2,115 (**Shilingi trilioni 1.44**); Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (**Shilingi Bilioni 363.11**); Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I Extension MW 185 (**Shilingi Bilioni 60**); na Mradi wa Ruhudji (**Shilingi Bilioni 10**).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2019/2020 ni **Shilingi 26,339,309,000** sawa na **asilimia 1.2** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 11,313,488,000** zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2019 Fedha zilizopokelewa kwa bajeti ya Wizara ya Nishati ni **Shilingi Bilioni 419.9** sawa na **asilimia 58.4** ya lengo la bajeti ya nusu mwaka. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa: **Shilingi Bilioni 7.40** ni fedha za matumizi mengineyo (O.C) ambayo ni sawa na **asilimia 98.6** ya lengo la nusu mwaka; na **Shilingi Bilioni 4.84** ni mishahara sawa na **asilimia 85.7** ya lengo kwa nusu mwaka.

Aidha, **Shilingi Bilioni 407.7** ni za miradi ya maendeleo sawa na **asilimia**

**57.8** ya lengo la Fedha za maendeleo kwa nusu mwaka 2019/2020. Fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni 365.3** sawa na **asilimia 56.0** ya lengo la Fedha za ndani na **Shilingi Bilioni 42.4** sawa na **asilimia 79.4** ya lengo la Fedha za nje katika nusu mwaka. Vilevile, miradi ya maendeleo hupokea Fedha za ndani na za nje kulingana na wakandarasi wanavyowasilisha madai (*certificates and invoices*). Aidha, baadhi ya miradi pia hupokea Fedha za nje moja kwa moja (*direct to Project funds*) ambazo taarifa zake huingizwa katika hesabu za Wizara mwisho wa mwaka husika wa fedha. Fedha za Maendeleo zilitolewa katika kipindi cha nusu mwaka zilihusu miradi minne (4) ambayo ni: Mradi wa Julius Nyerere MW 2,115 **Shilingi Bilioni 172.21**; kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) **Shilingi Bilioni 167.37**; Mradi wa Eyasi Wembere **Shilingi milioni 585.48**; na Mradi wa Hale **Shilingi Bilioni 7.5**.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zake ilitengewa jumla ya **Shilingi 49,466,898,200** Katika Mwaka wa Fedha 2019/20. Bajeti hii inajumuisha **Shilingi 42,427,088,000** sawa na **asilimia 85.77** ya bajeti yote kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,039,200** sawa na **asilimia 14.23** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 25,953,263,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 16,473,825,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Kwa upande wa Fedha za Maendeleo kiasi chote cha **Shilingi 7,039,810,200** ni cha fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, katika Kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba, 2019 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 20,627,989,432** sawa na **asilimia 97.2** ya makadirio ya nusu mwaka kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa katika kipindi cha nusu mwaka ni **Shilingi 20,627,989,432**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 7,724,844,832** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 12,903,144,600** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Wizara kuwasilisha taarifa zake, Taasisi zifuatazo ziliwasilisha taarifa kwenye Kamati na kujadiliwa:-

## 2.2.1 Wakala wa Nishati Vijijini ( REA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wakala wa Umeme vijijini (REA) kuhusu utekelezaji na hali ya upatikanaji wa Fedha za miradi ya umeme vijijini (REA) Katika kipindi cha nusu mwaka kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/2020, jumla ya **Shilingi Bilioni 423.10** ziliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini ili kugharamia miradi ya maendeleo na uendeshaji wa Wakala. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi Bilioni 363.10**, sawa na **asilimia 85.8** kutoka kwenye vyanzo vya ndani (Tozo ya Umeme na Mafuta) na **Shilingi Bilioni 60**, sawa na **asilimia 14.2** kutokana na michango ya Wabia wa Maendeleo.

Kulingana na Mpango wa Matumizi ya Wakala, kiasi cha **Shilingi Bilioni 405.05** sawa na **asilimia 95.7** zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi Bilioni 18.05** sawa

na **asilimia 4.3** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya usimamizi wa miradi na uendeshaji wa Wakala wa Nishati Vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2019, Wakala wa Nishati Vijijini umepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 227.45** kati ya matarajio ya **Shilingi Bilioni 211.55** ambacho ni sawa na **asilimia 108**. Kwa upande wa fedha za ndani, Wakala umepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 192.55** kati ya matarajio ya kupokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 181.55** kwa kipindi cha Julai – Disemba 2019 sawa na **asilimia 106**. Aidha, Wakala unapokea Fedha kulingana na mauzo ya mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za nje, Wakala umepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 34.89**. Aidha, Serikali ya Norway imetoa kiasi cha **Shilingi Bilioni 25.36** na **Shilingi Billion 9.5** imepokelewa kutoka Jumuiya ya Ulaya, sawa na **asilimia 116** kwa matarajio ya makusanyo ya **Shilingi Bilioni 30** kwa kipindi cha Nusu Mwaka kutoka kwa Wabia wote wa Maendeleo kwa mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2016 hadi Disemba, 2019 jumla ya **vijiji 6,623** vimepatiwa umeme na hivyo kufanya vijiji vilivyopatiwa umeme nchini kote kufikia **8,647** sawa na **asilimia 72.5**. Kutokana na miradi inayoendelea kwa sasa, **vijiji 2,172** vitapelekwa umeme hadi kufikia mwezi Juni, 2020 na hivyo kufanya vijiji vitakavyokuwa na umeme kufikia kipindi hicho kuwa **10,446** sawa na **asilimia 85.14** ya vijiji vyote nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri zinazoendelea kufanywa na Wakala wa Nishati Vijijini, Kamati ilijadili taarifa ya wakala na kubaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa Wakala huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

1) Hali isiyoridhisha ya utaratibu wa upatikanaji wa vifaa muhimu vya umeme kama Nguzo, Nyaya, Mashine umbu (*Transformers*) na viunganishi (*accessories*).

Sambamba na hilo, baadhi ya viwanda nchini havijawa na utaratibu wa aina moja au unaofanana wa utoaji wa vifaa hivyo kwa wakandarasi. Aidha, viunganishi vinavyoagizwa nje ya nchi kuchukua muda mrefu kuwasili nchini;

2) Mwamko mdogo wa wananchi katika kulipia gharama za kuunganishiwa huduma ya umeme katika baadhi ya maeneo ambayo tayari huduma ya umeme imefikishwa;

3) Mazingira magumu kwa baadhi ya maeneo ili kufika ofisi za TANESCO kulipia huduma kwa ajili ya kuunganishwa;

4) Viongozi wa maeneo ambayo miradi inatekelezwa bado hawashirikishwi ipasavyo katika kuamua wigo wa maeneo ya kutekeleza miradi;

5) Usimamizi usioridhisha kwa Wakandarasi katika baadhi ya maeneo ya utekelezaji wa Miradi hiyo.

### **2.2.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba 2019 limefanikiwa kuuza umeme wa **Shilingi Bilioni 783** sawa na **asilimia 94** ya lengo la kuuza umeme wa **Shilingi Bilioni 835**. Mauzo ya Shirika yameongezeka kwa **asilimia 3** yakilinganishwa na mauzo ya **Shilingi Bilioni 761** katika lengo la mauzo ya **Shilingi Bilioni 806** katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Mauzo haya hayajumuishi makato ya VAT 18%, EWURA 1% na REA 3%.

Aidha, katika kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Disemba 2019, Shirika limekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 963** sawa na **asilimia 87** ya lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 1,113** kutoka katika vyanzo vyake vyote vya mapato (mauzo ya umeme na vyanzo vingine). Makusanyo haya yameongezeka kwa **asilimia 2** ukilinganisha na makusanyo ya **Shilingi Bilioni 943** katika lengo la kukusanya **Shilingi Bilioni 1,049** katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Vilevile, katika kipindi cha miezi sita ya mwaka wa fedha 2019/2020, TANESCO kwa kutumia mapato yake ya ndani imelipa jumla ya **Shilingi Bilioni 947** katika kugharamia miradi inayotekelezwa na Shirika, gharama za uzalishaji na ununuzi wa umeme, matengenezo ya mitambo na miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme, kodi na tozo mbalimbali pamoja na gharama za uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Disemba, 2019 njia za usambazaji umeme msongo wa kilovoti 33 zilifikia kilomita **38,096.52**, msongo wa kilovoti 11 ulifikia kilomita **6,705.12**, na msongo wa kilovoti 0.4 ni kilomita **86,199.37** na jumla ya mashine umba (transformers) za usambazaji zimefikia **22,288**.

Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Disemba, 2019, Shirika limeweza kuunganisha wateja wapya **216,480** na hivyo kuvuka lengo la kuunganisha wateja **145,000** kwa kila nusu mwaka. Ongezeko hilo limewezesha kufikia jumla ya wateja **2,700,682** hadi kufikia Disemba, 2019 ukilinganisha na wateja **2,484,202** waliokuwepo hadi kufikia Juni, 2019 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 8.7**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Shirika kukusanya mapato juu ya malengo, na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Shirika, Wakati wa majadiliano na Kamati changamoto zifuatazo zilibainika:-

1. Mahitaji ya fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika.
2. Upotevu wa umeme kutokana na uchakavu wa mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.
3. Wizi na uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme.
4. Upotevu wa umeme kutokana na wizi wa umeme.
5. Gharama kubwa za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta hasa katika maeneo ambayo hayajaunganishwa katika gridi ya Taifa.
6. Gharama kubwa ya fidia kwa ajili ya upatikanaji wa ardhi.

### 2.2.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 imeipa TPDC jukumu la kutekeleza shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta na gesi nchini. Majukumu haya yanaenda sambamba na uwekezaji wa miundombinu wezeshi katika mnyororo wa thamani wa sekta ya mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika**, Faida zilizopatikana kutokana na ugunduzi wa gesi ni pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa umeme nchini ambapo kwa sasa **MW 892.72** za umeme zinazalishwa kwa kutumia gesi asilia ambazo ni sawa na **asilimia 57.02**

ya umeme wote unaozalishwa nchini katika Gridi ya Taifa. Vilevile, zaidi ya **MW 90** zinazalishwa nje ya gridi ya Taifa. Aidha, tangu gesi asilia ilivyoanza kutumika badala ya nishati mbadala kwa matumizi mbalimbali tangu mwaka 2004 hadi Disemba 2019, Serikali imeokoa zaidi ya Dola za Marekani **Bilioni 13,048** sawa na **Shilingi trilioni 30.225**. Shirika pia limepeleka **Shilingi Bilioni 135.41** katika Mfuko wa Mafuta na Gesi tangu mwaka 2016 na kulipa Serikalini gawio la **Shilingi Bilioni 2.5** katika mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2019 Shirika limefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 293.47** kutoka vyanzo vya ndani ikiwa ni sawa na **asilimia 75** ya lengo la makusanyo ya nusu mwaka (**Shilingi Bilioni 386.28**).

Mapato ya ndani yameongezeka kwa **asilimia 6.4** yakilinganishwa na mapato ya **Shilingi Bilioni 275.77** katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/19. Vyanzo vya mapato ya ndani ya Shirika vinajumuisha mauzo ya gesi asilia, mapato yatokanayo na shughuli za mkondo wa juu, mauzo ya condensate, gawio la uwekezaji Songas, na vyanzo vingine.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2019 limepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni 6.89** kutoka Serikalini ikiwa ni sawa na **asilimia 70** ya lengo la kupokea **Shilingi Bilioni 9.81** kwa kipindi cha nusu mwaka. Ruzuku imeongezeka kwa **asilimia 6.3** ikilinganishwa na mapato ya **Shilingi Bilioni 6.48** katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Shirika limeendelea kutumia **Shilingi Bilioni 3.44** kutoka kwa wahisani zilizopokelewa mwaka wa fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kazi nzuri inayofanywa na TPDC bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi mikubwa. Hata hivyo, Shirika limeainisha na kuanza utekezaji wa miradi ya kipaumbele ikiwemo ya usambazaji gesi viwandani na majumbani, ambayo itasaidia kupatikana kwa fedha za ndani kwa muda mfupi.

#### 2.2.4 Tume ya Madini

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2019/20 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilidhinisha jumla ya **Shilingi 13,396,281,500** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) ya Tume ya Madini. Pia, Fedha kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Tume (P.E) zilizoidhinishwa zilikuwa **Shilingi 8,008,682,391**. Hivyo, jumla ya **Shilingi 21,404,963,891** zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Recurrent budget). Vilevile, Tume ya Madini lilidhinishwa jumla ya **Shilingi 10,702,227,000** kwa ajili ya ununuzi wa magari na vifaa vya masoko.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) zilizopokelewa kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Disemba, 2019) ni **Shilingi 6,698,142,000** ikiwa ni sawa na **asilimia 100** ya lengo la kipindi husika. Aidha, kiasi cha **Shilingi 4,171,188,746** kilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (P.E) sawa na **asilimia 100** ya lengo kwa kipindi kinachorejewa.

**Mheshimiwa Spika**, Tume pia ilipokea kiasi cha **Shilingi 10,702,227,000** kwa ajili ya ununuzi wa magari 36 na vifaa vya masoko. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2019, Tume ya Madini imefanikiwa kukabidhiwa magari 32 kutoka Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) kati ya magari 36 yaliyogharimu kiasi cha **Shilingi 5,848,954,034**. Magari hayo ni mahususi kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli. Vilevile, Tume imenunua vifaa vya kijemoloji kwa ajili ya masoko ya madini.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kazi nzuri zinazotekelezwa na Tume ya Madini, zifuatazo ni baadhi ya changamoto zinazoikabili Tume ya Madini:-

1. Ufinyu wa bajeti ya Fedha za matumizi mengineyo (OC). Tume ya madini imepokea Fedha zote zilizopitishwa na Bunge kwa kipindi cha miezi sita (Julai-Disemba 2019) lakini fedha hizo hazitoshelezi. Hii ni kutokana na uwepo wa Ofisi za madini za mikoa Tanzania Bara pamoja na usimamizi wa masoko ya madini 28 na vituo vya ununuzi wa madini 25;

2. Tume ya Madini imerithi magari kutoka Wizara ya Madini na iliyokuwa TMAA hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa magari;

3. Uelewa mdogo wa Sheria ya Madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini na umma kwa ujumla na hivyo kusababisha uwepo wa migogoro na kutokulipwa kwa baadhi ya tozo.

## 2.2.5 Uendelezaji wa Jotoardhi nchini

**Mheshimiwa Spika**, rasilimali ya Jotoardhi ni moja ya vyanzo vya nishati jadidifu ambacho kinaendelezwa ili kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini. Tanzania ina uwezo wa kuzalisha umeme wa Jotoardhi usiopungua MW 5,000. Kwa sasa, lengo ni kuzalisha umeme MW 200 utokanao na Jotoardhi ifikapo mwaka 2025 kwa kuanzia na MW 30 ifikapo mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa chanzo cha kuzalisha umeme, jotoardhi kupitia miradi ya matumizi mengine (direct heat use projects) itachangia maendeleo ya sekta nyingine za uchumi kama vile uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mazao ya kilimo, ufugaji wa samaki, kuchakata mazao ya mifugo, kilimo cha maua na mboga, nyumba vitalu na utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TGDC inaendelea na utekelezaji wa miradi mitano (5) ya kipaumbele ili kufikia lengo la kuzalisha MW 200 ifikapo mwaka 2025. Miradi inayotekelezwa ipo katika maeneo ya Ngozi na Kiejo-Mbaka mkoani Mbeya, Songwe mkoani Songwe, Luhoi mkoani Pwani na Natron mkoani Arusha. Miradi hii yote ipo katika hatua ya kuchoronga visima vya utafiti ili kuhakiki rasilimali ya Jotoardhi, isipokuwa mradi wa Natron ambao upo katika hatua ya utafiti wa kina.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2019/2020 TGDC ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 14.12** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Matumizi ya kawaida (O.C na mishahara) ya Kampuni. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 9.75** ni kwa ajili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, **Shilingi Bilioni 2.25** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni 7.50** ni fedha za nje kutoka Geothermal Risk Mitigation Facility (GRMF).

Aidha, TGDC inaendelea kutekeleza kazi za mradi unaoendelea (on going Project) wa Ngozi kutoka katika bajeti ya mwaka 2018/19 ambapo **Shilingi Bilioni 20.71** zilipokelewa kati ya Fedha zilizokuwa zimetengwa. Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida, Kampuni ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 4.37** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na Mishahara. Vyanzo vya Bajeti ya Kampuni ni Serikali, TANESCO, Washirika wa Maendeleo na Vyanzo vya ndani vya TGDC.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Disemba, 2019 TGDC ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 2.05** kati ya **Shilingi Bilioni 2.45** zilizotarajia kupokelewa kutoka katika bajeti ya mwaka 2019/2020, sawa na **asilimia 88.5%**. Aidha, Shilingi **milioni**



**395.68** kutoka katika bajeti ya mwaka 2018/2019 ya mradi wa Ngozi unaoendelea (**Shilingi Bilioni 20.71**) zimelipwa kwa Mtaalam Mshauri (M/s Iceland GeoSurvey) kama malipo ya awali (*advance payment*) ya utekelezaji wa mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, kampuni ya TGDC inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

1. Leseni ya eneo la Songwe ilikuwa imetolewa kwa ajili ya uchimbaji madini;
2. Kutokuwepo kwa Sheria mahsus ya Jotoardhi nchini;
3. Kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha kutoka GRMF kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Ngozi, Kiejo-Mbaka na Natron.

## **2.2.6 Chuo cha Madini**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Madini baada ya kubaini kuwepo kwa changamoto za kitaaluma katika Chuo cha Madini iliona kuna uhitaji wa Chuo cha Madini kulelewa na Chuo Kikuu chenye uzoefu wa kufanya ulezi wa vyo vya namna hii hapa nchini.

Hivyo Wizara iliandika barua kukiomba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kukilea Chuo cha Madini ili kukiendeleza kitaaluma. Lengo la Wizara kuomba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kukilea Chuo cha Madini ni pamoja na kuongeza nafasi za udahili katika Chuo cha Madini; kukiwezesha Chuo cha Madini kuendesha programu zinazoendana na uhitaji wa soko la ajira; kuongeza ufanisi katika maeneo muhimu ya utafiti, uchapishaji; na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na Chuo cha Madini.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020, Chuo cha Madini kilidhinishwa na Serikali jumla ya **Shilingi 1,127,600,532.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo yaani *Other Charges* (OC). Hadi kufikia mwezi Disemba, 2019 Chuo kimepokea jumla ya **Shilingi 563,802,000.00** ikiwa sawa na **asilimia 50** ya bajeti yote iliyodhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hizi zimetumika kutekeleza shughuli mbalimbali kwenye Mpango wa Chuo katika kipindi cha kuanzia Julai mosi, 2019 hadi Disemba 31, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zinazokikabili Chuo cha madini ni hizi zifuatazo:

1. Upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya msingi ya Chuo kutokana na ufinyu wa bajeti;
2. Uhaba wa Wakufunzi katika fani za Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini, Sayansi za Mafuta na Gesi pamoja na masomo mtambuka;
3. Upungufu wa watumishi wa kada nyinginezo katika Kampasi ya Dodoma na Nzega kama vile watunza kumbukumbu, wakitubi, wahasibu, wahudumu wa ofisi na madereva;
4. Upungufu wa vitendea kazi kama vile vitabu, kompyuta, *printers* na *projectors*;
5. Upungufu wa vifaa vya Maabara.

## **2.2.7 Wakala wa Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo mwezi Julai, 2017 Serikali ya Tanzania ilifanya Marekebisho kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kupitia the *Witten*

Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No. 7 ya Mwaka 2017. Kufuatia Marekebisho hayo, Muundo wa GST ulifanyiwa marekebisho na ikatoka kwenye Wakala za Serikali na kuwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na majukumu yake yameainishwa katika kifungu 27A-sehemu 2(a-o). Pia, katika Marekebisho hayo majukumu mapya yaliongezeka kama vile kukusanya, kutathmini na kuhifadhi kumbukumbu zote za takwimu na taarifa kutoka kwa kampuni za utafiti na uchimbaji wa madini nchini kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu 27F (1), (2) na (3). Jukumu jingine jipya ni kufanya uchunguzi wa sampuli na kutoa matokeo ambayo yanawezesha mhusika kupata vibali vya kusafirisha sampuli nje ya nchi. Sampuli hizo ni pamoja na udongo, miamba choronge, miamba, maji na sampuli nyingine zinazohusiana na rasilimali madini kama ilivyoorodheshwa kwenye kifungu 27F (6).

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020, GST imepata fedha za matumizi kutoka katika vyanzo vikuu viwili (2) ambavyo ni Serikali Kuu na Mapato ya Ndani. Katika kipindi hicho, GST iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 5,348,747,653** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **shilingi 2,547,815,141** ni mishahara, **shilingi 2,321,322,512** ni Matumizi Mengineyo na **shilingi 479,610,000** ni maduhuli.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2019 GST ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,160,664,000.00** sawa **asilimia 100 katika kipindi cha miezi 6** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za mishahara ni **Shilingi 1,092,000,000.00** sawa na **asilimia 85.7** katika kipindi cha miezi 6 (upungufu huu unatokana kutokamilika kwa ajira mpya na baadhi ya watumishi kuhama na wengine kustaafu). Aidha, GST imekusanya kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kiasi cha **Shilingi 147,534,000.00** sawa na **asilimia 61.5** kwa miezi 6.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa taarifa ya GST changamoto zifuatazo zilibainika:-

1. Upungufu wa vitendea kazi hasa magari na vifaa vingine vya ugani na maabara;
2. Ufinyu wa bajeti ukilinganisha na majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na GST hasa baada ya kuongezewa majukumu mapya kupitia Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017;
3. Upungufu wa wataalamu wenye taaluma stahiki kama vile Wakemia, Wajiolojia, Wahandisi Jiolojia;
4. Uhitaji wa kuboresha maslahi ya wafanyakazi; na
5. Mabadiliko ya teknolojia na maendeleo makubwa ya jiosayansi Duniani yanaongeza gharama za uendeshaji wa kazi za GST.

## 2.2.8 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Madini la Taifa linamajukumu ya kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati ya utafutaji na uchimbaji madini; kuwekeza katika shughuli za uchenjaji, uongezaji thamani na uuzaji madini; kutoa huduma za kibiashara za uchorongaji miamba na utafutaji wa madini; kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na kiufundi katika Sekta ya Madini zikihusisha ushauri wa kijiolojia, kibandisi, mazingira pamoja na uandaji wa upembuzi yakinifu wa miradi ya uchimbaji au uongezaji thamani madini; na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitaalam kwa wachimbaji hao.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa Fedha 2019/2020, bajeti ya Shirika ni **Shilingi 8,080,977,399**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,195,703,907** zinatarajiwa kutoka Serikalini na **Shilingi 4,885,273,492** zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani vya Shirika.

Katika kipindi cha nusu Mwaka wa fedha 2019 /2020 (Julai – Disemba 2019) Shirika limefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,239,668,833.32** ambacho ni sawa na **asilimia 80** ya malengo ya **shilingi 4,040,489,699.50** ya bajeti katika kipindi husika. Katika makusanyo hayo fedha zilizopatikana kutoka Serikalini kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,409,344,540.00** kati ya **shilingi 1,597,852,953.50** sawa na **asilimia 88** ya makadirio ya kipindi hicho.

Fedha zilizokusanywa kutoka vyanzo vya ndani ya Shirika ni **Shilingi 1,830,324,293.32** sawa na **asilimia 74** ya makadirio ya makusanyo ya nusu mwaka ambayo ni **shilingi 2,442,636,746.00**. Mapato hayo yametokana na vyanzo mbalimbali vya Shirika ikiwemo mauzo ya makaa ya mawe, huduma za kibashara za uchorongaji, ada za pango na ada ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, **katika kuendeleza Mradi wa Ubia wa Dhahabu wa Buckreef, STAMICO iliingia mkataba wa ubia na Kampuni binafsi ya TANZAM 2000, ambayo ni Kampuni tanzu ya Tanzanian Royalty Exploration Corporation (TRX) ya Canada, mwezi Oktoba, 2011. Katika Mkataba huo STAMICO inamiliki asilimia 45 na TANZAM 2000 asilimia 55. Ubia huu unahusisha Leseni Maalum ya Uchimbaji Mkubwa (Special Mining License) Na. SML 04/92 na leseni 13 za utafutaji wa madini.**

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa Mradi una changamoto ya kuchelewa uzalishaji hali inayosababisha Shirika kukosa mapato. Hata hivyo, Tume ya Madini imemwandika mbia TANZAM2000 'default note' ikiwa ni jitahada ya kuangalia upya namna bora ya kuendeleza mradi huu kwa manufaa ya Taifa.

**Kamati inatoa Rai kwa Serikali kuwa ni vyema mkataba huu ukasitishwa kwani ni dhahiri kuwa hauna manufaa na kuna ukiukwaji mkubwa wa makubaliano ya ki mkataba hivyo Taifa linapoteza mapato ambayo yangetokana na uendelezaji wa mgodi.**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla Shirika la Madini linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

#### **1. Ufinyu wa Mtaji**

Shirika linaendelea kukabiliwa na changamoto ya ufinyu wa mtaji wa kununua vifaa na mitambo ya uchimbaji pamoja na usafirishaji wa makaa ya mawe.

#### **2. Miundombinu hafifu ya maeneo yanayozunguka migodi ya makaa ya mawe**

Barabara pamoja na miundombinu ya mgodi kuelekea mgodi wa Kiwira-Kabulo ni hafifu hivyo kuongeza gharama za uzalishaji wa makaa ya mawe. Kwa sasa Shirika linatumia barabara ya urefu wa kilomita 36. Endapo barabara inayounganisha Kiwira-Kabulo yenye urefu wa Kilometa 7 ingekamilika, gharama za usafirishaji wa makaa kutoka mgodini hadi sehemu ya kuuchakata zingepungua.

### 3. Kutokukamilika kwa Umiliki wa Hisa za Kampuni ya Makaa ya Mawe Kiwira

Mgodi wa Kiwira unakabiliwa na changamoto ya kutokukamilika kwa umiliki wa Serikali ambapo hisa asilimia 70 zinamilikiwa na Kampuni ya Tanpower Resources na asilimia 30 zinamilikiwa na Msajili wa hazina tangu ulipokabidhiwa STAMICO Mwaka 2014.

Shirika kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali inaendelea na suala la uhamishaji wa hisa na kwa sasa ufuatiliaji wa *tax clearance* kutoka TRA ili kuhamisha hisa hizo kisheria unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo hili limechukua muda mrefu sana, hivyo Kamati inaishauri Serikali kumaliza hii changamoto kwa sasa.

### 4. Madeni ya Wafanyakazi

Malipo ya wafanyakazi katika migodi mbalimbali bado ni changamoto kwa STAMICO. Mfano; mgodi wa Kiwira unakabiliwa na malimbikizo ya madeni ya kiasi cha Shilingi Bilioni 1.024 ambayo yanayohusisha stahiki na mapunjo ya watumishi ya waliokuwa wafanyakazi wa mradi wa Kiwira.

**Ni Rai ya kamati kuwa Shirika liendeele kufuatilia ulipwaji wa madeni haya ili wananchi waweze kupata stahiki zao kwakuwa Madeni haya yalishafanyiwa uhakiki na ulipwaji wake unaratibiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.**

**2.3 Sekta Ndogo ya Mafuta na hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) imeendelea kuratibu Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta nchini

(BPS) na kuhakikisha mafuta yanaingizwa nchini kwa njia ya ufanisi na kwa wakati. Aidha, kila mwezi Serikali kupitia PBPA hufanya tathmini ya mahitaji ya mafuta kwa matumizi ya nchi (*local use*) ili kujiridhisha na utoshlevu wake kabla ya kuratibu uagizaji wa mafuta kwa mwezi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kipindi chote cha Julai hadi Disemba, 2019 hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini imeendelea kuwa nzuri. Mchanganuo wa uwepo wa mafuta ni kama ifuatavyo; Mafuta (Dizeli, Petrol na Mafuta ya Ndege/Taa) yaliyoingizwa nchini kwa kipindi cha miezi sita (Julai hadi Disemba, 2019) ni jumla ya lita **3,241,658,788**.

Mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi (*local use*) ni lita **1,901,017,026** sawa na asilimia **58.6** na yanayopita nchini kwenda nchi jirani (*transit*) ni lita **1,340,641,762** sawa na asilimia **41.4**.

**Mheshimiwa Spika**, Mikataba ya uletaji mafuta kwa mwezi Januari na Februari 2020 imesainiwa kati ya Kampuni zilizoshinda zabuni za kuleta Mafuta nchini (Suppliers) na PBPA. Kiasi cha Mafuta kitakachoingizwa nchini Januari ni tani **429,700** na Februari ni tani **354,834** kiasi hicho cha Mafuta kinatosheleza mahitaji ya nchi hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2020. Vilevile, Zabuni ya Mafuta kwa ajili ya mwezi Machi itafanyika tarehe 30 Januari, 2020, kiasi cha Mafuta kitakachoshindaniwa kwenye zabuni hiyo ni tani **341,558**, Mafuta hayo yatatosheliza mahitaji ya nchi hadi mwishoni mwa mwezi Aprili. Hivyo, hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini ni nzuri wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, Gharama za Meli za Mafuta kusubiri katika bandari ya Dar es Salaam zimeendelea kupungua ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2018. Kwa SPM (*Single Point of Mooring*) ilishuka kutoka **Dola 1.7858/tani** hadi **Dola 1.6736/tani**, sawa na punguzo la **asilimia 6.28%**; na KOJ (Kurasini Oil Jetty) ilishuka kutoka **Dola 3.3474/tani** hadi **Dola 1.3510/tani** sawa na punguzo la **asilimia 59.64%**. Unafuu huu unatokana na kuendelea kuimarika kwa mfumo wa Uagizaji Mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imefanya shughuli mbalimbali za kiudhibiti kama ifuatavyo:

1. Kuendelea kupanga bei za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayosambazwa hapa nchini kwa kuzingatia mwenendo wa bei za mafuta katika soko la Dunia na kuhakikisha kuwa wakati wote nchi ina akiba ya mafuta ya kutosha angalau siku 15, kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (*Regulation 6*) ya *Petroleum General Regulations* za Mwaka 2011.

2. Kuendelea kusimamia ubora wa mafuta yanayosambazwa hapa nchini na kuhakikisha kuwa hakuna uchakachujaji na kusimamia ushindani kwa kuhakikisha mafuta ya magendo au ya kwenda nchi jirani na yaliyosamehewa kodi hayauzwi kwenye soko la ndani. Kati ya Julai na Disemba 2019, Mamlaka ilipanga kukusanya jumla ya sampuli 200 kutoka kwenye vituo vya kuuzia mafuta, maghala ya kuhifadha mafuta pamoja na mafuta yaliyokamatwa. Katika utekelezaji, jumla ya sampuli 212 za mafuta zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 106. Sampuli hizo zilipelekwa maabara ili kupima ubora wa mafuta husika. Kati ya hizo, sampuli 192 sawa na asilimia 88.21 zilikidhi viwango vya ubora. Aidha, katika kipindi hicho EWURA ilipima vinasaba kutoka kwenye vituo 269 na kati ya hivyo, vituo 259 sawa na asilimia 96.28 vilikuwa na mafuta yenye viwango sahihi vya vinasaba. Hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya wafanyabiashara waliokutwa na mafuta yasiyokidhi viwango; na

3. Kuendelea kuhamasisha uwekezaji wa vituo vya mafuta vijijini kwalo lango la kuongeza upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa wananchi walio wengi bila kuhatarisha afya, usalama na mazingira. Vigezo vya utoaji leseni vimerahisishwa na hivyo kuvutia wawekezaji kujenga vituo vyenye ubora katika maeneo hayo. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2019, jumla ya vituo 60 vya vijijini vililomba leseni kutoka EWURA. Kati ya hivyo, vituo 53 ambavyo ni sawa na asilimia 88 vimepewa leseni zenye masharti. Wamiliki wa vituo hivyo, wamepewa masharti ya kuboresha vituo vyao ili kukidhi viwango wakati wanaendelea na biashara. Aidha, vituo 7 havikupewa leseni kutokana na kutokidhi masharti muhimu ikiwemo usalama na afya.

**Ni rai ya Kamati kuwa EWURA iendeele na zoezi la kutoa leseni za masharti ambapo wafanyabiashara hao watapewa muda wa kuboresha vituo vyao ili vikidhi viwango kwa mujibu wa Sheria.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati kupitia wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA) pamoja na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa kuhakikisha hali ya upatikanaji wa mafuta nchini inakua nzuri na nchi imekuwa na akiba ya kutosha ya mafuta wakati wote.**

#### **2.4 Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la umeme nchini (TANESCO) linaendesha mfumo uliunganishwa na Gridi ya Taifa wenye mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maji, gesi asilia na mafuta. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 uwezo wa

mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulifikia **Megawati 1,565.72** ambapo **Megawati 573.70 (36.64%)** zinatokana na vyanzo vya nguvu ya maji, **Megawati 892.72 (57.02%)** ni vyanzo vya gesi asilia, **Megawati 88.80 (5.67%)** zinatokana na Mafuta na **Megawati 10.50 (0.67%)** zinalishwa kutokana na mabaki ya mimea na mazao (Biomass). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia **asilimia 86.50** na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia **asilimia 13.50**. Aidha, Shirika linamiliki mitambo ambayo haijanganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa yenye uwezo wa kufua **Megawati 36.598** na hivyo kufanya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia jumla ya **Megawati 1,602.318**. Mahitaji ya juu katika mfumo wa gridi ya Taifa yamefikia **Megawati 1,120.12** ambayo yalifikiwa tarehe **27 Novemba, 2019** ukilinganisha na **Megawati 1,116.58** zilizokuwa zimefikwa tarehe 30 Novemba, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, TANESCO inanunua umeme kutoka kwa Wazalishaji wadogo (SPPs) ndani ya nchi ambao ni Mwenga Mini Hydro Megawati 4, TPC Megawati 9, TANWAT Megawati 1.5, Yovi Megawati 0.95, Tulila Megawati 5, Darakuta Megawati 0.32, Andoya Megawati 0.5 na Matembwe Megawati 0.59. Aidha, TANESCO pia inanunua umeme toka nje ya nchi (imports) Megawati 17 toka Uganda kwa ajili ya mkoa wa Kagera, Megawati 1 kutoka Kenya kwa ajili ya Wilaya ya Longido na Megawati 5 kutoka Zambia kwa ajili ya mkoa wa Rukwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto mbalimbali zinazolikabili Shirika la Umeme nchini, hali ya upatikanaji wa umeme nchini inaendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa na Shirika la TANESCO linaendelea kujiendesha vizuri bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

## 2.5 Sekta ya Madini

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2019, Wizara ya Madini imeendelea kusimamia shughuli za uchimbaji mdogo kwa kutoa elimu juu ya Mabadiliko ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2018 katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Aidha, Wizara ilitenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuratibu utoaji wa leseni kumi na moja (11) za uchimbaji mdogo kwa vikundi kumi (10) vya wachimbaji wadogo Wilayani Nzega kwa lengo la kuwaendeleza. Vilevile, leseni 22 zilitolewa kwa vikundi 22 vya wachimbaji wadogo katika eneo la Bululu Wilayani Nyang'hwale.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ilikusudia kuanzisha masoko ya madini katika Mikoa yote inayozalisha madini nchini. Hadi kufikia Mwezi Disemba, 2019 jumla ya Masoko **28** yalikuwa yameanzishwa. Aidha, sambamba na masoko hayo, vilevile Wizara imeanzisha jumla ya vituo vya ununuzi wa madini vipatavyo **25**. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi za Mikoa inaendelea kusimamia utendaji kazi wa masoko hayo ili kuhakikisha yanafanya kazi kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Madini katika kuanzisha masoko ya madini, ni rai ya kamati kuwa masoko haya yazingatie kuendesha shughuli zake katika ubora na mazingira yanayoridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Madini imekamilisha kuandaa mfumo wa utoaji cheti cha uhalisia wa madini ya bati (ICGLR Certificate). Hatua hiyo itasaidia kukuza biashara ya madini ya bati yanayozalishwa hapa nchini na pia kudhibiti biashara haramu ya madini hayo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha nusu ya kwanza wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Madini kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama imeendelea kudhibiti utoroshaji wa madini na kufanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya **shilingi 448,833,381.16** katika maeneo ya Tunduru, Kyerwa, Mwanza, Mirerani, Holili, Babati, Hai, Dodoma, Nzega, Kahama, Dar es Salaam, Tabora na Mbeya. Wizara pia inaendelea kuhakikisha kuwa katika maeneo ya Viwanja vya Ndege, Bandari na Mipakani kunakuwa na usimamizi madhubuti kuhakikisha kuwa shughuli za madini zinakuwa na manufaa zaidi kwa Watanzania.

**Mchanganuo wa Madini yaliyokamatwa katika matukio mbalimbali ya Utoroshaji;**

NA.	AIN A	KIASI		THAMANI YA MADINI	
		GRAMU	KARATI	USD	TZS
1	Dhahabu	23,931.85	-	-	197,376,954.92
2	Vito ghafi	471,726.33	-	30,797.15	80,113,732.79
3	Bati	2,103,200.00	-	-	45,227,776.00
4	Almasi	-	61.27	-	126,114,917.45
		<b>2,598,858.18</b>	<b>61.27</b>	<b>30,797.15</b>	<b>448,833,381.16</b>

**Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kazi nzuri ya udhibiti wa utoroshwaji wa madini ni rai ya Kamati kuwa, wakati wa kutekeleza wajibu wake, vyombo vya ulinzi na usalama vihakikishe vinatenda haki kwa kukamata wahusika wanaostahili ili kuepusha kesi za kubambikizwa kwa watu wasio na hatia.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza sekta ya Madini nchini, Kamati inapenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa **Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli** kwa kazi anayofanya katika kuimarisha utendaji wa Sekta ya Madini hivyo kuleta chachu kubwa ya uwekezaji katika rasilimali madini na hatimaye kuifanya Sekta kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupata suluhu ya mkwamo wa kiuwekezaji na hivyo kuanzisha ubia na Kampuni ya Barrick. Ubia huu utaiwezesha Serikali kuwa na ushiriki katika maamuzi ya shughuli za uendeshaji wa migodi ya North Mara, Bulyanhulu na Buzwagi. Hali ambayo inaiwezesha Tanzania kama nchi kunufaika na rasimali ya madini yetu. Aidha, Makubaliano hayo pia yanaidhinisha uundwaji wa Shirika la Twiga Minerals linalomilikiwa na Barrick (84%) na Serikali (16%). Shirika litakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za Barrick nchini. Ni matarajio yetu kuwa Serikali imelenga kuongeza manufaa zaidi ya kiuchumi katika mpango huu.

### 2.6 Sekta Ndogo ya Gesi

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ilianza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi takribani miaka sitini (60) iliyopita. Kwa kipindi chote hicho, kampuni mbalimbali za kimataifa zimeendelea na utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali ya miamba tabaka nchini ikiwamo nchi kavu na baharini. Mpaka sasa kiasi cha gesi asilia kilichogundulika ni Futi za **Ujazo Trilioni 57.54.**

Kufikia Januari 2020, mikataba hai ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia iliyopo nchini ni kumi na mbili (12) ambayo inatekelezwa na kampuni za kimataifa nane (8).

Mikataba mitatu (3) kati ya hiyo ipo katika hatua za uzalishaji ambayo ni Songo Songo, Mnazi Bay na Kiliwani North; mikataba tisa (9) iko katika hatua ya utafutaji ambayo ni Kitalu Na. 1 na 2, Kitalu Na. 4, Ruvuma, Ruvu, Tanga, Rukwa, Kilosa-Kilombero, Bigwa Rufiji Mafia na Nyuni.

**Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Nishati, leseni 8 za utafutaji na uendelezaji wa gesi hapa nchini zimemaliza muda wake wa matumizi na kwamba mchakato wa uhuishwaji wa leseni hizo umechukua muda mrefu.**

**Mheshimiwa Spika,** kamati imebaini kuwa kutohuishwa kwa leseni hizi kumetokana na sababu za msingi ikiwemo kusubiri kukamilika kwa kazi ya mapitio ya mikataba ya utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi asilia (PSAs) yanayolenga kuhakikisha kuwa Serikali inanufaika ipasavyo kupitia mikataba hiyo. Pamoja na ukweli huo, athari zifuatazo zinazoweza kutokea iwapo mchakato wa kuhuisha leseni hizo utachukua muda mrefu:

### **1. Kupungua kwa Shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa PSA zilizopo, kila upande unaweza kutekeleza haki na wajibu wake ikiwa Serikali itatoa leseni za utafutaji na uendelezaji kwa TPDC. Aidha, pale ambapo muda wa leseni unakuwa umekwisha na taratibu za kuhuisha leseni hizo unacendelea, Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 inatoa fursa kwa wawekezaji kuendelea na shughuli baada ya kupewa comfort letter na Serikali ali mradi maombi hayo yalikiidhi vigezo vya kisheria. Hata hivyo, kufuatia mkwamo wa uhuishaji wa leseni hizo kwa sasa, imebainika kuwa baadhi ya Bodi za Wakurugenzi za Kampuni ambazo zinasubiri kuhuishwa kwa leseni baada ya leseni za awali kwisha muda wake zimeonesha kutokuwa tayari kutoa Fedha za uwekezaji. Mfano kampuni za Swala Oil and Gas Tanzania, Ndovu Resources, Shell na Equinor. Hii inatokana na wakandarasi kuwa na wasiwasi wa hatma ya maamuzi ya maombi yao ya leseni.

### **2. Kusudio la Force Majeure**

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya wawekezaji wameainisha uamuzi wa kutohuishwa leseni za utafutaji kuwa ni moja kati ya sababu zinazoweza kutafsiriwa kuwa janga (Force Majeure Event). Baadhi ya wakandarasi, kama vile Swala Oil and Gas Tanzania wameipa Serikali na TPDC notisi kuhusisha uhuishaji wa leseni na matukio ya majanga kwa mujibu wa PSA.

### **3. Ushindani katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia**

**Mheshimiwa Spika,** Uwekezaji katika Sekta hii unahitaji mtaji mkubwa, ambapo Serikali nyingi duniani hushirikisha sekta binafsi kwenye utafutaji na uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia. Tanzania inashindana kuvutia uwekezaji na nchi mbalimbali za Afrika kama vile Kenya, Uganda, Angola, Ghana, Mozambique na Nigeria pamoja na nchi za bara la Asia kama vile Qatar, Oman, Trinidad & Tobago na Papua New Guinea. Maamuzi ya Serikali yana mchango mkubwa katika kuvutia au kutokuvutia wawekezaji. Ikiwa Serikali haitahuisha leseni tajwa katika muda muafaka, kunaweza kuwepo athari za kupunguza uwekezaji kwa muda katika Sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa kuhuisha leseni husika kwa wakati, madhara



makubwa zaidi yanaweza kutokea endapo leseni hizo zitahuishwa bila kufanyika uchambuzi wa kina na wa kutosha katika mikataba (PSAs) iliyopo, umakini mkubwa unahitajika katika zoezi hili la mapitio ya mikataba.

Ni matumaini ya Kamati kuwa kazi ya kupitia mikataba (PSAs) itakapokamilika itawezesha Serikali na Taifa kwa ujumla kunufaika ipasavyo na rasilimali ya gesi asilia. **Aidha, ushauri wetu ni kwamba mapitio hayo ya mikataba yanayoendelea kufanywa na Timu ya Serikali kupitia Ofisi ya MwanaSheria Mkuu wa Serikali yakamilishwe haraka lakini bila kuathiri umakini unaohitajika kwa ajili ya kupata matokeo yanayolenga kunufaisha pande zote mbili.**

## 2.7 Uwekezaji katika Mradi wa Liganga na Mchuchuma

**Mheshimiwa Spika**, miradi ya Madini ya Chuma na Makaa ya Mawe ya Liganga na Mchuchuma ni miradi inayoendelezwa kwa pamoja (*Intergrated Projects*) na Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL). Kampuni ya TCIMRL ni Kampuni ya ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) lenye **asilimia 20** ya hisa na Kampuni ya Sichuan Hongda (Group) Company Limited ya China yenye hisa **asilimia 80**. Miradi hiyo ipo katika Wilaya ya Ludewa, Mkoani Njombe. Eneo la Liganga kuna madini ya Chuma yenye Mashapo yapatayo tani 126 milioni. Aidha, Katika eneo la Mchuchuma, kuna jumla ya tani 428 milioni za Makaa ya Mawe.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 15/01/2014, Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL) iliwalisisha maombi ya leseni ya uchimbaji mkubwa wa Madini (*Special Mining Licence*) katika maeneo ya Mundindi - Liganga na Mchuchuma yaliyoko Wilayani Ludewa Mkoani Njombe. Tarehe 09/10/2014, leseni zilitolewa kwa mradi huu, ambazo ni SML 533/2014 katika eneo la liganga lenye ukubwa wa **kilomita za mraba 30.41**; na SML 534/2014 katika eneo la Mchuchuma lenye ukubwa wa **kilomita za mraba 25.46**. Leseni hizo zilitolewa kwa kipindi cha miaka 25 na zitafikia ukomo tarehe 08/10/2039.

**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji unaotarajiwa kufanywa na Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Limited ni pamoja na ujenzi wa migodi katika maeneo ya Liganga na Mchuchuma, ujenzi wa kiwanda cha chuma cha Liganga, utandazaji nyaya za umeme kati ya Liganga na Mchuchuma na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha shughuli za migodi hiyo.

**Hata hivyo, pamoja na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali pamoja na Bunge ili mradi huo uweze kutekelezwa, imebainika kuwa Kampuni hiyo imekiuka kifungu cha 47 cha Sheria ya Madini Sura 123 kwa kushindwa kuanza kufanya shughuli za uchimbaji wa madini katika kipindi cha miezi 18 kama Sheria inavyoelekeza.**

Kutokana na ukiukwaji huo wa Sheria tarehe 09/04/2019 Wizara imeitaarifu Kamati kuwa Kampuni hiyo iliandikiwa hati ya Makosa na Tume ya Madini. Aidha, katika utetezi wao mwekezaji ameanisha sababu kubwa ya kushindwa kuanza shughuli za uchimbaji ni kutokana na Serikali kuchelewa kumpatia vivutio vya uwekezaji (*incentives*); vivutio ambavyo hata hivyo vinakinzana na Sheria ya nchi. Wakati hali ikiwa hivyo, Shirika la NDC ambalo ni mbia mweza katika mradi huo nalo limeonesha kutoridhishwa na mkataba na makubaliano waliyokubaliana na mwekezaji huyo kwa kuwa yanaonekana kutokuwa na masilahi kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali kwa kutumia Wizara zinazohusika ziongeze kasi ya kushughulikia suala hili ili ufumbuzi wa haraka upatikane na nchi iweze kunufaika na rasilimali hii. Kuchelewa kufanya maamuzi kunalinyima Taifa fursa nyingi za kiuchumi na kijamii.**

### SEHEMU YA TATU

#### 3.1 MAONI NA MAPENDEKEZO

#### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja na kukutana na Wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni yafuatayo;

1. Upo umuhimu wa Serikali kufuatilia kwa makini mchakato mzima wa zabuni za upatikanaji wa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA kwani kuna baadhi ya wakandarasi wanaonekana hawana uwezo wa kutosha kutekeleza kazi hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi hii kwa wakati;

2. Serikali iendeele kusimamia kwa karibu uzalishaji wa viwanda vyetu na utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya kutekeleza miradi ya REA kwasababu vipo viashiria vinavyoonyesha kuwa viwanda vya ndani vinazalisha chini ya uwezo. Aidha, utaratibu wa wakandarasi kutoa oda za vifaa unapaswa kufuatiliwa ili wasiagize vifaa kwa baadhi ya kampuni na kuacha nyingine, hii itasaidia kupunguza foleni ya upatikanaji wa vifaa katika makampuni machache ya uzalishaji hivyo kutoathiri upatikanaji wa vifaa kwa wakati;

3. Wizara ya Nishati inapaswa kuendelea kufanya tathmini na uhakiki wa miradi ya ujazilizi ili maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya umeme yaweze kufikiwa na wateja waweze kuunganishwa na huduma ya umeme;

4. Serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya wakandarasi wanao suasua katika kutekeleza miradi ya REA;

5. Kasi ya uunganishaji wateja kwenye huduma ya umeme kwenye maeneo ambayo miradi ya REA imekamili bado ipo katika kiwango cha chini, hivyo Serikali kupitia TANESCO wanapaswa kuongeza kasi ya uunganishwaji wa wateja wa huduma ya umeme kwasababu Serikali imewekeza na kutumia gharama kubwa katika miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini;

6. Mchakato wa kuwapata wawekezaji binafsi wa kuzalisha umeme kwa kutumia rasilimali tulizonazo kama Jua, Upepo na Makaa ya Mawe umechukua muda mrefu mno. Hivyo ipo haja Serikali ikaangalia kwa makini mchakato unaoendelea kwa kupunguza urasimu katika mchakato huo ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali tulizonazo katika kuzalisha umeme;

7. Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI zinapaswa kuchukua hatua za haraka katika kuhakikisha zinamaliza changamoto za utengenezaji wa barabara katika mradi wa Kiwira-Kabulo kwakuwa kutotengenezwa kwa barabara hii kunaliingizia hasara Taifa kutokana na uzalishaji wa makaa ya mawe katika

mgodi huo kufanyika kwa gharama kubwa;

8. Serikali kama wataona inafaa ni vyema wakavunja mkataba na kampuni ya TANZAM 2000 katika kuendeleza mgodi wa BUCKREEF kwani masharti hasi yako mengi na mbia mwenza amevunja masharti mengi mfano ununuzi wa mtambo bila STAMICO kushirikishwa pamoja na kutokuendeleza mgodi hadi sasa;

9. Ni rai ya Kamati kuwa katika maeneo ambayo STAMICO inashindwa kuendeleza uzalishaji ni afadhali maeneo hayo yakagawiwa kwa wachimbaji wadogo ili Serikali iendelee kukusanya mapato.

#### 2.4 Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuainisha maoni ya jumla ya Kamati kuhusu masuala ya msingi yaliobainika katika Sekta ya Nishati na Madini kwa ujumla wake, naomba kutoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

##### 3.2.1 Wakala wa Nishati vijijini (REA)

###### a) Hali ya Upatikanaji wa Vifaa vya kutekeleza miradi ya REA

**KWA KUWA** Serikali iliazimia vifaa vinavyotumika kutekeleza miradi hii vitengenezwe hapa nchini,

**NA KWA KUWA**, imebainika kuwa wakandarasi huweka oda za vifaa kwa kampuni chache na kuacha kampuni nyingine hivyo kusababisha foleni ya kusubirii vifaa kwa muda mrefu hali ambayo inaathiri utekelezaji wa miradi ya REA;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu madhubuti wa ufuatiliaji ili kuhakikisha vifaa vya kutekeleza miradi hii vinapatikana kwa wakati na vikiwa na ubora stahiki ili miradi iweze kutekelezwa na kuendana na mpango wa utekelezaji wa kumaliza miradi hii.

###### b) Wigo wa kutekeleza miradi

**KWA KUWA**, maneno mengi ya Vitongoji yanarukwa wakati wa usambazaji wa umeme;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababishwa na wakandarasi kupewa wigo mdogo wa maeneo ya kutekeleza mradi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuhakikisha inawashirikisha kwa kiasi kikubwa Viongozi wa wananchi katika uainishaji wa maeneo ya kupelekewa umeme ili maeneo muhimu ya kijamii na kiuchumi yapewe kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya REA.

##### 3.2.2 Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC)

###### a) Hali ya upatikanaji wa Fedha

**KWAKUWA**, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) linakabiliwa na changamoto ya Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi mikubwa.

**NA KWAKUWA,** Shirika limeainisha na kuanza utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ikiwemo ya usambazaji gesi viwandani na majumbani ambayo itasaidia kupatikana kwa Fedha za ndani kwa muda mfupi.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kupeleka Fedha za maendeleo kwa wakati. Aidha, TPDC inapaswa kuendelea kutekeleza miradi michache yenye manufaa na ikibidi ipewe kibali cha kukopa mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za fedha au kuingia ubia na sekta binafsi ili kuweza kupata fedha za kutekeleza miradi mikubwa.

### **b)Uendelezaji wa Miradi ya Liquefied Natural Gas (LNG)**

**KWA KUWA,** Serikali iliamua kutwaa ardhi ya wananchi wa Lindi ili itumike kujenga miundombinu muhimu ya kuchakata Gesi kwa makubaliano ya kuwapatia fidia;

**NA KWAKUWA** tathmini ya awali ya fidia ya ardhi husika ilifanyika mwaka 2015 na kurejewa tena mwaka 2017 na kisha Wizara ya Fedha na Mipango kufanya uhakiki wa fidia hizo mnamo mwezi wa Septemba 2019; na Bunge kwa kutambua haki ya wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa kwa miaka mingi bila ya kupewa fidia yoyote ili dhinisha takriban Shilingi Bilioni 7 katika bajeti ya mwaka 2019/2020 ili Fedha hizo zitumike kuwalipa fidia wananchi;

**KWA HIYO BASI** Bunge linaishauri Serikali kuwa kabla ya mwaka wa Fedha 2019/2020 kumalizika iwalipe stahili zao kikamilifu wananchi wote wanaodai fidia kutokana na ardhi yao kutwaliwa ili kupisha mradi.

### **c)Mapitio ya Mikataba ya Gesi Asilia (PSA's)**

**KWAKUWA** PSA zipatazo 8 kati ya 12 zilizo leseni zake zimeisha muda wake na hivyo wawekezaji kusita kuendelea na shughuli za utafiti na uwekezaji mitaji katika sekta ya gesi,

**NA KWAKUWA** utolewaji wa leseni hizi unapaswa kusubiri kukamilika kwa mapitio ya mikataba iliyopo kutokana na mikataba hiyo kuonekana kuikosha nchi mapato stahiki kwa mujibu wa Sheria zilizo sasa na kwakuzingatia ukweli kuwa zoezi la mapitio ya mikataba limechukua muda mrefu kukamilika tangu mwaka 2017 Bunge lilipoishauri Serikali kufanya mapitio; na kwamba kwasasa majadiliano ya HGA yamesimama kusubiri hatma ya mapitio ya mikataba ambayo yatajenga msingi wa majadiliano ya mradi wa LNG;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kuchukua hatua mahsusi zitakazowezesha zoezi la mapitio ya mikataba kukamilika ndani ya kipindi kifupi ili kuwezesha mchakato wa majadiliano ya mradi wa LNG kuendelea na hatimaye uwekezaji uweze kufanyika.

### **3.2.3 Uendelezaji wa Rasimali Jotoardhi Nchini (TGDC)**

**KWAKUWA,** Nchi yetu haina Sheria mahsusi ya Jotoardhi.

**NA KWAKUWA,** kukosekana kwa Sheria mahsusi kunakwamisha uwekezaji na uendelezaji wa rasimali ya jotoardhi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kumalizia mchakato wa uandaaji wa Rasimu ya Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Jotoardhi ili kuwasilishwa Bungeni kwajili

ya utungaji wa Sheria mahsusi ya Jotoardhi nchini.

### 3.2.4 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

**KWAKUWA**, Shirika linakabiliwa na changamoto ya upotevu wa umeme na uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme kunakosababishwa na vitendo vya wizi na hujuma;

**NA KWA KUWA**, changamoto hizi zinasababisha hasara kubwa kwa Shirika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuiwezesha TANESCO ili iweze kutumia teknolojia za kisasa katika kukabiliana na changamoto zilizopo. Aidha, Shirika liimarisha doria katika njia za umeme na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme kupitia mikataba na wananchi katika maeneo mbalimbali.

### 3.2.5 Chuo cha Madini (MRI)

**KWA KUWA**, Chuo cha Madini kinakabiliwa na changamoto ya Upungufu wa Fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya msingi ya Chuo kutokana na bajeti finyu;

**NA KWAKUWA**, Chuo pia kina upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali katika Kampasi ya Dodoma na Nzega kama vile watunza kumbukumbu, wakutubi, wahasibu na wakufunzi katika fani za Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini, Sayansi za Mafuta na Gesi pamoja na masomo mtambuka;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kukiongezea Chuo fedha ili kuwezesha shughuli za utoaji mafunzo ikiwa ni pamoja na mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi migodini, kununua vitendea kazi pamoja na kuajiri watumishi katika kada mbalimbali.

### 3.2.6 Taasisi ya Jiolojia na Utafiti (GST)

**KWA KUWA**, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vitendea kazi hasa magari na vifaa vingine vya ugani na maabara;

**NA KWAKUWA**, GST pia inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ukilinganisha na majukumu inayopaswa kuyatekeleza hasa baada ya kuongezewa majukumu mapya kupitia Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kufanikisha malengo yaliyowekwa na GST ikiwemo kupeleka Fedha kwa Taasisi hii ili iweze kujijendesha na kununua vifaa vya kutekeleza kazi zilizopangwa.

Aidha, Serikali iendeleo kuwezesha watumishi wa GST kupata mafunzo zaidi ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi ili kuwa na wataalam wa kutosha kutekeleza majukumu ya Taasisi hii.

### 3.2.7 Tume ya Madini

#### a) Uelewa Mdogo wa Sheria ya Madini kwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa Madini

**KWA KUWA**, kumekuwepo na changamoto ya uelewa mdogo wa Sheria ya Madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini na umma kwa ujumla;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo imesababisha uwepo wa migogoro na kutokulipwa kwa baadhi ya tozo kwa Serikali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuendelea kuipatia Tume ya Madini fedha za kutosha ili iweze kutoa elimu ya Sheria ya Madini pamoja na kuendesha mafunzo ya mara kwa mara katika maeneo ya wachimbaji wadogo na viongozi wa Serikali za Mitaa kwa lengo la kujenga uelewa wa Sheria hiyo na kupunguza migogoro baina ya wachimbaji;

#### b) Vitendea kazi na ofisi kwa ajili ya Makao Makuu ya Tume na baadhi ya Ofisi za Afisa Madini Wakazi (RMOs).

**KWA KUWA**, Tume ya Madini inakabiliwa na changamoto ya Vitendea Kazi,

**NA KWAKUWA**, uhaba huo unatokana na Tume ya Madini kuwa na ufinyu wa bajeti ya fedha za matumizi mengineyo (OC) ambazo fedha hizo hazitoshelezi hali ambayo imechangiwa na kupanuka kwa shughuli za Tume ya Madini ikiwemo uwepo wa Ofisi za madini za mikoa Tanzania Bara, usimamizi wa masoko ya Madini 28 yaliyoanzishwa kote nchini; na vituo vya ununuzi wa Madini vipatavyo 25;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Tume ya Madini kwa kuongeza wigo wa ukomo wa Bajeti kwa Tume ya Madini. Hii itasaidia Tume ya Madini kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuongeza mapato ya Serikali.

## SEHEMU YA NNE

### 4.1 HITIMISHO

### 4.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhafi kwako wewe mwenyewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika, Dkt. Tulia Akson (Mb) Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

- |   |   |                     |
|---|---|---------------------|
| 1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb      | - | <b>Mwenyekiti</b>   |
| 2. Mhe. Mariam Di topile Mzuzuri, Mb    | - | <b>M/Mwenyekiti</b> |
| 3. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb         | - | Mjumbe              |
| 4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb  | - | Mjumbe              |
| 5. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb   | - | Mjumbe              |
| 6. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb        | - | Mjumbe              |
| 7. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb | - | Mjumbe              |

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

8. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb	-	Mjumbe
9. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb	-	Mjumbe
10. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb	-	Mjumbe
11. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb	-	Mjumbe
12. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb	-	Mjumbe
13. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb	-	Mjumbe
14. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb	-	Mjumbe
15. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb	-	Mjumbe
16. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb	-	Mjumbe
17. Mhe. John Wegesa Heche, Mb	-	Mjumbe
18. Mhe. Yosepher Ferdinand Komba, Mb	-	Mjumbe
19. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb	-	Mjumbe
20. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb	-	Mjumbe
21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb	-	Mjumbe
22. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb	-	Mjumbe
23. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb	-	Mjumbe
24. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb	-	Mjumbe
25. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb	-	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, pia Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati chini ya uongozi wa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemari (Mb), Naibu Waziri Mhe. Subira Khamis Mgalu (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Hamisi Mwinyimvua (ambaye amemaliza muda wake wa utumishi kwa sasa) pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa ujumla wao. Aidha, Kamati inaipongeza pia Wizara ya Madini chini ya uongozi wa Mhe. Doto Mashaka Biteko (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Katibu Mkuu Prof. Simon Msanjila pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano waliutoa katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hivyo kuwezesha Kamati yako kutekeleza majukumu yake kwa ufansi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake na Kamati yetu. Pia namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi msaidizi Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Angelina Sanga pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

### 4.3 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

05 Februari, 2020

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kusoma maoni ya Kamati yako na kuweza kuiwasilisha vizuri kama ulivyofanya. Ahsante sana Kamati ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Sasa tunaingia kwenye eneo la uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele Manyanda. Mheshimiwa Maige tuanzishie.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa mtu wa kwanza kabisa kuchangia Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Februari, 2019 mpaka Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, acha nijikite kwenye Wizara zote tatu kwenye mambo muhimu ambayo nilifikiri kwamba yanahitaji kusukumwa ili kuleta ufanisi katika Wizara hizo. Naomba nianze na Wizara ya Mambo ya Ndani na nianze na kipengele kile cha Sekta ya Ulinzi Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Makampuni ya Ulinzi Binafsi yalianza hapa nchini mwaka 1980 yakiwa na makampuni mawili tu; *Ultimate Security* na *Group Four*. Makampuni hayo yamezidi, leo hii yako 2,000 na zaidi, yakiajiri askari walinzi wanaozidi 200,000, karibu 250,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sekta hii ilianza miaka 40 iliyopita na haina sheria yoyote, haina miongozo yoyote, haina kanuni yoyote, wala ilipoanzishwa haikuwa hata na GN. Kwa hiyo, ilianzishwa tu na matakwa ya aliyekuwa IGP Philemon Mgaya kutokana na ombwe la kuhitaji ulinzi baada ya Serikali kubadilisha Sera ya Mali kutoka mali za Serikali na kuwa mali za watu binafsi zilizokuwa zimetaifishwa wakati ule na mashirika mapya yaliyoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa muda wa miaka yote hii makampuni haya yaliyoanzishwa kwa kanuni kwamba walioanzisha walikuwa ni Askari wastaafu wakiwa na miaka 60 na leo kama bado wapo wana miaka 100; kwa hiyo, makampuni haya yameendeshwa kwa kurithiana.

Mheshimiwa Spika, waliorithi makampuni haya huenda hawana hata ujuzi kabisa wa Sekta ya Ulinzi Binafsi, kwa hiyo, wanakamata silaha, wana bunduki, na kadhalika, lakini vibali vilivyokuwa vinatoka havikuwa na kanuni yoyote ya kusema kampuni, mwenye kampuni, mradi yeye alikuwa Askari. Bahati mbaya walipofariki, wamerithi watoto, wamerithi wake zao na ndugu wengine ambao hawana taaluma ya ulinzi. Kwa hiyo, uko umuhimu sasa wa kuanzisha au Bunge lako litunge sheria ya sekta ya ulinzi binafsi.

Mheshimiwa Spika, nilifanya juhudi kubwa ya kuleta Sheria ya sekta ya Ulinzi Binafsi hapa Bungeni; nikaleta Ofisini kwako na baadaye Serikali wakaichukua wakasema wangeileta hapa Bungeni kwa sababu ni muhimu sana na imetokea hivi karibuni mali nyingi za binafsi na miradi inahitaji ulinzi na makampuni yamejimarisha kuleta wataalam wengine kutoka nje wenye uwezo mkubwa, makomandoo, wengine wakiwa ni Askari wenye *rank* za juu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri makampuni yameanzishwa na wataalam waliokuwepo wakati ule, ma-IGP wote waliostaafu wameanzisha makampuni ya ulinzi, viongozi wengi wa majeshi wameanzisha kampuni za ulinzi, lakini hakuna sheria ya kuya-control makampuni haya jinsi ya kujiendesha.



Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri na Kamati ilishauri kwamba sasa umefika wakati Serikali ilete sheria ile ambayo inashikilia mpaka sasa. Kwa hiyo, nategemea Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa ajaribu kutueleza sheria hii muhimu ya Sekta ya Ulinzi Binafsi inakuja lini Bungeni ili tuweze kuipitisha na baadaye itumike kwa ajili ya kuyaongoza makampuni? Hatuwezi kuyafukuza makampuni ya ulinzi, hatuwezi kuifunga Sekta ya Ulinzi Binafsi, ila tunaweza kui-control kwa kutumia sheria.

Mheshimiwa Spika, liko suala la NIDA. Katika Wizara ya Mambo ya Ndani, Taasisi ya NIDA imepewa jukumu la kugawa vitambulisho katika nchi yetu kwa wananchi wote nchini, lakini nasikitika sana NIDA imekuwa tatizo kubwa sana ambalo ni kichomi ambacho kimeshindwa kutatuliwa. Serikali imesaidia sana kuwapa fedha, lakini hatuelewi!

Mheshimiwa Spika, NIDA au Kitambulisho cha Taifa vijijini, nafikiri mpaka tutazeeka, tutaondoka wananchi wa Tanzania nzima hawatapata vitambulisho kwa sababu, hakuna msimamo au mkakati maalum wa kwenda vijijini kama ambavyo daftari la kupiga kura limeenda. Wananchi wote wanaotaka kupiga kura wamepata kadi za kupigia kura.

Mheshimiwa Spika, ulikuwa ni mpango mzuri wa NEC uliofanyika kufika vijijini. NIDA kijijini kwangu katika Jimbo langu sijawaona, hawajaenda, lakini wameenda sehemu ndogo tu, yaani sehemu za miji, basi. Hili limekuwa tatizo kubwa, limejitokeza hata wakati wa kusajili simu kwa vidole ambapo ilikuwa ni lazima NIDA uwenayo, imeonesha ni kiasi gani tatizo ni kubwa. Tusingejua kama tatizo ni kubwa kama kusingekuwa na kusajili line za simu. Kwa hiyo, nashauri na Kamati yetu imeshauri kwamba NIDA waje na mkakati mpya wa kufikia sehemu zote za vijiji.

Mheshimiwa Spika, liko suala lingine la wakimbizi. Wakimbizi kwa uungwana wetu Serikali iliwapa uraia, lakini bahati mbaya sana ikawaacha kwenye makambi yale yale waliyopatia uraia na wameanza kujiunda na kuunda na kuelewana wenyewe kwa wenyewe na wana mpango hata wa kuwa na Serikali yao ndani ya eneo lile walilomo; na kumekuwa na utata mkubwa sana, wakimbizi hawa sasa wanaishi kama raia wa Tanzania wa kawaida na wanasoma sana, wanajiingiza kwenye sehemu nyingine za kazi, sehemu za majeshi na sehemu za elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, tatizo linaonekana kwamba kwa vile wanakaa pamoja pale pale, mkakati wa kuwasambaza wakimbizi hawa ni suala la muhimu sasa ili wasije wakakaa na kuunda mkakati ambao utakuja kuleta hasara kwenye Serikali yetu na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye shughuli za kazi za Wizara ya Mambo ya Nje tuliongelea mambo ya mipaka yetu na tuligusa mpaka wa Uganda ambako kumekuwa na utata wa nyuzi ngapi mpaka wa Tanzania unapita, lakini pia suala la mpaka wa Malawi, iko haja sasa Wizara ya Mambo ya Nje ione umuhimu wa kuweka mipaka katika maeneo ambayo tunafikiri kwamba yana utata katika Ziwa Nyasa na kule Uganda.

Mheshimiwa Spika, mwishoni nitoe shukrani kubwa, sikupata nafasi ya kuongea wakati wa sekta hizi nyingine. Nitoe shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Joseph John Pombe Magufuli pamoja na Serikali yake ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo imeleta maendeleo makubwa katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu tumepata Kituo cha Afya kimoja kwa gharama ya shilingi milioni 850; pia, tumepata Hospitali ya Wilaya kwa shilingi bilioni mbili. Vile vile tumepata mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria ambao utakuwa kwenye vijiji 40, kwenye 500 vijiji 80. Pia mradi wa REA una vijiji 18 katika vijiji vile 82. Tunaomba basi tuongezewe idadi ya vijiji ambavyo vitapata umeme wa REA.

Mheshimiwa Spika, pia tumepata mradi wa Kituo cha VETA kwa shilingi bilioni tano na sasa hivi kuna mpango wa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi ambayo itagharimu mabilioni mengi. Yote haya kwa kweli yamekuwa njozi tulikuwa tunaota, lakini kwa kipindi cha miaka minne Mheshimiwa Rais ametuletea mambo haya yote. Wananchi wangu wanafurahi sana, wanamshukuru sana na wanamwomba maisha marefu Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Mheshimiwa Manyanda Masele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika hizi hotuba za Wenyeviti wetu wawili wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, nianze na hotuba ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Hotuba hii imeeleza vizuri kazi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanyika kwa Wizara mbili ambazo tunazisimamia, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote duniani ambayo imeendelea kiuchumi ina tabia ya kuwa na vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo ni imara. Kwa maana hiyo tunapotaka kujenga Tanzania ya Viwanda, ni muhimu pia kuwa na vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo pia vimewekeza katika masuala mtambuka ya silaha za kivita zikiwemo ndege, meli, mizinga na vitu vingine vyote ambavyo vinahusiana na habari ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, naishauri Serikali iendelee kuvipatia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama bajeti inayostahili ili kusudi mashirika yetu ya Nyumbu na Mzinga yaweze kuwekeza zaidi katika miundombinu ya uboreshaji silaha na nyenzo za kivita ili kuweza kulihami Taifa letu ambalo lina rasilimali nyingi ambazo Mwenyezi Mungu ametujalia kuwanazo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kutokana na utajiri wa nchi yetu ulivyo mkubwa nina uhakika kwamba tunao maadui wa kutosha kutoka nje na ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, tusipokuwa na vyombo madhubuti tunaweza tukajikuta ujenzi wa uchumi wetu ukawa sasa unapata pingamizi mbalimbali. Kwa maana hiyo, naishauri tu Serikali iwekeze vyakutosha katika vyombo hivi.

Mheshimiwa Spika, pia nalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuendelea na kuwa na mpango madhubuti wa kuweza kuwachukua vijana wetu na kuwajengea uzalendo katika makambi mbalimbali na pia Shirika letu la SUMA kwa kazi nzuri ambazo imekuwa ikizifanya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza JKT kwa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uzio wa Mererani na kazi nyingine ambazo Jeshi letu hili limekuwa likizifanya. Naiomba tu kwamba Serikali iendelee kuiunga mkono inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya ulinzi wa rai na mali zao na kwa vyovyote vile tunashukuru kwa sababu matukio ya uhalifu yamepungua katika nchi yetu. Kwa hiyo, naomba tu kwamba vyombo vyetu hivi vya ulinzi na usalama viendelee

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuungwa mkono kwa kupewa pesa kwa ajili ya kujenga nyumba za maaskari wetu na kwa maana hiyo tuweze kuwarahisisha maisha Askari wetu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza limekuwa ni chombo madhubuti ambacho kimekuwa kikisaidia kuwarekebisha Watanzania wanaokuwa na matatizo ya kiuhalifu. Kwa maana hiyo, naomba tu Serikali iendelee kulisaidia jeshi hili katika kuhakikisha kwamba msongamano katika Magereza unapungua na ikiwezekana Serikali itoe pesa zaidi kuweza kujenga Magereza mengi zaidi ili kuweza kuwapa nafasi watu hawa, pamoja na kwamba ni wavunjifu wa sheria na wakosaji, lakini ni muhimu wakapatiwa matunzo mazuri wanapokuwa katika kipindi chao cha kutumikia adhabu zao.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa na zoezi la kuwapatia raia wa nchi hii vitambulisho vya Taifa. Zoezi hili linafanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), lakini tumeshuhudia katika siku za karibuni kwamba mamlaka hii imekuwa na changamoto kubwa ya kushindwa ku-cope na mahitaji ya Watanzania. Watanzania walio wengi hawajapata vitambulisho hivyo. Tatizo kubwa linaonekana ni fedha. Kwa hiyo, naiomba tu Serikali isaidie mamlaka hii ili iweze kusaidia kutoa vitambulisho vya kutosha na wananchi wetu waweze kutambulika kama raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Naipongeza Wizara hii kwa sababu imekuwa ni kiunganishi kati ya Taifa letu na Mataifa mengine ya nje na tumeona ukuaji wa diplomasia ya uchumi, watu kutoka Mataifa mbalimbali wamekuwa wakija katika Taifa letu na kuwekeza na kwa maana hiyo kuchangia ukuaji mkubwa kabisa wa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iendelee kutoa pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Balozi zetu mbalimbali duniani ambapo tumeshuhudia wakati mwingine Serikali ikiingia gharama kubwa kupanga majengo kwenye Balozi zetu huko nje. Naomba Serikali iwekeze zaidi katika ujenzi wa nyumba na Ofisi ya Kibalozi huko Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Spika, nichangie katika Wizara ya Nishati. Naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo imeendelea kuongeza miradi mikubwa ya uzalishaji wa umeme ikiwemo Kinyerezi I, II, III pamoja na mradi mkubwa wa *Julius Nyerere Hydroelectrical Project* ambao unajengwa ambao utakuwa ni mkombozi wa matatizo ya umeme hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini wazi kabisa kwamba ongezeko la *Megawatt 2,115* itakuwa ni ingizo kubwa ambalo litasaidia sana katika kulifanya Shirika la Umeme (TANESCO) pamoja na Miradi ya REA kwenda katika maeneo mbalimbali nchini na Watanzania wengi watanufaika kwa kuwa na umeme ambao utakuwa na bei nafuu; na kwa maana hiyo Tanzania ya Viwanda itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali yetu kwa kuja na Mpango Mkakati na kubadilisha Sheria za Madini ili kuhakikisha kwamba Taifa letu linanufaika. Naipongeza Serikali kwa kuingia mkataba mpya na Kampuni ya Barrick ambako sasa imeanzishwa Kampuni ya Twiga ambayo Serikali yetu sasa itakuwa na hisa za asilimia 16 na manufaa yake tutayaona muda siyo mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba hata Makampuni mengine ambayo yamewekeza katika madini Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Augustine Manyanda Masele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa anafuatia Mheshimiwa John Wegesa Heche, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige. Mheshimiwa Heche taratibu eeh! *(Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi leo ya kuchangia kwenye Kamati hizi, nami nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa miaka ni 50 baada ya uhuru wetu tunapozungumza suala la umeme. Rafiki yangu Mheshimiwa Kalemami nampenda sana kwa sababu ni mtu msikivu, lakini tunapozungumza suala la umeme nchi hii, Watanzania waliounganishiwa umeme ni 2,800,000; yaani kwa miaka yote ambayo CCM wako madarakani wameunganishia umeme Watanzania 2,800,000. *(Makofi)*

**SPIKA:** Chanzo cha data yako Mheshimiwa.

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Spika, hizi ni data za Kamati. Mimi ni Mjumbe, naomba nichangie, baadaye wataniuliza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ni vizuri tuwe tunaelewana. Kaya 2,000,000 au watu 2,000,000?

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Spika, ukisema kaya, ukisema wateja, ndiyo wateja hao!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Spika, mimi nazungumzia wateja.

**SPIKA:** Kuna tofauti kubwa kati ya kaya na watu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Spika, nazungumzia wateja ambao wameunganishiwa umeme na ndiyo takwimu tulizonazo. Mmeunganishia umeme wateja 2,800,000 tu.

**SPIKA:** Hiyo takwimu ina makosa makubwa ya kiuandishi.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo hivyo.

**SPIKA:** Kaya moja inaweza ikawa na watu 20 humo ndani na kila chumba kina umeme, lakini TANESCO watahesabu kwamba huyo ni mteja mmoja.

Kwa hiyo ukichukulia kwamba ni watu milioni mbili kwa kweli is *wrong* lakini endelea. Mtunze muda wake. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Spika, naomba sana muda wangu tafadhali.

**SPIKA:** Ninasisitiza muda tu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, hiyo ni taarifa ya Wizara kuhusu wateja waliounganishiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisema hata kaya, kwani nchi hii ina kaya ngapi? Ni nyingi tu. Ukichukua kama tuna wateja 2,800,000 na hapa hatuzungumzi kwamba tuna-shortage ya umeme. Hivi tunavyozungumza tuna excess ya umeme zaidi ya megawatt 200 na kitu au 300.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wapo wanahitaji umeme na leo wakati Mheshimiwa Waziri wa Maliasili anajibu swali hapa, amezungumza kuhusu jinsi ambavyo nchi yetu misitu inakatwa kwa wingi sana, nchi inaendelea kuwa jangwa kwa sababu watu hawana nishati mbadala, wanategemea mkaa, kuni na hata Wabunge humu asilimia kubwa tunapika kwa kutumia mkaa na kuni kwa sababu hatuna umeme wa kutosha wa kupelekea watu nishati kule vijijini waache kupeleka hii nchi kuwa jangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri huu ni mwaka wa uchaguzi na lazima mijipime kwamba kwa miaka 50 wateja 2,800,000 na umeme mnaufanya kuwa kitu cha anasa, yaani kwamba mtu akiunganishiwa umeme anaonekana yuko *privileged*. Watu wapo, wanahitaji umeme. Hata hili suala la kusema sijui kuna gharama ya kuunganisha umeme, hivi wewe TANESCO unafanya biashara, mtu yuko tayari umuunganishie umeme, unamuunganishia kwa gharama ya kufanyia nini? Mara sijui nunua nguzo, mara sijui; huyu si ni mteja atakulipa bili kila mwezi! Kwa nini umwambie kwamba kunahitajika gharama? *(Makofi) (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa haya ndiyo yanafanya tunasema CCM na Serikali yake mmeshindwa, mnapaswa kutoka madarakani waingie watu wengine ambao watapeleka umeme bure na watafikisha umeme kwa watu wengi kwa kipindi kifupi. Hilo la kwanza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hii nahamia kwenye masuala ya madini. Mheshimiwa Doto mwaka 2019 mwezi wa 12 mmewapa watu barua pale matongo...

**SPIKA:** Mheshimiwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza, nimemsikiliza kwa makini sana kuhusiana na takwimu anazozitoa ambazo tunaamini zinaweza kupokelewa na wananchi zisieleweke vema.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli unapohesabu wateja haulinganishi na idadi ya watu, hilo ni jambo la kwanza. Unaweza ukawa na mteja mmoja lakini umeme unaotumiwa na watu katika mteja huyo mmoja wakawa 100 au 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo taarifa ikae vizuri kwamba tunapozungumza wateja hatulinganishi na idadi ya watu. Hilo ni jambo la kwanza. Jambo la pili, access ya umeme kwa sasa mijini umeongezeka kutoka asilimia 97 mwaka 2015 hadi 92.2 mijini na umeongezeka kutoka asilimia 49.5 vijijini hadi asilimia 72.5. Hii ni access ya kutumia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuweka kumbukumbu pia vizuri kwamba Serikali pamoja na hayo; na pamoja na umeme wa access unaobaki wa zaidi ya Megawatt 280 siyo kwamba Serikali haiendelei kujaziliza ule umeme mwingine, tunaendelea kuzalisha umeme na ndiyo tumeanza na mradi mkubwa wa Julius Nyerere wa megawatt 2,215 ili kufanya sasa umeme nchini kuwa wa uhakika ili wananchi waweze kufanya shughuli za kiuchumi kwa ajili ya shughuli za viwanda.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, amechukua dakika mbili uniangalizie...

**SPIKA:** Aah dakika zako nazitunza kabisa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Anakusahihisha tu kwamba umewahi kusoma takwimu huko nyuma, yaani ukaelewa *statistics*? Endelea kuchangia Mheshimiwa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, Mawaziri wakianza kujibu sasa hivi sijui watafanya kazi gani mwishoni wakija ku-respond! *(Makofi)*

**SPIKA:** Anaweka sawa sawa hesabu yako.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, kwani amezungumza nini tofauti na nilichosema?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Eti!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, amesema kuna wateja 2,800,000...

**SPIKA:** Amesema kwamba unaweza ...

Amesema kwamba ...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, wateja 2,800,000 miaka 50 ...

**SPIKA:** Subiri kidogo ...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Aje Waziri!

**SPIKA:** Amesema unaweza ukawa na mteja mmoja ana kiwanda lakini ana watu 500 ameajiri ndani ya kiwanda kile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukimchukua huyo mteja kama ni mmoja na ukalinganisha na idadi ya watu, ulinganisho huo siyo sahihi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, naomba niendee, Watanzania watasikia. Wateja 2,800,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwomba Mheshimiwa Doto, watu wa Matombo mmewaandikia barua na sasa hivi Serikali ina hisa kwenye *Barrick*, mmewazuia kuendeleza maeneo yao, watu wanashindwa kuzika ndugu zao pale kwenye maeneo yao kwa sababu wakizika baadaye mtasumbuana.

Mheshimiwa Spika, wanashindwa kuendeleza nyumba zao tangu mwaka jana, 2019. Naomba muwalipe wale watu, msitengeneze mgogoro mwingine kama ile iliyokuwa inatengenezwa baadaye mnawaita tegesha. Lipeni wale watu tafadhali. *(Makofi)*

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mwaka 2017 iliundwa Kamati ya Mruma na Mheshimiwa Rais. Kamati ikaenda kuchunguza baada ya makontena kukamatwa kwamba yalikuwa yanasafirisha madini yetu, wana-*under revalue* wanatoa gharama ya chini kuliko ambacho walikuwa wanauza na kupata mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, baadaye ikaundwa Kamati ya Osoro ikiwa na wanasheria na wachumi kwenda kuangalia gharama halisi ya madini yaliyokuwa mle. Tukaambiwa baadhi ya madini ni ya thamani mno hata ambayo tulikuwa hatujawahi kuambiwa hapa na ikasemekana kwamba kwa miaka yote *Barrick* wametorosha, wamekwepa kodi dola bilioni 190 ambazo ni sawa sawa na shilingi tririoni 400 na kitu.

Mheshimiwa Spika, *TRA* wakafanya *assessment* wakathibitisha Kamati ya Osoro ilichokisema kwamba kumetoroshwa shilingi trilioni 420 na hiyo ikapelekea kuletwa sheria nyingi, baadaye nitazizungumza hapa. Sheria mbili; Sheria ya *Permanent Sovereignty of Natural Resources* na nyingine.

Mheshimiwa Spika, naanza na shilingi trilioni 426 tulizoambiwa. Juzi ambapo Mheshimiwa Rais alikuwa anasaini mikataba tisa walikuwa wanaingia *agreement* na *Barrick*, hatujasikia popote wanazungumza kuhusu shilingi trilioni 426. Sasa nataka wanjibu, hizo fedha mmezisamehe? Mmesamehe mabeberu shilingi trilioni 426 za Watanzania? Je, kama hamjasamehe, hiyo Kamati ya akina Mheshimiwa Kabudi iliyokuwa inafanya majadiliano, ina mamlaka hayo. Kwa sababu Sheria ya *TRA* Kifungu cha 14 kinasema, kama *assessment* imeshafanyika, hamwezi tena kufuta hiyo *assessment* mpaka Bodi ya *TRA* ikae na Waziri a-*gazette*. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche nakukumbusha tu, siyo wewe peke yako na wachangiaji wengine; ni vizuri sana kuzijua taratibu za Kibunge. Taarifa iliyoko mezani, aliyetoa hoja ni Mwenyekiti wa Kamati. Sasa baadhi ya michango: Je, huyo Mwenyekiti wa Kamati ndiye aliyeingia huo mkataba? Yaani kweli Mwenyekiti atakuja kujibu haya maswali unayosema au ni kitu gani? Kwa sababu hoja hii siyo ya Waziri, ni hoja ya Mwenyekiti wa Kamati kuhusiana na kazi za Kamati za mwaka mzima. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunapochangia hapa, tuwe tunaelewa hoja hizi tunazielekeza kwa nani. Kwa hiyo, nikumbushe tu, hoja hizi mbili tunapokuwa tunachangia tunazielekeza kwa Mwenyekiti wa Kamati, tunaishauri Kamati, tunalishauri Bunge na Serikali pia. Kwa hiyo, nilitaka tu kuweka hilo vizuri.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, naye ni mjumbe wa Kamati...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, najua Mawaziri wanapata muda wa kuchangia...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mpaka dakika 20, 30...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, mpaka dakika 20, 30 Mheshimiwa Mkuchika alifanya hivyo jana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, haya ni mawazo ambayo nilitoa kwa sababu unajua wingi wetu mle kwenye Kamati. Kwa hiyo, naomba nichangie.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunahitaji majibu kuhusu hilo, kwamba shilingi trilioni 426 sita ziko wapi? Zimesamehewa au hazijasamehewa?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuna kitu kinaitwa kishika uchumba, dola milioni mia tatu zaidi ya shilingi bilioni 600 na kitu, hizo mlisema kwamba zitalipwa na mabeberu haraka sana kabla ya mjadala. Hizo shilingi bilioni 600 Serikali imekubali sasa kwamba walipwe kwa *installment* kwa kipindi cha miaka saba na ukiangalia zaidi ya shilingi bilioni 240 zinakwenda kwenye VAT, *refund* hakuna *cash* yoyote inayoingia kwenye Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nauliza, wale wazalendo waliokuwa wanapiga vigelegele kwanza walipaswa waone aibu hapa kwa sababu walichokuwa wanasema hakipo na hakijapatikana. (Makofi)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Wazalendo bandia hao!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, *smelter*. Tuliambiwa...

**SPIKA:** Ushakula nusu ya muda, sasa chungu huko unakoenda.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa na sheria ikatungwa kwamba kuanzia sasa madini yote ghafi hayatasafirishwa nje ya nchi, *smelter* itajengwa hapa hapa na madini yatachakatwa hapa hapa ili tuyape value ndiyo yasafirishwe.

Mheshimiwa Spika, hiyo *smelter* iko wapi? Tunataka mtujibu hiyo *smelter* mmejenga wapi?

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mheshimiwa Heche ambaye ni Mjumbe wa Kamati anafahamu kila kitu kinachoendelea, kwa sababu amekuwa akiuliza maswali kwenye Kamati, mimi najua nia yake ni pamoja na kunogesha, na kuweza kupata fursa ya kusema. Nataka nimweleza kwamba *smelter* anayozungumza si kama kujenga kibanda, ni teknolojia kubwa ambayo ukishatoa leseni ujenzi wake hauhitaji wiki mbili au mwezi mmoja. *Minimum requirement* ya *time* ya kujenga *smelter* moja kwa watalamu wote walikuja duniani kupresent Wizara ya Madini ni miezi 24. Sisi tumeshatoa leseni yakujenga *smelter* pamoja na kujenga *refinery*. Sasa kama tunataka kuzungumza kwa sababu tu tumeamua kuzungumza; mimi nataka Mheshimiwa Heche ajielekeze kwenye haya mambo kwa kusema ukweli walau kwasababu anaufahamu ukweli wenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Mwongo huyo.

**SPIKA:** Ni ushauri huo ummepewa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, miezi 24 nafikiri tangu mwaka 2017 imeshapita sasa hivi tunaelekea miezi 26 na kitu. Mimi nichozungumza, kama *smelter* inajengwa hapa kwa nini juzi mnasema kwamba makontena yatafute mteja yasafirishwe? Kwanini msisubiri mpaka *smelter* yetu ijengwe makontena yote yale 117 yabaki Tanzania? Kama mnajenga *smelter*? Ilhali sheria iliyotungwa humu Bungeni kifungu cha 11 ilisema wazi kabisa, sheria, kwamba itakuwa ni



marufuku kusafirisha madini nje ya nchi na juzi Rais amesema wateja watafutwe na madini yasafirishwe? Kwanini mnafanya hivyo wakati mnajua mnajenga *smelter* mnajenga?...

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika Taarifa

**MHE. JOHN W. HECHE:**... No! no! no!

#### TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Dotto Biteko, nimekuona.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sifurahi kujibizana hivi, lakini ikitokea uongo unasemwa hadharani inanisumbua. Nataka nieleze ni kweli sheria ya madini imezua kusafirisha madini ghafi nje ya nchi, sheria hiyo hiyo kifungu cha 59 kimetoa mamlaka kwa Waziri wa Madini kutengeneza kanuni ya kusafirisha madini yaliyoongezwa thamani kwa kiwango fulani. Kanuni hiyo imechapishwa kwenye gazeti la serikali na kanuni hiyo hiyo imetoa kipindi cha mpito wakati hatujawa na hizo *facility* kuwe na utaratibu maalumu wa biashara hizo kuendelea, ndio maana biashara zinaendelea kufanyika ndani ya nchi. Ingekuwa ni sheria inayozungumza leo marufuku kesho tungekuwa tunazunguza habari nyingine. Mheshimiwa Heche na sheria hizo anazifahamu ninaomba azungumze kwa kusema ukweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo maana siku moja niliwahi kuzungumza humu ndani kwamba hili neno upinzani lile neno lina shida, kwamba ni vizuri tukafikia mahala pa kuwa na ushindani badala ya upinzani. Kwa sababu upinzani hata kitu ambacho anakijua fika lazima apinge kwa kupotosha.

Kwa hiyo mnapokuwa ninyi ndio wajumbe wa Kamati ambao mmekaa huko mwaka mzima, Mheshimiwa Heche na wewe ukiwa mjumbe wa Kamati halafu mnatoka baada ya mwaka mnatupotosha sisi ambayo hatukuwa wajumbe wa Kamati sasa *where we are going to?* Itakuwa ni jambo lisilofaa hata kidogo. Lakini endelea tu, malizia dakika zako.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika kwamba sheria ya kifungu cha 11 inaweza kufutwa na kanuni ya Waziri hivi hiyo ya wapi hiyo? Unaojua tunaozungumza huku sio kwamba hatuna akili tunajua hivi vitu tuna akili timamu. Wala hatupigi makofi sisi, tunazungumza jambo mlilolileta hapa na sisi tukawaambia na Lissu akawambia hamtapa hata mbuni iko wapi mbuni mliyopata hapa iko wapi kati ya firion 400 mlizoandika tukawa *laughing stock* huko duniani; ipo wapi mbuni moja mliyopata muwaambie watanzania hapa. Sasa mnakuja kama kawaida mnayumba kama upepe kama kesho mpo huku mnapiga makofi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulisema hapa, kwamba mlitunga nyie wazalendo mkasema ninyi *you're a sovereign country*; kwamba hakuna kesi itakayokwenda kufanyika nje ya nchi, mlisema humu ninyi wenyewe, tukawaambia nyie mmesaini mikataba mmesaini *MIGA* na hamtaweza ninyi. Sasa hivi mmeleta Sheria ya *Arbitration Act* mnakuja kuondoa, mmeruhusu na wamewapa *Barrick waiver* ya kwenda kutushitaki popote wanapotaka. Sasa hayo mambo Heche akisema kwamba...

**SPIKA:** Hivi unajua kuna Waheshimiwa Wabunge nawatafuta siwaoni. Mheshimiwa Mwita Waitara yupo wapi leo? Samahani Mheshimiwa Heche endelea bwana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, mimi chuma usinione hivi. Unajua wazungu wamekwenda mwezini wamerudi, sisi Waafrika bado tupo kijiji hata aliyeko mjini mawazo yake

yapo kijiji vilevile. Sisi tunachozungumza hapa ni mambo tuliyojadili humu; kwamba tulikuja hapa tukatamba tukawatangazia Watanzania.

Mimi nilitegemea juzi mnaposaini mikataba msimame pale pale muwaambie Watanzania eehh! Trilioni 420 hizi hapa noah kila mtu apate. Sasa mmekosa mpaka kishika uchumba, kishika uchumba mmekosa. Sheria ambazo mlituaambia *you're a sovereign country* hamuingiliwi mmekwenda kupiga magoti kwa mabeberu mmerudisha sheria humu kuja kuzibadilisha. Nilitegemea Wabunge wengi wa CCM, ambao ndio wengi, muone aibu kwa sababu nyie mliyumba kipindi kile. *We told you*, tuliwaambia hapa, mkasema oooh sisi tunatumiwa na mabeberu. Sasa sisi na nyie nani anatumia na mabeberu?... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche muda wako umeisha, muda wako umeisha Mheshimiwa nakushukuru sana. Mheshimiwa Heche atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Ally Mohamed Keissy ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya hii, na nilikuwa namsikiliza mjumbe mwenzangu na najaribu kukuangalia hata wewe ulivyokuwa unahangaika kutupa maelekezo sisi wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, wala usishangae. Labda tu nikukumbushe ni vizuri wajumbe unapotuteua kutupeleka kwenye kamati ukafuatilia na michango yetu kwenye kamati na mahudhurio.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wajumbe umewateua wakishasaini wanaondoka haya ndio matatizo tunayopata. Haya tunayosema, tuna mahudhurio lakini pia tuna maoni kwenye maoni kwenye Kamati hakuna mahala ambapo Heche ameshawahi kuchangia, akisaini anasepa. Kwa hiyo ni vizuri pia ukatufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza vizuri mchangiaji mimi nilidhani mawazo alikuwa anayachangia kuhusiana na uchimbaji...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu, amenitaja jina.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:**... Mheshimiwa Spika, Heche sikutegemea kama atatoa haya mawazo...

#### KUHUSU UTARATIBU

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche kuhusu utaratibu tupe kanuni.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, kanuni ya 64...

**SPIKA:** Kanuni ya.....

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64(1)(a).

**SPIKA:** Haya isome.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, 64(1)(a).- Mbunge hataruhusiwa kusema jambo la uongo Bungeni...

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Wewe ndiwe ulianza kusema uongo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, na mimi...

**SPIKA:** Ngoja, ngoja Mheshimiwa Heche kanuni 24...

**MBUNGE FULANI:** ...Kanuni ya 64.

**SPIKA:**... Inasema kila Mbunge ataapa kiapo cha utii.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, nipo imara sana.

**SPIKA:** Mheshimimwa Msukuma endelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, unapaswa, kuwa, *impartial* nimesema 64.

**SPIKA:** Endelea, endelea.....

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, *no! no! no!*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msukuma endelea

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nadhani umeona, haya ndiyo yanayotokea kwenye Kamati. Nimemsikia rafiki yangu, mdogo wangu amesema yeye ni chuma, chuma kinaanzia kwenye kuokosea kanuni kama hivyo. Lakini la pili nimekusikia vizuri ukimtafuta Waitara usingehangaika hata Ester yupo hapa kiboko yake; na chuma chepesi huwa kinaanziwa kuyeyushwa na moto mdogo ule wa wahunzi, sasa moto mkubwa unakuja mzee nadhani ungejipanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Maneno aliyoyazungumza mchangiaji kama mjumbe wa Kamati ambaye kwa asilimia 90 naye ni kama Musukuma anategemea maisha ya wachimbaji nilitegemea angekuwa mtu wa kwanza kumpongeza waziri kwa kazi nzuri aliyofanya. Haya maeneo yangezumzwa na Msigwa rafiki yangu anayefuga mbwa kule wala tusingepiga kelele. Lakini kusema ukweli Heche hujatenda haki. Leo haya maneno kama wachimbaji wanakusikia unailaumu Wizara ya Madini ninakushangaa; na nina imani una muda mrefu hujaenda kutembelea wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Geita aje Heche tumuonyeshe *refinery* inaojegwa na hatua zilizofikiwa. Haya mambo hatubabaishi, yamefanyika na yako yanaendelea...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utararibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:**... Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri tu mambo mazuri yanapokuja kiukweli lazima kuwe na taratibu. Tunakuona vizuri sana Mheshimiwa Waziri unatusikia kwenye madini changamoto ndogo ndogo. Kwa mfano anayejenga (*smelter refinery*) kule Geita jaribu kuongea na Wizara ya Viwanda wampe vibali, amekwama kupata vibali vya EPZ, ili aweze kuendelea na uwekezaji wake kwa kuwa kuna vitu anakwamba kwenye kodi. Kwa hiyo ni vizuri ukazungumza na watu wa viwanda wajaribu kuwahisha michakato ili aweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi watu tunaokaa vijiji, leo ukizungumza umeme, wapiga kura wakakusikia unamlaumu Kalemani Waziri wa umeme, yaani sijui. Mimi nadhani wakati mwingine ni wivu tu na lile neno ulilolisema, upinzani. Mimi jimbo langu tulikuwa hatujawahi kuona umeme awamu zote; hata huko kwao Heche; leo kwenye awamu ya tano mzee kijiji changu kila mahali ni mjini, kuna umeme. Leo unasisimama humu kweli Mheshimiwa Heche hata kwa hicho ulichonacho? Mimi nadhani Waitara hakukosea kuchukua maamuzi ya kwenda hilo jimbo, nimeanza kuamini. Kwa *design* hii watu wako watachelewa kufika, kwa hiyo ni vizuri wakakupiga chini akaja mtu mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumezunguka hii nchi sisi wajumbe, kila mahala tumeenda kukagua utekelezaji miradi ya meme na nishati na madini Heche tulikuwa wote, leo unakuja huku unaanza kupiga kelele kupinga mafanikio makubwa yaliyofanyika? Mimi naomba nikukushukuru sana kunipeleka kwenye Nishati na Madini. Kwa kuwa mimi natoka kwenye madini nikisimama hapa nakwambia mzee ingekuwa Spika unatutembelea Wabunge wako njoo utembelee mkoa wa Geita sidhani kama kuna mbunge hata rudi humu ndani. Kwa sababu watu wetu wana maisha safi, kila mahala ambapo tulikuwa tunafukuzwa leo tunachimba; kila mahali tulipokuwa tunavumbua dhahabu tunaletewa mabomu leo mambo ni safi, halafu anasimama mtu anakuja anaongea anaponda Wizara! Kwa kweli mmefanya kazi nzuri na hii serikali iendelee kuwa na moyo huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri yapo ambayo ningependa kushauri. Kwamba ni lazima tujaribu kuangalia hata kwenye uongozi wa huko kwenye mikoa. Tunafanya vizuri, mimi naamini wawekezaji wengi wazuri wa kati tunawatafuta sisi wachimbaji wadogo wadogo kwa kutumia akili zetu bila kusaidiwa na serikali. Lakini tunapowaleta wawekezaji wetu masharti ni mengi mno Mheshimiwa Waziri. Mimi nina mfano nina mwekezaji yupo Geita, yupo Nyamauna wewe unamfahamu. Kila siku anapigwa faini mpaka amefunga mgodi. Mara OSHA mara idara ya kazi mara huyu *migration* faini milioni mia nane na kitu mchimbaji wa kati ataendelea kusaivaive namna gani?

Mheshimiwa Spika, nikiombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba utakuja kueleza vizuri una vyombo vyako, hao wawekezaji wachimbaji tunavyowatafuta mtu wa kuwalinda ni, wewe usikwepe mzigo. Kama wataondoka wanaopata kazi ya kwenda kuwatafuta ni sisi wachimbaji wadogo, hakuna mahala ambapo tunafurahia; tunaona, unamleta mtu mwenye mtaji wa bilioni tano anazopigwa faini, mara idara ya kazi, mara sijui hana kibali, mara sijui nini; milioni mia tisa na kitu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri; na kitabu ninacho hapa naweza nikakukabidhi; ukajionea adhabu mwekezaji huyu wa Nyamauna alivyopigwa; idara ya kazi, sijui osha, sijui nini hadi amefunga mgodi na ni mwekezaji ameajiri watu zaidi 500, hii haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe wewe Waziri na Waziri wa Kazi na wanao husika muwa-*guide* wale watu mikoani wasione wale wawekezaji kama chanzo kukamilisha ujenzi wa madarasa; hii haiwezekani nikuomba sana Mheshimiwa waziri uyazingatie haya.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kazi nzuri kamati hii ilivyozifanya nakupongeza Mwenyekiti kwa umetu-*guide* vizuri na wajumbe wengine wa CHADEMA wenye akili timamu nadhani wanaelewa. Ninakushuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie. Mimi mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tupo humu na baadhi ya Wabunge wapo humu hawajamaliza hata jimboni kwake kutembelea vijiji. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake wametembea kila jimbo katika nchi, kila kona na wakati huo huo nao ni Wabunge na wana majimbo yao. Wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaishia Dodoma - Dar es Salaam, hawaendi kwenye majimbo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa moja ametoka kuzungumza hapa, wa Kamati ya Madini, kwenye kamati yetu; yeye hahudhuri vikao, ni kesi mahakamani kila siku Dar es Salaam, na yeye ananiambia Mheshimiwa Keissy mpaka hela nimeishwa, anajijua. Ametoka kuchangia hapa kwa hasira na kwa kupiga kelele lakini ukienda kwenye *record* katika Kamati si mhudhuriaji.

Mheshimiwa Spika REA peke yake Tanzania tuna vijiji 12,268 vinawekewa umeme. Leo anazungumza kwamba wananchi hawajapata umeme nchini; labda kwake jimboni kwake; lakini sisi tunashukuru sana; majimbo yetu ya kule Mkoa wa Rukwa na Katavi ilikuwa ni mwisho kabisa wa nchi hatukuwa na umeme, hata mara moja kwenye vijiji vyetu. Kuna sehemu ambazo hazina hata barabara lakini REA wamepeleka nguzo na wanaendelea kufanyakazi na wananchi wanapata umeme.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Heche hawezi kusema Wizara haijafanya kazi, Wizara imefanya kazi; wewe ni jela na wewe, na kwasababu haudhuri vikao, kila siku Mahamani Dar es Salaam; na hiyo itaku-*cost* kwenye jimbo lako.

Mheshimiwa Spika, hii sekta ya nishati na madini ndiyo itakayotusaidia sana kwenye Serikali yetu, kwa sababu hatuwezi kwenda kwenye viwanda kama hatuna umeme, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, umeme ndiyo nguzo kubwa ya viwanda, huwezi kujenga kiwanda bila umeme, na serikali ina umeme wa ziada na huu umeme wa *Grid ya Taifa*; ndiyo sababu Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma tunauomba kwa sababu serikali inapata hasara sana kwa mafuta. Ifanye jitihada ipeleke umeme wa *Grid ya Taifa* kwenye mikoa mitatu; kwa sababu Serikali na TANESCO inapata hasara kila mwezi mabilioni ya fedha kwa kutumia mafuta. Kwa sababu tutaokoa; kwa sababu kuna mpango kabambe wa Serikali wa kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa yetu hivi karibuni. Serikali mpaka ikifikia mwaka 2021 itamaliza vijiji vyote katika nchi hii kupelekewa umeme, lazima tushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Madini vilevile amesaidia sana; ametembea nchi nzima, kila kwenye mgodi anafika na wamesaidia sekta ya madini mpaka sasa kuongeza pato la Serikali. sasa nashangaa anasimama hapa Mheshimiwa anasema sekta ya madini inazidi kushuka chini. Chukua *data* kwa Mheshimiwa Waziri, chukua data Wizarani kiasi gani tangu wewe umeingia ubunge mpaka leo hii ni kiasi gani cha pesa kimeingizwa? Wizara ya Nishati na Madini imeigiza kiasi gani? Mheshimiwa lia na lwako.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kama jimbo langu hakuna hata kijiji kimoja kitakosa umeme mpaka mwezi Juni, 2020. Vijiji vyote katika jimbo Nkasi Kaskazini vitapata umeme sasa nashangaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imesaidia sana Mheshimiwa Waziri. Nguzo tulikuwa tunaagiza nje, *transformer* tunaagiza nje, waya tunaagiza nje kila kitu tunaagiza nje; leo vyote vinatoka ndani ya nchi yetu. Tumeokoa kias gani fedha z kigeni katika nchi yetu? Hatupotezi hata senti tano kwaajili ya mambo ya umeme, vyote vinazalishwa katika nchi yetu na watu wanapata ajira katika nchi yetu. Tulikuwa kila siku tunaagiza nje, leo ndugu yangu unakaa unaiponda Wizara ya Nishati na Madini badala ya kuwasifu! Acha!

Mheshimiwa Spika, tumeingia gharama bilioni sita kwa ajili mradi wa Nyerere kule ili tupate umeme wa kuendesha reli yetu inayotumia umeme; leo unashindwa na ku-*support* Serikali? Lia na lwako Mheshimiwa. Ukiona namna hiyo ujue sasa; Mheshimiwa Heche nakuonea huruma rafiki yangu, wewe ni rafiki yangu sana; wewe wasema hali ni mbaya. Ninyi wenyewe mnasema kujenga *smelter* ni miaka miwili; Chama chao kina miaka 28 hata ofisi hawana. Miaka 28 unasema sawa nyumba ya kawaida wewe kujenga kiofisi unatumia *block* 3000 na bati hakuna ukuchojenga miaka 28,... (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** ... hakuna, wanapanga kaofisi pale kwenye kanyumba ka kulala pale Kinondoni...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:**... Makaburini pale, hata pa ku-*park* gari hakuna...

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Keissy kwa kweli kama kuna aiibu kwa chama cha upinzani chenye ruzuku ya mamilioni, hata ofisi ya chumba na sebule kwa kweli? Mheshimiwa Kessy endelea bwana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, tuna shida. Hata *CUF* pale Buguruni wana ghorofa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** *Chief Whip*, changamoto nyingine zichukue tu kazifanyie kazi, maana kunijibu itabidi utuonyeshe ofisi ilipo. Mheshimiwa Keissy tumsubiri *Chief Whip* atutajie ofisi yao iko wapi? Taarifa atupatie.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Eeh!

Mheshimiwa Spika, iko pale *Ufipa Street*, tena...

**SPIKA:** Ngoja kidogo basi atulie halafu uongee

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** ...karibu na makaburi pale Kinondoni.

**SPIKA:** Ngoja kidogo Mheshimiwa Keissy, unataka kuonyweshwa ofisi ilipo. Mheshimiwa Ester endelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, CHADEMA ina ofisi zaidi ya moja. Tuna ofisi kwenye kanda zetu na hatujapanga; na kwa ruzuku hiyo hiyo na tunaitumia vizuri. Tofauti yetu sisi na ninyi...

**MBUNGE FULANI:** Mwongo!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** ...mlirithi majengo ya Umma enzi ya Chama kimoja. Sisi tumejenga wenyewe na tuna mkakati wa kujenga ofisi hapa Makao Makuu ya Dodoma nyingine ya kisasa bila kutumia...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mwenyekiti.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Naomba tusikilizane Waheshimiwa. Taarifa hiyo anapewa Mheshimiwa Keissy. Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa siipokei maana yake Sabodo mwenyewe aliyewapa shilingi milioni 100 wajenge ofisi, lakini hawakujenga hata msingi. Sabodo aliwapatia shilingi milioni 100 na kwenye TV mlichangia pesa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** nanyi akina mama mnakatwa kila mwezi shilingi 1,200,000/=, zinakwenda wapi? Nye wenyewe mnakuja kuniambia Mheshimiwa tutetee, tunakatwa hela!

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, taarifa, taarifa!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Utanipaje taarifa wakati nye wenyewe mmeliwa hela za Sabodo...

**SPIKA:** Naomba tusikilizane. Mheshimiwa Dkt. Mollel, tafadhali.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa mzee wangu mzuri sana, Mheshimiwa Keissy kwamba asipate shida, aendelee na msimamo huo huo kwa sababu mwenzetu pale amepata kile cheo. Alianzisha harakati ya kudai shilingi bilioni 13 ambazo hazionekani za CHADEMA. Kwa hiyo, mwisho wa siku akahongwa hicho cheo, ndiyo sasa hivi anapambana kukitetea ili asiendelee kudai shilingi bilioni 13. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

*(Hapa Mhe. Ester A. Bulaya – Chief Whip wa Upinzani alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester wewe ni *Chief Whip* unajua taratibu, kwamba taarifa hiyo anayepewa ni Mheshimiwa Keissy. Kwa hiyo, mwache mwenye taarifa yake kwanza aipokee au aikatae. Kwa hiyo, tunarudi kwanza kwa Mheshimiwa Keissy aliyepewa taarifa. Mheshimiwa Keissy

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa kwa sababu CUF wana ofisi Magomeni inajulikana, ni ya ghorofa pale Buguruni; TLP wana ofisi pale Magomeni; NCCR wana ofisi pale Pangani...

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mnaruhusu hii nyumba ya Watanzania inafanyiwa hivi!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, sasa ile Ofisi pale jina la Ufipa lile makaburini, ndiyo ofisi yako. Hawana ofisi nyingine Makao Makuu, iko Ufipa. Vijana wa Ufipa!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naendelea na mchango wangu kuhusu nishati na madini.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Keissy.

**MBUNGE FULANI:** Endelea, endelea, ongea na Spika. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. ALLY K MOHAMED.:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini inafanya kazi na inajitahidi katika nchi hii, tulikuwa katika giza kwenye vijiji vyetu vyote katika nchi hii, lakini wanajitahidi na itafika mwaka 2022 hakuna hata kijiji kimoja katika nchi kitakosa umeme. Vijiji vyote vitawaka umeme. Hakuna hata kijiji kimoja kitakosa umeme!

Mheshimiwa Spika, hawaelewi. Waende mwambao mwa Ziwa Tanganyika ambapo hata barabara hakuna, lakini leo nguzo zinakwenda na wananchi wanapewa umeme na wananchi wanaishukuru sana Serikali na mtaona wenyewe mwaka wa Uchaguzi ndugu zangu umeme utatupa kura kwa kishindo. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, umeme utakuwa ndiyo miongoni mwa mambo ya kusema nasi tutakuwa kifua mbele kutetea kura zetu katika mwaka huu; mwezi Oktoba ni umeme katika nchi yetu. Hamwezi kuyumbisha wananchi, walikuwa ni shida. Mimi mwenyewe wakati naweka umeme katika Kijiji cha Kirando, hawa CHADEMA kwenye kampeni walisema haiwezekani labda umeme utoke *DRC Congo*, CHADEMA hawa! Leo ni ajabu, wanaona umeme unawaka Kirando na wameona ni waongo. Wenyewe kazi ni kuzusha vitu vya uongo; wanaweza kuwa na dhahabu wakakwambia shaba ukaamini. *(Kicheko)*

Sasa ndugu zangu tuwe wakweli. Leo ndugu zangu nyie umeme kwenye vijiji vyenu karibu vyote vinawaka umeme. Kaskazini huko mnakotoka nyie ndiyo mlianza kupata umeme, mkajiona nyie ndiyo safi. Sasa tunagawana kasungura kadogo kila kona. Kwa hiyo, ndugu zangu msituonee wivu, mwaka 2020 Oktoba, mtaona matokeo.

Mheshimiwa Spika, wakipita huko, wanaona kila kijiji kinang'aa. Leo ukipaa kwenye ndege mzee hata ukienda porini unaona kijiji kinang'aa kwa umeme. Sasa ndugu zangu tuangalie mabadiliko yanavyokuwa. Miaka hii minne hakuna vijiji visivyo na umeme. Tumeweka umeme zaidi ya 8,500. Anatoa tarakimu 2,800 ndiyo sijui ni kaya sijui nyumba wala haeleweki hesabu yake kama nilivyomwambia. Somo la hesabu mzee halidanganyiki! Hesabu haidanganyiki wala mtu hawezi kuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa watu wanazidi hesabu ya wenye umeme kwenye hizo nyumba zako.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keissy.



**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Ina maana nyumba laki 460,000 ndiyo zina umeme katika nchi hii kwa hesabu yake Mheshimiwa!

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nyumba 4,600 ndiyo zina umeme.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** ...wakati kila kona ya nchi hii kuna umeme, kila kona...

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy! Ahsante sana, inatosha, muda wako umeisha.

Nilitaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba Mbunge niliyekuwa namtafuta, sasa ameingia Bungeni, Mheshimiwa Mwita Waitara yuko ndani ya Ukumbi. Kwa hiyo, naona hapa sasa mambo mswano hapa kwa lugha ya Dodoma. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Peter Selukamba, tafadhali, ndio mchangiaji unayefuata.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba niwapongeze Wenyeviti; Mwenyekiti wa Kamati ya Madini na Nishati kwa ripoti zao nzuri sana. Nawapongeza sana Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Mzee Keissy kazi ya umeme inayofanyika Tanzania ni nzuri sana, naipongeza sana Serikali. Nataka niseme jambo moja ambalo nadhani kama Bunge lako, hatujalipa nafasi ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kilichofanywa na Rais, kilichofanywa na Serikali kuingia makubaliano mapya na wawekezaji wakubwa wa madini, kwa vyovyote vile ni jambo ambalo sisi kama Bunge tunapaswa kuipongeza Serikali. Wako wanaosema ambao mimi naelewa kwa nini wanasema, lakini najaribu kuangalia tutakachopata kama nchi kwa makubaliano haya makubwa na kwa uchumi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kwanza ukisoma kwenye yale makubaliano ambacho watu wengine wanaweza wakaona ni kidogo, ofisi za Barrick London, ofisi za Barrick Johannesburg, zote zinafungwa, zinakuja Tanzania. Maana yake wafanyakazi wale watakaa kwenye nyumba za Watanzania, watalala kwenye hoteli za Watanzania, watakula kwa Watanzania. Maana yake uchumi mkubwa katika nchi utaongezeka sana. Bado hapa sijaongea habari ya ajira. Ninayo hakika, leo ukienda Dar es Salaam na mikoa ya Mwanza na Arusha bei ya nyumba zimeshuka, lakini unapopata Kampuni kubwa kama Barrick, wafanyakazi wake wanakuja kukaa Tanzania, maana yake nyumba zetu zitarudi bei kuwa juu, kwa sababu wale watu wana-*income* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ziko faida za kiuchumi. Moja ya faida kubwa, ukiangalia pale, Serikali ina asilimia 16, lakini Tanzania tutapata *cooperate tax* 30%. Tutapata karibia 3% kwa ajili ya *Local Government*. Maana yake kwa uchumi tunakwenda kupata kila mwaka mapato ya zaidi ya 50% kwa *revenue* ya kampuni hii. Kwa vyovyote vile Mtanzania yeyote ukisimama unalaumu jambo hili, *then* maana yake hufahamu uchumi mpana unavyofanya kazi. *(Makofi)*

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, vile vile naangalia *social responsibility* ambapo kwa watu ambao wanazunguka na madini kule ambako madini yapo watafaidi zaidi kuliko Halmashauri nyingine za mbali ambazo sisi tunakaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia nataka niwaambie wenzangu, mimi nimeangalia vizuri sana, tunaanzisha kampuni mpya ya Twiga, ukiingalia watu watasema unapata 16% lakini mkishakuwa na kampuni maana yake baadaye ikiishaanza kufanya biashara, tutaipeleka kwenye *stock exchange*, kwa sababu ni kampuni mpya hii. Tukiipeleka kwenye *stock exchange*, watakaofaidi ni mimi na wewe na sisi. Haya ni mageuzi makubwa ya kishujaa ya kimapinduzi. Tanzania tume-*set tone Africa*. Leo hii Waafrika wote wanakuja kujifunza tuliyoyafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, habari ya *smelter*, hata kama isipojengwa hapa, ambayo naamini baadaye itajengwa, bado kwa sababu tumeweza ku-*identify a new company*, watu wetu watakuwemo kwenye Bodi, ofisi zitakuwepo hapa, usimamizi bado kama nchi tutafaidi ndugu Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naangalia, kwa mara ya kwanza, tutakuwa na *Board Members* kwenye kampuni hiyo Watanzania ambapo naamini jambo hili ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia kubwa zaidi ambalo wote hamlisemi, tulitunga sheria mwaka 2010 hapa; moja ya jambo kubwa tulilitunga, makampuni haya...

(Hapa Mhe. John W. Heche alisimama)

**SPIKA:** Mheshimiwa Heche, naomba utulie. Halafu wanaogeuzi kiti nyuma kwa Spika wanakosea. Mnatakiwa wote muwe mnamwona Spika anavyopendeza. (Kicheko/Makofi)

Tusikilize shule inayoshushwa na Mheshimiwa Peter Selukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, moja ya jambo kubwa lililofanyika, kuna maamuzi makubwa ambapo tulitunga Sheria ya Madini Mwaka 2010, kwamba makampuni yote ya madini fedha zao wataweka kwenye benki za Tanzania. Maana yake ni nini? Wakiweka fedha kwenye benki za Tanzania; NMB, CRDB na benki zote, fedha zile Watanzania wote tutazi-access kwenye mikopo. Maana yake fedha za Barrick, pamoja na kwamba zitafanya kazi ya kuchimba, zitafanya na kazi ya uchumi kwa Watanzania. Hili ni jambo kubwa, *uncles* wenzangu hatuelewi maana ya fedha kuja kwenye benki za Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wakileta; kwa mfano, leo najua watu kama GGM fikiria fedha zao zote wanaweka kwenye benki moja ya Tanzania, Barrick; maana yake ni nini? Siyo kwamba fedha zile ni kwa ajili ya kumpa *Barrick or Geita* peke yake, maana yake fedha zile kwa sababu ziko kwenye benki zitatumika na masikini wa nchi hii kuwakopesha kufanyia biashara. Huu ndiyo uchumi mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi leo nataka niseme, kwa muda huu ambao walikuwa wamesimamisha biashara, nenda leo kaangalie Kahama, Shinyanga na Mwanza utaona tofauti. Tumefaidika kidogo baada ya Waziri wa Madini ambaye nami nampongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Doto kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapewa nafasi ya kufanya kazi kubwa. Kama leo ingekuwa wachimbaji wadogo hawapo, tungekuwa na hali ngumu kiuchumi mikoa ile ya Kanda ya Ziwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, fikiria, tuna wachimbaji wadogo, tumewawekea *regulation*, tumewawekea masoko, wanaleta fedha, tunapata kodi na *on top of it* tunawaleta na wachimbaji wakubwa wanaanza kufanya biashara yao. Kwa vyovyote vile hili ni jambo kubwa. *This is a game change of the economic Tanzania*; na sisi kama Wabunge tunapaswa kuwa watu wa mwisho kuinyooshea kidole Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Mheshimiwa Heche amesema kwamba Wabunge wa CCM tunatakiwa kuona aibu. Nadhani kuna maeneo haelewi vizuri. Anasema tunabadilisha sheria. Wewe umekaa muda mrefu na wengine wachache wamekaa muda mrefu, kila mwaka tunabadilisha sheria. *Miscellaneous* maana yake nini? *Miscellaneous* tunaleta tubadilisha sheria ambazo aidha tulitunga tukakosea, tumefikiria, tunatunga upya. Suala la kubadilisha sheria halimaliziki leo. Mbona sheria nyingine hawasemi? Kazi ya Wabunge ni kutunga sheria. Ukitunga sheria leo, ukaanza kuitumia, ukaona haikuletei ulichokuwa unakitaka, *prudence* yoyote, unaleta unabadilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumetunga sheria nyingi hapa za fedha, tunakwenda tunagundua haifai, tunaleta tunaibadilisha. Kwa nini Sheria ya Madini tukiibadilisha iwe nongwa? Ni nongwa! Mimi naelewa kwa nini ni nongwa. Ni kwa sababu wanaona Chama cha Mapinduzi kinafanikiwa sasa. Ni nongwa kwa sababu wanaona Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kimeanza kuelewa na kuleta mageuzi makubwa ambayo kasi ya uchumi itakuwa kubwa, nafasi yao inazidi kupungua kadri siku zinavyoenda mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nawaomba watu wa Serikali, msiogope. Kama kuna maeneo tulifanya tukadhani hayatuletei faida, leteni tubadilisha, ndiyo kazi yetu. Nasema tulateeni! Moja ya kazi kubwa tukibadilisha sheria hii, maana yake tuna-*attract more investors*. tuki-*attract more investors*, maana yake uchumi wa Tanzania utakua; na ile *dream* ya Mheshimiwa Rais Magufuli ya kwenda kwenye uchumi wa viwanda, kwenda uchumi wa kati, tutai-*realize* kwa kuandika sheria nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ripoti ya Kamati. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Kwa taarifa hizi, ndiyo uchangiaji tunaoutaka. Kwa hiyo, *Chief Whip* mnaponiletea watu wa kuchangia kwa kweli ni vizuri mniletee watu wanaochangia, siyo mtu anasimama tu, ooh kijiji changu cha nanihii kule, kijiji change, aah! Hapa tuko kwenye mambo makubwa ya nchi. Tunaongelea habari ya mambo ya nje, ulinzi, usalama, nishati na madini, vitu vizito. (Kicheko)

Kwa hiyo, kwa kuwa tumefikia mwisho hapa, dakika hizi ni chache, niwahakikishie wale wote ambao majina yao ninayo na *Chief Whip* mnaruhusiwa kubadili mkiona kama kuna haja ya kufanya hivyo. Leo tuna wachangiaji wazito wazito hapa. Siyo kama jana akina rafiki yangu Mheshimiwa Lema ndio anapigapiga kelele hapa! Leo mmeona, ametulia kabisa! (Kicheko)

Namchokoza kidogo. Kwa hiyo, tutaendelea jioni na wale ambao nina majina yenu hapa msiwe na wasi wasi *unless* yatabadilishwa toka pande zote wala haina neno. Uchangiaji ni mzuri *so far*, *challenges* ni kitu cha kawaida, lakini ukweli ni kwamba kama kuna Wizara zimetubeba ni pamoja na Wizara ya Umeme na Wizara ya Madini.

Kwa hiyo, mkimwona rafiki yangu Mheshimiwa Heche anapiga kelele, ni kwa sababu anajua hizo hoja mbili na hasa kule Tarime Vijijini, hoja mbili; umeme na madini, yaani ndiyo penyewe pale pale ambapo ndiyo zitabeba sana CCM. Kwa hiyo, msishangae, lazima apige kelele kidogo.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kongwa kule katika vijiji vyote, vimebakia vijiji vitano; na vyenyewe hivyo vijiji vitano hivi sasa vingi ni vya milimani, nguzo zinapanda huko milimani. Kwa hiyo, safari hii ni iyena iyena tu, iyena iyena, nambari wani; kitakachotubeba nini? Umeme, basi! Kila mahali tunakapoenda ni umeme.

Kwa hiyo, tunaishukuru sana Wizara na mwendelee. Tena kule kwa Heche ndiyo mpeleke nguzo zaidi, kuanzia sasa hivi yaani kule pandisheni kila kijiji, maana yeye ni Mjumbe wa Kamati, kwa hiyo lazima apate umeme. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea tu vizuri, wala msiwe na wasiwasi, tutaendelea tena jioni saa 11.00, tukutane hapa tusikilize mambo yatakavyokwenda na yataenda vizuri. Ni mjadala mzuri, unaendelea vizuri tu.

Basi naomba nichukue nafasi hii sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 juu ya alama.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

### HOJA ZA KAMATI

#### TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019

### NA

#### TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Sasa tuanze na Mheshimiwa Bobali Hamidu atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe. Tuendeleo Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, leo nami nasherekea kumbukumbu ya siku yangu ya kuzaliwa, natimiza umri wa miaka kadhaa. Kwa hiyo nakushukuru kupata fursa hii, lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa umri alionijalia.

Mheshimiwa Spika, nianze suala la Uhamiaji hususan kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Mpaka kati ya Msumbiji na Tanzania sielewe kuna tatizo gani? Kuna ndugu zetu; ukienda Mtwara kuna watu wanahitwa Wamakonde. Hawa Wamakonde wapo kwenye nchi mbili; wanaotoka Msumbiji na wengine waliopo huku ng'ambo, Tanzania.

Mheshimiwa Spika, unakuta unapofika wakati wa uchaguzi wa Msumbiji hawa watu wanaletewa masanduku na wanapiga kura kuchagua Rais wa Msumbiji, halikadhalika watu hawa hawa ukienda unakuta wamejiandikisha kupiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili ni hatari sana. Namshukuru Afisa Uhamiaji wakati ule wa mchakato wa Serikali za Mitaa, Afisa Uhamiaji wa Mkoa wa Lindi tulishirikiana naye vizuri sana na kuna baadhi walikwenda wakawaondoa kwenye *list* ya watu waliojiandikisha kwa ajili ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kujua kwamba walishiriki kwenye uchaguzi wa Msumbiji. Kwa bahati mbaya, watu wale waliondolewa kwenye daftari la kupiga kura za Serikali za Mitaa lakini wapo wengine kwenye daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba jambo hili lifuatiliwe, hususan Waziri wa Mambo ya Ndani, namheshimu sana kaka yangu Komredi Simbachawene, hayupo lakini jambo hili ni muhimu sana kuhusu suala la uhamiaji. Unajuwa sasa hivi pale mpakani kati ya Mtwara na Msumbiji hali siyo nzuri sana, kumetokea mauaji hivi karibuni, lakini nafikiri kama kuna uholelaholela wa namna ya watu kupita pale, mwingiliano umekuwa wa kawaida sana, yaani huwezi kujuwa kama mtu anavuka anaenda upande wa pili; anaenda Msumbiji au anaingia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uholela mkubwa sana, inafikia hatua tuliona wakati fulani hapa mwaka uliopita 2019, kuna ndugu zetu kule Tandahimba walipoteza maisha na sijajuwa kama wale watu walishakamatwa au namna gani, lakini ni kwa sababu ya ule mwingiliano. Waziri wa Ulinzi, yupo anafahamu kwamba kuna watu wa Tanzania wanalima Msumbiji na kuna watu wa Msumbiji wanalima Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa lile suala la mpaka pale, namwomba Mheshimiwa Waziri alichukulie kwa umakini na kwa uzito mkubwa sana. Kumekuwa na uholela sana katika mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji kwenye kile kipande cha kule Mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Jambo lingine, pale Jimbo la Mchinga kuna Gereza moja linaitwa Kingurugundwa. Ni Gereza maarufu sana, wale wafungwa watukutu ndio wanapelekwa pale. Kwenye kadhia hii ya mafuriko yaliyotokea Mkoa wa Lindi, hili Gereza sasa hivi kama liko kisiwani vile; na wako mahabusu pale wanatakiwa wapelekwe Mahakamani, lakini takribani sasa karibu wiki ya pili inashindikana.

Mheshimiwa Spika, hata yale maji yakiondoka, barabara ya kutoka pale barabara kubwa kwenye eneo la Mkwajuni kwenda pale Kingulugundwa *almost too kilometers*, ni ngumu kulifikia. Kwa hiyo, naomba hili Gereza kwa sababu la umuhimu wake huo na haliko mbali kutoka barabara kuu, lakini wamekuwa wakipata shida sana ya usafiri, namna ya kusafirisha watuhumiwa au mahabusu kuwapeleka Mahakamani na hata wale Askari wenyewe, huduma zile za kiusafiri zimekuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi ukisikiliza juu ya *traffic* kubambikia kesi madereva. Jambo hili nalo ni kero kwenye jamii. Tunajadili suala la mambo ya ndani ya nchi, tunaangalia viashiria ambavyo vinaweza vikaleta shida kwenye nchi; suala la *ma-traffic* kubambikia kesi madereva limekuwa kubwa na wakati wengine hata sisi wengine linatukuta.

Mheshimiwa Spika, unamkuta *traffic* anakwambia *ume-over speed*, ukimwambia nionyeshe gari, wengine hawataki na akikuonyesha unakuta siyo gari yako kabisa. Kwa hiyo, hili limekuwa ni tatizo na wamekuwa watu wakibambikiwa na madereva wanalalamika sana kwamba kwa nini tunabambikiwa kesi namna hii? Inaonekana kama ni kitega uchumi cha kukusanya fedha, jambo ambalo kwa kweli siyo nzuri sana. Naelezwa hapa, wakati wengine wanakaa porini wanajificha kwa ajili ya kuchukuwa hizo picha.

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni kuhusu suala la matamko yanayotolewa na baadhi ya viongozi wa Vyama vya Siasa. Taifa hili letu wote na tunapenda tuendeleo na amani hii iliyokuwepo, lakini panapotokea viongozi wanatoa matamko ya kuashiria kama ni uchochezi, wakitoa upande fulani hawashughulikiwi, huoni hata wameitwa Polisi, wakitoa upande mwingine wanaitwa. Jambo hili kwa ustawi wa Taifa letu siyo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona juzi huko Arusha Mwenyekiti wa UVCCM ametoa tamko baya sana. Nilifikiri angalau angewahi kuitwa akahojiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, unajua watu wengine wala huna haja ya kupoteza muda. Niko na wewe, sikupingi, yaani wako watu, wewe hebu endelea na mengine tu.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kwa sababu ni matamko ambayo hakuna anayekubaliana nayo hata robo. Hakuna! Kwa hiyo, tutakuwa kama tunakuza kitu ambacho... mmh!

Nafikiri sisi kama Wabunge, tuko *above that*.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Okay.

**SPIKA:** Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu, ahsante.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho nilitaka niongelee dogo tu. Kwa kuwa tunazungumza Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi na furaha kwenye nchi; kuna jambo ambalo linaendelea sasa hivi hasa kwenye mitandao ya kijamii, watu wanalamika sana juu ya upendeleo wanaopewa timu ya samba. *(Kicheko/Makofi)*

Eeh, ndiyo! *Marefaree*, nilikuwa naomba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Bobali ngoja nikae vizuri. Ngoja nikae sawa sawa, unaweza ukaendelea Mheshimiwa Bobali. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na *tendency* ya watu watu kulalamika. Mambo haya, wakati timu fulani inapendelewa kulikuwa na viti vilivunjwa pale na wengine walirusha viti pale Uwanja wa Taifa. Ni jambo baya sana. Sasa hili lazima likemewe na Waziri wa Mambo ya Ndani lazima ahakikishe kuna amani. Sisi wote tunapenda furaha.

Mheshimiwa Spika, jana nimelala sikufurahi kabisa kwa sababu siyo Yanga ilifungwa, sikufurahi kwa sababu Timu ya Polisi walichofanyiwa jana *is not fair*. Kwa hiyo, jambo hili sasa imeonekana kama tabia inataka kukua na wananchi tuna mambo mengi ya kufurahia. Wengine tunapenda mpira, kwa hiyo...

**SPIKA:** Kuna taarifa unapewa, sijui! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Aah, hapana Mheshimiwa Spika! *(Kicheko)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, kuna taarifa bwana!

TAARIFA

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wao walipokuwa wanachangia bila kibali, sisi tulikuwa hatusemi. sasa inawauma, wakae watulie tu, ubingwa ni wetu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Pokea hiyo taarifa Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea, nakushukuru sana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Dah! Hii ligi ya safari hii nzuri sana. Kumbe watu inawauma eeh! Goli la dakika 94, duh! Ahsante sana.

Sasa nilishamtaja Mheshimiwa Salome, lakini sio Salome wewe. Salome huyu nilioandikiwa, anaitwa Salome Wycliffe. Karibu Mheshimiwa, dakika tano.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ndiyo taarifa niliyopata, dakika tano eeh!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Naam!

Mheshimiwa Spika, naitwa Salome Wycliffe Makamba. Najua unatamani ningekuwa Mgogo lakini ndiyo umechelewa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hata Wasukuma wana majina ya Kizungu! Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nianze utangulizi wangu nikijikita sana kwenye Mambo ya Nje. Dunia iligundua kwamba kuna nchi zina nguvu sana. Tuki-*apply* dhana ya *sovereignty of the state* kuna baadhi ya nchi inaweza ikaziumiza nchi nyingine. Kwa msingi huo, ikaja dhana ya kidiplomasia, kwamba hawa watu watatumia ushawishi, uwezo, mahusiano kuweza kufanya nchi hizi ziweze kuishi na kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Spika, nimetoa utangulizi huo kufuatia mambo yanayoendelea kati ya Tanzania na Marekani. *Secretary of the State* alitoa kauli kuhusu mwenendo wa nchi yetu kwenye mambo ya demokrasia, haki za binadamu na mambo mengine. Akaeleza, tusipokuwa makini, tunaweza tukaharibu mahusiano yetu na Marekani na matokeo yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, sasa anapotokea Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi yetu anajaribu ku-*confront statement* ya Marekani kwa kutishia kwamba watatufanya nini na tukitaka tutarudisha watu wao. Hiyo siyo diplomasia na huo siyo msingi wa diplomasia duniani.

Mheshimiwa Spika, hili narudia. Tuliposema tunahitaji Waziri wa Mambo ya Nje aliyebobea kwenye diplomasia, tulimaanisha mtu mwenye ushawishi, mtu mwenye uwezo wa kuimarisha mahusiano ili Tanzania, nchi masikini tuweze kuimarika kiuchumi na kuweza kutekeleza bajeti zetu kupitia *donor community*. Sasa hili inabidi tuliangalie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, 2019 mwishoni, Tanzania iliyopewa heshima ya kuwa Makao Makuu ya *the African Court on Human and People's Rights* tumetishia kama siyo kujitoa,

maana zimetoka kauli mbili za Mawaziri. Mheshimiwa Prof. Kabudi anasema tumejitoa, Mheshimiwa Mahiga anasema hatujajitoa, tumeomba wabadilishe *protocol*.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu iliyopewa tangu enzi za uhuru, AICC hapa Tanzania, tuna hii Mahakama ya Afrika, siyo kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, kusema tunajitoa kwenye AICC, kusema tunataka kujitoa kwenye *the African Court on Human and People's Rights*, ni kujaribu kuona ile heshima tuliyopewa hatukustahili.

Naiomba Serikali, tunayo haja kubwa ya kuimarisha diplomasia katika nchi yetu. Hili siyo jambo la kufanyia mizaha kwa sababu kurudisha heshima tuliyopewa, zipo nchi nyingi sana zinajaribu na wamekosa fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo kuhusu ndugu zetu walioko China, waliopata ugonjwa wa *coronavirus*. narudia tena, kazi ya kwanza ya Serikali ni kulinda, kuhudumia na kuhakikisha watu wake wapo salama. Sasa leo Mbunge anasimama Bungeni, anauliza swali mahususi: Tanzania itafanya hatua gani kuhakikisha watu wake wanarudi nchini salama? Serikali inasema, watu wabaki huko huko kwanza, haya mambo mengine tutashughulikia pole pole.

Mheshimiwa Spika, hili Bunge ni la wananchi. Serikali kazi yake ni kulinda ustawi wa wananchi na kulinda usalama wa wananchi. Tunahitaji kauli thabiti ya Serikali kuhusu *evacuation process*.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome, kuna taarifa.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa.

#### TAARIFA

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Salome kwamba tamko la kusema raia wa Tanzania ambao wapo nchini China ilikuwa ni kwa manufaa yao. Tumeshuhudia Serikali ya China ikiwashauri wananchi wao wenyewe wa Jamhuri ya Muungano wao wa China waendeleo kukaa ndani kutokana na maambukizi au mfumo wa maambukizi wa ugonjwa ule.

Kwa hiyo, kubaki kwao ndani kuweza kufanya *movements* za kutoka kwenye miji yao kuja mpaka Tanzania kunawaweka kwenye hatari zaidi kuliko kuendelea kuwa china.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome, poka ushauri huo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika kwa kulinda heshima ya kiti chako, ulielekeza Serikali hapa wiki iliyopita walete kauli, walete mpango wao wa *evacuation* kwa ajili ya ndugu zetu wanaoishi China. Leo ni Jumatano, watu wetu wanaishi kwa hofu, wazazi wao walioko Tanzania wana hofu. Hivi hii ni serikali gani isiyojua hili? Tumeelezwa kwamba Marekani wameshaanza *evacuation process*, watu wanarudishwa, Ujerumani wanarudisha watu Tanzania...



**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika Taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Tanzania watu wetu wanaishi kwa hofu na wale ni Watanzania wenzetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome, kuna taarifa unapewa. Nia ni kukusaidia tu Mheshimiwa Salome kupitia taarifa hiyo. Mheshimiwa Waziri Nchi, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, hatugombani katika jambo hili ambalo lina maslahi ya Watanzania na nchi kwa ujumla. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salome ajue kabisa kwamba hatugombani katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka ndani ya Mkutano huu wa Bunge Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa alishatoa maelezo, lakini Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Afya alishatoa maelezo yakinifu. Sasa tunachotaka kufanya hapa kwa muktadha wa jambo hili ambalo ni lenye afya tu, Mheshimiwa Salome anapaswa kushauri zaidi kuliko kulalamika ama kuishutumu Serikali haijachukua hatua zozote.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha kwamba Serikali imefanya kazi yake ipasavyo, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa tamko, Waziri wa Afya ameendelea kutoa tamko na hiyo yote ni Serikali. Hatulali, tunaendelea kulifanyia kazi jambo hilo. Kwa hiyo, tuko tayari kupokea ushauri, lakini siyo tuhuma kwamba Serikali haijajali wala kushughulikia suala hilo.

**SPIKA:** Unapokea taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa siipokei. Hivi unafikiri Bunge lako linajua Watanzania wangapi wanaumwa? Watanzania wangapi huenda wameshapoteza maisha? Watanzania watarudi tarehe ngapi mwezi wa ngapi hapa nchini? Marekani wamesharudisha watu wao nchini. Hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayojitapa ina ndege, itumie ndege hizo nane waweke moja Watanzania warudi nchini kwa maslahi ya Taifa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Dakika zako zimekwisha.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** ...na kwa ajili ya kuleta amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa anafuatia Mheshimiwa Mboni Mhita, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nilitamani sana niweze kumwelevesha ndugu yangu Mheshimiwa Salome. Sasa asiweze kunitoa kwenye reli na maelezo mazuri ambayo yamezungumzwa na mama yetu Mheshimiwa Jenista, naomba niendeleee.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya kipekee, kwanza kabisa nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Katika jarida la *The Diplomat* toleo la Januari, 2020 limetamka au limemwita

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni *A Game Changer* kwenye *mining industry*.

Sasa wenyewe tunaweza tukajipima na tukaona kama jarida kubwa kama hilo la *The Diplomat* limeweza kutambua wazi na kumwita *An African Mining Game Changers*, siyo *Tanzania Game Changer* kwenye *mining sector*, lakini *African Game Changer* kwenye Sekta nzima ya madini. Sisi tunajua na wao wanaanza kutambua hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Mambo ya Nje kwa namna ya kipekee katika kipindi hiki cha miaka minne ya utekelezaji wa Ilani, kimefanikiwa au Wizara imefanikiwa kuongeza Balozi saba.

Mheshimiwa Spika, naomba nizataje, ya kwanza ni Algeria, ya pili Israel, Sudan, South Korea, Quba, Namibia pamoja na Qatar. Hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo Wizara inaendelea kujipambanua kwenye kukuza uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya uchumi. Pia, ni jinsi gani ambavyo kupitia hizi Balozi zetu mpya itashughulika na watanzania ambao wako kwenye nchi hizo, nikiwa na maana ya *diasporas* lakini pia kupitia uchumi (*economic diplomacy*) itaendelea basi kushughulika na wawekezaji ambao wana *interest* ya kuja kuwekeza Tanzania. Vilevile kikubwa zaidi pia kuweza kuvutia utalii.

Mheshimiwa Spika, hapa niwe muwazi kabisa, kuna Balozi ambazo zimekuwa ni mfano wa kuigwa kwenye suala zima la watalii. Ubalozi wa kwanza ni China, Ubalozi wa pili ni Israel, Ubalozi wa tatu ni Urusi. Mabalozhi hawa wamekuwa; natafuta neno sahihi la kuwaita; lakini wazalendo kupindukia kwa sababu wamejitoa kwa namna ya kipekee kwa kujiongeza kufanya *marketing* kwenye sekta nzima ya utalii, na tumeshuhudia watalii ambao wamekuja nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto moja hapa; hawa mabalozhi hawana fungu lolote la *marketing*, *marketing funds* ziko kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Hivyo basi, naomba nitumie fursa hii kuwashauri wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje ione ni jinsi gani itakuja na utaratibu wa kuweza kupata fedha kidogo za kuweza kuwasaidia Mabalozhi wetu kwenye nchi hizo ili waendelee basi kujipambanua zaidi na kuja na njia *latest* au *more ways* za kuona ni jinsi ambavyo wanaweza kukuza utalii.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuipongeza sana Wizara kwa namna ya kipekee. Katika kipindi hiki kifupi tumeshuhudia SADC ikipitisha Kiswahili kuwa ni *an official and working language*; na tunakumbuka wazi kwamba SADC ina nchi 16 lakini wakati huo huo na nchi za Maziwa Makuu (*Great Lakes*) ambayo imekusanya nchi 13 nao pia wamepitisha kuwa Kiswahili kuwa ni *official language* na *official working language*. Wizara haikuishia hapo, imeenda mbali zaidi kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili imeanza kuandaa mitaala ambayo itatumika sasa katika nchi hizo. Hapa tumeona kwamba Wizara imeamua kujipambanua na imeamua ku-*champion* hili suala zima la Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Mambo ya Nje inamiliki nyumba 106 lakini wakati huohuo ina viwanja takribani 12. Naomba nitumie fursa hii kuishauri basi Wizara ione ni namna gani sahihi hivi viwanja 12 vitajengwa ili kuweza kupunguza gharama ambazo kwa sasa Serikali inapata lakini pia adha ambayo Maafisa wa Wizara ya Mambo ya Nje wanayopata kupitia kutokuwepo kwa nyumba za kudumu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie sasa, na ninaomba nimalizie kwa kuzungumzia Chuo cha Diplomasia ambacho ni chuo sasa hivi, au kilianzishwa kupitia uhusiano kati ya Tanzania na Mozambique, Tanzania wakiwa na asilimia 50 na Mozambique wakiwa na asilimia 50. Kwa

muda mrefu sana wenzetu wa Mozambique wamekuwa hawatoi mgao wao au hawachangii katika makubaliano yale; na kwa namna moja ama nyingine hiyo imekuwa inaturudisha nyuma. Nilikuwa naomba niishauri Wizara basi, kwa namna ya kipekee iangalie mfumo gani mzuri na wa kidiplomasia wa kuweza kuachana na wenzetu waweze kuendelea kwa sababu ni dhahiri kwamba hawana nia ya kuendelea na muungano huu na sisi tujiongeze. Tuna majengo ya kutosha Dar es Salaam sasa hivi Serikali imehamia Dodoma, tuna mitaala mipya katika sekta nzima ya diplomasia ya uchumi ambayo sasa; na ninaamini kupitia Wizara hii makini ikifanya hivyo kwa kutumia majengo yetu ambayo yako pale Dar es Salaam chuo kitaendelea kukua na kitasaidia vijana wengi ambao wanataka kujiongeza katika sekta nzima ya diplomasia.

Mheshimiwa Spika, niishie kabisa sasa kwa kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nje kwa kuendelea kuimarisha uhusiano wa kimataifa na nchi mbalimbali, nchi zetu ambazo tunapakana nazo nchi za Afrika Mashariki, nchi za African Union, nchi za ACP, European Countries, American Countries. Tumeshuhudia juzi wenzetu wa EU tuko nao wamekuja kutusaidia hiyo Euro milioni sitini lakini pia tumeshuhudia wenzetu wa Marekani jana tu wametoa vifaa vya kijeshi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Naomba kutumia nafasi hii Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na kuwatakiya kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii sasa kuishia hapa, nashukuru sana kwa kunipa fursa. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mboni ahsante sana kwa mchango wako mzuri uliopangwa kisawasawa bila *controversies*. Mheshimiwa Mwijage nilikutaja, endelea tafadhali.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia taarifa za Kamati hizi mbili zilizopo mbele yetu, lakini kwa sababu sijavaa vazi la kidiplomasia nitachangia sekta ndogo ya nishati upande wa mafuta na gesi nikikumbuka nguo nilizokuwa navaa miaka 36 iliyopita wakati nafungua valve.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Mheshimiwa Waziri. Nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba unaweza kuwa na kitu na usijue thamani yake. Kwa watu wanaojua historia ya mafuta nchini wakati watu wanapata mafuta kwa mgao ndiyo utaweza kujua kwamba Wizara ya Nishati leo inafanya kazi iliyotukuka. Nimeisoma vizuri taarifa ya Kamati, inavutia. Tunayo hifadhi ya mafuta ya kutosha miezi mitatu, lakini kipekee hifadhi hiyo imenunuliwa na *Private Sector*. Ina maana mfumo wa *Bulk Procurement* unaodhibitiwa na Serikali unaifanya sekta binafsi kuleta mafuta kuwa hapa bila fedha ya Serikali na watu hawawezi kugundua kwamba nchi ina upungufu wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, nipongeze suala lingine la *bulk procurement* ambapo kwa historia, najua hili unalifahamu vizuri; wakati meli zinakuja Dar es Salaam tulikuwa tunaweza kukalisha meli nje tukaingia gharama (*demurrage*) ya dola 20 mpaka 40. Taarifa ya Kamati inafurahisha, kwamba *demurrage charges* sasa ni chini ya dola mbili (dola 1.6). Ni jambo zuri sana niwafurahishe wanakamati kwamba muendee hivyo tuweze kwenda kwenye mambo mengine yanayofurahisha.

Mheshimiwa Spika, nitofautiane kidogo na Kamati; kwamba tathmini yao haijatupeleka kwenye malengo ya kuanzisha *bulk procurement*, pamoja na haya *availability of product*, *affordability* na *quality* ambayo kweli *quality* tumeiweza hatujaweza kujibu au taarifa yenu haikutueleza. Je, haya mafuta *margin* yake ni kiasi gani? Mwenyekiti wa Kamati anaelewa kwa sababu mimi ndiyo nilimpokea kazini nikamuonesha dawati na kumfundisha kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kitandula ni kijana wangu nilimpoke kazini mika hiyo kwa hiyo hii *success* ugomvi wa kuagiza mafuta uko kwenye ile *margin*. Je, unapokuwa umenunua *margin* iko kiasi gani, lakini Mwenyekiti wa Kamati nikueleze haujatueleza mafuta yanayopotea. Ugomvi mkubwa wa Wizara ya Fedha ni mafuta yanayopotea kutoka kwenye meli kuingia kwenye matenki, hili suala kamati yenu haijalijibu.

Mheshimiwa Spika, nimweleze Mwenyekiti wa Kamati kwamba kuna suala tata la *floor meter*, *floor meter* inayopigiwa kilele ambayo kimsingi mimi mwenyewe kama mtalaam wa shughuli siungi mkono, lakini *solution* ya upoteaji wa mafuta ni kuwa na *single receiving tanks*. Hili suala tata la *single receiving tanks* Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati haujalijibu, umekuwa wimbo wimbo wimbo wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, jambo moja la kufurahisha niwapongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuongeza *storage capacity*, kwamba leo nchi ina uwezo wa kutunza mafuta lita bilioni 1.3 ambayo matumizi ya nchi inakwenda kwenye lita karibu 3.8 bilioni. Jambo la kufurahisha ni kwamba mafuta ya jirani yetu yanayopita Tanzania ni takriban kiasi hicho cha *1.9 billion liters* kwa miezi sita. Maana yake ni nini, wakati una mafuta ya kutumia nchini kwa miezi mitatu una mafuta mengine ya jirani yako yanayopita; ina maana hatuwezi kulala njaa wakati mafuta ya jirani yapo. Kwa lugha ya kawaida huwezi kuwa umemuwekea mwenzako mihogo halafu baba hajatoka kuhemea watoto wakalala njaa, hapana utakula mihogo hiyo halafu kesho yake utakuja urudishie. Kwa hiyo niwapongeze Wizara ya Nishati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wakati nawapongeza tumeshindwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inayotuelekeza kwamba Dar es Salaam inapaswa iwe *trading hub* ya mafuta kwa nchi zilizotuzunguka. Kwa masikitiko watu wa Kenya wanatumia *bounded warehouse*, watu wa Uganda wanatumia *bounded warehouse*, Rwanda wanatumia *bounded warehouse*. Maana yake ni nini, kama mafuta yangeletwa yakazuiliwa Dar es Salaam tungefanya *re-export*. Ina maana kwenye lita zinazopita hapa *1.9 billion* kwa miezi sita tungeongeza cha juu tukaweza kuuza nje. Kwa hiyo tunapoteza fursa ambayo ingetuongezea kodi nyingine Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Yaani unaongeza *make up* inaitwa cha juu unaweza kuuza. Niwaeleze, watu kutoka nchi zilizotuzunguka hawapendi kununua kutoka nje. Ndicho kitu nilichokifanya kwenye sekta ya saruji; watu wa Rwanda na Burundi walikuwa wananunua saruji Pakistan lakini viwanda vya saruji vilipochangamka wakaja na malori wakanunua saruji kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nahimiza kwamba tutekeleze Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kujenga *storage tanks* zile za Tanga, tengeneza *bounded warehouse* tusimamie ile *damping* na *whatever* tuweze kuongeza kile cha juu *1.9 billion liters* ukiweka dola moja moja mambo ya kujenga madarasa tunaweza kufanikisha kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nipongeze wizara na TPDC; katika taarifa yenu mliwahi kuzungumza, mlirashiarashia kidogo. Zipo jitihada za TPDC kuanza kutafuta na kuchimba gesi. Si jambo jipya, mmerudi kule tulikoanzia, TPDC katika historia ya kutafuta mafuta imewahi kuchimba visima, Munazi Bay, Songosongo, akina Mzee Kaaya, akina Mzee Barongo walichimba visima na wakakuta gesi. Kwa hiyo jitihada za sasa ni lazima tuziendeleze. Msiwe na wasiwasi, kazi hii ina gharama kubwa. Kupata mafuta, kuchimba mafuta kwa gharama yako ni kubwa lakini *failure* ni kubwa. Mtachimba visima kwa gharama kubwa na unaweza kuchimba visima hata kumi usipate lakini ukipata ulichokipata ni cha kwako. Kwa hiyo hapo wanaofanya maamuzi lazima mkae chini mtulie. Libya kuja kupata kisima cha mafuta ya kutosha (*economic quantity*) walichimba visima zaidi ya 50. Kwa hiyo na sisi tunaweza kuchimba visima vingi lakini tukipata tumepata tunaondoa yale mashaka ya kwamba tunaliwa.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Suala la Utafutaji. Suala la utafutaji lina faida nyingi, utafutaji wa mafuta ni shule. Wako vijana wengi wanafanya suala la *geology, petroleum chemicals* na *whatever*, hawa vijana tunawapatia nafasi ya kuweza kujifunza hii sekta. Kitu kimoja kilichodokezwa na Kamati ambacho nawaunga mkono, naiomba Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi muharakishe kufanya maamuzi na kuzipitia PSA ambayo nina hakika Kamati yetu iliwahi kupitia, kuna Kamati ya Gesi iliwahi kupitia; lakini ukisoma mtu yeyote kuna makandokando ambayo kwa sababu ya kupitwa na muda tunaweza kufanya maboresho. Tufanye maamuzi kusudi watafutaji na wachimbaji waanze kuchimba kwa sababu hizi rasilimali haziko Tanzania peke yake, lakini hizi rasilimali zina rasilimali mbadala kwingine.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine sasa hizi *liquefied natural gas* si biashara tena, lakini anayekuwahi sokoni anakwenda kukamata mteja, mteja atakayechukuliwa na Mozambique wewe kuja kumtoa Mozambique uuze gesi yako itakuwa ni tatizo. Kwa hiyo naomba Serikali yetu fanya michakato usiku na mchana, pitia hizo PSA, pitia hizo leseni, waite hao watafutaji na wachimbaji watafute. Mimi nina uhakika Mwenyezi Mungu na sisi ametuwekea mafuta sehemu, ametuwekea gesi mahali, ningependa na sisi tuweze kuyafaidi haya mafuta si kwamba wajukuu wetu waje waseme babu zetu walikuwa wazuri, waliishi na mafuta wakayaacha ngoja sisi tuweze kufanya nini, tuweze kuyatumia. Tukiweza kupata mafuta yakaweza kuchochea zile sekta za kilimo na mifugo zikaziunga mkono tutaweza kwenda kwenye uchumi mkubwa haraka sana kuliko tunavyotegemea.

Mheshimiwa Spika, nilizungumze hili wakati nataka kumaliza. Safari yetu ni ya kwenda kwenye uchumi mkubwa, si uchumi wa kati, uchumi wa kati ni kituo. Kwa hiyo ili uende kwenye uchumi mkubwa unahitaji nguvu nyingi, moja wapo ya nguvu ni nishati na nishati yenyewe ni mafuta na gesi ambayo Mwenyezi Mungu alitujalia. Kwa hayo machache naomba niunge mkono hoja, ahsanteni Mheshimiwa Kitandula kwa repoti nzuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage ahsante sana, *as usual* umeweka rekodi, sasa naomba nimuite Mheshimiwa Mariam Mzuzuri.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye taarifa ya Kamati hizi mbili. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliotujalia afya na uzima kuweza kukaa kwenye kikao hiki leo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini lakini pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Kwa hiyo nipende kumshukuru sana na kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Kitandula kwa uongozi wake mahiri na kutuongoza vema. Tunamuomba afya na uzima ili aendelee katika majukumu yake. Pia nipende kuwashukuru sana wajumbe wa kamati hasa wale wanashiriki katika vikao na ziara kikamilifu; lakini pia niwatie joto wale ambao wanategatega katika kazi za kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inafanya kazi na wizara mbili, Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Madini, nipende kuwapongeza sana sana Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi pamoja na Manaibu wake, pamoja na Makatibu Wakuu lakini bila kuwasahau wataalam wa wizara hizo. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa katika kutafsiri maono ya Mheshimiwa Rais ya kuleta uchumi wa kati na Tanzania ya viwanda. Pia kubwa lile la kutaka sisi kujitegemea kama taifa huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati, nirudie kuunga mkono kauli ya mchangiaji aliyepita Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye amesema kwa uthubutu wa Viongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano kweli yanafanyika mapinduzi makubwa na ya kihistoria. Kwenye sekta ya nishati leo hii mtu anavyosema kwamba tuna umeme wa ziada, ndivyo taifa linatakiwa liwe kwa

sababu ulichonacho na huku una mipango endelevu lazima uwe na ziada na uwe na mipango ya kuongeza zaidi na zaidi. Huwezi kusema ninahitaji thelathini na nina hiyo hiyo thelathini halafu ukasema wewe ni taifa linaloendelea.

Kwa hiyo tunapoongea kwa sababu wamesema ooh, wateja ni hawa tu na huku tuna umeme wa ziada. Taifa lolote lenye mipango endelevu na ambalo liko katika process ya maendeleo lazima liwe na ziada. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeona mafanikio makubwa ya miradi hii ya umeme vijijini, awamu ya kwanza, awamu ya pili na sasa tuko kwenye awamu ya tatu ambayo ina mafanikio makubwa. Ilipanga kupeleka umeme kwenye vijiji 4,651; miezi 19 ya utekelezaji tayari vijiji 3,269 vimeshafikiwa na umeme ambayo ni sawa na asilimia 70 ya malengo waliyojiwekea. Wilaya ya Tarime ambayo ina majimbo mawili ina vijiji 88, kwenye vijiji 88 tayari vijiji zaidi ya 46 vina umeme, vijiji zaidi ya 26 vimeshaingia kwenye bajeti ya mwaka huu kazi zinaendelea kusimamisha nguzo na nyaya ili umeme uwake kwenye vijiji hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini katika nchi za Afrika ni takribani mataifa kama manne tu ikiwemo Nigeria ambao wanafanya process hii ya ku- *electrify rural areas*. Lakini kati ya yote sisi Tanzania tuko bora hata Angola wamekuja nyuma yetu wamekuja kujifunza Tanzania kufanya *electrification* kwenye vijiji vyao, kwa hiyo kazi inafanyika na sio kazi ndogo ni kazi kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto lakini uzuri wa viongozi wetu ni wasikivu. Tuliwaambia wigo (*scope*) ni mdogo ndio maana Wizara kupitia REA wakasema tulete awamu ya tatu mzunguko wa pili ili kufanya ujazilizi kwenye maeneo ambayo yamerukwarukwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto za vifaa kwamba hawa wakandarasi wanakuwa kidogo wana uzito katika kutekeleza majukumu na visingizio kwamba hawapati vifaa, lakini nashukuru kwa ushauri wa Kamati Serikali tumesikia juzi walikuwa na mkutano na wakandarasi kwa maana sasa wanachukua maoni yetu na kuyafanyia kazi. Bunge kazi yake ni kuisimamia na kuishauri Serikali, ukiacha kupitisha bajeti. Mafanikio mema ya Serikali ndio mafanikio yetu sisi Bunge. Sasa leo hii ukisimama kama Mbunge na kubeza mafanikio ya Serikali labda kwa vile ndio uki upande wa kukataa, lakini ukweli upo na unaonekana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la TANESCO ni shirika la umma. Serikali hii ilipoingia madarakani Awamu ya Tano TANESCO ilikuwa ni shirika la madeni na shirika ambalo lilikuwa linaendeshwa kwa kupokea ruzuku kutoka Serikalini. Lakini leo tunavyoongea TANESCO inalipa madeni, TANESCO haipokei ruzuku, TANESCO haizalishi madeni, TANESCO inasonga mbele. Tunasema mapinduzi makubwa leo hii tuna ziada ya umeme, lakini bado Serikali hii kwa kutumia fedha za ndani ambazo Bunge hili ndio limeidhinisha tuna ujenzi wa umeme kwenye Bwawa la Rufiji la Nyerere. Kwa hiyo kwa kweli mambo ni makubwa na sisi kama Kamati/Wajumbe tuwatie moyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye sekta ya madini kwa kupitia sheria zile mbili za mwaka 2017 lakini pia mabadiliko ya sheria ndogo ya mwaka 2019 tujivunie, Tanzania leo hii madini ni mali ya Watanzania. Leo kuna masoko ya madini, leo kuna kipengele kwa kuanzisha Tume ya Madini, kuna kitu kinaitwa *local content*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mpaka mayai, kabichi yalikuwa yanaingizwa kutoka nje ya nchi, leo mama wa kawaida pale nyumbani kwa Mheshimiwa Spika anauza mayai mgodini. Sasa kama hatutofurahi kuona kwamba haya manufaa yanashuka kwa wananchi wa chini tunalipenda

Taifa letu, utabeza mambo yote haya ambayo yanamgusa mpaka Mtanzania wa kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo hii kule Geita inajenga *refinery* ambayo itaenda katalisha haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi. Kwanza hiyo *refinery* Afrika Mashariki ndio itakuwa ambayo ni *modern* kuliko zote, itaweza ku-*process* zaidi ya tani 100 ya dhahabu kwa mwaka. Dhahabu yote inayozalishwa Kanda ya Ziwa itakuwa inapandishwa thamani pale. Mambo ni makubwa nan i mengi lakini tumeona mapato, Mheshimiwa Rais alisema hatutaki sisi ndio haya mambo sasa hivi tunapiga watu wa Marekani. Wewe Marekani umemzuia sisi Mkuu wa Mkoa wetu ni mtu mkubwa, yule ni *president appointee*, sasa leo unamzuia asiingie nchini kwako na sisi tusijibu kisa wanatupa hela za msaada ndio maana tunataka kujitegemea ili mtu anapotoa kisu na sisi tunatoa panga msichukue tafsiri nyingine nimetumia mfano maana kwa kunani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo hii tuna shirika la *Twiga Mining Company* hayo siyo mafanikio? Kweli hatuendi kwenye uchumi wa kati. Leo hii *Tanzanite* kwa ujenzi wa ukuta ilikuwa inapatikana *Tanzanite* kilo 147.7 leo tunapata kilo 949; mapato kwenye madini yametoka kutoka bilioni 196 mwaka 2016 mpaka bilioni 310 inachangia katika pato la Taifa utasema mambo hayajafanyika! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huwezi kujua umuhimu wa hivi vitu kama hujatoka nje ya mipaka ya Tanzania. Ulinipa heshima kwenda kushiriki *round table* ya viongozi wa nchi wa SADC kwenda kutoa maoni namna gani ya kubadilisha *policies* na sheria ili kuboresha *extractive industry* iweze kutufaidisha sisi kama wazawa, kila nchi ilikuwa ina-*present* mawazo, Tanzania tulikuwa ni nchi mfano, *a model country*. Walisubiri sisi tuwasilishe ili wao waweze kupata dondoo. Nakushukuru na ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Nakushukuru sana kwa mchango wako mzuri sasa tumsikilize Mheshimiwa James Mbatia na atafuatiwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Mheshimiwa Mbatia tafadhali.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii, kwanza kabisa niwapongeze Kamati zote mbili Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Nishati na Madini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nishauri tu kwamba nimesikiliza mijadala tangu asubuhi ili mijadala yetu iweze ikawa na afya tuzingatie misingi ya utu wakati tunajadili, misingi ya kuwa na utulivu wa fikra, misingi wa rasilimali muda baadaye rasilimali fedha kwa muda utakaotumia katika mijadala yetu. Na wazo zuri ni wazi zuri usiangalie limetoka upande upi. Tujadili pamoja, tufakari pamoja na hatimaye tushauri pamoja. Hii italeti tija na itatusaidia sana kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu tukigawanyika na yote mazuri ambayo tunayazungumza ambayo nimeyasikia hapa na mengine yanaonekana basi kauli zetu kwa sababu sayansi nilishawahi kusema tena narudia sayansi ambayo imekuwa duniani kwa miaka 300 hivi inaonesha hisia kunuia na kutenda kwa mwanadamu hasa zile nguvu zinazotoka kwenye moyo wake zinaitwa *magnetic force* hasa *spoken words* maneno yanayotumika neno likishatoka limetoka na kipaji chetu cha kusikiliza.

Mheshimiwa Spika, nimeanza na hilo kwa sababu dunia ya leo tunaenda kwenye *artificial intelligence*. Kwenye diplomasia ya kiuchumi kwenye *artificial intelligence* yaani mashine zimeanza kufikiri kama binadamu, mashine zimeanza kutoa majawabu kama binadamu na kwenye *logic* naanza kufikiria na kwenye *logic* unaenda kwenye *tautology*, wale waliosoma hesabu, *if and only if* na kwenye *tautology* unaongea nini na nani mahali gani

wakati gani halafu hii halafu inaenda kwa kasi kubwa sana. Unaongea nini narudia unaongea nini na nani, mahali gani, wakati gani, halafu hii halafu ndio iliyo nzito zaidi kuliko yote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na kwenye *artificial intelligence* tunaangalia dunia na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje yupo hapa. Kwenye diplomasia ya kiuchumi wakati Taifa hili linaasisiwa Mwalimu Nyerere alianza na kanuni ya utu, binadamu wote ni ndugu zangu, hakusema Afrika wote ni ndugu zangu, alisema binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja.

Sasa tukishasema binadamu wote ni ndugu zangu tuchunge sana ndimi zetu hasa kutoa lugha ambazo zinaudhi wengine, tunatoa lugha ambazo zinadhilisha wengine na hili ni kwetu sote tu. Kwa mfano tukitoka lugha za kukebehi na kujadili mataifa mengine tuangalie lengo la kumi na saba la malengo endelevu ya dunia linazungumzia *global partnership*, linazungumzia ushirika wa kidunia halizungumzii ushindani wa kidunia. Leo hii tuko humu ndani tunazungumza ushindani wa kivyama badala ya kuzungumza ushindani wa Taifa katika ushirika wa dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mijadala kama hii na sisi tunaisimamia na kuishauri Serikali. Niishauri tu Wizara ya hasa Mambo ya Nje kwenye suala la *global partnership* ili yale malengo kumi na sita na lile la kumi na saba la *global partnership* badala ya kusema mimi unasema sisi, badala ya kusema yangu unasema yetu. (Makofi)

Sasa katika misingi hiyo umimi huu au ubabe huu hautatusaidia sana, lugha ni lugha tu nafasi yetu Tanzania katika mahusiano ya kimataifa, diplomasia yetu ya kiuchumi katika mataifa mengine, tunashauriana namna gani, tunasikilizana namna gani, kwa sababu mataifa yetu ni mataifa huru (*a sovereign state*). Unakaaje na wenzako kama wametoa kauli mnazungumza kwa lugha ya staha badala ya kutoa lugha tu, labda wakoloni hawa, mabeberu hawa, wamefanya hivi hata tukipiga kelele sana wao wanajibu kwa vitendo na tukiri kwenye *artificial intelligence* leo hii wenzetu wanaenda kwenye mashine za namna hiyo wakati sisi bado tuna upungufu hata kwenye shule zetu za miundombinu ya vyoo kwa takribani asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *we must think big and we must think globally while we want to have a local solution*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye diplomasia ya kiuchumi kwa mfano nilibahatika mwaka juzi kwenda Israel, tulialikwa na Chuo cha *True Man Institute* kwenye masuala ya ushirikiano kati ya Afrika na Israel. Waisraeli leo hii wanavuna maji yaliyo safi na salama kwa kutumia hewa angani, lakini dunia ya leo zaidi ya watu bilioni moja hawana maji safi na salama. Sasa ni namna gani mahusiano yetu kwenye hii *free market* ya dunia ya leo mahusiano yetu ya kuweza kuvuna rasilimali hii *knowledge* hii katika kuisaidia taifa letu la Tanzania tukiwa wamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wakati wa Mwalimu mahusiano kati ya Wapalestina na Waisraeli mwaka juzi tulipokuwa kwenye hicho chuo cha *True Man Institute* tulikuwa na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Marekani akina Poel, wakina Mheshimiwa Raila Odinga, Balozi mmoja wa Israel aliwahi kuwa Kenya akiwa anashughulikia Afrika Masharikia akasema uso mzuri hauitaji urembo. Nanukuu maneno yake; "uso mzuri hauitaji urembo." Maana yake nini kwamba chema chajiiza, kibaya chajitembeza. (Makofi)

Sasa tukifikiri tukiwa na utulivu mzuri tu, tukaangalia sisi sasa tunatumia namna gani nafasi hii kuvuna teknolojia hii, kuweza kuona namna gani inatusadia katika maji, basi Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje inashirikiana na zile Wizara nyingine zinazohusika tunasimama wote kwa pamoja kama Taifa kwa sababu hili lina maslahi kwa wote kama ni maji ni yetu sote katika



## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

majimbo yetu, kama ni suala la umeme ni letu sote katika majimbo yetu, kama ni suala lolote lile sote tunasimama kama Taifa na vita hivi vya kiuchumi tutavishinda tukiwa wamoja kama Taifa la Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo tunakumbuka Zimbabwe ilivyokuwa kwenye hali n zuri tu mwaka 2002 nikiri nilienda Zimbabwe tulitumwa na Rais Mkapa kuangalia uchaguzi wa Zimbabwe, lakini walikuwa wamegawanyika. Tulienda Bulawayo tukaenda Tumbuiza, tukaenda Harare mpaka *Victoria Falls* sasa wanatumia nafasi ya mgawanyiko ndani ya Taifa ili kutugawa. Sasa tusijaribu kuona kwamba tunafanya tu upande mmoja tufikiri kwa pamoja, tuwe na utulivu kwa pamoja, tuone ni namna gani ya kuweza kuvuka katika hali ya namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niishauri Kamati na niombe Kamati na hasa ya Mambo ya Nje ukiangalia Taifa la India leo hii na teknolojia yao ya afya na vijana wao wanavyojitahidi kwenye afya namna gani mgogoro ulioko kati ya India na Pakistan hasa mambo ya Jammu na Kashmir. Kwa sababu kila mara India wanauliza wao wanataka wafanye mazungumzo yao, sasa Tanzania sisi tunasimamia wapi kwenye mahusiano yetu kati ya Pakistan na India hasa masuala ya Kashmir, halafu tunakuwa na msimamo gani ili sisi wote tunaweza tukafaidi yale mengine ambayo ni makubwa badala ya kutoa lugha tu ambazo sio nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nizungumzie kidogo masuala ya usalama katika Taifa letu. Yako haya mambo yanayoendelea kwenye Taifa letu hata juzi yalitokea mauaji huko Kilimanjaro ambayo lazima tujiulize sote na tutafakari kwa sote kwa pamoja. Nimejaribu kujuliza maswali yafuatayo kwenye suala la ulinzi na usalama wa taifa letu. Kwanza nitoe tena pole kwa vifo vilivyotoke kule, lakini kwenye masuala ya hivi vikundi mbalimbali tujiulize je, kuna matatizo au vikwazo au changamoto gani katika jamii yetu labda ya kikatiba, kisheria husika na kanuni zake, jamii kujitambua, mifumo yetu ya kitaasisi hasa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama mfano *public order* (usalama wa raia), *public health* (masuala ya afya), *peace* (suala la amani ya Taifa), *crowd management* na *disaster preparedness* endapo jambo lolote lile linatokea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na tujiulize kama taifa na hasa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa nini haya yote na matakwa yake ya kisheria yanatokea mambo ya namna hii, je, ni maadili yetu ya kitaifa yamemomonyoka, je, elimu ya kimungu ndani ya madhehebu yetu yenyewe yako katika misingi ya namna gani.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na tafakuri ya kina sote kwa pamoja tunaamini kwamba tutabaki kuwa pamoja na wakati wa mijadala hasa wakati huu tunashauri Serikali, tunashauriana Wabunge na hasa Kamati tuhakikishe kwamba kipindi cha mwaka kama hiki sisi kama Wabunge yale majukumu makuu manne ya Mbunge tunasimamia kwanza jukumu la kwanza ambalo ni kwa Taifa lako, la pili kwa jimbo lako la uchaguzi yale ya vyama na mengine unaweka pembeni Taifa linakuwa pamoja tunashiriki pamoja, tunajadiliana pamoja, taifa letu litasonga mbele na tumpe upendo mama Tanzania kwa maslahi ya wote.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia, umeamua kuwa *states man*. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, utafatiwa na Mheshimiwa Selemani Said Bungara

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kuchangia jioni ya leo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizishukuru Kamati zote mbili ambazo zimewasilisha hapa taarifa zao, zimefanya kazi vizuri, zimetuonesha Wabunge kwamba kitu gani kinafanyika kwenye Kamati zao lakini kipekee nimshukuru Waziri wa Nishati Dkt. Kalemari ambaye kwa kweli ni mtambo wa bidii, kijana anayetembea kijiji kwa kijiji, hatua kwa hatua, transfoma kwa transfoma, nguzo kwa nguzo, nyaya kwa nyaya, anafanya kazi nzuri sana tunapaswa hata tulete pongezi hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuwapongeze kwa kazi pamoja na Naibu wake na watumishi wake wote kwa kazi nyingine zinazofanywa na Mawaziri hapa iko siku tufanye kama mlivyofanya juzi kwenye Maspika waliokuja hapa tuanze kuwapa tunzo Mawaziri wanaofanya kazi vizuri humu ndani kwani sisi tuna kosa gani. Mawaziri wanaofanya kazi vizuri kwa mwaka kama huu tunaomalizia tunawapa vyeti au tunawapa zawadi maalum hata tukisema siku moja wachukue posho yetu ya siku moja sio mbaya, wanaofanya kazi vizuri. Kwa hiyo Waziri wa Nishati anafanya kazi nzuri sana na Naibu wake na watendaji wake wote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Ulinzi kwa kweli sijui tunasemaje, katika watu ambao nimewahi kuwaona wanashinda vishawishi vya binadamu hapa duniani wakiwa hai ni Waziri Mwinyi, anafanya kazi vizuri sana. Ameshinda vishawishi vya binadamu na tama za binadamu anafanya kazi vizuri sana. Nimpongeze Mheshimiwa Doto kijana huyu kama tunamtunza vizuri na tunampa moyo atakuwa kiongozi bora katika nchi hii, ana nidhamu ya kutosha, anafanyakazi vizuri, lakini pia nimpongeze pacha mwenzangu Waziri Lugola ambaye ajali imempata kazini, amefanya kazi vizuri huku nyuma, ametufanya sisi Wabunge leo tukitembea barabarani trafiki wanapisha uongo au kweli?

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Kwa hiyo, amefanya kazi, kwa ajali iliyompata ni ajali tu, aendelee kuhangaika na ajali yake lakini alifanya kazi nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri mwenzake aliyekuja alinde yale maslahi ambayo tunaona yapo kwa Wabunge. Pale ambapo tunakamatwa tunafanyaje tukipiga simu apokee haraka. Kwa hiyo niwapongeze wote kwa kazi nzuri waliyofanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge hili katika orodha ya Mabunge, maana yake watu huwa wanasahau, Bunge hili katika orodha ya Mabunge yaliyopita, hili Bunge ni la mfano. Limemsaidia Mheshimiwa Rais kufanya kazi kubwa sana za Kitaifa na lazima tuandikwe kwenye historia.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ndiyo limeleta Bwawa la Nyerere, limetengeneza barabara za flyover, limesaidia Rais kuleta Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya na limetoa elimu bure. Kwa hiyo, Wabunge walioko hapa wote kwa ujumla hata wanaopiga kelele hapa na wenyewe wanaandikwa tu. Maana kelele hapa ni za Bungeni tu, wakienda mitaani kule wanasema nimeleta umeme, nimeleta hospitali, nimeleta hiki. Hawa hawa ndio wanapiga kelele humu ndani. Wakiambiwa wapige kura hapa, wanapiga hapana. Wakienda huko wanajivunia maendeleo ya Chama cha Mapinduzi. Hawana kingine wanachoweza kujivunia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Machi, 2017, Rais wa Marekani anaitwa Donald John Trump alimpongeza Rais wa Tanzania. *What is so special?* Kwa sababu ni Rais bora wa Afrika, alimpongeza Trump. Watu wajue sera zetu za Chama cha Mapinduzi za nchi yetu ya kutofungamana na upande wowote ziko pale pale. Hii habari ya kusema sijui nini kimefanyika huko, sijui Pakistani twende, sijui jambo limetokea tukio mahali twende, sijui nani amesema hivi; hatuendi huko! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sisi ni nchi ambayo inajitegemea, ambayo haifungamani na upande wowote. Watu waje, Marekani ni marafiki zetu. Wakija na upande wa ushoga, hatutaki ushoga. Tutakataa! Maana nawashangaa watu, tunakuwa kama vile mazoba fulani hivi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Rais wa Uganda, Yoweri Museveni amekataa hadharani. Sasa kama kweli hoja yetu ni kukubali ushoga ili tuwe na maadili bora ya nchi hii, hatuwezi sisi mambo ya namna hiyo! Kama ni ushoga, waende kwa wanaoutaka ushoga uko! Sisi hatuwezi kuwa na ushoga. Wanaoutaka ushoga waushabikie. CCM na viongozi wake na Wabunge wake, hatutaki ushoga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwa ndugu yangu Dkt. Kalemami. Naomba Dkt. Kalemami sasa tuelewane na hapa sasa nitaongea pole pole. TANESCO umetembea sana kwenye vijiji, lakini bado uzalishaji wa accessories wanaita viunganishi ni tatizo kwenye nchi yetu. Bado mita ni tatizo kwenye maeneo yetu, bado nguzo kwenye viwanda, Wakandarasi wanaenda kulipa fedha, hawapati nguzo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, bado TANESCO hawajawa vizuri bado, isipokuwa TANESCO Mara kwangu wamekuwa vizuri. TANESCO hawajawa vizuri, hawawezi ku-react haraka kwa watu. Kwa hiyo, tunaomba sasa, kwa kuwa umefanya kazi kubwa sana ya kutembea ardhini, sasa rudi ofisini uwashughulikie wale ambao hawafanyi kazi vizuri ili tuweze kufanya kazi vizuri kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Rais amesema soko lile liitwe Ndugai, lakini najiuliza, tuna jengo la Utawala hapa linaitwa Annex, liko hapo, lina jina gani? Kwa nini Mheshimiwa Rais akuone huko akupe, sisi Wabunge hatuwezi kusema Annex ya Utawala apewe Ndugai? Kuna utata gani hapa? Mimi mbona sioni shida hapa!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi natoa pendekezo, Annex iliyoko hapo iitwe Ndugai, kwani kuna ubaya gani? Amefanya kazi kubwa sana ya Serikali hapa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Nilishamtaja Mheshimiwa Selemani Said Bungara, lakini yupo au ametoka?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Lakini huyu atachafua hali ya hewa, ngoja tuendeleo na mwingine... *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Bungara endelea.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuletea mafuriko katika Wilaya ya Kilwa na familia au kaya 4,000 hazina mahali pa kulala, kaya 4,000 hazina chakula, kaya 4,000, *Allahu Akbar!*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu na nawapa pole wahanga wote wa mafuriko Mkoa wa Lindi. Ninaomba wasamaria wema wote wa Tanzania pamoja na Bunge lako tukufu mtusaidie katika mchango.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Wabunge wote tuwasaidie wananchi waliopata mafuriko, tunaomba sana. Hili liangalie sana, hali siyo nzuri. Mimi nimekwenda Kilwa, nimekaa siku nne, lakini wananchi hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba tufanye mchango tuwasaidie watu hawa. Hata ukisema aah, lakini tulipata tetemeko la ardhi Bukoba Wabunge tulichanga.

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Sasa wewe unayesema, aah, kwa kuwa tumepata mafuriko sisi watu wa Kilwa, sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa mujibu wa Katiba, inasema wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani. Kama kweli nchi yetu tumejenga misingi ya udugu na watu wa Kilwa na Lindi wamepata mafuriko, wewe unasema aah! Basi ile misingi ambayo tumejiwekea kwa mujibu wa Katiba na sisi tumeapa kwa mujibu wa Katiba tumeishika Biblia, na Misahafu, halafu unasema aah, basi *Inshaallah*.

Mheshimiwa Spika, nasema tena, angalia sana, hali siyo nzuri Kilwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa, si utoe hoja basi uone wangapi wanakuunga mkono?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nachangia, nitatoa hoja baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa misingi hiyo ya uhuru, haki, udugu na amani itatekelezwa katika jamii yenye demokrasia ambapo Serikali yake husimamiwa na Bunge lenye Wajumbe waliochaguliwa na wananchi, pia yenye Mahakama huru zenye wajibu wa kutoa haki bila uoga wala upendeleo wowote, hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binadamu zinadumishwa, kulindwa kwa wajibu wa mtu anayetokelezwa kwa uaminifu;

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, Katiba hii imetungwa na Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi. Unajua nchi yetu, sisi tumeapa. Mimi sikuapa kuilinda Katiba ya CUF, sikuapa hivyo! Wala mtu wa CCM hajaapa kuilinda Katiba ya CCM, hatukuapa hivyo. Sisi tumeapa kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini ndani ya mijadala yetu hii sasa hivi hapa ni kwa uchama tu, sijui CCM itashinda! Nyote ndani mtakuwa CCM, CUF mtashindwa!

Mheshimiwa Spika, huko Zanzibar hakuna CUF hata mmoja, hakuna CHADEMA hata mmoja? Mko CCM watupu! Kinachofanyika kitu gani? Haya, mwakani muwe ninyi nyote CCM, Bunge lenu, maana mnasema mtashinda, mtashinda; haya, wote muwe CCM watupu, sisi wengine tusiwepo ndani. Jambo lenu mtasimamia Katiba tu, wala hamsimamii CCM. Tena mtapata taabu sana kwa sababu wa kuwasokola mtakuwa hamna ndani. Mtasokolana wenyewe kwa wenyewe. Badala ya kutushambulia sisi, mtashambuliana wenyewe kwa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana, tuache mambo ya uchama. CCM imeundwa; imeanza kuundwa Tanzania halafu ndiyo CCM; imeanza kuundwa Tanzania halafu ndiyo CUF. Naomba sana tuache mambo ya uchama. Wangapi walikuwepo humu? Wako wapi sasa hivi? Wangapi? Mtu unakuja ndani humu, Bwege utakuwa sio Mbunge. Kwani mwanzo nilikuwa Mbunge? Hata kama nikikosa Ubunge! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba usalama wa nchi yetu, amani ya nchi yetu na amani haipatikani bila haki. Leo tunaongea hapa, tunasema hapa Serikali inajifanya haisikii. Ndiyo maana pia wameenda kumsema Marekani huko, ninyi hamsikii hapa. Mtu akipambana anapambana kwa njia yoyote ile, ndani ya nchi na nje ya nchi. Akienda nje ya nchi, oh msaliti! Usaliti gani wakati ninyi hamsikii hapa!

Mheshimiwa Spika, mimi niliwaambia Waislamu kule wamepigwa risasi, wameuliwa, Serikali iko kimyaa! Msaliti nani? Tukiwaambia hamsikii. Mnaangalia nani kasema? Hamwangalii kasema nini. Tunaitaka Serikali ijue nini inasema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara nilitaka tu kukukumbusha neno moja...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** *Inshaallah*. Nikae!

**SPIKA:** Hapana usikae. Kwa suti uliyopiga leo, *blue* bahari inataka leo upige taratibu taratibu, maana yaani leo uko vizuri. (*Kicheko*)

Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, leo tunasimama hapa, Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sio Mbunge wa CCM wewe, wewe ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi yako ni kuisimamia Serikali. Siyo kila kitu Serikali ikisema baya, ndiyo! Zuri, ndiyo! *Why?* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge sasa hivi mmekuwa kama mbumbumbu; umeshiba? Eeh! Una njaa? Eeh! *Why?* Unachokisimamia hukijui! (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Jamani Wabunge wote wa CCM mmepigwa ganzi? Hakuna hata Taarifa? (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Taarifa ipo.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, unanichanganya bwana!

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara unapewa taarifa bwana, tafadhali. (*Kicheko*)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ananipa nani taarifa? Haya.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa.

#### TAARIFA

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) ambayo inaniongoza niweze kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa kwamba Wabunge wa CCM kwa wingi wao wamekuwa wakitoa ushauri ndani ya Bunge hili ndani ya Kamati za Kudumu za Bunge na wamekuwa pia wakitoa ushauri kwenye mabadiliko mbalimbali ya sheria kwa kuleta *schedule of amendments* ambazo zimekuwa zikichangiwa humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimpe taarifa kwamba tuko vizuri na tuko imara na tunafahamu kazi vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bwege, pokea taarifa hiyo, halafu endelea.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, nimemwelewa sana, lakini nataka nimwulize swali moja halafu ukatoe ushauri. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sisi ni nchi ya kidemokrasia ya vyama vingi vya siasa. Sasa katoe ushauri kuzuia mikutano ya siasa, kuzuia Bunge *Live!* Sasa katoe ushauri huko kwamba ndiyo sheria? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Katiba inasema katika Ibara ya 9 kwamba Sheria za nchi zilindwe na zitekelezwe. Sasa kwa kuwa wewe unasimamia sheria za nchi na zilindwe na kutekelezwa, Sheria ya Mfumo wa Vyama Vingi inavyosema ni kwamba mikutano ya hadhara na maandamano ni haki, wewe unaizuia; kaishauri Serikali yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria inasema lazima isimamiwe na itekelezwe. Sasa kwa kuwa wewe unajua kushauri sana na kuisimamia sana Serikali, sisi vyama vingi tunaambiwa mikutano ya hadhara hakuna, Wabunge tunazuiwa; wewe unasemaje kuhusu hilo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemjibu taarifa yake, akaishauri vizuri Serikali waifuate Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba sana, nawasifia kidogo kuhusu mambo ya umeme. Aaah, kwa umeme *Alhamdulillah!* Kwa umeme aah, mnatufikisha mahali pazuri! Kama mtaendelea hivi kuhusu umeme na mkafanya *speed* katika maji, mkawalipa wakandarasi wa umeme hela zao vizuri, mkawalipa wakulima wa korosho hela zao wote, mkawaongeza mishahara kwa wafanyakazi, kukawa hakuna kesi za kubambikia, kukawa maandamani yapo, aaah, CCM itashinda! Mashehe wale waliokuwa ndani kwa miaka minane mkiwaachia, aaah CCM dole! Ikiwa wenyewe tunalia umeme, Mashehe hawatoki, mishahara hamwongezi, wakulima hamwalipi na kadhalika, aaah, hesabuni kumia tu 2020. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bungara, sijui; ninyi Makatibu mbona hamwangalii muda? *(Kicheko)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninawaomba Wabunge wote mtuchangie watu wa Kilwa, natoa hoja Waheshimiwa mniunge mkono.

**SPIKA:** Hoja haijaungwa mkono bado. Jamani Mheshimiwa ametoa hoja, mnasemaje?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Tunaomba Mkoa mzima wa Lindi, kama tunachangia Mkoa mzima wa Lindi...

**SPIKA:** Hilo tutalifanyia maamuzi baadaye Mheshimiwa Bungara. Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na kimsingi nilikuwa nimeshasimama kwa ajili tu ya kusemea hili la maafa. Kimsingi mimi nimesimama kuunga mkono hilo wazo, lakini nilichotaka kuomba ni kwamba chochote tutakachokifanya kiwe ni kwa Tanzania nzima kwa sababu madhara yako kwa nchi nzima, isiwe kwa Kilwa peke yake. *(Makofi)*

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba nami nirudi kwenye mada. Nazipongeza sana Kamati zote mbili, kwa niaba ya Bunge lako zimefanya kazi kubwa sana. Kipekee naomba niipongeze sana Serikali yangu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesifu, kazi zinazofanyika ni kubwa na nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wamesema Waheshimiwa Wabunge wengi, nikianza na Sekta ya Umeme, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa rafiki yangu Dkt. Medard Kalemani na Wizara kwa ujumla, wamefanya kazi nzuri na kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nifafanue tu kidogo kwa sababu katika Jimbo langu la Msalala tulinfuika na REA II ambayo katika Kata 18, Kata 12 tayari zilishaunganishiwa umeme; na hivi sasa kwenye hii REA III utekelezaji wa mradi unaendelea lakini umeanzia upande wa Halmashauri nyingine. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wanalifahamu hili, lakini angalau ule mpango wa ujazilizi uende kwa kasi kidogo kwa sababu tayari kuna Kata 12 tuna umeme, lakini hata maeneo hayo ambayo umeme umeshafika kama Busangi, Segese, Lunguya na Kakora, umeme upo lakini bado haujasambazwa vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili na ninaamini anaweza kwa sababu kama ambavyo wengi tunamwona, amefika kwangu mara mbili, amelizungumzia suala hili na ninaamini kwamba litafanikiwa kwa mapema. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nitumie muda mwingi zaidi kwenye eneo la madini. Kama ambavyo unafahamu mimi natoka ulipo mgodi wa Bulyanhulu na kwa miaka yote 15 ambayo nimekuwa Mbunge nimekuwa nalalamikia sana namna ambavyo sisi wananchi tuliopo pale ambavyo tumekuwa tukiishi na mgodi wa Bulyanhulu.

Mheshimiwa Spika, na baada ya Mheshimiwa Rais kuwa amechukua hatua hizo alizochukua hizo alizochukua mwaka 2017, nilisimama hapa Bungeni nikampongeza sana, na nilisema kwamba kiukweli kwa sisi tunaoifahamu Acacia ilivyokuwa, ilikuwa haiwezekani kuleta mabadiliko kwenye sekta ya madini bila kuwa na Rais mwenye msimamo na approach ambayo Rais Magufuli ametumia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba tu nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba manung'uniko kwenye sekta ya madini hayajaanza leo na jitihada za kurekebisha mambo yalivyo kwenye sekta hiyo haijaanza kwa Mheshimiwa Rais Magufuli. Mwaka 2005 Mheshimiwa Rais Kikwete anaingia madarakani, moja ya vitu alivyovizungumzia na kuvifanyia kazi ni suala la madini. Alianzisha Tume ya Bomani na mimi nilikuwa mjumbe, tukafanya kazi kubwa. Baadaye ikasababisha kupendekezwa na kupitishwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010; na tukaanza zoezi la kuwaomba hawa wawekezaji waingie kwenye platform mpya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lile halikuzaa matunda makubwa kwa sababu ya Acacia. Ikumbukwe kwamba Acacia ndiye mwekezaji mkubwa kwa Tanzania, ana migodi mitatu. Kwa mwaka 2012 dhahabu iliyozalishwa Tanzania wakia milioni 1.3; migodi ya Acacia ilizalisha zaidi ya asilimia 60. Kwa nguvu hiyo walivyokuwa nayo walikuwa ni kikwazo kikubwa sana katika kuleta mabadiliko kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa na Tume ya Bomani ilikuwa ni kuhakikisha wananchi waliopo jirani na maeneo ya mgodi wanalipwa fidia stahiki. Wenzetu wa Mgodi wa Geita walifanya hivyo; Vijiji vya Mtakuja, Nyamalimbe na Katoma vikalipwa fidia. Toka mwaka 1996 mpaka leo Mgodi wa Bulyanhulu ulipoanzishwa hakuna kijiji hata kimoja kilicholipwa fidia pamoja na kwamba mgodi upo kwenye eneo la vijiji. Kisa

ukiwauliza wanasema tuna *MDA the issue is the government*, sisi ni wawekezaji; kwa kifupi walikuwa wanagoma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukapendekeza, na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ikapendekeza mrabaha utoke asilimia tatu hadi asilimia tano na baadaye asilimia sita; migodi mingine ikakubali wao wakawa wamekataa. Tukasema *service levy* isilipwe kwa *lump sum* ya dola laki mbili, iwe 0.3 percent migodi ya *Geita GGM* wakaanza kulipa, *Acacia* wakakataa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kila kilichokuwa kikifanyika, *Acacia* walikuwa ni kikwazo. Ilikuwa haiwezekani kufanya mabadiliko kwenye Sekta ya Madini bila kuwa-engage seriously hawa. Na pale jitihada za kuwa-engage kidiplomasia kwa lugha ya kawaida ambayo wengine wanapenda zitumike, zilipofanyika ilishindikana. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais baada ya kuja na hii *approach* ambayo ilisababisha dunia nzima kujua kwamba kweli Maige amekuwa akisema *Acacia* ni wezi, imekuja kuthibitika kwamba kweli wamekuwa wakitorosha madini.

Mheshimiwa Spika, tusingeyakamata yale makontena ambayo yapo Dar es salaam na kufanya uchunguzi wa kilichomo mle na kuitangazia dunia kitu gani kipo mle, dunia isingejua. Kwa kufanya hivyo kwa kuonesha kwamba kweli *Acacia* wana matatizo, ilisababisha *the whole word* ikawa *on our side* na ndio maana wao wenyewe wakaja mezani na wakawakana *Acacia* wakaja *Barrick* wanasema tuzungumze. Wangukuwa hawatendi makosa au wangukuwa hawakutenda makosa wasingekubali na tusingefika hapa tulipofika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi nampongeza sana Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa sana na Mungu azidi kumsaidia. Akifika; na wote mnajua mliofika Kakola na Bulyanhulu mnajua kilio cha wananchi wale, leo hii ukifika Kakola, Bulyanhulu na Msalala wananchi wana furaha sana hatua iliyofikiwa ni kubwa sana. Naipongeza sana Serikali na nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hiyo hatua ambayo imefanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais lakini Mheshimiwa Waziri amelisimamia vizuri sana suala hili, suala la wachimbaji wadogowadogo. Baada ya kuwa Serikali imeanza kubana hawa wawekezaji wakubwa mwaka 2015, uzalishaji wa dhahabu ukasimama Mgodini wa Bulyanhulu, tulitegemea uzalishaji wa dhahabu na mapato yanayotokana na dhahabu yashuke; lakini cha ajabu mapato yanayotokana na sekta ya madini yameongezeka kutoka bilioni 130 hadi zaidi ya bilioni 300. Nini kilichofanya matokeo hayo; ni kwa sababu ya kuruhusu wachimbaji wadogowadogo.

Mheshimiwa Spika, leo hii soko dogo la Kakola pale kwangu linauza zaidi ya kilo nne za dhahabu kila siku. Soko la Madini la Kahama linauza zaidi ya kilo 20 za dhahabu kila siku, na hizi zote zinatoka kwa wachimbaji wadogowadogo. Maeneo ambayo wakati wa nyuma yalikuwa yamezuiwa yamewekwa kwenye utafiti wa makampuni makubwa, leo wanafanya wachimbaji wadogo na hizi dhahabu tunapata na maisha yanaendelea. Nawapongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kwa hii dakika moja/mbili zilizobaki nizungumzie maboresho kidogo ambayo yanapaswa yafanyike. Na Mheshimiwa Waziri Biteko naomba unisikilize sana. Kwa kuwa maeneo mengi hayana *proper licenses*, wachimbaji wanaochimba sasa hivi ni wale wenye vikundi; kumekuwepo matatizo mawili; la kwanza kumekuja mtindo wa wasimamizi kuwa wanachukua asilimia 30 ya mawe yanayochimbwa, hili jambo linaleta mgogoro mkubwa. Hii ada ya usimamizi ili Serikali ipate asilimia saba yake, anapewa mtu asilimia 30 ya ada ya usimamizi, wapi na wapi? Ndiyo maana unakuta mgogoro pale Namba Tisa unajua nilikueleza.



Mheshimiwa Spika, wanakuja watu sasa hivi tunaanza kupambana na mabeberu wa ndani kwa sababu vile vikundi vya wananchi wa pale havipewi nafasi, wanakuja mabeberu wa ndani, na nilishakupa majina, wale watu wanapewa usimamizi. Leo hii Wisolele wanasema wachimbaji wadogo wadogo wa pale hawawezi wakapewa kibali cha kuchimba mpaka yule mtu aliyemtaja ambaye nilisema anahusiana na mtu fulani kwenye kamisheni na yule mwingine na yule mwingine. Ninatunza majina kwa sababu Mheshimiwa Waziri tulishaongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo yake sasa hivi kumeanza kutokea manung'uniko, hebu Mheshimiwa Waziri lirekebishe hili wachimbaji wadogowadogo kupitia vikundi vyao ambao wapo kwenye maeneo wapewe vibali na waendeleo kuchimba, hili litatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri nijaribu tu ku-observe, kwamba hivi sasa Kamisheni ya Madini inachukua asilimia saba ya mawe, lakini pia wanapokwenda ku-process kwenye ile mialo, dhahabu inayopatikana na kwenye *elusion* wanapopata dhahabu nako inachukuliwa asilimia 7. Ukiangalia kiuhalisia ni kwamba kuna *double royalty*; tusichukue marabaha kwenye mawe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi tumeshadhibiti utoroshaji wa dhahabu, tuchukue mrabaha kwenye dhahabu, haya mawe yasimamiwe vizuri, yaende kwenye *proper registered* sijui kiingereza wanaitaje lakini kwa Kiswahili tunaita mialo, yaende kwenye *proper registered* mialo, pale dhahabu ikipatikana asilimia saba ichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, unajua wachimbaji wadogowadogo waliopo kule wengi wao unakuta wapo kwenye vikundi wanakuwa kikundi cha watu 20, wanapata mifuko 50 wakichukua mifuko 50, mifuko ya Serikali inakuwepo labda mifuko nane. Ikishachukuliwa mifuko nane wanatoa na gharama zingine unajikuta kila mchimbaji anapata mfuko mmoja au robo mfuko, wanatesema sana. Wale wachimbaji kabisa kwa maana ya wale wanaoingia kwenye mashimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, hatua hizi ni kubwa na nzuri lakini haya madogomadogo ambayo nimeyazungumzia yaweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho; tumefanya makubwa na tumefikia hatua kubwa ya kuanzisha hii kampuni ya Twiga. Niombe madai ya wananchi wa Bulyanhulu toka mwaka 1996 kama migogoro mingine ya wafanyakazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ezekiel bahati mbaya muda haupo upande wako.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, sentensi moja tu. Na migogoro ya hawa wafanyakazi waliofukuzwa na wengine wagonjwa, hebu tuimalize. Mheshimiwa Waziri tulishaongea lipo kwenye hatua ya mwisho. Basi kwa hayo, naunga mkono hoja naamini Serikali itaendelea kutenda mema, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jesca Kishoa, tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya nje.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchukua fursa hii kukishukuru Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ngazi ya Kamati Kuu kwa kuiteua kuwa mgombea wa nafasi ya Naibu Katibu Mkuu Baraza la Wanawake upande wa Bara. Pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Kamati Tendaji ya Baraza Taifa ambao wamenipa ushindi wa kishindo wa asilimia 84 kwa nafasi ya Naibu Katibu Mkuu upande wa Bara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie, na nijikite upande wa Wizara ya Nishati. Nitazungumzia upande wa TPDC hoja ambayo kwenye hotuba ya kamati imezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada ambazo zinaonekana kufanywa na TPDC bado kuna changamoto kubwa ambayo inaendelea kwenye Kampuni hii ya mafuta na gesi ya Taifa hili; na changamoto hii ni kukosa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa. Ni bahati mbaya sana tumekuwa na changamoto kubwa ya viongozi ambao wamekuwa wakitoa kauli za mazoea. Kuna kauli mbili ambazo zimekuwa zikitamkwa na viongozi pale ambapo wanakuwa wanaona joto la wananchi wa Tanzania lipo juu kuhusiana na utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, moja ya kauli ambayo wamekuwa wakiisema, wamekuwa wakisema kwamba mradi huu haujatekelezeka kwa sababu majadiliano yanaendelea, hiyo ni kauli namba moja. Kauli namba mbili wamekuwa wakisema mradi huu haujatekelezeka kwa sababu majadiliano kuchukua muda mrefu ni jambo la kawaida sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo moja. Si kawaida kabisa majadiliano kuchukua muda mrefu, *this is very primitive thinking*, haya ni mawazo mgando, ni lazima tuseme. Nilisoma jarida la *The East African* la mwaka jana mwezi wa 5 tarehe 15 kuna kampuni moja kubwa sana inaitwa Delloitte; kati ya makampuni 4 makubwa, Delloitte ni mojawapo ambayo imeeleza *specifically* Tanzania imepoteza sifa ya kuwa nchi yenye vivutio vya kuwekeza kwa sababu tu ya kuchelewa (*delays*), kuwa na mawazo mgando, mawazo ya kujadiliana muda mrefu, majadiliano yasiyokwisha, miradi isiyotekelezeka; tumeingia kwenye rekodi kama taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mradi wa LNG ni moja ya mradi ambao unaonesha namna ambavyo Serikali inashindwa kuchukua maamuzi kwenye mambo mazito na makubwa kwa maslahi ya taifa. Serikali kwenye mradi wa LNG umekuwa ukitoa kauli za mara kwa mara kwamba majadiliano yanaendelea. Ni mwendo wa konokono, kwa maana ya kwamba hakuna kinachoeleweka mpaka dakika hii, miaka na miaka hakuna kinachofanyika, *investment* ya over 30 billion dollars katika Taifa letu, *investment* ambayo ni kuwa East Africa nzima hakuna lakini Serikali inashindwa kufanya maamuzi sahihi, wanakimbilia kusema kwamba kuna migogoro kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, *let me ask you something*. Kwa muda gani tunakwenda kusubiri kuona migogoro ya wawekezaji inakwisha, *what if* kama migogoro yao ikichukua miaka 50? Tunakwenda kuwasubiri kwa muda kwa kiasi gani? Mlitafuta kampuni kwa ajili ya ku-*negotiate on behalf of the Government* kwenye mradi huu wa LNG kwa sababu ya ukubwa wake. Mmeshindwa kweli kuibana/ku-deal na kampuni hii ikaja na majibu ya uhakika ya namna gani mnavuka /mnakwenda kutekeleza mradi wa LNG kwa kuwepo na huu mgogoro ambao ni wa wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, mambo kama haya, mradi mkubwa kama huu ambao unaangaliwa kwenye mataifa mengi ndivyo hivi vitu vinavyo-*test credibility* ya Serikali katika Taifa letu. Sasa ni vema Serikali ikatuambia kwenye mradi wa LNG, mradi ambao ni mkubwa sana na unakwenda kusaidia wananchi wengi sana katika Taifa letu; kampuni hii imeshindwa kweli kutekeleza/kutusaidia kuvuka hapa na tukahakikisha kwamba tunaweza kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Spika, bado kuna suala la mwendo wa konokono kwenye mradi wa Bomba la Mafuta la Hoima. Nimemsikiliza Mkurugenzi wa TPDC mwaka jana mwezi wa tisa anasema mradi huu utatekelezeka lakini bado majadiliano yanaendelea; bado tupo palepale mwendo wa konokono, haya majadiliano yanakwenda mpaka lini? Haya majadiliano yanakwenda kwisha lini? Dunia inakwenda speed sana, lazima tu-cope na speed ambayo dunia inakwenda.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa kiwanda cha mbolea kule Lindi (*Fertilizer Plant*). Kuna makampuni matatu makubwa kutoka Ujerumani ambayo yameomba kujenga kiwanda cha mbolea Mkoani Lindi na kiwanda hiki kinakwenda kutumia gesi, lakini cha kusikitisha ni kwamba pamoja na kwamba kiwanda hiki kinakwenda kuwa kikubwa Afrika nzima lakini Serikali kupitia TPDC bado inakwenda mwendo wa konokono. Ni vema tukaelewana hapa vizuri sana. Kupitia vyombo vya habari nilishuhudia Mheshimiwa Rais akiongea na *Chancellor* wa Ujerumani wakizungumza namna gani wanakwenda kutekeleza mradi huu lakini mpaka sasa hivi ni story tupu, hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Spika, labda nizungumze kidogo kuhusiana na mradi labda mnaweza mkaelewa kuanzia hapo. Kama tunataka ku-*transform* Taifa hili kwenye sekta ya *agriculture*, hiki kiwanda hakiepukiki kwa namna yoyote ile. Hakiepukiki kwa sababu wote tunajua kwamba 75 percent ya wananchi wa Tanzania wanashiriki kwenye Sekta ya Kilimo. Serikali imekuwa ikiagiza mbolea kutoka nje; asilimia 90 inayotumika Tanzania inatoka nje.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mwaka 2016/2017 zinaonesha Serikali iliagiza tani za mbolea takribani 150,000, lakini kama ikitokea tukakubali mradi huu/kiwanda hiki kikajengwa, tunakwenda kutengeneza tani 1,300,000 za mbolea kwa mwaka. Kwa hesabu za haraka haraka ni kwamba nchi hii ili iweze kupata mbolea ya kutosha inahitaji mbolea zaidi ya tani 580,000, kwa hiyo tukipata tani 1,300,000 tuna uhakika wa kupata mbolea ndani na tuna uhakika wa kuuza mbolea nje, tunasubiri nini? *What are waiting for?* Hiki kiwanda kinakwenda kutengeneza zaidi ya ajira 500,000 kwa wananchi wa Tanzania lakini shida inabaki palepale, ukiuliza unaambiwa majadiliano bado yanaendelea yaani ni mwendo wa konokono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mimi nafikiri huu mwendo wa konokono tukawa na jambo moja, unatokana na hofu ya viongozi kwenye sekta husika, wanahofu ya kutumbuliwa. Kumekuwa kuna shida hii kubwa, maamuzi magumu ambayo yanatakiwa yafanywe kwa maslahi ya Taifa, viongozi wa Serikali wameingwiwa na hofu wanashindwa kuyafanya kwa kuhofu kutumbuliwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuiomba Serikali iipe nguvu TPDC, TPDC haiwezi kufanya kazi kama hamuwezi kuipatia fedha kwa namna yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie na hoja ya TEITI; nilizungumza hapa mwaka jana kwamba na kwenye taarifa ya kamati imezungumzwa. TEITI iligundua kuna ubadhilifu wa zaidi ya bilioni 30 kwenye sekta ya madini; lakini tangu mwaka jana mpaka hivi ninavyozungumza hatujaona taarifa yoyote ambayo inaweza kuelezea na kudadavua suala hili. Nilipozungumza suala hili mwaka jana, Waziri wa Madini wa wakati huo Mheshimiwa Angella Kairuki alisimama na kusema suala hili lipo kwa CAG na litafanyiwa kazi mpaka kufikia mwezi wa 12... (*Makofi*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:**... lakini mpaka hivi ninavyozungumza hakuna tatizo...

## TAARIFA

**SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa kuna taarifa unataka upewe.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe tu taarifa mchangiaji anayechangia sasa kwamba viongozi wa Serikali wakiwemo Mawaziri, Wabunge, RAS pamoja na RAS wa Mkoa wa Songwe Mheshimiwa Kafulila wapo vizuri hawa hofu yoyote na ndio maana nchi yetu ya Tanzania inaendelea kupaa, miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa. Sasa kama anachangia aende kwenye hoja za msingi asizungumzie suala la viongozi wana hofu, wapo vizuri, imara na wanatekeleza majukumu yao ipasavyo, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Shemeji umepewa taarifa hiyo, unasemaje? (Kicheko/Makofi)

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, kunaona kuna taarifa kupokea hapo? Kwanza nimuulize *TEITI* ni kitu gani, *do you know what is TEITI*, unajua *TEITI* ni kitu gani? Tunazungumzia *issues*, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunazungumzia *issues*, *we are not doing politics here* tena *cheap politics*; tunazungumzia masuala kwa maslahi ya Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka wakati Waziri wa Madini au Waziri wa Nishati, maana *TEITI* bado haijajulikana iko Wizara gani, anapokuja kuhitimisha hapa atuambie fedha zetu bilioni 30 ambazo zimeonekana zimepotea kwenye Wizara ya Madini zimekwenda wapi, kwa sababu ni taarifa ya kutoka *TEITI* na *TEITI* ni shirika la Serikali.

Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Ngoja upokee taarifa Mheshimiwa Jesca.

## TAARIFA

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ili tumsaidie mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakati anahitimisha hoja yake, awe *focused*, ninataka tu nimpe taarifa msemaji na kwa kweli Mheshimiwa Angellah Kairuki wakati akiwa Waziri alilieleza vizuri sana; hakuna fedha iliyopotea. *TEITI* kinachotokea ni kwamba makampuni yanapeleka hesabu na wao wanakwenda kuangalia kule mnakopeleka fedha kwa ajili ya kufanya *reconciliation*.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni kwamba yule mtu aliyekwenda kufanya *reconciliation* alivyokwenda kwenye *source* akakuta kilichoripotiwa na makampuni na kile kilicholipwa kuna *difference* ya hizo fedha. Na sasa kinachotokea ni kwamba kuna mahali pengine ambapo wameripoti wamelipa shilingi kumi halafu kuna mahali hiyo shilingi kumi imeripotiwa mara mbili. Kwa hiyo CAG anachokwenda kufanya ni *verification* ya hiyo *reporting*, huo sio wizi. Na kwenye ripoti hiyo imeelezwa sio wizi, ni *reconciliation*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpa taarifa hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kishoa, malizia maana yake muda hauko upande wako.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana, napokea taarifa yake kwa sababu amekiri kwamba kuna fedha bilioni 30 hazionekani. Lakini pia kuna shida gani kumpa CAG akakagua hizi bilioni 30 zimekwenda wapi? Kwa nini suala hili limepigwa danadana toka mwaka jana, shida iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri hakuna sababu ya Waheshimiwa Mawaziri kuendelea kujitetea kwenye hili, ni suala la mambo kuwekwa wazi kuonekana kwamba, *okay reconciliation* inatakiwa ifanyike; imefanyika? Hizo fedha ambazo zimepotea zimekwenda wapi? Kwa nini maswali haya yanakosa majibu? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, ni kengele ya pili. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Jesca. Mheshimiwa Joseph Selasini uwe mchangiaji wa mwisho halafu Naibu Waziri wa Mambo ya Nje.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na mimi nimeomba nafasi hii kwa sababu ya mambo madogo mawili tu ambayo nilifikiri ni muhimu niyazungumze katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 85 ya watu wa Rwanda ni wakristo, na kama mtakumbuka mauaji ya Kimbari yaliyotokea Rwanda wakristo hawa hususan Wakatoliki wenzangu walihusishwa sana na yale mauaji, na ni kweli kwa sababu kuna wahanga walikimbilia katika makanisa, lakini baadhi ya mapadre wakawatosa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ili baadaye nieleze ninachotaka kusema ninakumbusha miaka ya 1980 kulikuwa na mihadhara inaendelea nchini kwetu, na mihadhara hii iliwahusu sana Wakristo na Waislam. Wakristo tulilalamika sana Waislam walipokuwa wanalitaja jina la Bwana Yesu na walikuwa wanasema kwao ni Nabii Issa Aleyhi-Salam, lakini mapambano yalikuwa makubwa matokeo yake mihadhara iliachwa. Hakuna asiyekumbuka kipindi kile hali ilivyokuwa mbaya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kusema ili niweze kueleza vizuri hoja yangu, Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli anahimiza Watanzania tufanye kazi ili kila mtu aweze kupata ujira wake na kipato chake kutokana na kufanya kazi, na hata vitabu vya dini vinahimiza kazi. Mtume Paulo kwa Wakristo mnajua anasema asiyefanya kazi na asile chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu ya hoja ya ulinzi na usalama tunayojadili na sasa hapa nataka ku-refer Wizara ya Mambo ya Ndani. Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo inayosajili vikundi vya dini katika nchi yetu na kwa maoni yangu ni kwamba sheria iko wazi na kanuni zipo na Wizara inajiridhisha kabla ya kufanya huo usajili. Na niseme wazi mimi sina tatizo na kikundi chochote cha dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yapo matendo ambayo yanafanywa na baadhi ya vikundi vya dini yasipoangaliwa na nchi na wenye mamlaka yanaweza yakalitumbukiza Taifa hili mahali pabaya kwa sababu ya hofu ya kuingilia uhuru wa dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama anasimama Mchungaji au Askofu anawaambia watu fungueni mapochi yenu hela ziingie na anatoa hotuba labda kuanzia asubuhi mpaka jioni, ni wazi vijana wataacha kufanya kazi, watakwenda kufungua mapochi yao wakisubiri fedha ziingie kwa upepo wa kisulisuli. Sasa hii si sahihi. Na ndiyo maana nasema kama Wizara inavijua vigezo vya kusajili haya makanisa, mambo kama haya Wizara inapaswa iingilie kati kwa sababu jambo kama hili likiendelezwa linaharibu nchi. *(Makofi/Kicheko)*

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, wako wengine anasajili kanisa, baba ni askofu, mama ni mchungaji, kijana anaokota sadaka wanaweka maturubai barabarani ndiyo kanisa, wanawadanganya wananchi kwa kuwapa maji wanasema ni ya upako, wala maji hayo hatujui kama yamepitia TBS, wanawapa mafuta wanasema ni ya upako, hatujui kama yamepitia TBS, halafu matokeo yake watu wanachukua wanabugia tu wanaokota sadaka. Kwangu mimi anapomtaja Bwana Yesu au Roho Mtakatifu katika hoja kama hiyo mimi naona ni kashfa kwa sababu huyo sio Roho Mtakatifu ni roho mtaka vitu. Na lazima Wakristo wanajua tofauti ya Roho Mtakatifu na roho mtaka vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mengi yanayoendelea, na wanaoumia ni akina mama. Sijui ni kwa sababu gani kwa sababu akina mama wengi ndio wanaoonekana kwenye makanisa hayo. Mtu anawaambia akina mama waondoe nguo za ndani wapunge hewani ili wapate ujauzito, tunaona tu na Serikali ina mkono mrefu nina imani hata kwenye haya makanisa Serikali ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa iko siku wanaoamini katika roho na kweli hao wakwelikweli wataamua kumtetea Yesu Kristo, bwana na mwokozi wa kweli baada ya kuchoka kashfa hizi na itakuwa mbaya.

Sasa mimi naiomba Serikali isogope kupitia sheria inayosajili hivi vikundi vya dini. Kama kuna haja ya kuihusha iihushie ili iweze kuangalia ni vikundi gani kweli vya dini au ni vikundi gani vimekuja nchini kuja kufanya utapeli kwa ajili ya kuwaibia Watanzania. Serikali inao wajibu wa kulinda raia wake na kitu kidogo ambacho raia wanapata ili matapeli wasije wakaingia wakawapora.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumza ni kwamba tunakwenda kwenye uchaguzi na Mheshimiwa Rais wiki iliyopita amesema kwamba atahakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Sasa uko ushauri amekuwa akipewa, wiki hii amepewa ushauri na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, nina hakika atauzingatia na ninamuomba auzingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini na mimi nataka nimpe ushauri ambao tumekuwa tukiusema mara nyingi, wapo Watanzania wengi wanaoishi nchi za nje wakifanya biashara au wapo katika balozi zetu, sasa hivi tunahusha daffari la kupiga kura bado hakuna kauli ya wazi ni namna gani Watanzania hawa watapata nafasi ya kujiandikisha kupiga kura au ni namna gani watakavyopiga kura. *(Makofi)*

Kwa hiyo ninaomba wakati ushauri mbalimbali ukitolewa na kuzingatiwa basi jambo hili ambalo tumelizungumza muda mrefu kwa miaka mingi lizingatiwe kwa sababu ni haki ya Kikatiba ya kila Mtanzania kuchagua uongozi wa nchi, kuchagua viongozi wanaowataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni kwamba mtu akiwa mfungwa au akiwa mahabusu hapokwi haki zake. Hata jana au juzi tulimsikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali akisema kuna haki ambazo wafungwa wamepewa na hazipaswi kuondolewa. Haki moja wapo ni hii ya kuchagua, wale wafungwa na wenyewe tunaomba wakati mazingatio yakifanyika ya namna tutakavyokwenda kwenye uchaguzi huru na wa haki, nao waweze kupewa nafasi ya namna ambavyo watajiandikisha na namna ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ninawaomba Watanzania wa vyama vyote, wa taasisi zote, kwa kawaida tunapokwenda kwenye uchaguzi lazima mihemko inapanda kwa kila mtu. Juji Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi aliwakemea wale vijana ambao walikuwa

wanawaalika wenzao kwa ajili ya kuwadhhibiti vijana wa vyama vingine, hili ni jambo zuri alilofanya na kwa kweli nampongeza kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini twende mbele zaidi, ile ni jinai, watu wanaofanya jinai namna hiyo wasikemewe tu kwa sababu watazoea kukemewa, watazoea kudekezwa. Imani yangu ni kwamba kama Serikali watu wa namna hiyo isipoanza kuwadhhibiti tangu mapema zikaanza kutolewa kauli za kutishana namna hii, matokeo yake tunaweza tukafika kwenye uchaguzi tukiwa hatuko salama, tukafika kwenye uchaguzi nchi ikiwa vipande vipande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba sana sisi Wabunge, viongozi wa vyama, wa taasisi za vyama na mabaraza ya vyama tujiepushe na kutoa kauli za kuwachochea Watanzania, za kuwachochea vijana wetu katika muda huu kwa sababu uchochezi huu unaweza ukaligawa hili Taifa na hatuna nchi nyingine zaidi ya Tanzania na tunao wajibu wa kuilinda Tanzania kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Sasa Waheshimiwa Mawaziri naomba tujitahidi tu kutumia muda tulionao ambao ni mdogo sana wa dakika tano/tano. Tuanze na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kalemani wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote nitoe shukrani za dhati kwa Kamati kwa taarifa yao nzuri ambayo wamewasilisha leo katika Bunge hili tukufu na ambayo kwa uwazi kabisa imesifia utendaji mzuri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa hizo ambazo tumezipokea kwa mikono miwili toka kwenye Kamati zinatokana na kazi nzuri ambayo Wizara inaifanya katika kudumisha mahusiano ya kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipimo cha mahusiano ya kidiplomasia kipo cha aina tofauti. Kila mtu anaweza akajaribu kutaka kupima kwa vile anavyopenda yeye lakini kuna vipimo rasmi ambavyo wataalam wanavitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja, tunaangalia tuna balozi ngapi katika nchi mbalimbali na balozi ngapi zina uwakilishi hapa nchini. Kwa kipimo hicho tumefanya vizuri sana na tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunaangalia tunashirikiana kiasi gani na nchi mbalimbali. Hivi juzi Waziri wa Ulinzi amepokea msaada wa magari ya jeshi kutoka Marekani. Hicho ndicho kipimo cha uhusiano wetu wa kidiplomasia kati ya Tanzania na Marekani, uhusiano mzuri kiasi kwamba tunaweza kushirikiana hata katika masuala ya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mahusiano yetu na Jumuiya ya Ulaya ni mazuri sana. Jumuiya ya Ulaya imeleta Balozi wake, ameshawasili na anafanya kazi vizuri na sisi tumepeleka Balozi Brussels na kwa maana hiyo tayari Jumuiya ya Ulaya imeshaweza kuleta fedha, Euro milioni 62, kuthibitisha mahusiano hayo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuelewa misingi ya diplomasia duniani, watu wengi sana wamechangia na niwaombe wote waliochangia kwanza wakasome *Montevideo Convention* ya mwaka 1933, lakini pili, wakasome *Westphalia Treaty* ya mwaka 1648, hizi nyaraka mbili ndiyo

miongozo thabiti ya kidiplomasia duniani. Tusije tukachangia tukadandia gari wakati hatujui gari linaelekea mwelekeo upi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe ufafanuzi kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge na kwa faida ya Watanzania wote ambao wanatuangalia. Mheshimiwa Salome Makamba wakati anachangia amesema kwamba Wizara ilitoa majibu mabaya dhidi ya Serikali ya Marekani. Naomba niliambie Bunge lako tukufu kwamba Wizara haijatoa kauli yoyote kujibu Serikali ya Marekani na kwa misingi hiyo, nimuombe Mheshimiwa Salome Makamba alithibitishie Bunge hili ni taarifa ipi ambayo Wizara imetoa dhidi ya Serikali ya Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia limeongelewa suala la wanafunzi na Watanzania waliopo China na fishio la ugonjwa unaosababishwa na *virus* anaitwa *corona*. Kwa sababu suala hili ni muhimu, nalo naomba nilitolee ufafanuzi; mpaka tunavyoongea hivi sasa, katika Jimbo la Huan na Mji wa Hubei kuna wanafunzi wa Kitanzania 437 na kuna familia moja ya Kitanzania yenye watu wanne, hivyo kufanya Watanzania waliopo katika jimbo hilo kuwa 441.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ambazo tunazipata mara tatu kwa siku, kama vile dozi ya *panadol*, hakuna Mtanzania ambaye ameathirika na ugonjwa huo. Hivyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba Watanzania waliopo China katika Jimbo la Huan wako salama salimini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeruhusu Watanzania wengine kutoka kwenye majimbo mengine waweze kurejea pale wanapopenda wao kurejea kwa sababu tunaheshimu uhuru wao wa kuweza kutembea na kuja huku kusalimia ndugu kwa sababu hawatoki katika jimbo hatarishi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje. Muda ni mfupi, najua ulipenda utufafanulie mambo kadhaa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Kalemani, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kwa hatua hii kwa sababu mambo ya msingi ambayo tunatakiwa tuyazungumze leo yana itifaki kubwa sana katika mustakabali wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kuendesha mjadala huu vizuri, na unaweza ukaona pande zote zinaridhika kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kazi vizuri sana katika masuala yote ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, kaka yetu Mheshimiwa Kitandula na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati. Lakini kwa aina ya pekee naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kipindi chote cha miaka minne iliyopita, wamekuwa wakitoa msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapoona Wabunge wanakuja kwenye kiti chetu hapa si kwamba wanakuja kuomba misaada au miradi ya umeme vijijini kwa upande wao, mara nyingi huja



kutoa ushauri. Na kwa kiasi kikubwa tunawashukuru sana, tumezingatia sana ushauri wenu na ndiyo maana tumefika hatua hii. Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo sasa kuchangia kwenye mada ya leo. Yapo mambo mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa sababu ya muda nitaongea kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. Katika awamu hii, yako mambo mengi sana ambapo Tanzania itakumbukwa katika vitabu vya Watanzania kwa historia ya miaka mingi ijayo. Kuna miradi mikubwa sana ya vielelezo ambayo imetekelezwa na kila mtu ni shahidi. Mradi wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji almaarufu Julius Nyerere, kama ambavyo mnafahamu, unaenda kuondoa kero zote zilizokuwepo katika masuala ya undeshaji wa nishati hapa nchini. Kwa hiyo, ni hatua kubwa sana Awamu ya Tano imefanya katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nami nawashukuru Waheshimiwa Wabunge jambo hili mnalifahamu. Jambo la pili katika hili, tumeingia katika historia ya kidunia. Mradi huu tumekuwa tukisema mara zote na ninapenda nirudie tu, ni mkubwa sana katika mabwawa yote duniani. Kwa mara ya kwanza tunaingia kwenye kitabu cha kidunia cha kutekeleza miradi mikubwa kama hii. Ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kabla ya mwaka 2015 tulikuwa na uhaba mkubwa sana wa umeme. Tulikuwa na upungufu wa umeme takribani Megawati 270, ndiyo maana tulikuwa tuna mgao wa umeme, kwa maana ya kugawiana kidogo tulichokuwa nacho. Kwa leo mnaona kuna mabadiliko makubwa sana, tuna zaidi ya Megawati 280 mpaka 320 kwa siku. Hii ni hatua kubwa sana imefanyika kufikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia sasa kwenda kwenye jambo kubwa sana la pili la kihistoria kwa nchi yetu; kuendesha treni itakayotumia umeme katika mwendo kasi. Hii ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kuanza kutumia umeme, kuendesha treni ya mwendo kasi. Tumetenga takribani ya Megawati 70 na treni kama mnavyojua, itakwenda umbali wa speed kubwa. Huu ni umbali mrefu sana, tunajenga mradi huu kwa umbali wa kilometa 160 na gharama yake ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwamba haya ni mabadiliko makubwa ambayo hayatasahaulika. Ingawaje halijajadiliwa hapa, lakini niseme, haya masuala mawili katika miaka miwili ijayo mradi mkubwa utakamilika Juni, 2022, na huu mradi wa SGR utakamilika hivi karibuni ikiwezekana mwakani, mtaona matokeo yake jinsi nchi itakavyopaa kiuchumi na tunasema Tanzania inaweza ikawa ni Tanzania ya miaka zaidi 40 kwa mfano wa nchi za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye hali ya umeme nchini. Ni kweli hali ya umeme imeendelea kuimarika sana. Nyote ni mashahidi, wote mliokuwa mnapita Kariakoo, mliokuwa mnapita Manzese, mlikuwa hamwezi kupokea sumu kwa wakati huo kwa sababu ya kelele za majenereta. Leo hii Awamu ya Tano imezima majenereta, unaweza ukaongea na simu wakati wowote, maeneo yoyote bila kuwa na wasiwasi. Ni kielelezo rahisi sana lakini ni rahisi kukiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la msingi kabisa, toka mwaka 2015 mtandao wa umeme nchini ulikuwa ujafikia asilimia 70, leo tunapongeza hapa katika nchi yetu tumeshatandaza umeme kwa umbali wa kilometa 130,000 nyaya kote nchini zimeshapita, hakuna mahali nyaya ya umeme haijafika kwenye nchi hii. Ni jambo ambalo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na idadi ya nguzo kwa wakati huo milioni 1.1, leo tuna idadi ya nguzo zilizosimikwa na zenye umeme milioni 3.3, ni jambo kubwa sana. Tulikuwa na transfoma takribani 65,000, leo tuna transfoma 142,000. Ni kazi kubwa sana zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa sababu ya muda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia ya mwisho.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mambo ya msingi ambayo ningependa nizungumzie hapa ni umeme Vijijini. Mwaka 2005 tulikuwa na umeme katika vijiji 231; mwaka 2008 tulikuwa na umeme katika vijiji 561, mwaka 2015 tulikuwa na umeme katika vijiji 218; leo tunapooonga kwa heshima ya Watanzania wote, tuna vijiji takribani 8,674 vina umeme hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili unaweza ukaliona ni jepesi. Kwa Afrika sisi kwa sasa hivi ukiondoa Nigeria ambao wameshafikia asilimia 72 na wanaelekea 75, sisi tunategemea kufikia asilimia 76 mwakani na kuipita Nigeria. Kwa hiyo, tunaweza tukaanza kuongoza katika umeme Vijijini. Jambo hili ni kubwa sana na tunaomba sana tuipongeze sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na kupeleka umeme katika vijiji nilivyotaja, nchi yetu ina takribani ya Wilaya 180 na kitu; hivi sasa Wilaya 34 tumekamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyake vyote. Wilaya hizo tutapeleka umeme kwenye Vitongoji tu, lakini kama Wilaya tumeshakamilisha. Hata kwako, vile Vijiji vya Saigoni, Makutupa pamoja na Soni na Laiboni, tumeshakamilisha na kwa kwako tutapeleka Vitongoji tu. Kwa hiyo, niseme kwa niaba ya Watanzania, nawashukuru sana wananchi kwa kukubali hili. Kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, umeme tunaopeleka katika Vitongoji kwa kweli ni mara ya kwanza mnashuhudia, hakuna nyumba ya Mtanzania inayoachwa bila kupelekewa umeme. Nyumba za aina zote wananchi wanafurahia; wa maisha ya chini, kati na juu wanafurahia katika mpango huu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, la mwisho LNG...

**SPIKA:** Nakushukuru sana, ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kazi iliyofanyika hata Mheshimiwa Selemani Bungara amekiri, kwa hiyo, tunakushukuru. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, kweli kabisa!

**SPIKA:** Mheshimiwa George Simbachawene.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Spika, tena wanapongeza mpaka ile hela ya kuwekea umeme imepungua, nawapongezeni. Kwa hapo tu, *Alhamdulillah!* *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Unamwona Mheshimiwa Dkt. Kalemani! Tunashukuru sana. Mheshimiwa George Simbachawene tafadhali, dakika tano, chache.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kukushukuru kwa kusimamia vizuri mjadala huu na pia kwa shughuli zote ambazo unafanya kwa Bunge hili na kwa nchi hii tutakukumbuka sana na historia yako itabakia. Ni katika kipindi chako mambo makubwa na mengi yanafanyika katika nchi ambayo nchi hii inaweka msingi mzuri wa kwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili namshukuru sana Kamati ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Salum Rehani, Mbunge wa Uzini kwa kazi kubwa na maoni mengi mazuri ambayo wameyatoa, nasi kama Serikali kusema kweli baadhi yake tunakubaliana nayo na tutayachukua.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa waliochangia na kugusa Wizara ya Mambo ya Ndani sio wengi sana, lakini kwa hawa wachache wamezungumza mambo ambayo yanagusa maeneo makubwa na kwa sababu ya muda nitajaribu kuongea kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakimbizi tulionao hapa nchini ni wengi, hadi jana walifikia kiasi cha tunawakimbizi hapa nchini 293,931. Katika idadi hii, wakimbizi wengi zaidi wanatoka Burundi ambao wako 217,501.

Mheshimiwa Spika, jitihada kubwa zinafanyika kuhakikisha kwamba wakimbizi hawa wanarudishwa makwao. Mwezi Novemba, 2019 mwaka jana yalifanyika makubaliano kati ya UNHCR, Serika ya Tanzania na Burundi juu ya utaratibu mpya. Kwa sababu pamoja na wale waliokubali wenyewe kwa hiari yao kurudi kwao, lakini *logistic* namna ya kuwarudisha nyumbani imekuwa kidogo zina mchakato mgumu. Kwa hiyo, tumekubaliana kuweka malengo kwamba kila wiki tutarudisha wakimbizi 2,000, ni imani yangu kwamba kama hili likitoka tukalisimamia, basi idadi kubwa ya wakimbizi watakuwa wameondoka nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia jambo la pili ambalo lilizungumzwa hapa ni juu ya vitambulisho vya Taifa jukumu ambalo linafanyika na NIDA. Kazi kubwa imefanyika sana tu, kwa sababu mchakato wa kutoa vitambulisho vyenyewe kuwakabidhi wananchi ni wa mwisho kabisa; lakini kuandaa mpaka kufikia kutoa vitambulisho, ndiyo kazi ngumu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii imefanyika, lengo letu ilikuwa ni kutoa vitambulisho milioni 24,200,000. Katika usajili, tumesajili 20,131,014, alama za kibaolojia tumeweza kuchukua 18,157,624, lakini kuingiza kwenye mfumo, tumeingiza 16,240,341. Kwa hiyo, utakuta kwamba karibu tumefanya kwa haya yote yote kwa kiasi kikubwa vizuri, kasoro ile hatua ya mwisho. Kwa upande wa vijijini tumeweza kuhakiki wananchi 15,488,766, pia tumetoa namba za utambulisho 13,872,281, lakini vitambulisho tulivyovitoa ni vichache na sababu kubwa ni mtambo wa kuzalishia vitambulisho hivi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa jitihada kubwa inafanywa kukamilisha mtambo ambao tayari umenunuliwa, una kasoro kidogo ambazo ni chache, unarekebishwa na tunaufunga pale Kibaha ili tuweze kutoa vitambulisho vingi; na uwezo wa mtambo huo ni kutoa vitambulisho 9,000 kwa siku moja. Kwa hiyo, ninaamini kwamba tutaweza kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, zimezunguziwa jitihada za kupunguza mahabusu. Jitihada kubwa zimefanyika lakini hata hivyo, pamoja na kufanyika jitihada hizo za kupanua Magereza hasa na kurekebisha miundombinu ya Magereza ni lazima pia jitihada nyingine hizi

tuweze kuziendeleza. Tumeamua kuunda Kamati ya kusukuma kesi, pia DPP anazunguka katika Magereza na kuhoji mahabusu waliokaa muda mrefu ili kesi zao ziweze kusikilizwa kwa haraka. Kwa hiyo, jitihada zote zinaweza zikasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni hili la uhuru wa kuamudu ambao upo kwa mujibu wa Katiba. Hoja iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, pamoja na uhuru huu lakini lazima tuangalie namna ya kuudhibiti au kuuwekea utaratibu uhuru huu. Nakubaliana kabisa kwa asilimia 100 kwamba kanuni zetu hazioneshi namna nzuri zaidi ya kuweza kuweka mfumo mzuri wa udhibiti wa uhuru wa kuabudu. Serikali haiingilii kamwe na wala haitaingia kamwe uhuru wa kuabudu, lakini kuweka utaratibu unaohakikisha amani na usalama ya wanaoabudu ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, tumejaribu kujifunza kutoka kwenye nchi nyingine, wenzetu kwa mfano Nigeria wenyewe hawana masharti yoyote, lakini tunaona yanayotokea huko. Wenzetu wa Rwanda wameweka utaratibu na wameweka hata elimu ya mtu anayeweza kutoa au kuanzisha *ministry* au huduma ya namna hiyo, lazima awe na aina fulani ya elimu. Wenzetu Kenya walijaribu wakaenda nalo lakini hawakulimaliza na Uganda vilevile na wenyewe wanaendelea nalo.

Mheshimiwa Spika, nasi nadhani iko haja ya kuchukua maoni haya na kubadilisha hata kama siyo sheria, basi kanuni zilizopo kwa haraka ili tuweze kuwa na mfumo mzuri wa namna ya kuabudu. Sitaki niseme zaidi ya hapo kwa sababu, ni leo hii mchana nimekutana na wahusika wa dhehebu lile la *Calvary Assemblies of God* ambao Boniphace Mwamposa anafanya kazi katika lile dhehebu na kwamba ile huduma anayoitoa siyo huduma iliyosajiliwa nasi hatuna usajili wa huduma ile, lakini ile ni *slogan* tu; lakini yeye amesajiliwa na wenye lile dhehebu wamekuja wamekiri kwamba ni mtumishi wao, ni mfanyakazi wao, ni kiongozi ambaye anahudumu Dar es Salaam na Kilimanjaro na amekuwa akifanya hivyo mara zote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea na hatua nyingine za jambo lile kama kioo na Mwalimu wa mengine yasitokee huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja ya Kamati. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi utumalie upande huo, karibu sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii iliyokuwa mbele yetu. Naomba niishukuru Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni waliyotoa juu ya Wizara yangu ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa maoni kwamba kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa kunaathiri ufanisi. Napenda niwaeleze tu kwamba sasa hivi tuko pazuri sana. Sera hii ilichelewa kwa muda kwa sababu tulikosa maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi kirefu, lakini nafurahi kulijulisha Bunge lako kwamba maoni yameshapatikana kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kwamba kwa sasa wadau wanashirikishwa kwa maana ya vyombo vyote vya ulinzi na usalama kupitia maoni hayo; na rasimu ya sera yenyewe ili hatimaye ikamilishe mchakato ambao ni kupita katika Baraza la Makatibu Wakuu na hatimaye Baraza la Mawaziri. Nina imani kwamba suala hili litakamilika ili tuweze kupata sera na kazi zetu ziendele vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, kukosekana kwa *beacons* za mipakani kunaathiri ulinzi. Ni kweli kwamba katika mipaka yetu kuna wananchi wamekuwa wakitoa *beacons* zile na kufanya

shughuli za kibinadamu katika maeneo ya mipaka. Hili suala limeshughulikiwa kwa maana kwamba Wizara zote zinazohusika na suala hili; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Ardhi, pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje, tulishakaa tukaamua kwamba sasa wakati muafaka umefika wa kurudisha beacons katika maeneo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vikao vilifanyika na wenzetu wa Kenya, Uganda na nchi nyingine na zoezi limeanza. Kwa upande wa Kenya tumesharudisha baadhi ya beacon na vilevile tunaendelea katika mpaka wa Tanzania na Uganda kurudisha beacon hizi. Kwa hiyo, suala hili linashughulikiwa na kiwango kikubwa kazi imeanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala la madeni ya Suma JKT kwa upande wa matekta. Ni kweli kwamba fedha bado hazijalipwa takribani shilingi bilioni 34, lakini juhudi kubwa zimefanyika na hivi karibuni tumeweza kukusanya zaidi ya shilingi bilioni tatu katika hatua hizo mpya. Tumeingia mikataba mipya na wale wote waliokuwa wamekopa ili sasa tuweze kuwafuatilia kwa karibu. Vilevile tumeweka Kampuni ya Udalali ya Suma JKT ambayo itakuwa inawapitia wote wanaodaiwa kwa madhumuni ya kuwadaa na kuweza kurudisha fedha hizo. Kwa hiyo, hatuna shaka kwamba baada ya muda siyo mrefu tutaweza kuwa tunazirudisha fedha hizi ili ziweze kutumika kwa makusudio yaliyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya kutotolewa kwa fedha kwa Shirika la Nyumbu kunaathiri shughuli za utafiti wa shirika hilo. Ni kweli kwamba kwa muda mrefu fedha zinazotolewa kwa nyumba zimekuwa haba, mwaka huu wa fedha tuna shilingi bilioni 2.5 katika bajeti yao ambayo haikidhi kwa kweli. Nyumbu wamekuja na utaratibu mpya wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi wa Shirika ambao wameutengeneza vizuri na wameweka bajeti ambayo kwa kweli itapita Serikalini. Tukiweza kupata fedha hizo shirika litarudi katika utaratibu wake wa awali wa kufanya tafiti za mazao ya kijeshi ili hatimaye tuweze kulirudisha katika ile dhamira ya kuwepo kwa shirika hili la Nyumbu.

Mheshimiwa Spika, ukiacha Kamati ambayo hoja zake zilikuwa ni hizo ambazo nimeshazitolea ufafanuzi, Mheshimiwa Maige alizungumzia kurudisha beacons ambayo na yenyewe nimeshaizungumza na Mheshimiwa Masele alisema Serikali iendelee kuipatia bajeti mashirika ya Nyumbu na Mzinga ili yaendelee kuzalisha mazao ya kijeshi na kudhibiti ulinzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, mashirika yote mawili la Nyumbu na lile la Mzinga wameshatengeneza Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano kwa Nyumbu na Miaka Kumi kwa Mzinga. Kwa maana hiyo, ni kwamba katika mipango ile ya muda mrefu wameweka bajeti zao pia, ni matarajio yetu kwamba bajeti hizo zitapatikana mwaka hadi mwaka katika kipindi hicho ili waweze kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna pongezi kwa Suma JKT kwa kazi nzuri ya ujenzi wanayoifanya katika maeneo mbalimbali kama Mererani, Ofisi za Serikali hapa Dodoma na kutoa mafunzo kwa vijana wetu. Tunapokea pongezi hizi na tunaahidi Bunge lako kwamba Suma JKT wataendelea na kazi zao za msingi za kulea vijana na vilevile kuzalisha mali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tunakushukuru sana. Sasa Wenyevidi wangu naomba msogee muwe karibu karibu hapa. Tuanze na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, tunahitimisha hoja zetu kwa dakika kumi kumi.

Wenyeviti naomba muwe karibu hapa ili tuokoe muda. Tuko mwisho kabisa. Nishati na Madini na wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pia awe karibu hapa, tujitahidi kutumia dakika kumi. Mambo mengi Waheshimiwa Mawaziri wameshatusaidia pia. (Makofi)

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika hoja yetu. Katika mjadala huu, Waheshimiwa Wabunge ambao waliochangia Taarifa yetu ni Wabunge 14. Sehemu nyingi ya michango hii ilikuwa ni ushauri, tunaichukua michango ile kama ushauri lakini yako mambo machache ambayo nilidhani ni vizuri tuyatolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Kaka yangu Mwijage amesema hapa kwamba mimi nimepitia kwenye mikono yake, ni kweli. Kipindi kile naanza kufinyangwa katika Utumishi wa Umma nilianza pale TPDC na miongoni mwa watu waliofanyakazi kubwa ya kutuonyesha sekta ya Nishati iko vipi ni Kaka yangu Mwijage, na siku zote manshukuru sana kwa kazi kubwa aliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwijage ameibua mambo makubwa katika Taarifa yetu. Kwanza ameonesha hofu kwamba yapo mambo ya msingi hatukuyatendea haki katika taarifa yetu. Jambo kubwa alilolizungumzia ni uwekezaji unaofanywa na TPDC katika suala zima la kutafiti mafuta na gesi. Ukipitia taarifa yetu ni kweli hatulisema kwa undani jambo hili; na tulifanya hivi makusudi kwasababu mbili:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili tumekuwa tukilisema mara kwa mara kwenye Taarifa zetu zilizopita; ni jambo ambalo Serikali inalifanyiakazi. Nataka nimtoe hofu; katika Bajeti tuliyopitisha hapa tulitenga fedha kwa ajili ya kazi ya utafiti; ipo kazi inaendelea kufanywa na TPDC. Hata hivyo kama Kamati tuliamua kufanya uamuzi wa makusudi wa kutoliibua sana jambo hili ndani ya nyumba yako hii kwasababu tuna mfano halisi, nchi inapojenga matumaini makubwa kwa wananchi msipoya-*manage* matumaini hayo mnaweza kuzalisha tatizo ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo kimsingi tuliamua ku-*manage expectation* kwa taifa letu; na kama kuna jambo ambalo huwa linajenga matumaini makubwa kwa wananchi ni wanaposikia suala la mafuta. Ukiwaambia tu kuna utafiti kesho yake asubuhi wanakwambia nchi yetu ina mafuta. Kwahiyo tulidhani tuwe makini katika kufanya jambo hili. Itoshe kusema, katika bajeti ya mwaka huu tulitenga shilingi bilioni 33.2 kwa ajili ya Kitalu cha Mnazi Bay kule Kaskazini. Ipo kazi inafanywa kule na TPDC, zipo kazi zimeshafanyika, anatafutwa mshauri mwelekezi ili aweze kushauri jinsi ambavyo tunaweza kufanyakazi ya kuchoronga visima kwa ajili ya utafiti wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye kitalu cha Easi Wembere nako tulitenga bilioni 6.3, ipo kazi inafayika na kazi inakwenda vizuri. Pia lipo eneo la Kitalu Namba Nne kwenye maji ya bahari ya kina kirefu, tulitenga bilioni 22.62, ipo kazi inaendelea. Nataka niliambie Bunge hili kwamba utafiti uliofanya na TPDC ulitumia *the best technology in the World* katika kufanya utafiti wa kupata mambo haya. Kwahiyo, itoshe kusema kwamba ipo kazi kubwa inafanyika.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine kaka yangu Mwijage amelisema. Hili msingi wake ni kazi ambayo Kamati imekuwa ikiifanya kwa muda mrefu. Hoja ya kuwa na hifadhi ya pamoja (*Strategic reserve*) ya mafuta katika nchi hii ni hoja ambayo Kamati yangu imekuwa ikiishughulikia kwa muda mrefu. Hivi tunavyozungumza, TPDC ina mkakati wa kutumia matenki

## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yaliyopo Kigamboni kufanya ukarabati ili matenki yale yaweze kuhifadhi mafuta. Kama haitoshi, TPDC imeshapata maeneo kule Tanga kwa ajili ya kujenga matenki ya kuhifadhi mafuta.

Mheshimiwa Spika, vilevile yamekuwepo mazungumzo kwamba tunaweza kutumia refinery yetu iliyoko kule Kigamboni ili kuwa na mfumo huu wa uingizaji wa mafuta kwa pamoja. Imekuwa na changamoto zake, wadau wamekuwa wakipishana, na jambo hili alikabidhiwa TR ili kuweza kuja na majibu ya jinsi gani tunatoka hapa. Kuna kazi inaendelea, kwasababu haijafika sehemu nzuri tulidhani tusillibue ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, wenzetu wa Mamlaka ya Bandari nao huenda wakaingia wkenye kujenga matenki haya ili yaweze kutumika katika uhifadhi wa mafuta. Ninachoweza kukubaliana nae ni kwamba ni kweli, jambo hili ni la msingi sa, pengine tumechelewa kulifanyiakazi, ni vizuri Serikali ikaongeza kasi katika kushughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, amezungumzia katika suala la upotevu wa mafuta, amezungumzia suala la *flow meter* na *margin*; haya ni mambo ambayo yanajenga ule msingi wa dhamira yetu ya kuwa na hifadhi ya pamoja ya mafuta. Kwahiyo, nimuondoe hofu, mambo haya Kamati inayashughulikia.

Mheshimiwa Maige kuna jamno amelibua la utozaji wa *loyalty* katika mawe lakini vilevile katika dhahabu. Hili tunalichukua, nikuahidi Kamati itali-persue tuone tunatokaje katika mkwamo huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja, ahsante sana. (Makofi)

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Luka Kitandula. Sasa baada ya hitimisho jema, naomba niwahoji Waheshimiwa Wabunge kwamba Bunge sasa mpokee na kukubali Taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu shughuli za Kamati hiyo za Mwaka 2019 pamoja na Mapendekezo yake.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019 ilipitishwa na Bunge)

**SPIKA:** Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa rehani karibu tafadhali. (Makofi)

**MHE. SALUM MWINYI REHANI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kuweza kunipatia muda tena wa kuja kuhitimisha hoja yetu tuliyoanza nayo asubuhi, lakini kwa makofi mengi yaliyopigwa hayo yanaanshiria kwamba sasa hivi niko ki-*diplomatic* zaidi. (Vicheko)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamepata fursa ya kuchangia kwenye Wizara zetu hizi tatu, na mimi niseme wazi kwa dhati kabisa nimechukua maoni yote na mawazo waliyokuwa wametushauri. Yako ambayo yametolewa ufafanuzi na baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri na yako ambayo sisi kama Kamati tutakwenda kuyafanyiakazi. Hata

hivyo na mimi nilitaka niyaweke sawa tu baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza na kuahisi kwamba haya tutakwenda kuyafanyiakazi.

Mheshimiwa Spika, lilikuja suala zima la Sera na Sheria ya Ulinzi binafasi; hili lazima tukubali ukweli katika eneo hili watu wengi wameajiriwa na hatuwezi kutaacha kundi la watu zaidi ya 250,000 wasiwe na sera na sheria inayoweza kuwaongoza. Makampuni mengi kama tulivyokwishasema ni ya kurithiwa tu. Wazee wao walianzisha wao wakarithi watoto na hakuna sheria inayoweza kuwasimamia.

Kwahiyo hilo bado tutarudi kuweza kuhakikisha kwamba Wizara inaitokeleza na kuiwasilisha hapa Bungeni ili kuweza kupata sheria itakayoweza kuwalinda na kuweza kuwa na Mashirika au Kampuni ambazo zinajiendesha kwa sheria iliyo thabiti.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni suala la NIDA; bado kwetu kama Kamati tumeliona kama ni donda ndugu. Watanzania wengi hawajapata fursa ya kupata Vitambulisho vya Taifa na bado wengine wako waliokuwa hawajaandikishwa. Sisi kama Kamati tumeshalizingumza lakini tunasema wazi kwamba bado tunakwenda kulikalia na kuhakikisha kwamba mitambo iliyokuwa imewekwa kuweza kutoa vile vitambulisho kwasababu tulikuwa na ahadi ya vitambulisho milioni 20 Disemba mwaka jana, ahado ambayo kwa mitambo iliyokuwepo haikuweza kufikiwa; kwahiyo tunakwenda kusimama na mitambo mipya kuhakikisha kwamba ahadi hiyo Watanzania wanapata vitambulisho vyao mapema na kila mmoja atakuwa anatambulika kihalali.

Mheshimiwa Spika, lingine dogo lilidokezwa na Mheshimiwa Masele; suala la uwekezaji kwenye sekta ya ulinzi; nalo hili tumelichukua na bado tutaendelea kuisgauri Serikali iweze kuwekeza kwenye suala zima la ulinzi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bobali aliligusia suala la mipaka; ni kweli kabisa Tanzania ina mipaka mirefu sana na hasa upande huu wa. Mimi nilipata fursa ya kuwa mwangalizi katika uchaguzi ule wa Msumbiji, maeneo yale ya Tunduru ukiangalia mipaka zaidi ya kilometa 70 na ina *Panya road* zaidi ya 300 na zaidi. Kwahiyo, hili nalo ni suala ambalo linatakiwa tujipange zaidi kuhakikisha kwamba haipitishi wahalifu katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi linalojitokeza hapa, wenzetu, hasa wa ule upande wa Kusini wa Msumbiji wamekuwa wakijiegesha au wanasema kwamba wanatoa fursa ya kuolewa kwa wingi Tanzania ili kuweza kupata uraia wa Tanzania na hivyo kutumia fursa hiyo ya ile mipaka kuweza kujipenyeza na kuishi huku isivyohalali lakini baadaye wanakuwa halali kwasababu wengi wao wanaomba kuwa raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala la Magereza tumelichukua

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa hapa ni suala la Diplomasia. Mimi niseme wazi kwamba tunakwenda vizuri kwasababu Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi kwa kweli tuseme wazi kwamba tumepata hazina nzuri, ni nguzo ya Nchi yetu, ana uwezo mzuri wa kuisemea Tanzania ndani na nje ya nchi. Katika eneo hili haogopi kitu na amekuwa akisimama kizalendo kuhakikisha kwamba thmanai na hadhi ya Tanzania inaweza kutambulika na kuweza kupewa hadhi inayostahili ndani ya sura ya Dunia. Nimpongeze sana na nishukuru kwa uzalendo na nguvu ambayo anaitumia kuhakikisha kwamba nchi hii haiweze kuonewa wala haiweze kudhulumiwa kwa njia nyingine yoyote ile. Sisi kama Kamati tuseme wazi kwamba tutashirikiana naye kwa karibu zaidi kuona kwamba tunaweza kufanikiwa kwa kila ambalo tumekuwa tukilipanga.



## NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini hata lile ambalo tunasema kwamba halikuguswa, la maradhi ya Corona kule China tuseme wazi kwamba sisi kupitia Wizara hii tumezungumza kwenye Kamati na Mabalazi wetu wanafnya uratibu wa watu wetu ambao wako katika nchi mbalimbali duniani kuhakikisha kwamba Watanzania hawawezi kuathirika. Lolote litakalotokea nchi yetu itatoa taarifa kupitia viongozi hawa wa Mabalazi pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje kuijulisha hali ilivyo kwa maradhi haya lakini na maradhi mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nimdokeze Dada yangu Salome, kwamba nchi haijajitoa kwenye suala zima la ICC, bado maelezo yaliyokuwepo ya kwamba nchi imejotoa si kweli na tunajua msimamo wa Tanzania ulivyo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tumeweza kulishughulikia kama Kamati ni suala zima la kuhakikisha kwamba diplomasia ya uchumi kwa Mabalazi wetu inafanyakazi; na ndiyo maana kipindi hiki cha karibuni wameletwa Mabalazi hapa nchini kuja kuona vivutio na fursa zilizopo ndani ya nchi na kujua kwamba wakienda kule wanakokwenda waweze kuitangaza Tanzania kwenye diplomasia ya uchumi. Wameona miradi mikubwa ya umeme, reli ya mwendokasi, Bandari pampja na utayari wa Watanzania tulivyoweza kujipanga kwenye suala zima la utalii. Moja ya task ambayo wamepeva ni kuhakikisha kila Balazi analeta watalii ndani ya nchi hii na kuongeza Pato la Taifa lakini kuongeza watalii ambao wanaitembelea nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ambayo tumeweza kuyaangalia na kuyatolea ufafanuzi niseme wazi kwamba yale ambayo yaliyokuwa hayakuguswa au wale Wabunge ambao hawakuguswa mawazo yao yote tumeyachukua sisi kama Kamati tutayafanyia kazi na tutayaleta majibu yake kwa maandishi kwa wahusika ambao wanayahitaji hayo majibu.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo mimi nikushukuru na niombe tena kutoa hoja ili niweze kukamilisha hoja yangu hii ya *report* hii ya nusu Mwaka 2019/2020 kwa awamu hii ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ahsante sana na sasa ni wajibu wangu kwamba niweze kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa mpokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati hiyo kwa Mwaka 2019 pamoja na mapendekezo yake yote.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019 ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa niaba yenu basi nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati zote mbili kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya Mwaka mzima. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni Kamati muhimu, ni Kamati nyeti, mambo yenu mengi sana mnayamaliza huko huko. Kwa kweli karibu kipindi chote hicho iliongozwa na Mheshimiwa Zungu, tunakushukuru sana kwa Utumishi wako katika Kamati hiyo. Naamini uliowaacha wakiongozwa na Makamu wako wataendeleza gurudumu na mambo yenu mengi hamuwezi kuyaleta hapa sisi tunafahamu kwasababu katika Kamati hii yako mambo mengi, mazito na nyeti ambayo huwa

hayaongelewi hadharani. Tunajua mnashauri mambo mengi, mambo muhimu ya nchi na kwa kweli mnafanyakazi kubwa sana.

Pia Kamati yetu ya Nishati na Madini chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Kitandula na Makamu wake Mheshimiwa Mariam Ditopile wamefanya kazi kubwa sana katika Mwaka huu wa 2019, wamesaidiana sana na Mawaziri hawa wa Nishati na Madini na ndiyo maana mnaona kuna utulivu mkubwa katika Wizara hizo mbili. Kumbukumbu zangu za miaka ya nyuma huko, wale Wabunge waliokuwepo kwenye Ukumbi ule wa Msekwa wakati Bunge likiwa kule kabla ya hili halijajengwa watakumbuka wakati Wizara hizi zikiwasilisha Bajeti yake ilikuwa ni vita, ilikuwa ni vita kubwa sana. Aliyekuwa anakaa hapa mezani alikuwa na kazi kubwa mno ya kufanya.

Mimi nilikuwa ni mmoja wa Wenyeviti wa Bunge lakini nilikuwa nakimbia kwasababu wakati ni Wizara moja ya Nishati na Madini ilikuwa ni mapambano kweli kweli; lakini leo hii kwa kweli chini ya awamu hii ya tano ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mambo mengi sana yamepigwa pasi vizuri, mambo yanakwenda. Maana kama kuna Wizara zilikuwa zimeoza huko nyuma ilikuwa Nishati na Madini. Kila Mbunge alikuwa haridhiki na hali halisi ilivyokuwepo. Kila Mbunge alikuwa akilia na umeme yaani ilikuwa ni tabu sana, kwenye Madini ndiyo usipime; tulikuwa tukilalamika sana kwa kupunjwa, kwa kuliwa, kwa kudhulumiwa na hali halisi iliyokuwepo.

Vijasalimia vya mgao vilikuwa vidogo, kwanza havionekani, havieleweki, ukija kwenye almasi huko kwanza hata kinachopatikana hakifahamiki; hivyo vihela hata vinakowekwa sijui London huko havieleweki, hata mfuko wenyewe jinsi gani basi hivyo vihela vya almasi haieleweki yaani ilikuwa ni maswali mengi sana. Sasa leo hi ni uwazi na ukweli na kazi inachapwa, tunawapongezeni sana, sana, sana, sana kabisa. Sasa kurekebisha mahali Bwana si tukio ni mchakato. Kwahiyo tusaidiane na wenzetu Mawaziri hawa tena ni vijana, tusaidiane nao katika mchakato huu tuweze kuvuka pamoja. Tunaamini katika miezi hii iliyobakia mpaka Bunge hili litakapofungwa tutaendelea kuwasaidia Wizara hizi mbili ziweze kufanya vizuri zaidi na zaidi na zaidi na zaidi na sisi tunawaahidi ushirikiano.

Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Simbachawene na timu yako tunakutakia kila la heri, Ulinzi na usalama baridi huko Maafande huko wala hakuna maneno huko mmetulia tuli. Tunaendelea kuwatakiwa kila la heri askari wetu wazidi kubarikiwa. Wenzetu wa mataifa makubwa katika maombi yao wanapoziomba nchi zao huwa hawasahau kuyaombe ana majeshi yao pale pale. Kwahiyo na sisi tunawaomba wanajeshi wetu, askari wetu wa ngazi zote kuanzia jeshi la akiba na majeshi mengine yote mpaka Jeshi la Ulinzi na Usalama wazidi kuwa imara kwasababu bila wao sisi hatuwezi tukalala usingizi tukakoroma kama tunavyofanya Tanzania. Tunawaaminia, tunajua bado wanamahitaji ya mambo mengi askari wetu na bajeti yetu ndiyo hiyo Wizara ya fedha wanajitahidi. Hata hivyo kadri hali yetu inayokuwa bora zaidi tunaamini kabisa na askari wetu watazidi kuwa na hali nzuri zaidi na Bunge hili linawapenda sana maafande wote wa Tanzania.

Basi Waheshimiwa Wabunge tumemaliza shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya siku ya leo yene kwa wakati. Keshokutwa kama tulivyopanga mwanzoni wakati wa Briefing tuliambiana jioni tutakuwa tunafunga kazi hapa mezani. Uzuri wa Bunge ni chombo chenye kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu. Nafikiri ni taasisi chache zinazo-*match* na utendajikazi wa Bunge maana tunapanga kwamba tumeanza tarehe fulani saa 03:00 asubuhi na tunamaliza Ijumaa tarehe saba kwenye saa 10:00 au 11:00, pale pale, na shughuli zetu tulizopanga zinakuwa zimetokelezeka kwa siku ile kama ambavyo tulipanga leo tutamaliza Saa 03:00 na kuamliza saa 01:45 na kweli kwa uendeshaji wa kisayansi tunamaliza 01:45 kama ilivyopangwa. Kwa maneno

*NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

hayo sasa nimualike *Surgent at Arms* aweze kuja, na kwa jinsi hiyo basi, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 01:43 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 6 Februari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*